CAPTURE OR KILL

1

IKULU - DAR ES SALAAM

Wageni wachache walioalikwa Ikulu kushuhudia kuapishwa kwa Mathew Mulumbi kama mkuu mpya wa Shirika la UjasusiTanzania, waliwasili na kuchukua nafasi zao.Miongoni mwa wageni waliofika kushuhudia kiapo hicho ni marafiki wa karibu wa Mathew ambao ni Papi Gosu Gosu na Ruby Rafael.

Hafla hiyo ya uapisho haikuwa ikirushwa mubashara kama ilivyozoeleka

pindi viongozi wanapokula kiapo Ikulu.Hata uteuzi wa Mathew ulikuwa wa kimya kimya haukutangazwa bali

walifahamishwa watu wachache wa muhimu kama viongozi wakuu serikalini na wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama.

Hatimaye Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliingia katika ukumbi mdogo ambao hafla ya uapisho ilifanyikia.Watu wote wakasimama.Wimbo wa taifa ukaimbwa. Bila kupoteza muda kiapo kikaanza.Mathew akaitwa.Akala kiapo mbele ya Rais kisha akaweka sahihi kiapo chake.Akapewa mkono wa pongezi na Rais.

Hakukuwa na hotuba yoyote iliyotolewa siku hiyo hivyo baada ya kiapo, likafuata zoezi la upigaji picha.Baada ya kukamilika, wageni

wakatawanyika kwenda kuendelea na majukumu yao ya kila siku.Mathew Mulumbi akabaki Ikulu.Alikuwa na mazungumzo ya faragha na Rais.

“Hongera sana Mkurugenzi na karibu sana Ikulu,” alisema Rais.

“Ahsante sana mheshimiwa Rais kwa imani yako kwangu. Hasa kwa kuniteua katika nafasi hii muhimu kabisa ya usalama wa nchi yetu,” Mathew alijibu. Wakatabasamu wote wawili.

“Ninakushukuru kwanza kwa kuipokea nafasi hii.Ungeweza kukataa uteuzi huu na hakuna adhabu yoyote ile iwapo ungekataa,” Rais Pius aliongeza kisha cheko likaibuka kati yao.

“Kukubali kwako kuitumikia nafasi nyeti kama hii ni heshima kwa

niliyekuteua na kwa Watanzania ambao mimi niko hapa kwa niaba yao.Mathew,tambua ya kwamba umebeba majukumu mazito,hasa kwa wakati huu ambao nchi yetu iko katika vita kubwa ya kiuchumi" Rais alinyamaza kidogo

"Kama nchi tunapiga hatua kubwa kimaendeleo.Tunapambana kuelekea katika kujitegemea wenyewe kwa kutumia rasilimali zetu tulizo nazo lakini si safari nyepesi hata kidogo.Kupiga kwetu hatua ni jambo linalowaumiza sana mabeberu.Pamoja na mipango yao miovu dhidi yetu, nimeshaamua nchi hii itasonga mbele na tutakuwa nchi inayojitegemea kiuchumi.Hakuna taifa litakalotuyumbisha.Ili tuweze kushinda

vita hii, tunahitaji sana kuliimarisha shirika letu la Ujasusi" alisema Rais na kunyamaza. Akainua glasi ya maji akapiga funda kadhaa kisha akaendelea.

"Kwa nini tunahitaji shirika imara la ujasusi? Akauliza na kumtazama Mathew kwa sekunde kadhaa halafu akaendelea

"Kama nilivyokwambia mabeberu hawafurahishwi na mbio zetu kuelekea kujitegemea hivyo hujuma ni nyingi.Tunavyozidi kupiga hatua kimaendeleo tunatengeneza pia maadui.Tunao maadui wa nje na wa ndani pia.Kwa hapa ndani, wapo watanzania wasiopenda kuona nchi ikipiga hatua kimaendeleo.Wanazo sababu zao za kutaka hivyo.Wengine

sababu za kisiasa,wengine kimaslahi nakadhalika.Hawa wamegeuka mawakala wa mabeberu.Siri za mipango yetu ya maendeleo zimekuwa zikiibwa na kupelekwa katika mataifa ya nje,lengo likiwa kutudhoofisha.Hawa ni Watanzania wachache wasaliti kwa nchi yao ambao wako tayari hata kuona nchi hii inaingia vitani ili wawafurahishe mabeberu.Nataka ulishughulikie hilo na tuwajue wasaliti wa taifa hili!" Alisema kwa ukali Rais Pius.

"Kutoka nje ya nchi, kuna mipango mingi ya kutudhoofisha inayofanywa na mataifa makubwa.Wameanza kuyatumia hata baadhi ya mataifa majirani zetu kutuhujumu.Kwa mfano,Tanzania hivi sasa tuna umeme wa uhakika,hii

imepelekea tuwe na viwanda vingi vinavyozalisha bidhaa nyingi zenye ubora mkubwa na kwa gharama nafuu.Kwa hakika, hili halijawapendeza mataifa makubwa hivyo basi yametolewa maelekezo kwa baadhi ya mataifa yanayotuzunguka kuweka kodi kubwa katika bidhaa zote zinazotoka Tanzania kwa lengo moja tu la kuhakikisha bidhaa zetu haziingii katika masoko yao.Nchi hizo zinazofanya hayo zinapewa misaada mikubwa kutoka kwa mabeberu.Mathew hii ni vita lazima tupambane kuhakikisha uchumi wetu unakua kwa gharama zozote" Rais akanyamaza tena kidogo na kusukumia na funda la maji yaliyokuwa mezani.

“Mathew,kwa maelezo hayo machache naamini umeelewa ni kwa nini ninataka kuliimarisha shirika letu la ujasusi.Nataka majasusi wetu wapenye na kuzidaka mbinu chafu za mabeberu dhidi yetu.Nataka wadake mbinu na mipango yote ya wapinzani wetu kibiashara.Nataka makuwadi wote wa mabeberu walioko hapa nchini wafahamike na wawekwe katika uangalizi mkali wa karibu bila wao kufahamu.Nataka wakipanga mpango usiku wa leo,kesho asubuhi tuwe na taarifa za walichokipanga kukifanya.” alisema Rais Pius.

“Mheshimiwa Rais, hayo yote uliyonieleza ninayafahamu na ninakuahidi kuyashughulikia.Matokeo

yake utayaona kinagaubaga.Sitakuangusha mheshimiwa Rais," alisema Mathew.

"Ahsante sana.Tukiacha hayo,kuna suala lingine ambalo nataka nikueleze ulishughulikie kwa uzito mkubwa lakini kimya kimya bila watu kufahamu" Rais alinyamza kidogo halafu akaendelea.

"Wiki moja iliyopita,waziri wetu wa Mambo ya Nje Dr. Magnus Kalebi aliuawa akiwa nje ya nyumba yake akisubiri kufunguliwa geti.Alikuwa anatokea nchini Rwanda ambako nilimtuma kwa kazi maalum lakini kabla hajaniletea taarifa ya kile nilichomtuma,akauawa na mkoba wake wenye taarifa zote ukachukuliwa.Nina kila sababu ya kuamini kuwa mauaji yale

ya waziri Magnus yana mkono wake kutoka nje ya nchi.Nitakueleza kwa nini ninaamini hivyo," Rais akanyamaza tena kidogo. Uso wake ukaonekana kuingiwa na huzuni.Dhahiri mauji ya Dr. Magnus yalimkwaza.

"Kuna mazungumzo ya siri yanaendelea hivi sasa kati yangu na marais wa Rwanda na Burundi.Tunazungumza namna ya kuziunganisha nchi hizi tatu kuwa nchi moja" Rais akanyamaza kidogo baada ya mshangao kuonekana usoni kwa Mathew.

"Sijakuelewa Mheshimiwa Rais," alisema Mathew.

"Kuna mazungumzo ya siri yanaendelea hivi sasa kati yangu na

marais wa Rwanda na Burundi ili kujaribu kuziunganisha nchi hizi tatu iwe nchi moja," Rais akarudia kauli yake ile ile kisha akamtazama Mathew ambaye ni wazi alionesha kuhitaji maelezo zaidi.

"Sura yako inaonesha unahitaji maelezo zaidi, nitakueleza kwa sababu nataka upate picha pana zaidi ya hili jambo," alisema Rais.

"Miaka miwili iliyopita,kundi la waasi wanaojiita jeshi la ukombozi la Congo lilivamia vijiji vya nchi ya Rwanda vilivyo katika mpaka wa nchi hizo mbili na kuua watu zaidi ya mia tatu,kupora na kuharibu mali.Serikali ya Rwanda ilituma haraka sana vikosi vyake kwenda katika vijiji vilivyovamiwa na waasi ili kukabiliana nao,lakini vikosi

hivyo vilijikuta vikishambuliwa vibaya sana na waasi waliokuwa na silaha nzito.Vikosi zaidi viliongezwa, lakini bado mapigano yakawa makali zaidi,waasi walipata ushindi na kuvirejesha nyuma vikosi vya serikali na kutwaa maeneo mengi zaidi.Hapo ndipo ilipomlazimu Rais wa Rwanda kuomba msaada wa jeshi la Tanzania ili kukabiliana na kundi hilo la waasi.Nililipokea ombi la Rwanda kwa mikono miwili.Bila kuchelewa,nikatuma vikosi vya jeshi la wananchi wa Tanzania kwenda Rwanda kuungana na jeshi la nchi hiyo katika kukabiliana na waasi.Hayakuwa mapambano rahisi hata kidogo.Tulishangazwa na uwezo wa waasi hao wa jeshi la ukombozi wa

Congo,ndipo tulipowatuma majasusi nchini Congo kuchunguza kuhusu kundi hilo la waasi. Taarifa zilizopatikana zilituonesha waasi hao walikuwa wakisaidiwa na serikali ya Congo iliyowapatia silaha nzito na vifaa vingine vya mapigano.Tuligundua kuwa Rais wa Congo wa wakati huo Jean Francois Kazadi na kiongozi wa waasi hao Samwel Kanyimbu ni marafiki wa karibu sana.Wote walikuwa jeshini kabla ya Jean Francois Kazadi kumpindua Rais aliyekuwa madarakani na kuchukua urais.Baada ya Jean Francois Kazadi kuwa rais, kufuatia mapinduzi ya kijeshi,kulitokea mgawanyiko katika jeshi la Congo.Hapo ndipo moja ya kundi lililojitenga kutoka jeshi la serikali

wakaanzisha kundi lao la waasi na kuliita jeshi la ukombozi wa Congo.Taarifa hiyo ilionesha kundi lile la waasi wa jeshi la ukombozi lilianzishwa kwa mkakati maalum wa kuanzisha machafuko kati ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Rwanda.

Taarifa hizo zilinipelekea niongeze vikosi zaidi vya jeshi nchini Rwanda.Niliwapa maelekezo ya kuhakikisha wanakiondoa kikundi hicho cha waasi katika ardhi ya Rwanda.Wanajeshi wa Tanzania wakisaidiana na wale wa Rwanda, walifanikiwa kuwarejesha waasi katika nchi ya Congo.Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo Meja Jenerali Jean Francois Kazadi,alitangaza kuwa

Tanzania na Rwanda wana mipango ya kuvamia nchi yake.Alitoa vitisho vya kuishambulia Tanzania kama itaendelea kuisaidia nchi ya Rwanda.Vitisho vile havikunishtua.Licha ya kuondolewa katika ardhi ya Rwanda,waasi hao waliendelea kufanya mashambulizi wakitokea nchini Congo wakirusha maroketi kuelekea Rwanda.Baada ya kuona hivyo, niliamuru vikosi vya ushirika vya Tanzania na Rwanda kuingia nchini Congo kuwasaka waasi hao.Kama alivyoahidi Rais Jean Francois Kazadi kuishambulia Tanzania,alituma ndege vita zikadondosha mabomu mkoani Kigoma na moja ya bomu lilianguka katika shule ya bweni ya wasichana.Zaidi ya wanafunzi arobaini

walifariki.Nilipata hasira nikapeleka jeshi zaidi na kutoa maelekezo ya kusonga mbele hadi Kinshasa kumuondoa dikteta huyo Jean Francois Kazadi.Katika kuunga mkono mapambano hayo, Burundi nayo ilitoa vikosi vyake.Baada ya miezi minne vikosi vya pamoja vikafanikiwa kumuondoa madarakani Jean Francois Kazadi.Alikimbia baada ya kuona anashindwa kwani hata wanajeshi wake walimuasi wakajiunga na vikosi vya umoja.” alisema Rais Pius na kunyamaza kidogo.

“Nadhani unafahamu nchi ya Rwanda ina ukubwa wa kilometa za mraba 26,338,Burundi 27,834 naTanzania 945,087.Nchi ya Rwanda

inaingia kwa Tanzania mara 36 na Burundi mara 34.Hizi ni nchi ndogo ukilinganisha na nchi kama Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo ambayo zilipigana nayo.Kwa ukubwa wa Rwanda inaingia zaidi ya mara sabini kwa nchi ya Congo, hivyo ni nchi ambayo kwa namna yoyote ile haiwezi kupigana na taifa hilo la pili kwa ukubwa barani Afrika likitanguliwa na Algeria.Kitendo alichokifanya Rais Jean Francois Kazadi cha kuwatumia waasi kuivamia Rwanda kiliwapa hofu marais wa Rwanda na Burundi.Kwa hiari yao wenyewe waliamua nchi zao mbili zijiunge na kuwa sehemu ya Tanzania.Sababu nyingine iliyowasukuma marais wa nchi hizo mbili kutaka kuziunganisha nchi zao

na Tanzania, ni viashiria vingi vya kutokea kwa machafuko makubwa hasa katika nchi ya Rwanda.Kuna hofu ya kutokea kwa mapigano ya kikabila.Taarifa za kiintelijensia zinaonesha kwamba kumeanza kupandikizwa chuki baina ya makabila makuu ya Wahutu na Watutsi.Njama hizo zinafadhiliwa na mataifa ya nje ambayo lengo lao ni kuingia Rwanda kwa gharama yoyote ile.Ipo sababu kwa nini wanatumia nguvu kubwa kutaka kuingia Rwanda," akanyamaza kidogo.

"Mpakani mwa Rwanda na Burundi, kumepatikana madini yenye thamani kubwa zaidi duniani yanaitwa Kardistone ambayo hayapatikani sehemu nyingine duniani.Ni madini ambayo yanafaa zaidi

kutengeneza vifaa vya kielektroniki kama vile kompyuta, simu na kadhalika.Mataifa makubwa yanamezea mate utajiri huo mkubwa wa madini hayo ndiyo maana inatumika kila mbinu ili waweze kuingia Rwanda.Moja ya mbinu yao chafu ilikuwa ni kutumia kikundi cha waasi wa jeshi la ukombozi wa Congo.Lengo kuu la kuunda kundi hilo la waasi lilikuwa kudhibiti sehemu yenye madini ya Kardistone.Kwa msaada wa jeshi la Tanzania, hilo halikuwezekana.Kundi lilifurushwa na kibaraka wao Jean Francois Kazadi akang'olewa.Wakubwa hawakufurahishwa na jambo hilo.Wakaanza kubuni mikakati mingine.Moja ya mkakati wao ulikuwa

kupandikiza chuki baina ya makabila ya nchini Rwanda ili yatokee machafuko,wao wapate nafasi ya kupenya katikati ya machafuko hayo na kuanza kupora madini. Kwa upande wa nchi ya Burundi, wanawatumia wanasiasa.Kumekuwa na vurugu za mara kwa mara nchini humo ambazo zimepelekea mamia ya watu kupoteza maisha.Hii yote ni mipango ya mabeberu.Marais hao wawili waliona njia pekee ya kuzinusuru nchi zao ni kwa kuziunganisha na Tanzania," alisema Rais Pius na kunyamaza kwa nukta chache kisha akaendelea.

"Nililipokea wazo lao kwani ni wazo jema kabisa na mazungumzo yakaanza baina ya marais.Ni mazungumzo ya siri

sana, ila kuna watu wachache ambao tumewashirikisha ambao ni mawaziri wa mambo ya nje wa nchi zetu.”alisema Rais Pius.

“Hatua ipi imefikiwa hadi sasa katika mazungumzo ya kuziunganisha nchi hizi tatu?” Mathew aliuliza.

“Kuna mambo mengi ya kukubaliana kabla ya kufikiwa kwa muafaka wa kuziunganisha nchi hizi.Kwa kuwa Rwanda na Burundi zote ni nchi ndogo,sisi Tanzania tunataka muungano wetu uwe kama ilivyokuwa kwa Tanganyika na Zanzibar.Yaani, nchi hizo zisimezwe na nchi kubwa. Iwe nchi moja, lakini bado Rwanda na Burundi ziendelee kuwa na serikali zao za ndani kama ilivyo kwa Zanzibar.Marais wa

Rwanda na Burundi hawataki hilo wanataka kuwe na serikali moja tu.Hawataki kuwa na serikali zao ndogo za ndani.Hapo ndipo mazungumzo yalipokomea hivi sasa,ninaamini tutapata muafaka siku si nyingi,”alisema Rais Pius.

“Mheshimiwa Rais, unadhani raia wa nchi hizo watakubali jambo hilo pale litakapofikishwa kwao kwa ajili ya kupigiwa kura ya maoni?”Mathew aliuliza.

“Endapo kila kitu kitakwenda vizuri kama mnavyopanga,je, tayari mmepata jina la kuiita nchi hiyo mpya?”Mathew aliuliza.

“Nchi itakuwa ile ile Tanzania,” alijibu Rais na ukimya mfupi ukapita kisha akaendelea.

“Dr. Magnus, nilimtuma Burundi na Rwanda ikiwa ni mwendelezo wa mazungumzo haya ya kuziunganisha nchi zetu.Aliuawa mara tu aliporejea kutoka Rwanda.Nina uhakika mkubwa kwamba kuuawa kwake kumechangiwa na suala hili tunaloendelea nalo.Kinachonipa uhakika huo ni kuchukuliwa kwa mkoba wake wenye nyaraka ambazo alitakiwa kunikabidhi mimi.Jeshi la polisi linaendelea na uchunguzi wake hivi sasa kuwabaini wale waliofanya tukio hilo lakini ninaamini mzizi wa mauaji hayo uko nje ya nchi hivyo ninataka ulishughulikie

hilo ili tujue nani ambao wako nyuma ya mauaji hayo” alisema Rais Pius.

“Mheshimiwa Rais kwa maelezo uliyonipa naamini hizi ni njama za mabeberu ambao hawataki mazungumzo hayo ya muungano yaendelee.Wanafahamu fika muungano huo utakuwa mwiba kwao na hawataweza tena kukipata kile wanachokitafuta.Mheshimiwa Rais,nitalichimba jambo hili hadi mzizi wake.Hata hivyo, ninakuomba jambo moja,” alisema Mathew

“Jambo gani,Mathew?” Rais Pius alihoji.

“Kuna watu wangu ambao ninataka niwaingize katika shirika letu ili wanisaidie.Ni watu ambao ninawaamini

sana na watanisaidia katika kutimiza majukumu yangu,hasa hilo ulilonipa la kuchunguza mauaji ya Dr Kalebi" alisema Mathew.

"Ni akina nani hao? Wana sifa za kufanya kazi katika shirika letu la ujasusi? Rais aliuliza.

"Mheshimiwa Rais, ni watu wangu ninaowaamini sana.Nimeshiriki nao katika misheni kadhaa.Wanajua wanachokifanya" alisema Mathew na kuufungua mkoba wake, akatoa mafaili mawili akamkabidhi Rais faili la kwanza.

"Anaitwa Ruby Rafael Magalla.Huyu ana utaalamu mkubwa wa mambo ya elektroniki.Uwezo wake katika elektroniki ni wa kushangaza.Huyu atatufaa sana katika

kuongoza kurugenzi ya mawasiliano na elektroniki” alisema Mathew.Rais Pius akalifungua faili la Ruby,akalipitia,akaliweka pembeni. Mathew akampatia faili la pili.

“Huyu anaitwa Papi Gosu Gosu.Huyu ana asili ya jamhuri ya kidemokrasia ya Congo.Alichukuliwa na waasi, akapelekwa msituni tangu akiwa mtoto mdogo.Ameishi huko kwa miaka zaidi ya ishirini akipigana vita hadi alipokimbia na kuja Tanzania. Ujasiri wake ni wa kipekee sana. Hana hofu ya kitu chochote.Anaweza akaingia sehemu yoyote ya hatari.Ni mtu ambaye ninamuhitaji sana katika Shirika la Ujasusi Tanzania,” alisema Mathew.

“Umesema huyu Gosu Gosu ni raia wa Congo?” Rais aliuliza.

“Ndiyo, ana asili ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, lakini kwa sasa tayari ni raia wa Tanzania,” alijibu Mathew.Rais akalipitia faili la Gosu Gosu nukta kwa nukta kisha akalifunika.

“Sawa,unaweza ukawatumia vile utakavyo.Mathew, nimekutwisha jukumu zito hivyo ajiri yeyote unayeona anaweza akawa na msaada.Ninachokihitaji mimi ni matokeo ya haraka.Hasa katika hili suala la kuuawa kwa waziri wa mambo ya nchi za nje.” alisema Rais.

Waliendelea na majadiliano kwa muda halafu wakaagana.Mathew akaondoka Ikulu tayari kwenda kuanza kutimiza majukumu yake aliyopewa

kama mkuu wa Shirika la Ujasusi Tanzania.Kabla ya kwenda kuripoti ofisini kwake alipita kwanza nyumbani kwa Ruby ambako aliwakuta Ruby na Gosu Gosu wakimsubiri.

“Mkurugenzi, karibu!” alisema Ruby akimkaribisha Mathew ndani akamletea kinywaji chapchap.Mathew akalegeza tai yake halafu akasema

“Nilikuwa na mazungumzo marefu sana na Rais kuhusu majukumu yangu kama mkurugenzi wa Shirika la UjasusiTanzania. Kwa yakini, ni majukumu mazito nimeyabeba.Lazima niwe muwazi kwenu kuwa ninawahitaji sana ninyi watu wawili mnisaidie katika majukumu yangu mapya.Nimekuja kuwafahamisha kwamba, tayari

nimeshamueleza Rais na ameridhia hivyo kuanzia sasa, ninyi ni wafanyakazi wa Shirika la Ujasusi Tanzania.Ruby, utaongoza kurugenzi ya elektroniki na mawasiliano. Hii ni kurugenzi muhimu sana.Nahitaji mtu atakayeongoza kurugenzi hiyo awe teknolojia imejaa kiganjani kwake.Ujasusi umebadilika sana zama hizi huku teknolojia ikichukua nafasi kubwa.Karibu Ruby katika majukumu yako mapya," alisema Mathew.

"Ahsante sana,Mathew, kwa kuniamini," alisema Ruby.

"Gosu Gosu,wewe utaongoza kurugenzi ya operesheni," Mathew aliongea kisha akaweka tuo. Akanywa kinywaji kusuuza koo kisha akaendelea.

“ Ninahitaji mtu jasiri asiyeogopa,mwenye uwezo wa kudaka risasi kwa mkono.Una sifa hizo Gosu Gosu na utanisaidia sana katika kurugenzi hiyo,” alisema Mathew. Safari hii alitoa kicheko kidogo.Gosu Gosu nae akacheka

“Umenipamba sana Mathew, hata hivyo, ninashukuru kwa kuniamini na kunipa nafasi ya kukusaidia katika majukumu yako mapya,” alisema Gosu Gosu.

“Hamnisaidii mimi, bali tunalisaidia taifa.Nawashukuru ndugu zangu kwa kukubali nafasi hizo.Kesho asubuhi nitawatambulisha rasmi kwa wafanyakazi wengine na kazi zitaanza mara moja.Tutafanya kazi usiku na

mchana hivyo nataka kila mmoja afanye maandalizi na kesho saa mbili asubuhi muwe mmeripoti tayari kwa ulinzi wa taifa.Kuna jambo amenieleza Rais,tutaanza na hilo kulishughulikia," Mathew aliwaeleza akina Ruby kuhusiana na mpango wa kuziunganisha nchi za Rwanda na Burundi kuwa sehemu ya Tanzania.

"Rais anahisi waziri Dr. Magnus Kalebi aliuawa kwa sababu ya jambo hilo.Nani kamuua waziri wa mambo ya nje?Hilo ndilo swali ambalo kila mmoja wetu alale akitafakari," alisema Mathew na kuagana na akina Gosu Gosu kwa miadi ya kukutana kesho yake saa mbili asubuhi katika ofisi za Shirika la Ujasusi Tanzania.

2

Siku ya kwanza ya Mathew Mulumbi kama mkurugenzi wa Shirika la Ujasusi Tanzania ilikuwa ndefu.Alikuwa na majukumu mengi ya kufanya na hakutoka ofisini hadi ilipotimu saa tatu za usiku ndipo alipoondoka kurejea nyumbani kwake.

Alifika nyumbani kwake akafungua geti kwa kitanza mbali akaingia ndani,

akalipeleka gari moja kwa moja katika nyumba ya kuhifadhia magari.Alishuka garini akaelekea katika mlango wa kuingilia sebuleni.Kulikuwa kimya kabisa, akaufungua mlango, akaingia ndani moja kwa moja hadi chumbani kwake.Akawasha taa akaenda katika redio yake kubwa akaiwasha na kuweka mziki laini halafu akaelekea bafuni kuoga.Hata wakati akioga bado kichwa chake kilijaa mawazo kuhusiana na majukumu ya ofisi yake.Baada ya kumaliza kuoga,alitoka bafuni huku akiimba kufuatisha wimbo.Mara tu alipoufungua mlango wa bafuni ghafla akavamiwa na watu asiowafahamu akawekewa kifaa chenye chaji za umeme shingoni akapoteza fahamu.

****

Mathew alipiga chafya mfululizo baada ya kupuliziwa dawa Fulani puani,akazinduka na kujikuta katika chumba chenye mwanga mkali.

“Hallo,Mathew Mulumbi!” alisema jamaa mmoja aliyekuwa amevaa mavazi meupe.Mathew hakumjibu.Yule jamaa akatoka ndani ya kile chumba.

“Nimetekwa.Hawa jamaa ni akina nani? Wanaonekana kunifahamu vyema,waliwezaje kuingia ndani mwangu bila walinzi kujua?”Mathew alijiuliza mara mlango ukafunguliwa tena, wakaingia jamaa wengine wanne.

“Mnataka nini kwangu, ndugu zangu?” Aliuliza Mathew.

“Usihofu,Mathew! Muda umefika wa kufahamu kwa nini uko hapa,” alisema jamaa mmoja kisha Mathew akavishwa mfuko kichwani na kutolewa ndani ya kile chumba akapelekwa katika chumba kingine.Akakalishwa sofani,pingu zikafunguliwa na mfuko kichwani ukavuliwa.Akajikuta akitazamana na kijana mmoja mwenye asili ya Kiarabu aliyevalia nadhifu.

“Hallo, Mathew Mulumbi,” alisema yule jamaa kwa lugha ya Kiarabu ambayo Mathew anaifahamu vyema.

“Wewe ni nani?”Mathew aliuliza huku akimtazama yule kijana kwa hasira,akawafanyia ishara watu wake

watoke ndani ya kile chumba.Akabaki na Mathew pekee.

“Mathew, kwanza samahani kwa usumbufu huu mkubwa niliokusababishia usiku huu.Nina mazungumzo nawe muhimu ndiyo maana nimetumia njia hii kukuleta hapa.”alisema yule jamaa.Akafungua mkebe wa sigara uliokuwa mezani.Akatoa sigara moja.Akaiwasha, akavuta mikupuo kadhaa.

“Unavuta sigara Mathew?”Kijana aliuliza.Mathew akatikisa kichwa kukataa halafu akauliza.

“Nini unakitaka kwangu?”

“Tufahamiane kwanza.Ninaitwa Fahad Abdulkhareem Ghedi,”alisema yule kijana.Sura ya Mathew

ikabadilika,Fahad alitabasamu halafu akavuta tena sigara.

“Una mahusiano ya kindugu na Mahmoud Fadil Ghedi?” Aliuliza Mathew.

“Nilitegemea swali hilo.Ndiyo nina mahusiano ya kindugu na Mahmoud Fadil Ghedi.Ni babu yangu,” alijibu Fahad na kupuliza moshi huku Mathew akiendelea kumtazama kwa macho makali.

“Nini unakitaka kwangu Fahad?” Aliuliza Mathew kwa sauti ya ukali.

“Mathew,nimeona mabadiliko katika uso wako baada ya kukiri nina mahusiano ya kindugu na Mahmoud Fadil Ghed.Babu yangu ni gaidi na kwa sasa yuko hapa Tanzania anashikiliwa

katika mahakama ya Afrika jijini Arusha.Ameua watu wengi na mimi siko hapa kwa ajili ya kumtetea. La hasha!Niko kinyume kabisa na mambo anayoyafanya ya ugaidi. Si ubinadamu na ni kinyume na mafunzo ya dini pia.Hakuna dini yoyote ile inayoelekeza mwanadamu kumuua mwanadamu mwingine.Mwenye uwezo huo ni Mungu peke yake.Hivyo basi, Bwana Mathew, naomba unione kama rafiki, badala ya adui.Mimi si gaidi japo nimetokea katika familia ya magaidi," alisema Fahad.

"Japokuwa umekiri huungi mkono matendo ya kigaidi, lakini una chembe chembe za ugaidi ndani yako.Umeniteka nyara na kunileta hapa bila ridhaa

yangu.Huoni kama uko sawa na babu yako?”Mathew aliuliza kwa ukali.

“Hapana,Mathew Mulumbi.Naomba unipe nafasi nikueleze kwa nini uko hapa.,na kwa nini nataka mimi nawe tuwe marafiki badala ya kuniona kama adui,” alisema Fahad na kuvuta sigara akatoa moshi mwingi mdomoni na puani.

“Baba yangu mzazi anaitwa Abdulkhareem Fadil Ghedi.Ni mtoto wa kwanza wa babu yangu Mahmoud Fadil Ghedi.Nitakueleza kidogo kuhusu baba yangu” alitulia kidogo akavuta sigara halafu akaendelea

“Babu na bibi ambaye ni mama wa baba yangu walitengana,bibi akarejea kwao Libya.Kisa cha kutengana kwao ni kwa sababu bibi hakuunga mkono

matendo ya kigaidi.Wakiwa nchini Libya, bibi alifariki dunia.Baba na shangazi Zahra waliishi maisha ya taabu nyingi baada ya mama yao kufariki.Baada ya mahangaiko ya muda mrefu,hatimaye baba alipata ufadhili wa masomo nchini Ufaransa.Baada ya kuhitimu masomo yake,akapata kazi huko huko Ufaransa, akamchukua shangazi wakaishi wote huko,"Fahad aliweka kituo akavuta sigara halafu akaendelea.

"Akiwa Ufaransa, baba alifuatwa na maafisa kutoka shirika la ujasusi Ufaransa ambao walitaka kumtumia katika mipango yao nchini Libya.Ufaransa walimtaka baba amsaliti baba yake Mahmoud halafu achukue

uongozi wa kundi la Ansar al sharia kisha aende nchini Libya akaanzishe mapambano ya kuitoa madarakani serikali ya Libya.Baba alikubali akarejea Somalia kwa babu akijifanya kutaka kuungana naye kumbe anachukua siri zake na kuwatumia majasusi wa Ufaransa.Baada ya kupata taarifa za kutosha,Ufaransa ikawapa Tanzania taarifa zote za Mahmoud mahala alipojificha. Tanzania waliokuwa wakimsaka Mahmoud kufuatia mashambulizi kadhaa ya kigaidi aliyoyafanya hapa Dar es salaam,wakamkamata babu na kulisambaratisha kundi lake. Baada ya babu kukamatwa, baba akatwaa uongozi wa kundi la Ansar al Sharia alilokuwa

analiongoza babu lakini hakuendelea nalo nchini Somalia, bali alikwenda nchini Libya ambako alianzisha mapigano na vikosi vya serikali.Akiungwa mkono na Ufaransa, alipewa silaha kali mno.Ndani ya muda mfupi kundi lake likawa tishio na kufanikiwa kuiteka miji kadhaa.Mipango ikiwa ni kuitawala Libya" Fahad akanyamaza tena.Akamalizia sigara yake,akatupa kichungi katika sahani.

"Nilizaliwa nchini Ufaransa.Mama yangu ni Mwarabu, lakini ana uraia wa Ufaransa.Baada ya baba kwenda kuanza harakati zake nchini Libya,mama alijitenga naye na kuhamia nchini Marekani." alisema Fahad.Akafungua mkebe, akatoa sigara nyingine.

“Utanivumilia Bwana Mathew Mulumbi.Mimi ni mvutaji mkubwa sana wa sigara.Hasa ninapokuwa nazungumza mambo mazito kama haya”alisema Fahad.Akavuta mikupuo kadhaa halafu akaendelea

“Marekani ina maslahi yake nchini Libya na imekuwa ikilisaidia kwa siri kundi moja la waasi kupambana na serikali ya Libya.Kuibuka kwa kundi la Ansar al Sharia na ndani ya muda mfupi tu wakawa na mafanikio makubwa kuliwapa hofu Marekani.Wakaanza kutafuta namna ya kuweza kulimaliza kundi hilo.Baada ya uchunguzi waligundua mimi ni mtoto wa kiongozi wa kundi hilo.Walinichunguza wakagundua siungi mkono mambo

anayoyafanya baba yangu.Wakanifuata wakanitaka wanitumie katika mpango wao wa kulisambaratisha kundi la Ansar al Sharia.Kifupi, walihitaji mtu wa karibu na baba ili waweze kupata taarifa zake za siri nami nikakubali hasa ukizingatia malipo yalikuwa manono na mimi kwa wakati huo sikuwa na ajira.Maandalizi yalianza, nikapelekwa katika mafunzo.Baada ya kuhitimu,ndipo nilipokutana na Carmelita, tukapendana tukaingia katika mahusiano na hatimaye tukampata mtoto Lebron.” Akanyamaza kwa sekunde chache

“Nilikwenda Tripoli kuanza harakati zangu za kutaka kumuondoa baba na kulisambaratisha kundi lake.Alinipokea vizuri.Tukamaliza tofauti

zetu.Nilimdanganya kuwa nilipata mafunzo ya kijeshi nchini Marekani lakini niliamua kuachana na jeshi, ili nikaungane naye katika harakati za kuiondoa madarakani serikali ya Libya. Alifurahi sana.Akaniahidi nafasi ya juu katika serikali pindi atakapokuwa amekamilisha lengo lake.Kilichotibua tena mahusiano yetu, ni pale nilipomwambia kuhusu Carmelita.Hakuwa tayari nimuoe Carmelita kwa sababu kwanza ni Mmarekani, pili ni mtu mweusi, na tatu si dini yangu.Alinitaka niachane naye, akatamka kwa ulimi wake kuwa mtoto yule aliyebeba damu yetu ni haramu na anatakiwa kuuawa.Tulishindwa kuelewana.Nikaondoka zangu na

kuelekea nchini Ujerumani.Nikiwa huko, baba alitengeneza mpango ili nikamatwe kwa kosa la kukutwa na silaha bila kibali.Wakati nikiwa nchini Libya, nilitengeneza mtandao ili kuweza kupata siri za baba.Mtu wa kwanza ambaye nilimuweka katika mtandao wangu ni msaidizi mkuu wa baba.Nikiwa Ujerumani,huyu ndiye aliyenieleza kila kitu kuhusu mpango wa baba kuniwekea mtego ili nikamatwe na silaha na hatimaye nifungwe gerezani.Niliwataarifu viongozi wangu Marekani, mipango ikawekwa sawa na serikali ya Ujerumani.Mpango wa baba ukafanikiwa, nikabambikiwa silaha,nikakamatwa na kutupwa gerezani.Nilitolewa kwa siri nikarejea

Marekani kimya kimya bila baba kufahamu," alisema Fahad na kuvuta tena sigara.Akapuliza moshi mwingi.

"Wakati akijua niko gerezani nchini Ujerumani, baba akaanza kuandaa mpango wa kuwaua Carmelita na mwanangu Lebron.Aliweka watu wa kumfuatilia Carmelita na kugundua kuwa ana safari ya kuja Tanzania kutalii.Mpango wake ni kuwaua Carmelita na Lebron wakatakapofika Tanzania.Tayari mipango imekwisha anza akishirikiana na baadhi ya watu hapa Tanzania.Sitaki mpenzi wangu na mwanangu wauawe.Ninawapenda sana.Niko tayari kufanya chochote kwa ajili yao ndiyo maana niko hapa kutafuta

msaada," alisema Fahad.Mathew akavuta pumzi ndefu kisha akasema.

"Fahad nini hasa sababu ya kunieleza hayo yote?"Mathew aliuliza.

"Mathew, nimekueleza historia yangu na familia yangu kwa kusudi maalum.Ninataka uwaokoe Carmelita na mwanangu wasiuawe," alisema Fahad.Mathew akatoa kicheko.

"Kwanini unacheka,Mathew? Mambo niliyokueleza ni ya kijinga?" Fahad aliuliza kwa hisia.

"Si mambo ya kijinga, Fahad.Kwanza kabisa, ninakushukuru kwa kunieleza historia yako.Ninakupongeza pia kwa kuchagua kutokuunga mkono ugaidi.Nakupongeza pia kwa jitihada za kuhakikisha mpenzi

wako Carmelita na mwanao wanakuwa salama.Hata hivyo, umekosea kuja kwangu.Mimi si mtu sahihi kwa mpango huo.Labda nitakachokusaidia, ni kufikisha taarifa hizi kwa vyombo husika," alisema Mathew.

"Mathew Mulumbi, sijakosea kuja kwako.Ningeweza kuonana na mamlaka za hapa na kuwaomba wanisaidie katika mpango wangu huo.Lakini nimeamua kuja kwako kwa sababu wewe ndiye hasa ninayekuhitaji.Ni mtu sahihi kabisa," alisema Fahad na kunyamaza akimtazama Mathew.

"Fahad vipo vyombo ambavyo vinashughulika na suala kama hilo lako.Nitakakusaidia kulifikisha suala

lako sehemu linapotakikana ili wakusaidie," alisema Mathew.

"Sikiliza,Mathew, nafahamu kitu ninachokuomba ukifanye ni kikubwa.Mimi pia nimejiandaa kwa malipo makubwa," alisema Fahad..

"Fahad sihitaji fedha.Lengo langu ni kukusaidia kama binadamu mwenzangu.Mwenyezi Mungu amenijaalia, ninaendesha miradi kadhaa hapa nchini inanitosha kabisa kusukuma gurudumu la maisha yangu.Fahad, tusifanye jambo hili likatuchukulia muda mrefu sana mimi niko tayari kulifikisha suala lako sehemu ambako linaweza kushughulikiwa kwa ukamilifu mkubwa," Mathew alisema.

“Mathew Mulumbi.Ninaposema kuwa nimejiandaa kwa malipo mazuri simaanishi fedha.Ninafahamu unazo za kutosha,” alisema Fahad.Akanyamaza.

“Kitu gani unataka kunilipa?”Mathew aliuliza.

“Ninazo taarifa muhimu sana ambazo mtu pekee ninayeweza kumueleza ni wewe mkurugenzi wa Shirika la Ujasusi Tanzania,” alisema Fahad.Mathew akakaa vizuri akimtupia jicho makini Fahad.

“Taarifa gani unazo, Fahad?”Mathew aliuliza .

“Ninazo siri za mipango ya mataifa makubwa dhidi ya Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla.” Alisema Fahad

“Ninakusikiliza nieleze tafadhali.Nitapima kama zina uzito kisha nitaangalia nikusaidiaje,” alisema Mathew. Fahad alitoa sigara nyingine, akaiwasha.Akavuta na kutolea moshi puani kwa wingi.

“Taarifa hiyo imegawanyika katika sehemu mbili kama si tatu.Nitakueleza kwa awamu pia.Nitaanza kwa kukupa taarifa mbili muhimu,” alisema Fahad na kuvuta tena sigara yake kwa mkupuo.

“Kwanza kuna mpango wa kumuua Rais wa Tanzania,” alisema Fahad na kunyamaza.Sura ya Mathew ilibadilika

“Mpango wa kumuua Rais wa Tanzania?”Mathew aliuliza kwa hamaki.

“Ndiyo.Kuna mpango wa kumuua Rais wenu!”

“Nani wanataka kumuua.Na kwa nini?”Mathew alizidi kutaka kujua undani wa mambo.

“Iko hivi, Tanzania imenunua ndege mpya kutoka China aina ya COMAC C939 ambayo inategemea kuwasili nchini hivi karibuni.Ndege hiyo ndiyo imepangwa kutumiwa katika kumuua Rais wenu,”alisema Fahad.

“Naomba unifafanulie hapo tafadhali.Wanataka kumuua vipi? Kuna bomu katika hiyo ndege au kuna nini?” Mathew aliuliza.

“Nisikilize vizuri Mathew,ni ukweli usiopingika kuwa Rais wa Tanzania Jenerali mstaafu Pius Mawingu hapendwi na nchi kubwa tajiri ambazo kwa miaka mingi zimekuwa zikichuma

utajiri kutoka katika nchi za Afrika.Tangu ameingia madarakani,amekata mirija yote ya kinyonyaji.Mikataba yote ya kinyonyaji ambayo Tanzania ilikuwa imeingia na mabeberu, ameifumua na mingine kuitupilia mbali.Jambo hili halijawapendeza hawa wakubwa waliokuwa wakinufaika kwa kiasi kikubwa na rasilimali kutoka Tanzania.Alichokifanya Jenerali Pius kimeanza kuigwa pia na mataifa mengine ya Afrika.Hii imeongeza hofu kwa mataifa haya makubwa ya kutokuendelea kufaidika na rasilimali za Afrika.Jenerali Pius ameonekana rais mwenye ushawishi mkubwa sana barani Afrika.Wanahofia kama asipodhibitiwa haraka, anaweza

akawa na athari kwao hivyo njia pekee ni kumuua" Fahad alisema na kunyamaza kwa nukta chache.

"Sababu ya pili ya kutaka kumuua Jenerali Pius, ni vita ya kibiashara baina ya mataifa makubwa duniani.Kuungana kwa makampuni ya kutengeneza ndege ya COMAC China na UAC ya Urusi inatajwa kuwa ni mkakati wa kuua makampuni makubwa ya ndege ya Marekani na Ulaya.Ndege zinazotengenezwa China zina ubora mkubwa zaidi,hata bei yake pia ni nafuu ukilinganisha na bei za ndege katika mataifa ya Amerika na Ulaya.Kama nilivyoeleza awali kwamba, kwa sasa Tanzania inaonekana kama jicho la Afrika kisiasa, na kiuchumi pia.Kila

inachokifanya kinatazamwa na mataifa mengi ya bara la Afrika hivyo kitendo chake cha kununua ndege kutoka China, ni ishara ya wazi kuwa mataifa mengine ya Afrika yangebadilika na kuanza kununua ndege kutoka China.Mtu kama huyu ambaye anahatarisha makampuni makubwa ya kutengeneza ndege ya nchi tajiri yaporomoke hawezi kupendwa na mataifa hayo.Naamini umeanza kunielewa Mathew Mulumbi," alisema Fahad.

"Ninakuelewa, Fahad.Endelea!" Mathew alisema.

"Walitumwa majasusi nchini China katika kampuni iliyotengeneza ndege hiyo.Kazi waliyotumwa kuifanya, ni kuweka vifaa fulani viwili ndani ya

ndege ambavyo ndani yake kuna hewa ya sumu.Vifaa hivyo vimewekwa karibu na mlango wa kuingilia ndani ya ndege.Vinaonekana kama karatasi ya urembo yenye maandishi lakini nyuma ya hiyo karatasi ndipo vilipo vifaa hivyo ambavyo vimeunganishwa na satelaiti," Fahad akanyamaza kidogo.

"Imezoeleka kila ndege mpya inaponunuliwa na kuwasili nchini Tanzania, Rais huwa wa kwanza kuingia ndani ya ndege hiyo.kisha hufuata viongozi wengine.Kifaa hicho kuwekwa katika mlango wa kuingilia ni kwa sababu maalum.Imepangwa kwamba mara tu, Rais atakapoanza kupanda ngazi za ndege kuelekea ndani ya ndege,kwa kutumia satelaiti watakiwasha kifaa

hicho.Hewa ya sumu itatoka na Rais anapofika katika mlango, hutumia sekunde kadhaa kugeuka na kupunga mikono, hivyo ataivutia hapo hewa ya sumu.Baada ya kuvuta hewa hiyo ya sumu, kitawashwa kifaa kingine cha kutoa hewa ambayo itaimaliza ile hewa ya sumu ndani ya ndege.Rais akiivuta hewa hiyo ya sumu hatamaliza saa mbili atafariki dunia.Kazi yako Mathew ni kuhakikisha mpango huo haufanikiwi.” alisema Fahad aliyemwacha Mathew katika kibarua kizito cha mawazo juu ya uhai wa rais wake.

“Taarifa hizi umezitoa kutoka vyanzo vyenye uhakika?”Mathew aliuliza.

“Ndiyo,Mathew.Ni taarifa ambayo vyanzo vyake ni vya kuaminika,” akajibu Fahad na ukimya ukatawala kwa nukta chache.

“Mathew, naamini umenielewa,”Fahad alisisitiza.

“Nimekuelewa, Fahad, lakini kwa nini tusizijulishe mamlaka husika jambo hili zilifanyie kazi?”Mathew aliongeza.

“Hapana.Jambo hili halipaswi kujulikana.Ninataka jambo hili lishughulikiwe kwa namna nyingine ambayo haitawafanya mabeberu wajue kuwa mpango wao umegunduliwa,” Fahad alisema.

“Namna gani nyingine ya kuweza kulishughulikia suala hili bila ya

kuzitaarifu mamlaka husika?”Mathew aliuliza.

“Ni kwa kuipoteza ndege!”

“Kuipoteza ndege?” Mathew aliuliza kwa mshtuko.

“Ndiyo.Tunatakiwa kuipoteza ndege hiyo kisha kuipeleka sehemu ambako tutaviondoa vifaa hivyo na baadaye tutairudisha ndege nyumbani,” alisema Fahad.

“Sijakuelewa, Fahad, unataka tuipoteze vipi ndege hiyo?” Mathew aliuliza kidadisi.

“Umeshasikia ndege kadhaa zimewahi kupotea angani na hazijawahi kuonekana mpaka leo? Aliuliza Fahad

“Ndiyo” Mathew alijibu

“Basi hii pia tutaipoteza kama hizo lakini hii haitapotea moja kwa moja bali itapatikana baada ya muda.Ndege hiyo ina mfumo wa kuiwezesha kutokuonekana katika mfumo wowote wa rada hata zile za kijeshi.Tutakachokifanya ni kuuzima mfumo huo kisha tutaipeleka mafichoni.Ili kuuzima mfumo wa rada,lazima kuiteka kwanza hiyo ndege,” Fahad alisema.

“Kuiteka ndege?” Mathew aliuliza.

“Ndiyo ndege hiyo inatakiwa kutekwa kwanza.Mathew, hapa tunazungumzia maisha ya rais wenu hivyo inabidi kila njia itumike kuhakikisha anakuwa salama.Ni bora kuiteka ndege hiyo ikiwa na watu

wachache ndani yake kuliko kumpoteza kiongozi huyu shupavu.Tukio hilo nataka ulifanye wewe Mathew na si mtu mwingine.Tafuta namna ya kuweza kuingia katika hiyo ndege na uiteke. Hata kama itakulazimu kuua we' fanya hivyo alimradi zoezi hilo likamilike.Kumbuka unafanya hivyo ili kumlinda Rais wako asiuawe" alisema Fahad na ukimya ukapita Mathew akawaza halafu akauliza.

"Baada ya kuiteka ndege na kuiondoa katika mfumo wa rada, ni wapi itapelekwa?"

"Hapo ndipo ninaingia katika jambo la pili" alijibu Fahad na kunyamaza kidogo .

“Hivi sasa nchini Libya kuna makundi kadhaa yanayopigana ili kutwaa uongozi wa nchi hiyo.Kuna serikali ambayo inajiita ya watu wa Libya ambayo inatambuliwa na umoja wa mataifa.Makao yake makuu ni Tripoli.Yapo pia makundi mengine yanayopigana na serikali hiyo ambayo yanaungwa mkono na nchi mbalimbali kubwa likiwamo kundi la Ansar al Sharia ambalo ni kundi linalotishia kwa kiasi kikubwa sana serikali hii ya watu wa Libya.Mpango wowote wa kuliondoa kundi hilo lazima utapokelewa kwa mikono miwili na serikali ya Libya.Ninataka tushirikiane na serikali ya watu wa Libya kuliondoa kundi hilo na kumuua Abdulkhareem Fadil Ghedi

kiongozi wa kundi hilo.Mathew ninataka uende Libya uzungumze na rais wa serikali ya watu wa Libya, umfahamishe kuhusu mpango wetu wa kumuondoa Abdulkhareem Fadil Ghedi na kundi lake la Ansar al Sharia,"alisema Fahad.

"Nitampataje Rais huyo wa Libya?.Sina mtu wa karibu anayeweza kuniunganisha na rais huyo wa Libya" alisema Mathew.

"Mathew, nimekuja kwako kwa kuwa ninafahamu wewe ni mtu wa kazi ambaye ukitaka kuingia sehemu yoyote ile huwezi kushindwa.Naamini utaweza kuingia katika Ikulu ya Tripoli kuzungumza na rais wa Libya.Tafuta namna," alisema Fahad kwa msisitizo.

“Fahad unanibebesha mzigo mzito sana huu,”alisema Mathew aliyeonekana kuzongwa na mawazo.

“Ni mzito lakini unaweza kuubeba.” alisema Fahad.Mathew akatafakari kwa muda halafu akasema.

“Kama nikifanikiwa kuonana na mtawala wa Libya na akakubali mpango huu ni namna gani tutaweza kumuondoa Abdulkhareem?”Mathew aliuliza.

“Tutashirikiana na vikosi vya serikali.Mimi kwa kuwa tayari nina watu wangu ndani ya kundi la Ansar al Sharia, ni rahisi sana kupata taarifa ambazo tutazitumia kulisambaratisha kundi hilo.Malipo ya kumuondoa Abdulkhareem na kundi lake ni sisi kuruhusiwa kuipeleka ndege yetu Libya

baada ya kuiteka na hapo ndipo tutakapoweza kukiondoa kifaa hicho kilichowekwa kwa ajili ya kumuua rais.”Alisema Fahad

“Umesema kifaa hicho kimeunganishwa na satelaiti, je, hawa jamaa hawataweza kufuatilia na kujua mahala ndege hiyo ilipo?”Mathew aliuliza.

“Tukifanikiwa kuzima mfumo wa rada tutakuwa tumezima mfumo wote wa mawasiliano wa ndege hiyo hivyo hawataweza kujua mahala ilipo.”

“Kama ni hivyo, basi kuna ulazima gani wa kwenda Libya? Tunaweza tukazima mfumo wa rada na kisha ndege ikatua Dar es Salaam”

“Hapana.Haiwezekani.Lazima tuipeleke Libya.Nina sababu nyingine kubwa,” alisema Fahad na kunyamaza kidogo.

“Huo mpango wa kumuua Rais Pius, ni mpango wa kwanza lakini kuna mpango wa pili,” alisema Fahad na kunyamaza kidogo akachomoa sigara nyingine akawasha akavuta.

“Ansar al Sharia wamepanga kufanya shambulio hapa Tanzania,” alisema Fahad.

“Wanataka kufanya shambulio la kigaidi hapa Tanzania?” Mathew aliuliza.

“Ndiyo.Kila mwaka barani Afrika hufanyika mkutano unaitwa *Afrika asili yangu* ambao huwakutanisha watu

wenye asili ya bara la Afrika wanaoishi nchi za Ulaya na Amerika.Kwa mwaka wa pili mfululizo Tanzania wamekuwa waandaaji wa mkutano huo na utafanyikia jijini Arusha katika ukumbi wa KICC.Magaidi wamepanga kuuteka ukumbi huo wa KICC wakati mkutano ukiendelea na kuwashikilia mateka wajumbe wa mkutano huo ambao wengi watakuwa ni wageni”

“Nini hasa sababu za kutaka kufanya shambulio hilo la kigaidi?” Mathew aliuliza.

“Sababu kuu ni kuitaka serikali ya Tanzania imuachie Mahmoud Fadil Ghedi,”alijibu Fahad.

“Serikali ya Tanzania haimshikilii Mahmoud Fadil Ghedi bali anashikiliwa

na Mahakama ya Afrika ambayo Tanzania ni mwanachama na kamwe haiwezi kuingilia mahakama hiyo,”alisema Mathew.

“Wanalifahamu hilo na wanajua haliwezekani kutekelezeka, lakini kuna sababu nyingine kubwa nyuma ya shambulio hilo,” alisema Fahad.

“Sababu gani hiyo? Aliuliza Mathew.

“Bado sijaipata sababu hiyo kubwa lakini nitaipata na kukueleza,ila taarifa niliyoipata ni kuwa kuna mateka ambao watachukuliwa katika shambulio hilo la Arusha na kupelekwa Libya ndiyo maana nikasisitiza kuwa baada ya kuiteka ndege lazima tuipeleke Libya.” alisema Fahad.

“Fahad,hatuwezi kukubali shambulio hilo likafanyika.Lazima kutoa taarifa kwa vyombo vinavyohusika na kupambana na ugaidi ili waweze kujiandaa kuwazuia magaidi hao kutekeleza mashambulio yao hapa Tanzania,” alisema Mathew.

“Mathew, hatuwezi kuzuia shambulio hilo lazima lifanyike.Kama nilivyokueleza kwamba kuna jambo kubwa nyuma ya shambulio hilo ambalo bado nasubiri taarifa zake kutoka kwa vyanzo vyangu.Tukilizuia shambulio hilo kutokea tunaweza tukashindwa kupata kile ambacho magaidi wamekilenga.Mathew, ninaomba kwa namna yoyote ile shambulio hilo lisikwamishwe.Tuliache lifanyike ili

tujue kile kilichoko nyuma yake," alisema Fahad.

"Fahad, wewe unafahamu ni namna gani magaidi wanavyotekeleza mashambulio yao.Watu wengi wasio na hatia wanaweza kupoteza maisha,"alisema Mathew kwa masikitiko.

"Ni kweli,Mathew, watu lazima watapoteza maisha lakini kile ambacho kitapatikana kutokana na shambulio hilo ni kikubwa sana kwa nchi yenu."

"Unasema ni kitu kikubwa kwa nini hutaki kuweka wazi kitu chenyewe? Mathew aliuliza kidadisi na kwa msisitizo.

"Kama nilivyokueleza,Mathew, kwamba bado hata mimi sina taarifa

kamili. Ndiyo maana nikashauri kwamba tusifanye chochote ambacho kinaweza kusababisha shambulio hilo lisifanyike.Hata wenyewe wanafanya mambo kwa siri ili kuepuka mipango yao kuvuja. Ninaendelea kusubiri taarifa kutoka kwa vyanzo vyangu," alisema Fahad na Mathew akainamisha kichwa chini kutafakari kwa kina.

"Mathew,ninafahamu huwapendi magaidi na hupendi kusikia wamefanya shambulio Tanzania lakini katika hili, tuwaache wafanye na ninakuhakikishia kuna mengi makubwa yatapatikana," alisema Fahad.

"Nataka sana kukubaliana na wazo lako, lakini inaniwia ugumu kukubali magaidi wakatekeleza shambulio lao

hapa Tanzania huku tukiwatazama”alisema Mathew.

“Mathew, niamini nikwambiavyo.Kuna mengi makubwa ambayo yatapatikana kutokana na shambulio hilo,” alisema Fahad aliyeonekana kushikilia msimamo wake. Ukimya ukatawala.

“Mathew, hii yote ni mipango ya nchi kubwa dhidi ya Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla.Nadhani sasa unakubaliana nami kuwa nimeyafikisha sehemu sahihi kabisa,” alisema Fahad.

“Ahsante sana Fahad kwa haya yote uliyonieleza,” alisema Mathew.

“Mathew, nimekueleza haya yote kama malipo kwa kazi ya kuhakikisha Carmelita na Lebron wanakuwa

salama.Wao ni kila kitu kwangu na niko tayari kufanya chochote kwa ajili yao.Nataka kusikia jibu lako.Je, uko tayari kunisaidia kuwaokoa Carmelita na Lebron wasiuawe?" Fahad alihitimisha.

"Nimekuelewa Fahad na ninakuahidi kuwa mpenzi wako Carmelita na mwanao Lebron watakuwa salama,"Mathew alijibu.

"Nashukuru sana Mathew.Ni hicho tu ambacho nilitaka kukisikia kutoka kwako.Kwa leo mazungumzo yetu yanaishia hapa.Ninachokutaka kuanzia sasa,anza kushughulikia haya niliyokueleza." alisema Fahad na kumpa Mathew namba yake ya simu.

"Hii ni namba ya simu ambayo tutaitumia kuwasiliana.Tafuta simu

nyingine ambayo watu hawaijui kwa ajili ya mawasiliano kwani jambo hili ni siri kubwa na watu hawapaswi walifahamu” alisema Fahad na kuinuka.

“Imekuwa siku nzuri sana kuzungumza nawe Mathew Mulumbi.Tuendelee kuwasiliana,” alisema Fahad akaagana na Mathew akatoka mle ndani.Baada ya muda mfupi wakaingia jamaa wanne wakamvisha Mathew mfuko kichwani wakamtoa nje wakamuingiza garini wakaondoka naye bila Mathew kujua ni mahala gani alikuwa amepelekwa.

****

Mlango wa gari ulifunguliwa Mathew akasukumwa nje na gari likageuzwa haraka likaondoka.Mathew alijizoa zoa pale chini akatoa ule mfuko aliovishwa kichwani,alikuwa mbele ya nyumba yake.Hakuliona lile gari tayari lilikwisha potea.Aliwatazama walinzi wake wa getini walikuwa wamelala fofofo.

“Wale jamaa waliwalaza kwanza usingizi walinzi wangu ndipo wakaweza kuingia ndani.Ni nani wale jamaa?Nawasifu kwani nwanaifahamu vyema kazi yao.Hata hivyo upo ulazima wa kuongeza ulinzi hapa nyumbani.Sipaswi kujiamini sana.Kama wale jamaa wangekuwa na lengo ovu la kutaka kuniua hivi sasa tayari ningekuwa

mfu” aliwaza Mathew na kuingia ndani. Akaenda kuchukua kopo Fulani dogo. Akarejea kwa walinzi na kuwapulizia puani,baada ya muda mfupi wale walinzi wakaanza kupiga chafya.Mathew hakuwauliza chochote akarejea ndani.Alifungua friji akachukua chupa ya maji ya kunywa akanywa yote halafu akazama katika tafakari

“Mambo aliyonieleza Fahad ni mazito.Hizi nchi kubwa haziwapendi sana marais wa nchi za bara la Afrika ambao wanasimama kidete kusimamia rasilimali za nchi zao.Nitafanya kila linalowezekana kuhakikisha ninaizima mipango yote ya mabeberu.” aliendelea kuwaza Mathew.

3

BAADA YA MIEZI MIWILI
DAR ES SALAAM

Rais wa Tanzania Jenerali mstaafu Pius Mawingu aliingia katika chumba cha mikutano ikulu jijini Dar es salaam.Wajumbe wote walisimama Kumpa heshima mheshimiwa rais ambaye aliwataka waketi.

“Ahsanteni sana kwa kufika.Kikao chetu ni kifupi.Nimewaita hapa kwa dharura ili tupeane taarifa kuhusu hali ya usalama wa nchi kabla na wakati wa mkutano muhimu kabisa wa *Afrika Asili Yangu*.Mheshimiwa Waziri Mkuu na baadhi ya mawaziri walifanya ziara leo jijini Arusha kukagua maandalizi ya mkutano huo yanavyokwenda,watatupa taarifa ya kile walichokibaini katika ziara hiyo.Karibu Ndugu Waziri Mkuu,” alisema Rais Pius na Waziri Mkuu akawaeleza kile walichokipata katika ziara yao ya Arusha na kuwahakikishia kwamba kwa asilimia zaidi ya tisini maandalizi yamekamilika.

“Tunashukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa taarifa hiyo.Ninataka

kusikia pia upande wa usalama tumejiandaa vipi? Tunawategemea marais saba kutoka nchi mbalimbali za Afrika kuhudhuria mkutano huo. Vilevile kutakuwepo na wawakilishi wa marais kutoka nchi mbali mbali.Ugeni huu ni mkubwa.Tuna kila sababu ya kuhakikisha ulinzi unakuwepo wa kutosha kabla na wakati wa mkutano.Kwa kuwa wakuu wote wa vyombo vya ulinzi mko hapa, nataka kila mmoja anieleze katika idara yake amejipanga vipi kuhakikisha kwamba usalama unakuwa wa kutosha," alisema Rais Pius.

Wa kwanza kuwasilisha taarifa ya kiusalama alikuwa mkuu wa majeshi ya Tanzania, ambaye alimuhakikishia

mheshimiwa rais kwamba ulinzi umeimarishwa katika mipaka yote ya nchi na hakuna hofu ya uvamizi wowote kutoka nje.Mkuu wa Jeshi la Polisi naye akasimama na kuwasilisha taarifa yake mbele ya kikao kile. Naye alimuhakikishia mheshimiwa rais namna ulinzi ulivyoimarishwa katika viwanja vya ndege na katika sehemu zote ambazo wageni walitegemea kufikia. Sehemu watakazotembelea na katika sehemu zote itakamofanyikia mikutano midogo midogo ya kibiashara baina ya wafanya biashara.

Baada ya kupokea taarifa kutoka kwa wakuu wa vyombo mbalimbali vya usalama na namna walivyojipanga katika kuhakikisha kwamba mkutano wa *Afrika*

Asili Yangu unafanyika kwa amani bila tatizo lolote,mheshimiwa Rais akafunga kikao cha dharura na kwenda kuendelea na majukumu yake mengine.Aliwakumbusha wajumbe kuhusu kuwasili kwa ndege mpya ya Tanzania siku inayofuata ikitokea China ilikonunuliwa.Aliwataka wote kufika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere kuipokea ndege hiyo.

DAR ES SALAAM.
UWANJA WA NDEGE WA
KIMATAIFA
WA JULIUS NYERERE

Wakazi wa jiji la Dar es Salaam walijitokeza kwa wingi sana katika

uwanja wa ndege wa Julius Nyerere katika mapokezi ya ndege mpya ambayo serikali ya Tanzania iliinunua kutoka nchini China.Ndege hiyo ya kisasa aina ya C939 yenye uwezo wa kubeba abiria 390 ilitengenezwa nchini China kwa ushirikiano wa makampuni mawili ya Commercial Aircraft Corp ya China (COMAC) na United Aircraft Corp ya Urusi.

Katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere,wageni mbalimbali waliendelea kuwasili huku vikundi vya burudani vikiendelea kutumbuiza na kuwaburudisha watu waliofika uwanjani hapo kuipokea ndege mpya.

Saa kumi alasiri Rais wa Tanzania, Jenerali Mstaafu Pius Mawingu aliwasili uwanjani na kupokewa kwa shangwe kubwa kutoka kwa wananchi waliokuwa wamefurika kuipokea ndege mpya.Baada ya rais kufika, ratiba ilianza kwa wimbo wa taifa kuimbwa ,zikafuata dua,kisha salamu za mkoa na ratiba nyingine ikaendelea.

Wakati shughuli ikiendelea, Mkurugenzi wa Shirika la Ndege la Tanzania alifuatwa na kuelezwa kitu.Akainuka haraka na kuelekea ofisini kwake.Baada ya dakika tano, akarejea kwa haraka na kumfuata rais.Akamnong'oneza jambo,rais akageuka na kuwaelekeza jambo makamu wa rais na waziri mkuu. Wote

wakainuka, akawafanyia ishara viongozi wakuu wote wa vyombo vya ulinzi na usalama wainuke.Wote walielekea katika ofisi ya Mkurugenzi wa Shirika la Ndege.

“Kitu gani kimetokea?” Rais aliuliza baada ya kuingia katika ofisi ya Mkurugenzi wa Shirika la Ndege.

“Mheshimiwa Rais, tukiwa pale jukwaani niliitwa na kupewa taarifa na waongoza ndege kwamba ndege yetu ambayo tunaitegemea kuipokea jioni hii imepoteza mawasiliano ghafla.”

“Nini?” Rais alimaka.

“Sijakuelewa Dr Njau.Unasema nini kimetokea?” Aliuliza tena Rais Pius ili kujiridhisha na kile alichokisia hapo awali.

“Mheshimiwa Rais, ndege yetu tuliyokuwa tunaisubiri, imepoteza mawasiliano ghafla na wataalamu wanajitahidi kuitafuta,”alisema Dr Njau huku akitweta.

“Mawasiliano yamepoteaje?”Rais aliuliza.

“Kwa mujibu wa waongoza ndege,wanadai ndege ilikaribia kuingia katika anga la Tanzania,lakini ghafla mawasiliano yakakatika na mpaka sasa bado hawajafanikiwa kurejesha mawasiliano.Bado wangali jitihadani kujua ni nini kimetokea!”

“Dr Njau,ni nini unakimaanisha hapa? Ndege yetu imeanguka?”Aliuliza kwa ukali sana Jenerali Pius.

“Mheshimiwa Rais, bado mapema mno kusema kwamba ndege yetu imeanguka.Waongoza ndege wetu wanajitahidi kuitafuta na kujua nini sababu ya mawasiliano kupotea ghafla,” alijibu Dr. Njau ambaye sauti yake ilishikwa na kitetemeshi.

“Dr Njau, bado tunahitaji kupata picha kamili ya nini hasa kimetokea? Hebu tulia na utueleweshe kilichotokea na ni kipi kinaweza kuwa sababu ya mawasiliano kukatika ghafla?” Alisema Waziri Mkuu.Dr Njau akaenda katika ramani kubwa ya dunia iliyokuwa ukutani na kuanza kutoa maelezo ya kina namna mawasiliano yalivyokatika.Rais Pius hakuridhika na maelezo yale

akataka waende katika sehemu ya kuongozea ndege akapate maelezo zaidi.

Wananchi waliendelea na shamra shamra za kuisubiri ndege mpya,vikundi mbalimbali vya burudani viliendelea kuburudisha huku jua likiendelea kuchwea.Kuondoka kwa viongozi wakuu pale mezani bila maelezo yoyote na kuchukua muda mrefu kurejea kulianza kuwapa hofu wananchi waliokuwa wanaisubiri ndege mpya.

Jua taratibu lilianza kupotea bila viongozi kurejea na bila kuwepo na dalili zozote za ndege kuwasili japo waongozaji shughuli ile waliendelea kuwahakikishia wananchi kwamba ndege iko njiani waendelee kuvumilia.Taratibu kiza kilianza kuingia na nyuso za watu

waliokuwa pale uwanjani wakiisubiri ndege zilionyesha kuanza kupoteza matumaini na wale waliotoka mbali walianza kuondoka.Watu walijiuliza maswali mengi nini kimetokea lakini hakuna aliyekuwa na jibu.

Saa moja za jioni, rais na viongozi wengine wakarejea, waziri wa uchukuzi na mawasiliano akamkaribisha rais ili aweze kuzungumza jambo.

“Ndugu zangu wa Dar es Salaam mliojitokeza kwa wingi sana siku ya leo katika mapokezi ya ndege yetu mpya na Watanzania wote ambao mnafuatilia tukio hili katika vyombo vya habari. Tulitegemea kupokea ndege yetu saa kumi na mbili na dakika tano za jioni, lakini imekuwa tofauti na ninajua mna

hamu ya kujua nini kimetokea hadi muda huu ndege yetu haijatokea.Ndugu Watanzania, kwa masikitiko makubwa ninapenda kuchukua nafasi hii kuwajulisheni kwamba ndege yetu aina ya C939 ambayo tulitegemea kuipokea jioni ya leo imepoteza mawasiliano ikiwa angani!”

Sauti za watu wakishangaa na wengine wakilia zikasikika.

“Tusikilizane ndugu zangu!” alisema Rais Pius na kuwatuliza watu

“Najua taarifa hii imewastua na hamkuitegemea, lakini lazima niwaeleze ukweli kwamba ndege yetu ilipoteza mawasiliano na waongoza ndege wetu wakati ikikaribia kuingia katika anga la Tanzania. Mpaka sasa jitihada za

kuitafuta au kujua nini kimetokea hadi mawasiliano yakapotea, hazijafanikiwa.Tayari uchunguzi umeanza tukishirikiana na nchi nyingine jirani ili kujua ni nini kimetokea.Tutaendelea kuwajulisha kila taarifa tutakayoipata.Kwa sasa naomba turejee majumbani kwetu na tuwaombee wale wote waliomo katika ndege hiyo waweze kuwa salama," alisema rais na kumalizia hotuba yake fupi kisha akashuka jukwaani haraka haraka akiwa amezungukwa na ulinzi mkali.Akaingia katika gari lake, msafara wake ukaondoka akifuatiwa na viongozi wengine wakuu wote wakielekea Ikulu.

BAADA YA SIKU 1

ARUSHA

Ukumbi unamofanyika mkutano wa *Afrika Asili yangu* ,ulifurika watu waliokuwa wakisubiri ufunguzi rasmi wa mkutano huo.Saa moja za jioni mgeni rasmi ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliwasili ukumbini.Watu wote wakasimama kwa heshima yake hadi alipoketi.Ratiba ikaanza rasmi.Kama jinsi itifaki inavyotaka, watangulizi wawili walihutubia ikafuata zamu ya mheshimiwa Rais wa Tanzania kuufungua rasmi mkutano wa *Afrika Asili Yangu.*

“Ndugu Rais wa taasisi ya Afrika Asili Yangu na viongozi mbalimbali wa

kitaifa na kimataifa mliohudhuria itifaki ikizingatiwa,wageni waalikwa mabibi na mabwana.

Ninasimama mbele yenu kwa heshima kubwa kwa niaba ya Watanzania wote kuwakaribisha katika mkutano huu wa Afrika Asili Yangu unaofanyika kwa mara ya pili katika jiji hili la Arusha.Mwaka uliopita mkutano kama huu ulifanyika hapa hapa Arusha na kwa mara nyingine tena nchi ya Tanzania imechaguliwa kuwa mwenyeji wa mkutano huu mkubwa na muhimu kwa bara la Afrika.

Ninawashukuru kwa namna ya pekee kabisa viongozi mbali mbali waliokuja kuungana nasi kutoka mataifa tofauti na wengine waliotuma wawakilishi wao.

Ninawashukuru vilevile wageni wote kutoka Marekani,Karibean,Afrika na kwingineko kote duniani kwa kufika nchini kwetu.”

Hivyo ndivyo alivyoianza hotuba yake mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwakaribisha viongozi wa mataifa na wageni mbalimbali waliohudhuria mkutano huo mkubwa wa *Afrika Asili Yangu.*

Ilikuwa ni hotuba ndefu iliyosheheni mambo mengi kuhusiana na Tanzania na Afrika kwa ujumla.Baada ya ufunguzi ule,rais na viongozi wengine wa kitaifa wakaondoka kurejea Dar es Salaam ili kufuatilia kwa karibu utafutaji wa ndege iliyopotea.

IKULU - DAR ES SALAAM

Saa tatu za asubuhi Ikulu jijini Dar es Salaam, karibu viongozi wote wakuu wa kitaifa na wale wa vyombo vya ulinzi na usalama walikutana ili kupata taarifa ya awali ya utafutaji wa ndege iliyopotea ambayo Tanzania iliinunua kutoka China.Wakati wakiendelea kupokea taarifa hiyo,Rais akapigiwa simu na mkuu wa Mkoa wa Arusha aliyempa taarifa iliyomshtua kuwa, kulifanyika mashambulizi ya kigaidi jijini Arusha.Magaidi waliuteka ukumbi wa mikutano wa KICC na kuwashikilia mateka wajumbe zaidi ya mia tatu waliokuwamo ndani ya ukumbi huo kuhudhuria mkutano wa *Afrika Asili*

Yangu.Kama haitoshi,magaidi waliwateka pia wanafunzi zaidi ya sabini waliokuwa ziarani jijini Arusha kuhamasisha wasichana kusoma masomo ya sayansi.Miongoni mwa wanafunzi hao ni mtoto wa rais.

Ilikuwa taarifa iliyowashtua sana viongozi wale.Kikao kikalazimika kubadilika na kuanza kulishughulikia tukio la Arusha.Wakiendelea na kikao,mmoja wa wasaidizi wa rais akaingia na kumnong'oneza kitu.Rais akasimamisha kikao kwa muda na kusema.

"Nimepewa taarifa kwamba, katika laini ya simu kuna mtu anayedai ni kiongozi wa magaidi waliofanya shambulizo Arusha anahitaji

kuzungumza na mimi," alisema Jenerali Pius Mawingu na kuvuta pumzi ndefu.Chumba chote kikawa kimya. Watu wote walitaka kumsikia kiongozi huyo wa magaidi.Rais akabonyeza kitufe cha kupokelea simu iliyokuwa mbele yake.

"Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anaongea hapa!" Alisema Jenerali Mawingu.

"Habari yako mheshimiwa Rais!" Ilikuwa sauti nzito ya kiume kutoka upande wa pili akizungumza kwa lugha ya Kiingereza.

"Nazungumza na nani?" Rais Pius aliuliza.

"Mheshimiwa Rais,naamini tayari umepata taarifa za mashambulio

yaliyotokea asubuhi hii jijini Arusha. Mimi ndiye kiongozi wa kikundi kilichofanya mashambulio yote ya leo.Mimi na vijana wangu tunawashikilia watu zaidi ya mia tatu katika ukumbi wa mikutano wa KICC na vilevile tunao wasichana sabini ambao tumewateka. Miongoni mwao yupo mwanao”alisema huyo jamaa. Rais akamkatisha.

“Nini kusudi la kufanya haya mashambulio?” Aliuliza kwa ukali Jenerali Pius.

“Tuna ombi moja tu,Mheshimiwa Rais na liko ndani ya uwezo wako.Kama ukilitekeleza, basi wasichana na mateka wote katika ukumbi wa KICC wataachiwa huru.”

“Mnataka nini?” Aliuliza rais kwa ukali.

“Tunataka Mahmoud Fadil Ghedi kiongozi wa kundi la Ansar Al Sharia la Somalia ambaye anashikiliwa katika mahakama ya Afrika iliyopo Arusha Tanzania,aachiwe huru.Tunatoa muda wa saa moja tu, toka sasa tuwe tumempata mtu huyo na tutawaachia wasichana wote pamoja na wajumbe tunaowashikilia katika ukumbi wa KICC.” Jenerali Pius akavuta pumzi ndefu kisha akasema.

“Naomba unisikilize kwa makini sana!”

“Nakusikiliza,Mheshimiwa Rais!”

“Kwanza, futa kabisa wazo lako kwamba tutatekeleza maagizo yenu.

Tanzania hata siku moja haiwezi kufanya makubaliano na magaidi.Kitu cha pili, ni kwamba huyo kiongozi wenu Mahmoud Fadil Ghedi mnayemtaka hataachiwa huru.Jambo la tatu na la mwisho, ninalotaka ulifahamu ni kwamba serikali ya Tanzania itawakomboa mateka wote mnaowashikilia ikiwa ni pamoja na kuwakamata au kuwaua wewe na wenzako wote!”Alisema kwa ukali Jenerali Pius.

“Mheshimiwa Rais,ahsante kwa kuweka wazi msimamo wako. Lakini tayari nimekwisha kutaarifu tunachohitaji na nimekupa muda wa saa moja toka sasa.Baada ya muda huo kupita, tutaua watoto wawili na katika saa ya pili tutaua watoto

wanne.Tutaendelea kuua watoto hadi pale utakapoamua kutekeleza maagizo yetu.Mheshimiwa Rais,muda unaanza kuhesabiwa sasa!" Alihitimisha mkuu wa magaidi kisha simu ikakatwa.Rais Pius akagonga meza kwa hasira.

"Nyote mmesikia alichokisema huyu shetani.Nataka hatua zianze kuchukuliwa.IGP utaelekea Arusha mara moja kuongoza zoezi la kuhakikisha ukumbi unakombolewa.Idara nyingine zote mtawasiliana na IGP ambaye ndiye ataongoza misheni ya kupambana na magaidi hawa," alisema Rais Pius kisha akakaa kimya kwa nukta chache.

"IGP, this a Capture or Kill Mission! Hakuna huruma kwa yeyote aliyeshiriki katika upuuzi huu mkubwa!"Alisema

rais na mkuu wa jeshi la polisi akasimama akapiga saluti ishara ya kupokea maelekezo,halafu akatoka haraka katika ukumbi ule tayari kwa safari ya kuelekea Arusha.

“Mheshimiwa Rais,kuna jambo nataka kulishauri,”alisema waziri mkuu.

“Endelea Mheshimiwa Waziri Mkuu,” alisema Rais Pius.

“Magaidi wametoa muda wa saa moja kabla ya kuanza kuua watoto wetu.Hawa jamaa hawatanii Mheshimiwa Rais.Tunatakiwa kulitazama vizuri suala hili na kama ikiwezekana, tuzungumze vizuri na mtu huyu na kujaribu kufanya makubaliano ambayo yanaweza kututoa katika janga hili.Maisha ya wat…” alikatishwa

maongezi yake na Rais Pius kabla ya kuendelea.

“Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba tuelewane kwamba tuko katika janga zito.Hivyo lazima tuwe makini sana katika kila maamuzi tunayoyachukua.Tunachotakiwa kufanya sasa ni kutafuta namna ya kuhakikisha maisha ya Watanzania yanakuwa salama na hakuna tena tishio lolote la mashambulio.Vilevile kuhakikisha tunawakomboa mateka wote.Msimamo ninaouweka hapa ni kwamba hatutajadiliana chochote na magaidi.Wametushambulia, wamewachukua mateka watoto wetu na wanaendelea kuwashikilia wajumbe zaidi ya mia tatu,kwa hiyo watu kama hawa si

wa kujadiliana nao hata kidogo.Ninaomba katika kikao hiki kusiwe na mazungumzo yoyote yanayohusiana na kujadiliana na magaidi.Lazima tuwaonyeshe magaidi hawa kwamba Tanzania si mahala ambako unaweza ukafanya chochote unachokitaka na ukabaki salama.Ndugu zangu, nataka wote tuzungumze lugha moja mkumbuke pia pamoja na janga hili la kigaidi, pia ndege yetu imepotea hivyo mambo ni magumu sana kwetu na tusitafute urahisi!" Alisema Jeneral Pius kwa sauti ya amri na hakuna aliyejibu chochote.Kikao kikaendelea.

BAADA YA SAA MOJA

Saa moja aliyoitoa kiongozi wa magaidi waliofanya mashambulio jijini Arusha ilimalizika bila ya rais kutekeleza kile walichomtaka akifanye.

Ikulu jijini Dar es Salaam,bado kikao kizito kiliendelea.Wakati kikao kikiendelea, mmoja wa wasaidizi wa rais akaingia na kumnong'oneza jambo.Jeneral Pius akainamisha kichwa akafikiri kidogo halafu akasema.

"Ndugu wajumbe, nimetaarifiwa kwamba kuna video imerushwa katika mtandao na magaidi.Ngoja tuitazame," alisema rais na wajumbe wote wakaigeukia runinga kubwa iliyokuwa ukutani.Mlinzi wa rais akaiwasha na video ikaanza kucheza.

Mtu mmoja aliyejifunika sura yake alijitokeza na kusema.

“Ndugu Watanzania,ninayezungumza nanyi ni kiongozi wa kikundi ambacho siku ya leo kimefanya shambulio jijini Arusha.Tumewachukua mateka wasichana sabini miongoni mwao ni mtoto wa rais wenu.Wote wako salama.Tunawashikilia vilevile wajumbe zaidi ya mia tatu katika ukumbi wa mikutano ya kimataifa wa KICC.Tulimpa rais wenu maelekezo ambayo alipaswa kuyatekeleza lakini amepuuza.Nilimuonya kama akishindwa kutekeleza maagizo yangu, tutaua wanafunzi wawili.Kwa kuwa ameonesha kiburi,tunataka kumuonyesha kwamba

sisi hatuna mzaha.Tukitoa maelekezo lazima yatekelezweTunaua watoto wawili sasa hivi na tutaendelea hivyo kila baada ya saa moja." Akafanya ishara na wasichana wawili waliokuwa wamefungwa vitambaa machoni wakiwa na sare zao za shule wakaletwa na kupigishwa magoti mbele yake. Akawafungua vitambaa.

"Binti unaitwa nani?" Alimwuliza mmoja wao.

"Naitwa Lucy Nswami!"

"Lucy una miaka mingapi?

"Nina miaka kumi na tano"

"Na wewe unaitwa nani?" Alimuuliza na yule mwenzake

"Naitwa Husna Ayoub."

"Husna una miaka mingapi?

“Nina miaka kumi na sita.Tafadhali naomba msituue.Ongeeni na baba yangu ni tajiri atawapa kiasi chochote cha pesa mnachohitaji.Tafadhali naomba msituue!” Yule jamaa akamtazama na kusema.

“Husna angalia ile kamera na umuombe rais wako awaokoe kwa kutekeleza maagizo yetu!”

Huku uso wake umefunikwa na machozi Husna akaiangalia kamera na kusema.

“Mheshimiwa Rais baba yetu,tunaomba utuokoe.Tumetekwa na tunahitaji msaada wako.Tumeambiwa usipowapatia wanachohitaji watatuua wote. Tunakuomba rais tuokoe tusiuawe.Sisi bado ni wasichana wadogo

na tuna malengo mengi ya maisha. Tuokoe ba……” akashindwa kuendelea akaangua kilio.

“Ndugu Watanzania,wasichana hawa wanakwenda kupoteza uhai wao angali wadogo kwa sababu ya ukaidi wa rais wenu.Kila baada ya saa moja uhai wa wanafunzi kadhaa utapotea ikiwemo na mtoto wa rais,” alisema yule jamaa na kunyoosha mkono akafanya ishara akatokea tena mtu mwingine aliyejifunika sura na mwenye mwili uliojaa akiwa na kisu kikali.Akawafunga vitambaa usoni wale wasichana na bila kupoteza muda kwa kutumia mkono wenye nguvu akamkata kichwa Lucy Nswami akakitenganisha na kiwili wili.

Mwili wa msichana yule mdogo ukaanguka chini akakiweka kichwa juu yake halafu akamuinamisha Husna Ayoub na kumchinja bila huruma.Kiongozi wa magaidi wale akaigeukia kamera na kusema.

“Hawa ni wa kwanza.Tutaendelea kuua zaidi baada ya saa moja.Mheshimiwa rais damu ya wasichana hawa ni juu yako.Tekeleza maagizo yetu na kama ukikaidi tena baada ya saa moja kutoka sasa nitarejea hapa!” Video ile ya kutisha ikafika mwisho.Jenerali Pius akainamisha kichwa chini.Kila mmoja ndani ya kile chumba akabadilika sura na kuonesha hofu kubwa baada ya wasichana wale wawili kuchinjwa.

“Huu ni ukatili usiovumilika!” Aliwaza Jenerali Pius.

Hali katika chumba cha mikutano ikabadilika.Ukimya mkubwa ulitawala mle chumbani kwa dakika kadhaa halafu kikao kikaendelea.Wakati kikao kikiendelea simu ya mezani ikaita, Rais akaipokea na kujulishwa kuwa kiongozi wa magaidi anapiga na anataka kuzungumza naye.

“Hallow!” alisema rais.

“Mheshimiwa Rais, dakika sitini zinakaribia kumalizika.Fahamu sisi tunaongea kwa vitendo.Tunatekeleza kile tunachokiahidi.Tunajiandaa kuua wasichana wanne katika saa hii ya pili.Nataka kujua, je, uko tayari kutekeleza maelekezo yetu?” Aliuliza

kiongozi wa magaidi.Rais Pius akavuta pumzi ndefu halafu akasema

“Nawaomba tafadhali msitishe mauaji ya watoto wetu,hawana hatia!” Alisema rais.

“Tutasitisha pale utakapotekeleza maagizo yetu!”

“Mahmoud Fadil Ghedi anashikiliwa katika mahakama ya Afrika na sisi hatuna uwezo wa kuiingilia mahakama hiyo.Nataka nipewe muda zaidi wa kufanya kila niwezalo kuhakikisha anapatikana.Nataka wakati nikiendelea na zoezi hilo mauaji ya watoto yakome.Sitaki tena mtoto mwingine auawe.Unanielewa?”Alisema Rais Pius.

“Mheshimiwa Rais, nimelikubali

ombi lako.Hatutaua tena watoto wengine ila ninakupa hadi saa kumi na mbili za jioni uwe umempata Mahmoud Fadil Ghedi.Ukifika muda huo bado haujampata, tutaua mateka wote tukianza na mwanao.Jambo lingine….” alisema mkuu wa magaidi kisha akaweka tuo. Ukimya ukapita kwa nukta chache akaendelea.

“Mmepeleka vikosi vingi vya askari na wanajeshi karibu na ukumbi wa KICC.Nataka uviondoe vikosi vile vikae mbali mita mia sita kutoka katika eneo la ukumbi huo.Narudia kuwaonya kuwa msithubutu kujaribu kutaka kuingia ndani.Tumetega mabomu katika ukumbi ule,vile vile vijana wangu waliomo mle ukumbini wote wamevaa fulana zenye

mabomu,hivyo namna yoyote mtakayotaka kuingie mle ndani mtaambulia nyama na mifupa ya mateka.Nataka ndani ya dakika kumi kuanzia sasa vikosi vyote viondoke karibu na jengo la KICC kama mnataka kuwapata mateka wenu wakiwa salama wa salmini," alisema yule jamaa na kukata simu.

Pamoja na kiyoyozi kilichokuwa kikivuma katika ukumbi wa mkutano, rais bado akatoa kitambaa na kujifuta jasho.

"Kwa nini ametoa muda mrefu namna hii hadi saa kumi na mbili za jioni?" Aliuliza Rais na hakuna aliyemjibu. Ukumbi ulikuwa kimya

kabisa.Wajumbe wote walionekana kuingiwa na hofu

“Kutoka sasa hadi saa kumi na mbili za jioni ni muda mrefu ambao tunaweza kuutumia kuwakomboa watoto wetu.Tuutumie kikamilifu.Kila idara ijipange vyema sasa,” alisema Rais Pius na kufunga kikao.Akawataka kila idara waendelee na mikakati ya kuhakikisha mateka wanakombolewa kabla ya saa kumi na mbili jioni.

4

Rais Jenerali Pius akiwa katika tafakari nzito, simu yake ikaita.Alikuwa ni Maurine Kyaso mkurugenzi wa idara ya siri ya usalama wa ndani wa nchi (Secret National Security Agency)

“Maurine,” alisema rais baada ya kuipokea.

“Mheshimiwa Rais,kuna jambo ninataka kukufahamisha,” alisema Maurine.

“Endelea Maurine nakusikiliza,” alisema Rais Pius.

“Mheshimiwa Rais, kuna jambo tumelipata kuhusiana na ile ndege yetu iliyopotea.”

“Nini mmekipata katika suala hilo?” Rais aliuliza.

“Mheshimiwa Rais,taarifa tuliyoipata ni kwamba, ndege hiyo baada ya kuondoka Shanghai ilikwenda kutua jijini Guangzhou kwa ajili ya kuwachukua maafisa wawili wa shirika la ndege la Tanzania waliokuwa jijini hapo kikazi.Taarifa inaonesha kwamba hapo Guangzhou badala ya kupanda

watu wawili,aliongezeka mtu mwingine wa tatu ambaye si mfanyakazi wa shirika la ndege la Tanzania.Huyu ni Mathew Mulumbi.”alisema Maurine

“Mathew Mulumbi?” Jenerali Pius aliuliza kwa mshangao.

“Ndiyo mheshimiwa Rais!”

“Maurine una hakika ya kwamba, Mathew Mulumbi alikuwemo katika ndege hiyo?”Rais aliuliza kwa mshangao kidogo.

“Ndiyo,Mheshimiwa Rais!” akajibu Maurine na Rais akavuta pumzi ndefu.

“Umenishtua sana,Maurine.Sikujua kama Mathew Mulumbi alikuwemo ndani ya ndege hiyo,Huyu ni mkurugenzi wa shirika letu la ujasusi.Halafu katika majina yaliyotolewa awali ya watu

waliokuwamo ndani ya hiyo ndege mbona jina la Mathew halikuwemo?" aliuliza Rais Pius.

"Ni sababu hiyo iliyotufanya tulitazame suala hili kwa mtazamo tofauti mheshimiwa Rais."alijibu Maurine.

"Sijakuelewa,Maurine.Mathew Mulumbi ana mahusiano gani na kupotea kwa ndege yetu?" Rais aliuliza.

"Mheshimiwa Rais,vyombo vyote vinavyoshughulika na uchunguzi wa suala hili la kupotea kwa ndege yetu vimejielekeza baharini vikiamini ndege hiyo itakuwa imeangukia baharini.Sisi baada ya kufahamu uwepo wa Mathew Mulumbi ndani ya ndege hiyo, mtazamo wetu umekuwa tofauti tunaamini upo

uwezekano mkubwa ndege hiyo haijaanguka mheshimiwa rais kama inavyodhaniwa,!”

“Kama haijaanguka iko wapi? Imetekwa? Na kama imetekwa nani ameiteka?” Rais aliuliza.

“Mheshimiwa Rais, ni mapema sana kusema chochote kwa sasa.Tunaendelea kulifanyia kazi suala hilo na tutakapopata chochote, tutakujulisha!”alisema Maurine

“Ahsante Maurine kwa taarifa hiyo.Lifanyieni kazi suala hilo kwa haraka na mnijulishe tafadhali kile mtakachokuwa mmekipata.”alielekeza Rais

“Sawa Mheshimiwa Rais” Maurine alijibu na kukata simu.

“Hili jambo kweli limechukua sura mpya.Ilikuaje Mathew Mulumbi naye akawemo katika ndege hiyo mpya? Iweje uwepo wake ndani ya ndege hiyo umefanywa siri?” Alijiuliza Rais Pius.

SECRET NATIONAL SECURITY AGENCY (SNSA)

Maurine Kyaso Mkurugenzi wa Idara ya Siri ya Usalama wa Ndani wa Nchi(Secret National Security Agency - SNSA) alitoka ofisini kwake akashuka ngazi na kuingia katika ukumbi mkubwa ambamo wafanyakazi wa SNSA

walikuwa wakiendelea kutimiza majukumu yao ya kawaida.

“Naomba tusikilizane!” Alisema Maurine na watu wote wakaacha shughuli zao, kumsikiliza kiongozi wao anataka kuwaambia nini.

“Kuna mambo mawili makubwa ambayo yanaendelea hapa nchini kwa sasa,” alisema Maurine kisha akaweka tuo. Akameza funda la mate kidogo kusafisha koo halafu akaendelea.

“Kwanza,ni tukio la ugaidi lililotokea kule Arusha.Pili, ni kupotea kwa ndege yetu mpya iliyokuwa inakuja nchini ikitokea China.Sisi tumejielekeza katika suala la kupotea kwa ndege.Kuna jambo la dharura limejitokeza ambalo inatubidi tulifanyie kazi mara moja,”

Maurine alinyamaza kidogo halafu akaendelea.

“Nimefanikiwa kuipata orodha ya watu waliokuwamo ndani ya ndege iliyopotea.Watu hao ni marubani wanne wa Tanzania, wahudumu wawili pamoja na baadhi ya maafisa wa shirika la ndege la Tanzania ambao waliifuata ndege hiyo nchini China.Taarifa niliyoipata ni kwamba, ndege hiyo iliondoka Shanghai China na kwenda hadi Guangzhou.Sababu ya kwenda Guangzhou ni kuwapitia maafisa wawili wa shirika la ndege la Tanzania waliokuwa hapo kwa shughuli za shirika.Ikiwa hapo Guangzhou, aliongezeka mtu mwingine wa tatu ambaye si mfanyakazi wa shirika la

ndege la Tanzania.” Maurine akanyamaza na kuigeukia runinga ya ukutani akabonyeza kitanza mbali na picha kubwa ikajitokeza.

“Anaitwa Mathew Mulumbi.Huyu ni mkurugenzi wa Shirika la Ujasusi Tanzania.Kwa wale wasiomfahamu, wanaweza wakamuona kama abiria wa kawaida ndani ya ndege hiyo, lakini kwa sisi tunaomfahamu,uwepo wake katika ndege iliyopotea unatufanya tulitazame tukio hili kwa jicho la tatu.Tunapaswa kujiuliza Mathew Mulumbi, si mfanyakazi wa shirika la ndege aliwezaje kupata nafasi ya kusafiri na ndege hiyo mpya? Swali lingine kwa nini katika orodha iliyotolewa awali jina lake

halikuorodheshwa kuwa alikuwemo ndegeni?” aliuliza Maurine

“Nataka tuchunguze tufahamu aliondoka lini hapa nchini na alielekea wapi baada ya kuondoka.Tuchunguze mawasiliano yake kabla ya kuondoka alizungumza na akina nani na walizungumza nini? Maafisa wa shirika la ndege ambao walikuwepo kikazi jijini Guangzhou ni Silvia Mwalule na Aneth Severino.Nataka maafisa hawa wachunguzwe pia kwa kina tujue kama kuna mmoja wao ana mahusiano yoyote na Mathew Mulumbi.Ninaamini kabisa kwamba lazima kuna mtu aliyemsaidia Mathew kupata nafasi ndani ya ndege hiyo kwani uwepo wa maafisa hawa jijini Guangzhou na Mathew Mulumbi

kisha wote wakaingia katika ndege moja kunazua maswali mengi.Nataka kila mmoja ajielekeze katika jambo hili na nipate majibu haraka,” alisema Maurine na kurejea ofisini kwake.

****

Maurine Kyaso alifungua mlango wa chumba cha mikutano namba mbili kilichokuwa pembeni ya ofisi yake,watu wanne walikuwa wakimsubiri ambao ni viongozi wa idara zilizomo ndani ya SNSA.

“Kuna chochote mmekipata katika yale niliyoelekeza yafanyiwe kazi?” Aliuliza Maurine.

“Ndiyo mkurugenzi.Kuna mambo tumeyapata,” alisema Liberatus msaidizi wa Maurine.

“Mathew Mulumbi aliondoka hapa nchini siku nane zilizopita na ndege ya shirika la ndege la Tanzania kuelekea Guangzhou China.Ndani ya ndege hiyo alikuwemo pia Silvia Mwalule ambaye ni mmoja wa maafisa wa shirika la ndege la Tanzania,naye alikuwa akielekea Guangzhou China,” alisema Liberatus.

“Tumekwenda mbali zaidi na kufuatilia mawasiliano ya Mathew Mulumbi, tukagundua kwamba, kwa muda wa miezi miwili amekuwa akiwasiliana na Silvia Mwalule na kwa namna wanavyowasiliana hakuna shaka wawili hawa wana mahusiano ya

kimapenzi.Wamekuwa wakitumiana ujumbe wa mahaba na nyakati nyingine wakikumbushana kuhusu mambo waliyoyafanya.Wakiwa Gungzhou, wote walifikia hoteli ya nyota tano ya Hilton Gungzhou Tianhe na walilala chumba kimoja.Taarifa kutoka shirika la ndege la Tanzania zinadai Silvia ambaye anahusika na masuala ya fedha katika shirika hilo alikwenda Guangzhou kikazi na alipomaliza kile kilichompeleka huko, aliomba kuisubiri ndege mpya ili aweze kurejea nayo Tanzania," alisema Liberatus.

"Kazi nzuri sana mmeifanya.Sasa tumepata jibu Mathew alimtumia Silvia ambaye ana mahusiano naye ya kimapenzi kupata nafasi ndani ya ndege

mpya.Baada ya kulifahamu hilo, bado tuna maswali tunahitaji kuyatafutia majibu.Kwanza, lazima tufahamu nini kilimpeleka Mathew Mulumbi China na katika jiji la Guangzhou tena kwa wakati ambao Silvia alikuwa anakwenda huko kwa shughuli za kikazi? Je, safari yake hiyo ina mahusiano yoyote na tukio la upoteaji wa ndege? Nataka mawasiliano ya Mathew Mulumbi yachunguzwe zaidi kwa mara ya pili na safari hii tuanzie kuchunguza pale ambapo mawasiliano kati ya Mathew na Silvia yalianza.Bado kuna kitu tunakikosa," alisema Maurine.

5

Papi Gosu Gosu mkuu wa kurugenzi ya operesheni katika Shirika la Ujasusi Tanzania,alirejea nyumbani saa nne asubuhi akitokea kazini.Alilazimika kukesha kazini kufuatilia operesheni moja muhimu sana.Akiwa chumbani kwake amepumzika,simu yake iliita.Akainuka kiuvivu akaichukua na kutazama mpigaji.Namba zilikuwa ngeni katika simu yake.Akaipokea

“Hallow” alisema Gosu Gosu.

“Gosu Gosu,unazungumza na Mathew.Tafadhali naomba usitamke jina langu kama uko karibu na watu.”

“Niko hapa nyumbani ninapumzika.Nimekesha leo tukiwafuatilia wale

Wagiriki.Unaendeleaje,
Mathew?”aliuliza Gosu Gosu

“Gosu Gosu,amka.Kuna jambo la kushughulikia sasa hivi”alisema Mathew.

“Kuna nini, Mathew?” Gosu Gosu aliuliza.

“Nadhani umesikia kile kilichofanywa na magaidi kule Arusha”

“Ndiyo Mathew nimesikia.Ni shambulio baya sana.” alisema Gosu Gosu.

“Gosu Gosu, nisikilize vizuri.Kuna madai ambayo magaidi wameyatoa wakiitaka serikali kuyatekeleza ili waweze kuwaachia mateka wanaowashikilia.Wanamtaka Mahmoud Fadil Ghedi.Madai hayo ni danganya

toto.Kuna mambo mazito nyuma ya shambulio hilo.Unanisikia Gosu Gosu?”Mathew aliuliza.

“Nakusikiliza Mathew!” alisema Gosu Gosu.

“Kuna mtu anaitwa Profesa Fabrice Kayembe, ni mmoja wa watu waliokuja Tanzania kushiriki mkutano wa *Afrika Asili Yangu*.Huyo ndiye sababu ya shambulio hilo.Magaidi wanamlenga yeye,hivyo kwa namna yoyote ile, hakikisheni mnafanya kila linalowezekana muweze kumuokoa kutoka ndani ya ukumbi kabla hajaingia mikononi mwa magaidi”alisema Mathew.

“Mathew, samahani kwa kuuliza,huyu mtu ni nani? Unaweza

ukanipa maelezo zaidi kuhusiana naye tafadhali?” Gosu Gosu aliuliza.

“Gosu Gosu, kwa sasa shughulikia hilo nililokwambia.Hakikisheni mnamuokoa kutoka katika ukumbi huo.Narudia tena kwa namna yoyote ile hakikisheni mnamuokoa Fabrice Kayembe.Magaidi hawapaswi kumpata” alisema Mathew.

“Mathew, wewe uko wapi?” Gosu Gosu aliuliza.

“Gosu Gosu, tafadhali usimweleze mtu yeyote yule kama nimekupigia simu na kukupa maelekezo haya. Fanyia kazi hayo niliyokueleza!”alisema Mathew na kukata simu.Gosu Gosu akahisi kuchanganyikiwa.

“Kumekucha! Alisema Gosu Gosu na kushusha pumzi

“Ni nani huyu Fabrice Kayembe?” Alijiuliza Gosu Gosu.

“Sitakiwi kupoteza muda.Suala hili ni nyeti na linahitaji utekelezaji wa haraka sana,” aliwaza na kuchukua simu, akatafuta namba ya Ruby, akampigia.

“Gosu Gosu,” alisema Ruby baada ya kupokea simu.

“Ruby, uko wapi?”

“Gosu Gosu, hata salamu hakuna halafu unaniuliza mahali nilipo?”Ruby aliuliza.

“Samahani,Ruby,uko wapi sasa hivi? Hebu niambie”

“Niko nyumbani.Kuna nini?” Ruby aliuliza

“Ninakuja hapo kuonana nawe,” alisema Gosu Gosu.

“Gosu Gosu, ninapumzika tafadhali.We’ mwenyewe unafahamu kazi tuliyoifanya usiku wa kuamkia leo,”alisema Ruby. Lakini Gosu Gosu hakuridhika na kauli ya Ruby akasema.

“Ruby, ninakuja kwako kuna jambo la dharura na la muhimu mno. Si la kusubiri kesho” alisema Gosu Gosu na kukata simu.Akainuka akavaa suruali ya *jinzi*,fulana na koti kisha akachukua bastola yake akaifunga kiwambo cha sauti na kuifutika katika koti.Akashuka haraka kutokea juu nyumbani kwake, akapanda gari na kuondoka kuelekea kwa Ruby.

****

“Kuna nini, Gosu Gosu? Umenishtua sana!” alisema Ruby baada ya Gosu Gosu kufika nyumbani kwake.

“Ruby, kumekucha!” alisema Gosu Gosu na kuweka tuo. Akameza funda la mate.Ruby akahamanika. Akamtazama vizuri mwenzake. “Gosu Gosu, unazidi kuniogopesha ujue.Kuna nini kwani?”Ruby aliuliza na Gosu Gosu akamweleza kile alichoelezwa na Mathew Mulumbi.

“Umenichanganya sana na taarifa hiyo.” alisema Ruby

“Ruby,tutafanyaje kumuokoa huyo Fabrice Kayembe kutoka katika ukumbi wa KICC unaoshikiliwa na magaidi?

Hilo ndilo jambo tunalotakiwa kulijadili kwa sasa,” alisema Gosu Gosu.

“Hili si jambo dogo, Gosu Gosu!”Alisema Ruby.

“Ninafahamu,si jambo dogo, lakini Mathew amesisitiza kwa namna yoyote ile lazima tumuokoe Fabrice Kayembe.Unamfahamu Mathew asingeweza kutoa maelekezo haya kama jambo hili halina umuhimu.Lazima tutafute la kufanya kumuokoa Fabrice kutoka mikononi mwa magaidi,” alisema Gosu Gosu.

“Gosu Gosu, suala hili ni gumu na sisi wawili peke yetu hatuna wezo wowote wa kuingia katika ukumbi wa KICC kumchukua huyo Fabrice Kayembe.” alisema Ruby.

“Kwa nini tusiliwasilishe kwa shirika letu la ujasusi tukalifanyia kazi kwa haraka?” aliuliza Gosu Gosu na Ruby akatafakari kidogo kisha akasema.

“Zipo idara mbali mbali zinazolishughulikia suala hili. Tungeweza kuwapa taarifa hii,lakini tatizo ni kwamba,haijajitosheleza.Watahitaji kujua huyu Fabrice Kayembe ni nani? Sisi hatuna maelezo yoyote ya kutoa kama tukiulizwa swali hilo,” alisema Ruby.

“Uko sahihi Ruby.Kwa nini basi tusimshirikishe rais?” Gosu Gosu aliuliza.

“Ni wazo zuri, lakini ni vipi kama naye akitaka kufahamu zaidi kuhusu

jambo hili hasa kuhusu Fabrice Kayembe? Swali lingine kwa nini Mathew hajampigia Rais akampa taarifa hii? Ruby aliuliza akijiweka sawa kumsikiliza Gosu Gosu.

“Ruby hatuna mtu mwingine wa kutusaidia kwa sasa zaidi ya rais.Mpigie mwambie taarifa hii imetoka kwa Mathew Mulumbi lazima ataipa uzito.” alijibu Gosu Gosu.Ruby hakupoteza muda akampigia simu Rais Pius.

“Hallow” alisema Rais baada ya kupokea simu.

“Mheshimiwa Rais, unazungumza na Ruby mkuu wa kurugenzi ya teknolojia na mawasiliano katika Shirika la Ujasusi Tanzania” alisema Ruby baada ya rais kuipokea simu yake.

“Mathew amekwisha nipa taarifa zako.Unasemaje,Ruby?”alisema Rais Pius.

“Mheshimiwa Rais, mimi na mwenzangu Gosu Gosu tuna taarifa muhimu ambayo tunataka kukupatia.Ni taarifa ya muhimu sana kutoka kwa Mathew Mulumbi!”

“Mathew Mulumbi?” Aliuliza rais kwa mshangao mkubwa.

“Ndiyo Mheshimiwa Rais.Kuna taarifa tuimeipata kutoka kwake ambayo inahusiana na tukio la kigaidi lililotokea leo,” alisema Ruby.

“Ruby, tafadhali nakuomba uje hapa Ikulu haraka sana,” alisema Rais Pius.

“Ahsante Mheshimiwa Rais.Tunakuja sasa hivi,” alijibu Ruby, rais akakata simu.

“Mathew Mulumbi, amewasiliana na akina Ruby? Ni kweli? Kama ni kweli, je, yuko hai? Hakuwemo katika ndege iliyopotea?” Rais aliendelea kujiuliza maswali huku akifuta jasho usoni.Mara simu yake ikaita, alikuwa mkuu wa jeshi la polisi.Akaipoka mara moja,akajulishwa kile kilichokuwa kinaendelea jijini Arusha katika harakati za kuwakomboa mateka wanaoshikiliwa na magaidi.

****

Ruby na Gosu Gosu waliwasili Ikulu na kupelekwa moja kwa moja katika ofisi ya rais ambaye kwa wakati huo alikuwa amebadili mavazi na kuvaa mavazi ya kijeshi.

“Mheshimiwa Rais, shikamoo” walisema akina Ruby baada ya kuingia ofisini kwa rais.

“Marahaba.Karibuni vijana!”

“Tunashukuru Mheshimiwa Rais,” alisema Ruby na wote wakaketi

“Ahsanteni sana kwa kuitika wito.Hatuna muda wa kupoteza tuna mambo mengi sana siku ya leo.Naomba twende moja kwa moja katika kitu cha msingi kilichotukutanisha hapa.Uliniambia kwamba una taarifa

kutoka kwa Mathew Mulumbi,”alisema rais akijiegemeza sofani.

“Ndiyo Mheshimiwa Rais.Taarifa kutoka kwa Mathew Mulumbi, inasema kuwa maelekezo waliyoyatoa magaidi wakitaka kuachiwa kwa kiongozi wao,Mahmoud Fadil Ghedi ni hadaa.Kuna sababu iliyojificha nyuma ya shambulio lao.Mathew anadai kwamba magaidi wanamtafuta mtu anaitwa Fabrice Kayembe ambaye naye anashikiliwa mateka ndani ya ukumbi wa KICC.Ametoa maelekezo kuwa tujitahidi kufanya kila kinachowezekana ili tumuokoe huyo Fabrice Kayembe,” alisema Ruby na rais akashusha pumzi.

“Ni nani huyo Fabrice Kayembe?” Aliuliza rais.

“Mathew hajaweka wazi Fabrice Kayembe ni nani na kwa nini awe ni lengo la magaidi,” alijibu Ruby.

“Mathew Mulumbi amewasiliana nanyi kwa njia gani?” Aliuliza rais.

“Alipiga simu,” alijibu Ruby.

“Mna hakika ni yeye kweli?” Rais Pius aliuliza.

“Ndiyo, Mheshimiwa Rais ni yeye,” alijibu Ruby. Rais Pius akaegemea kiti. Dhahiri alishtushwa na taarifa hiyo.

“Mathew aliwaeleza yuko wapi?” Rais aliuliza.

“Hapana. Hakueleza mahali alipo,”alijibu Gosu Gosu.

“Vijana wangu, kuna jambo ambalo nataka kuwajulisheni ili kwa pamoja tusaidiane kwa sababu naona jambo hili

limekuwa kubwa mno," alisema Rais Pius.Akanyamaza kidogo.

"Kabla ya kutokea kwa tukio hili la kigaidi, kulitanguliwa na tukio la kupotea kwa ndege yetu mpya.Inasadikiwa ndege hiyo imepotelea baharini na juhudi za kuitafuta zinaendelea.Taarifa niliyoipata asubuhi ya leo ni kwamba ndege hiyo ilikuwa imebeba marubani wanne,wahudumu wawili na baadhi ya maafisa wa shirika letu la ndege.Baadaye nilipokea tena taarifa nyingine ikidai kuwa ndege ilipotoka Shangai ilikwenda Guangzhou kuwafuata maafisa wa shirika waliokuwepo hapo kikazi.Hapo Guangzhou ambapo walitakiwa kupanda watu wawili, aliongezeka mtu wa tatu

ambaye ni Mathew Mulumbi,”alisema Rais.

“Mathew alikuwemo katika ndege hiyo iliyopotea?”Ruby aliuliza kwa mshangao.

“Ndiyo.Taarifa ya SNSA inaonesha kuwa Mathew alikuwemo ndani ya ndege hiyo iliyopotea” alijibu Rais

“SNSA ni nini? Ruby aliuliza

“Hii ni idara ya siri ya usalama wa ndani wa nchi ambayo iko chini ya ofisi ya Rais”alisema Rais Pius

“Kwa mujibu wa SNSA Mathew alikuwemo ndani ya hiyo ndege.Wamechimba zaidi, wakagundua kwamba mmoja wa maafisa wa shirika la ndege la Tanzania waliotakiwa kuchukuliwa na ndege hiyo jijini

Guangzhou, ana mahusiano na Mathew Mulumbi.Afisa huyo jina lake ni Silvia Mwalule.Tunaamini Silvia ndiye aliyemsaidia Mathew kusafiri na ndege hiyo.Taarifa kuwa Mathew amewapigia simu imenistua sana.”alisema Rais Pius.

“Mheshimiwa Rais, nimeshtuka pia kusikia kwamba Mathew Mulumbi alikuwemo katika ndege inayodaiwa kupotea.Lakini kwa simu hii aliyopiga, ni wazi yuko hai na kama yuko hai ni kiashiria tosha kuwa hata ndege yetu kuna uwezekano mkubwa haijaanguka majini.Tunahisi kuna jambo kubwa linaloendelea hapa nchini ambalo Mathew hajaliweka wazi bado” alisema Ruby.

“Tunatakiwa kumpata Mathew Mulumbi ili atueleze nini kimetokea na tufahamu mahali ndege yetu ilipo.!”alisema Rais Pius.

“Mheshimiwa Rais, nina ushauri.Kutokana na maelezo yako ninaamini Mathew Mulumbi, yuko katika misheni muhimu.Inawezekana kuwepo kwake ndani ya ndege hiyo ni moja wapo ya misheni anayoendelea nayo hivi sasa.Ushauri wangu tuyafanyie kazi maelekezo yake.Ninaamini lazima tutapata kitu,” alisema Ruby.

“Ushauri wako ni mzuri Ruby,lakini tunapaswa kabla ya kuchukua hatua zozote, tujiridhishe kama kweli Fabrice Kayembe yuko hapa nchini na kama yuko ndani ya ukumbi huo unaoshikiliwa

na magaidi," alisema Rais Pius.Akampigia simu Maurine Kyaso mkurugenzi wa SNSA na kumtaka amsaidie kutafuta taarifa za mtu anayeitwa Fabrice Kayembe.

Baada ya dakika nne,Maurine akampigia simu Rais akamjulisha kuwa Fabrice Kayembe ni raia wa Ufaransa mwenye asili ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.Ni profesa katika chuo kikuu cha Paris.Yuko nchini kuhudhuria mkutano wa *Afrika Asili Yangu.*

"SNSA wamethibitisha ni kweli Fabrice Kayembe yuko hapa nchini.Ugumu uliopo ni namna ya kuingia ndani ya ukumbi wanaoushikilia magaidi.Mpaka sasa……." alisema Rais

akanyamza baada ya simu yake kuita.Alikuwa kiongozi wa magaidi

“Kiongozi wa magaidi anapiga,” alisema Rais na kuvuta pumzi ndefu.Akaipokea ile simu.

“Hallow,” alisema Rais.

“Mheshimiwa Rais, wakati tunasubiri utekelezaji wa maagizo yetu,ninahitaji madaktari ndani ya ukumbi. Kuna watu wamejeruhiwa wanahitaji matibabu ya haraka.Ninataka nikukabidhi mateka wako wote wakiwa katika hali nzuri,” alisema mkuu wa magaidi.

“Madaktari wangapi na wa aina gani unaowahitaji?” Aliuliza Rais Pius.

“Ninahitaji madaktari wawili tu wenye uwezo wa kufanya upasuaji. Waje

na vifaa na madawa," alisema kiongozi wa magaidi.

"Watawezaje kuingia ndani ya jengo ilhali mmefunga kila mahali?" Rais aliuliza.Akanyamaza kumsikiliza kiongozi huyo atasemaje.

"Mheshimiwa Rais, tuma madaktari sisi tutawaingiza ndani ya ukumbi.Tafadhali, usijaribu kuwatumia kwa namna yoyote ile katika mipango yako ya kutaka kuvamia jengo walimo watu wangu.Utakuwa umefanya kitu kibaya sana na utawakosa mateka wote!"alisema kiongozi wa magaidi.

"Endapo nitatuma madaktari wangu waje kuhudumia watu mnaowashikilia, unanihakikishia kwamba watakuwa salama?" Rais aliuliza.

“Watakuwa salama. Japo hatutawaachia hadi pale utakapokuwa umetekeleza maelekezo yetu ndipo tutawaachia pamoja na mateka wengine,” alisema kiongozi wa magaidi.

“Hakuna daktari atakayekubali kuhatarisha maisha yake kiasi hicho.Endapo nitatuma madaktari, nataka watakapomaliza kazi yao waachiwe huru.”

“Hilo haliwezekani, Mheshimiwa Rais.Hatuwezi kuwaachia huru.Lakini watakuwa salama nakuhakikishia hilo.” Alisema kiongozi wa magaidi. Kimya kikatawala kwa nukta chache kisha akaendelea.

“Mheshimiwa Rais, kuna mateka wamejeruhiwa. Wanahitaji msaada wa

haraka wa madaktari.Endapo wakipoteza maisha, lawama zitakuwa juu yako hivyo amua mwenyewe kama ungependa kupokea maiti za mateka ambao kama wangeweza kupatiwa matibabu haraka, wangepona," alisema kiongozi wa magaidi.

"Sawa.Nitatuma madaktari. Naomba muda kidogo ili niweze kufanya maandalizi.Ni vigumu kupata madaktari kwa haraka ambao wanaweza wakajitolea kuja kutibu mateka ndani ya ukumbi huo," alisema Rais.

"Utakapowapata, utanijulisha kwa kutumia namba hii ya simu.Nakuonya mheshimiwa Rais,msithubutu kutaka kufuatilia simu hii kujua mahali niliko.Nitajua mara moja na nitakata

vichwa watoto kumi” alisema mkuu wa magaidi na kukata simu.Rais akavuta pumzi ndefu.

“Mambo magumu!” alisema Rais Pius.

“Kuna nini, Mheshimiwa Rais?” Ruby aliuliza kwa shauku.

“Magaidi wanahitaji madaktari kwenda kuwatibu baadhi ya mateka waliopata majeraha.”

“Hakuna tatizo, Mheshimiwa Rais. Jambo hili limekuja kwa wakati muafaka kabisa ambao tunahitaji kujiridhisha kama kweli Fabrice Kayembe yuko ndani ya ukumbi.Tutafute madaktari ambao tunaweza kuwatuma humo ndani ya ukumbi” alisema Ruby.Rais

akamtazama kwa umakini kisha akasema.

“Wametoa sharti moja kwamba madaktari watakaoingia ndani ya ukumbi, hawataruhusiwa kutoka baada ya kumaliza kutoa huduma. Nao pia wataunganishwa na mateka.Hapo ndipo kuna ugumu kwani hakuna daktari atakayekubali kujipeleka mwenyewe mikononi mwa magaidi,japo tunahitaji sana kuwahudumia majeruhi ndani ya ukumbi huo ambao wengi ni raia wa kigeni”

“Mheshimiwa Rais, nitakwenda mimi,” alisema Gosu Gosu.

“Gosu Gosu?”Ruby akashangaa.

“Gosu Gosu, wewe ni daktari?” Rais aliuliza.

“Mheshimiwa Rais, mimi ni mwanajeshi nina uzoefu mkubwa wa mapambano. Asili yangu ni Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.Nimeishi msituni tangu nikiwa mdogo hivyo nina uzoefu mkubwa wa mapambano.Hapa Tanzania nimeshirikiana na Mathew Mulumbi katika misheni kadhaa za kupambana na magaidi,” alisema Gosu Gosu.

Rais akaendelea kumkazia macho. Ukimya tena ukapita, Rais Pius akainua glasi ya maji ya kunywa iliyokuwa mbele yake akapiga funda kadhaa na kuirudisha tena juu ya meza. Akamtazama vizuri Gosu Gosu..

“Lakini, Gosu Gosu, wewe si daktari.Anahitajika mtu mwenye taaluma

ya udaktari kwa sababu wakigundua wewe si daktari, mambo yatakuwa magumu zaidi.Wanaweza hata kukuua wakijua umekwenda kuwachunguza.”

“Ninafahamu namna ya kutoa huduma ya kwanza.Naamini kutakuwa na watu walioumizwa, vilevile waliopatwa na mstuko.Umetamka kuna kitu kinaitwa SNSA.Tunaweza kushirikiana nao katika misheni hiyo.Naamini wanao madaktari katika idara yao hivyo wanaweza wakaniongoza pale nitakapohitaji msaada” alisema Gosu Gosu

“Mheshimiwa Rais wazo la Gosu Gosu ni zuri.Gosu Gosu atawekewa kifaa maalum kidogo cha mawasiliano sikioni ambacho kitatusaidia sisi kuweza

kuwasiliana naye.Tutampa maelekezo nini cha kufanya endapo itatokea kuna mgonjwa ambaye ana tatizo kubwa.Wamesema wanataka madaktari wawili. Endapo tukimpata mtu mwingine ambaye ataongozana na Gosu Gosu, basi tutamfunga kamera ya siri ambayo itatuwezesha kuona kile kinachoendelea ndani ya ukumbi.Hiyo itasaidia kujua magaidi wamejipanga vipi,wako wangapi na tutawezaje kuingia ukumbini kuwakomboa mateka.Mheshimiwa Rais, hii ni nafasi muhimu sana tumeipata ambayo lazima tuitumie vyema kujua hali ikoje mle ndani," alisema Ruby.

"Huo unaonekana ni mpango mzuri sana.Kuna mtu anaitwa Agai Sempa. Ni jasusi ambaye alikuwa katika kizuizi kwa

kosa la kuharibu misheni.Mathew alinileta faili lake na kuomba aachiwe.Leo nilipitia faili lake nikaelekeza aachiwe huru.Tayari amefika hapa Ikulu, nilikuwa na mpango wa kumtumia katika kazi nyingine lakini kwa kuwa imejitokeza kazi hii basi ataungana na Gosu Gosu kwenda Arusha katika hiyo misheni,”alisema Rais Pius.

Akatulia kidogo kisha akapiga simu.Akaelekeza Agai aingie ofisini kwake.Akamtambulisha kwa akina Ruby halafu akamueleza kuhusiana na misheni ile. Agai bila kigugumizi akakubali kushirikiana na Gosu Gosu.

“Kwa kuwa tayari tumekwisha wapata madaktari, hakuna muda wa kupoteza twendeni ofisi za SNSA haraka

tujadili kuhusu misheni hii na maandalizi yakafanyike mara moja ili akina Gosu Gosu waelekee Arusha” alisema Rais kisha akampigia simu Maurine Kyaso mkurugenzi wa SNSA akamjulisha kuwa anaelekea huko.Bila kupoteza muda wakatoka na kuingia katika helkopta ya Rais wakaelekea idara ya siri ya usalama wa ndani wa nchi (SNSA).

****

Helkopta ya Rais ilitua SNSA. Maurine Kyaso alimpokea Rais na watu alioongozana nao . Wakaelekea moja kwa moja ofisini kwake.Rais akawatambuilisha watu alioongozana nao halafu akamueleza Maurine kile

kilichowapeleka pale.Walijadiliana namna wanavyoweza kutekeleza mpango ule.Haikuchukua muda Gosu Gosu na Agai,walianza kuandaliwa.Walipewa maelekezo kadhaa na madaktari wa SNSA namna ya kutumia baadhi ya vifaa watakavyoingia navyo ndani ya ukumbi.

Waliwekewa vifaa vya mawasiliano katika masikio ambavyo vilifunikwa na gozi laini iliyobandikwa juu ya sikio ili kuficha kabisa kifaa kile kisionekane.Agai Sempa, akawekewa kamera ndogo ya kijasusi katika mfuko wake wa koti.Baada ya kila kitu kukamilika, wakaondoka na helkopta ya Rais wakaelekea katika uwanja wa ndege wa kijeshi kwa ajili ya kutumia ndege za jeshi kuelekea Arusha.

“Ruby, wakati tukisubiri misheni hii ya akina Gosu Gosu nataka turejee lile suala la Mathew Mulumbi.Bado sijapata jibu ni nini hasa kinachoendelea,”alisema Rais Pius.

“Mheshimiwa Rais, ninamfahamu Mathew Mulumbi, lazima atakuwa katika misheni.Naamini hata kuwepo kwake katika hiyo ndege iliyopotea si kwa bahati mbaya. Kuna sababu maalum nyuma yake,”alisema Ruby akimtazama Rais.

“Unadhani kupotea kwa ndege hiyo kuna mahusiano na tukio la leo?” Rais aliuliza kimshangao.

“Sina hakika sana, Mheshimiwa Rais.Ni Mathew pekee ambaye anaweza akatupa majibu ya nini hasa

kinachoendelea.Kwa kuwa yuko hai, ninaamini atatupa majibu.Mheshimiwa Rais, jambo hili la Mathew naomba liwe ni siri kubwa kwa sasa kama alivyotaka mwenyewe," alisema Ruby.Mazungumzo yakasimama baada ya Maurine kuingia.

"Kila kitu kiko vizuri! Watu wetu wa Arusha wamerusha *drone* juu ya jengo linaloshikiliwa na magaidi.Muda mfupi ujao kutoka sasa tutaanza kupata picha za mahali hapo kutokea juu" alisema Maurine.Wote sasa wakayaelekeza macho katika runinga.

"Hawa magaidi hawawezi kuitungua hiyo *drone* wakiiona inaruka juu ya jengo?" Rais aliuliza.

“Mheshimiwa Rais,*drone* zinazotumiwa na SNSA si hizi za kawaida.Zinaruka umbali mrefu si rahisi kuonekana kwa macho.Zina nguvu kubwa mno ya kuona eneo husika kutokea mbali” alisema Maurine.Punde katika runinga wakaanza kupata picha za jengo la KICC kutokea katika *drone* iliyorushwa na watu wa SNSA Arusha.

Juu ya jengo kulikuwa na watu wanne waliovalia mavazi ya kijeshi na sura zao zikiwa zimezifunikwa kwa vitambaa.Mkononi wakiwa na bunduki nzito za udunguaji.Mmoja wao alikuwa na kombora la RPG akiwa katika mkao wa utayari endapo kungetokea helkopta yoyote kwa juu.Licha ya silaha

walizokuwa nazo,wote walikuwa wamevaa fulana zenye milipuko mwilini.

“Inanishangaza sana.Wamewezaje kuingiza silaha hizi zote ndani ya ukumbi pamoja na ulinzi mkali uliokuwepo? Ukumbi ule umekaguliwa sana na vyombo vya ulinzi walishindwaje kugundua uwepo wa silaha hizi kali?” Aliuliza Jenerali Pius.

“Mheshimiwa Rais, inaonekana huu mpango haukuanza hivi karibuni.Wamechukua muda mrefu kufanya maandalizi na wakaweza kuingiza silaha zile ndani ya jengo.Huu ni mtandao mrefu, Mheshimiwa Rais,” alijibu Ruby.

6

ARUSHA

Ndege za kijeshi walizopanda Gosu Gosu na Agai zilitua katika uwanja wa ndege wa Arusha ambao ulikuwa umefungwa kwa muda kufuatia mashambulio yale ya magaidi.Leon Danford mkuu wa SNSA ofisi ya Arusha tayari alikuwepo uwanjani hapo kuwapokea.Ilikuwa safari ya kimyakimya na gari zilikwenda kwa mwendo mkali hadi walipowasili katika ofisi za SNSA Njiro Arusha.

“Karibuni sana ndugu,hapandipo ofisi za SNSA Arusha.Tumepewa maelekezo na ofisi kuu tufanye maandalizi na tayari yamekamilika kama tulivyoelekezwa”alisema Leon.Akawaonesha akina Gosu Gosu gari la kubebea wagonjwa walilioliandaa.Ndani yake kulikuwa na madawa na vifaa vingine ambavyo wangevihitaji.

“Agai una uhakika unataka kuendelea na misheni hii?” Gosu Gosu aliuliza kujihakikishia kama wapo pamoja na mwenzake.

“Usihofu, Gosu Gosu, niko tayari!” Agai alijibu kisha wakaingia katika gari.Safari kuelekea katika ukumbi wa kimataifa wa mikutano wa KICC

ikaanza.Makao makuu Dar es Salaam wakajulishwa kuwa Gosu Gosu na Agai tayari wameelekea KICC.

Askari polisi walitapakaa katika kila kona ya jiji la Arusha wakilinda majengo mbali mbali ya umma na wengine wakifanya doria mitaani.Magari yalikuwa machache barabarani na hakukuwa na mikusanyiko.Jeshi la polisi lilikataza mikusanyiko ya aina yoyote ile. Watu walishauriwa wabaki majumbani mwao.

Barabara inayoelekea katika jengo la KICC ilifungwa.Kuliwekwa kizuizi cha polisi kutoruhusu mtu au gari kuelekea katika eneo la ukumbi.Mita mia tano kutoka jengo la KICC,vikosi vya askari na wanajeshi vilikuwa vimejiweka tayari

vikisubiri amri ya kuvamia jengo hilo.Mkuu wa jeshi la polisi ambaye ndiye aliyekuwa kiongozi wa operesheni ya kuwakomboa mateka wanaoshikiliwa na magaidi alipigiwa simu na Rais akampa maelekezo ya kuliruhusu gari la wagonjwa la akina Gosu Gosu lisizuiliwe.

“Tumevuka kizuizi cha polisi.Sasa tunaelekea katika geti kuu la kuingilia ndani ya jengo,” Gosu Gosu aliwajulisha SNSA.Tayari makao makuu ya SNSA jijini Dar es salaam,walikwisha anza kuliona gari lile la akina Gosu Gosu kupitia *drone* iliyokuwa angani.

“Msiwe na wasi wasi, Gosu Gosu, tunawafuatilia!” alisema Ruby akiwa makao makuu ya SNSA Dar es

Salaam.Wakati Gosu Gosu akikaribia geti kuu la kuingilia jengo la KICC, Rais Pius akampigia simu kiongozi wa magaidi na kumjulisha kwamba madaktari wanalikaribia geti kuu.Taratibu geti likafunguliwa kutokea ndani.

“Kila la heri, Gosu Gosu!” alisema Ruby baada ya akina Gosu Gosu kulivuka geti kuu na kisha likajifunga.Mara tu geti lilipojifunga, wakatokea watu sita waliofunika nyuso zao wakiwa na bunduki nzito huku wameizungusha mikanda ya risasi mwilini mwao.Wakapiga risasi juu Gosu Gosu akasimamisha gari.

“Kazi imeanza.Mtuombee!” alisema Gosu Gosu.Akazima gari.Magaidi

wawili wakalisogelea gari huku wengine wakiwa makini wameelekeza bunduki zao tayari kama kungetokea shambulio lolote.Gosu Gosu na Agai wakaamriwa kushuka ndani ya gari.Wakapigishwa magoti.Vifaa vyote vilivyokuwamo ndani ya gari vikashushwa chini.Gari likakaguliwa lote kama lilikuwa na silaha, lakini hakukuwa na silaha yoyote.

“Wanafanya nini?” Rais Pius aliuliza.Alikuwa bado yungali SNSA akifuatilia kwa karibu misheni ile.

“Magaidi hawa ni wajanja sana. Wanahisi yawezekana akina Gosu Gosu wamefungwa vifaa vya kijasusi,” Ruby alijibu.

“Vipi kama wakiigundua kamera ile aliyofungwa Agai?” Rais aliuliza.

Hakuna aliyemjibu.Wote walikuwa wameyaelekeza macho yao runingani kufuatilia kilichokuwa kikiendelea.

Gosu Gosu na Agai wakavuliwa nguo zote wakabaki watupu.Wakakaguliwa kama kuna kifaa chochote wanacho mwilini mwao.Vile vifaa vya mawasiliano vilivyowekwa masikioni havikuweza kuonekana kutokana na kufunikwa na ile ngozi maalum iliyochukua rangi ya ngozi ya mwili.

Gosu Gosu na Agai walionekana kuhojiwa maswali kadhaa,halafu wakapewa mavazi mengine wakavaa.Yale mavazi waliyokuwa nayo yakatupwa ndani ya gari,likawashwa moto kutokomeza kabisa uwezekano wa

kufuatiliwa. Akina Gosu Gosu na Agai wakaingizwa ndani.

“Misheni imefeli.Hatutaweza tena kuona chochote ndani ya ukumbi!” alisema Rais Pius. Kwa hakika alikata tamaa.

“Misheni inaendelea,Mheshimiwa Rais.Hatutaweza kuona, lakini tayari tuna watu wetu ndani ya ukumbi. Hawa watakuwa jicho letu la kutuhabarisha kitakachokuwa kinaendelea mle ndani kwani wanavyo vifaa vya mawasiliano” alisema Ruby.

Gosu Gosu na Agai walipelekwa moja kwa moja katika ukumbi mkubwa ambako mateka wote walikuwa wamekusanywa sehemu moja.

“Tusikilizane!!alisema mmoja wa magaidi akitumia lugha ya kiingereza.

“Nimewaleteeni daktari kuja kuwahudumia.Kama kuna yeyote ambaye hajisikii vizuri atawaona madaktari na kuhudumiwa,” alisema gaidi huyo.Akaelekeza kutengwa meza maalumu ya kuhudumia mateka hao.Gosu Gosu akisaidiana na Agai, wakaanza kuwahudumia mateka waliokuwa na majeraha mbalimbali.Nyuma yao kukiwa na watu wawili wenye bunduki wakiwasimamia

“Gosu Gosu kutoka hapo ulipo, unaweza kumuona Fabrice?”Ruby aliuliza kutokea Dar es Salaam.Gosu Gosu akainua kichwa kutazama

mateka.Mara akaguswa na mtutu wa bunduki kichwani.

“Endelea na kazi!”Gosu Gosu aliamriwa na mtu aliyekuwa nyuma yake.Gosu Gosu akaendelea kumuhudumia mmoja wa wagonjwa aliyekuwa ameumia kidole.Akajifanya anazungumza naye halafu akasema.

“Hayupo!”

Mlinzi aliyekuwa nyuma yake hakugundua chochote.Alidhani Gosu Gosu anazungumza na mgonjwa aliyekuwa akimfunga kidonda.

“Fabrice, hayumo ndani ya ukumbi! Gosu Gosu amethibitisha hilo,” alisema tena Ruby.

“Kama hayupo ndani ya ukumbi yupo wapi?” Rais aliuliza.

“Tuwape nafasi akina Gosu Gosu watajua nini cha kufanya,” alisema Ruby.

“Ninarejea Ikulu.Nataka muendelee kufuatilia jambo hili mtanijulisha kila kinachoendelea.” Akaondoka kuelekea katika helkopta yake akarejea Ikulu.

****

Gosu Gosu na Agai walimaliza kuwahudumia watu waliokuwa wamepatwa na majeraha mbali mbali.Hakukuwa na mtu yeyote mwenye tatizo kubwa kama walivyokuwa wamedai magaidi.Baada ya kumaliza, wakaamriwa kumfuata gaidi mmoja akawaongoza hadi katika chumba

ambacho kilikuwa kinalindwa na watu watatu wenye silaha.

Walipoingia ndani, wakakuta jamaa mmoja amefungwa katika kiti amechafuka damu.Hakuwa na nguvu.Uso wake ulivimba kutokana na kipigo kizito.Gaidi aliyeonekana ndiye kiongozi, akaingia ndani ya kile chumba.

“Hal’ant jarah”(wewe ni daktari wa upasuaji?) aliuliza yule gaidi kwa lugha ya kiarabu

“Sijui lugha ya Kiarabu.Ninazungumza Kiingereza,Kiswahili au kifaransa tu,” alisema Gosu Gosu kwa lugha ya kiswahili

“Ala tufhimani hal’ant jarah?” (Hunielewi? Wewe ni daktari wa

upasuaji?) aliuliza tena yule gaidi mkuu. Ikamlazimu Gosu Gosu kumfanyia ishara kwamba haelewi lugha ambayo alikuwa anaitumia. Gaidi akazungumza Kiarabu na mmoja wa watu wake waliokuwamo ndani ya kile chumba kana kwamba anamtuma kitu.Yule jamaa akatoka.Baada ya muda, akarejea akiwa na jamaa mwingine ambaye alizungumza naye kwa Kiarabu halafu akamsemesha Gosu Gosu kwa lugha ya Kiswahili.

“Unaulizwa wewe ni daktari wa upasuaji?” Alisema yule jamaa kwa Kiswahili sanifu kabisa kilichomshangaza Gosu Gosu.

“Kuna mgonjwa wa kumpasua?” Gosu Gosu aliuliza.Akaambiwa

anatakiwa kumfanyia upasuaji jamaa aliyekuwa katika hicho chumba.

“Anaumwa nini huyu?” Gosu Gosu aliuliza.

“Anatakiwa kupasuliwa pajani.”

“Ana tatizo gani katika paja?” Gosu Gosu aliuliza. Yule kiongozi wa magaidi akachomoa bastola.Akamnyooshea Agai huku akizungumza Kiarabu.

“Anakwambia utafanya upasuaji au huyu mwenzako auawe?”Alisema yule jamaa aliyekuwa akitafsiri.

“Gosu Gosu, fanya upasuaji” alisema Agai.

“Nitafanya lakini nataka kwanza nielezwe mgonjwa ana tatizo gani?” Gosu Gosu aliuliza. Akaelekezwa

sehemu katika paja la yule jamaa anayetakiwa kupasuliwa.

“Pasua hapa!”alisema kwa kufoka kiongozi wa magaidi akionesha mahala panapotakiwa kupasuliwa.

Mahala alipooneshwa Gosu Gosu apasue kulikuwa na kovu.Dhahiri paliwahi kupasuliwa na kushonwa.Haraka haraka yule jamaa akafunguliwa kamba na kulazwa katika meza iliyokuwamo mle chumbani.

“Fanya haraka haraka!”Alisema kiongozi wa magaidi.Gosu Gosu hakujua aanzie wapi.Akakohoa mara tatu kuashiria kuhitaji msaada kutoka SNSA.Daktari wa SNSA aliyekuwa akiwapa maelekezo, akaanza kumpa maelekezo ya kufanya.Gosu Gosu

akaanza upasuaji.Wakati akifanya upasuaji, jamaa aliyekuwa anapasuliwa aliuma meno kwa maumivu makali aliyoyahisi.Gosu Gosu hakumjali,akaendelea na upasuaji.Kiongozi wa magaidi alikuwa amesimama pembeni ya Gosu Gosu,akishuhudia kinachoendelea.Mara Gosu Gosu akahisi kugusa kitu kama nailoni gumu.Akashtuka.

Kiongozi wa magaidi akazungumza kwa kiarabu na yule mtafsiri wake

“Kuna kitu umekigusa?”Aliuliza yule jamaa kwa Kiswahili.

“Kuna kitu nimekigusa hapa!” Alijibu Gosu Gosu.

“Kitoe!”

Mkuu wa magaidi,akawageukia wenzake huku akizungumza kwa Kiarabu.Walionekana kufurahia jambo

Gosu Gosu akavuta kile kitu alichokigusa.Ni kweli ilikuwa nailoni ngumu iliyofungwa kiustadi.Ndani yake kulionekana kuwa na kitu kigumu pia.Kwa kasi ya ajabu, mkuu wa magaidi akainyakua ile nailoni. Akaifuta damu. Akapongezana na wenzake huku wakizungumza kiarabu

“Gosu Gosu,tunafuatilia mazungumzo yao.Wanafurahia kwamba wamekipata kitu walichokuwa wanakitafuta.Ni kitu gani wamekipata?”Ruby aliuliza. Gosu Gosu akakohoa mara mbili kuwapa ishara kwamba hawezi kuzungumza kwa muda

ule.Nailoni ile ikachanwa na ndani yake kulikuwa na diski mweko(flash disc).Yule kiongozi akatoa maelekezo na gaidi mmoja akaitwa haraka akafika akiwa na kompyuta.Akapewa ile diski mweko akaichomeka katika kompyuta yake.

“Kuna nini ndani ya hiyo diski?”Mkuu wao aliuliza. Akaonekana kuwa na shauku kubwa ya kutaka kujua kile kilichomo ndani ya ile diski.Baada ya muda akasema.

“Kuna maelekezo jinsi ya kulipata sanduku jeusi,” alisema yule gaidi aliyekuwa akidurusu taarifa kutoka ndani ya diski.Kiongozi akainamia kompyuta ili aweze kusoma yeye mwenyewe kile kilichomo.Baada ya kuridhika,

akachukua redio ndogo waliyokuwa wakiitumia kwa mawasiliano akaiwasha,akaanza kuwasiliana na mtu mwingine.

“Mungu mkubwa.Tumepata tunachokitaka.Tayari tumepata maelekezo ya mahali sanduku jeusi lilipo,” alisema mkuu wa magaidi kwa lugha ya Kiarabu.Akamueleza mtu aliyekuwa anazungumza naye mahali liliko sanduku jeusi.Baada ya kumaliza kutoa maelekezo,huku furaha isiyo kifani ikitawala usoni mwake, akawageukia akina Gosu Gosu.

“Ashonwe haraka sana huyu mtu jeraha lake muhakikishe anakuwa katika hali nzuri bado tunamuhitaji!”alisema kiongozi yule na kutoka.Ndani ya

chumba walibaki magaidi wawili wakiwa na bunduki ili kuhakikisha akina Gosu Gosu wanamalizia kazi waliyopewa.

Maongezi yote ya kiongozi wa magaidi walioteka ukumbi wa KICC yalisikilizwa na SNSA Dar es Salaam na Arusha kupitia vifaa vya mawasiliano walivyokuwa navyo Gosu Gosu na Agai.SNSA walitumia programu maalum iliyofanya tafsiri ya mazungumzo yale ya magaidi hivyo waliweza kujua kila alichokizungumza japo ilikuwa kwa Kiarabu.

“Wanazungumzia kuhusu sanduku jeusi.Ni kitu gani hicho?”Ruby aliuliza.

“Hatuwezi kujua ni kitu gani hicho hadi pale tutakapokuwa tumelipata hilo

sanduku wanalolizungumzia.Maadamu tumesikia maelekezo yaliyotolewa, basi tunatakiwa kuwahi kabla hawajafika.Tuchukue hilo sanduku halafu tuweke mtego ili watakapofika watakaotumwa kulichukua sanduku hilo tuwatie mikononi mwetu.Hao ndio watakaotupeleka mahala waliko wenzao na waliko watoto waliotekwa," alisema Maurine.

Bila kupoteza muda, zile taarifa za kijiografia walizozipata kutoka kwa magaidi zilifanyiwa kazi na SNSA wakagundua kwamba mahala palipotajwa, ni sehemu iliyo nje kidogo ya jiji la Arusha.SNSA Arusha wakapewa maelekezo ya kufika mahala hapo haraka sana kabla ya magaidi

hawajafika na kuona kilichopo.Makachero sita kutoka SNSA Arusha, wakiwa wamejihami kwa silaha wakaingia katika magari mawili na kuelekea mahala walikoelekezwa na makao makuu.

Ndani ya ukumbi wa KICC,Gosu Gosu na Agai waliendelea na zoezi la kumshona yule jamaa waliyempasua.Hali yake haikuwa nzuri kutokana na kupoteza damu nyingi.Wakati zoezi hilo likiendelea,nyuma yao walikuwa wamesimamiwa na magaidi wawili wenye silaha.Wakizungumza kwa Kiarabu.Gosu Gosu akakohoa mara tatu kama ishara ya kutaka kuzungumza na

SNSA.Ruby kutoka ofisi ya Dar es Salaam akasema.

“Gosu Gosu, ile diski mweko iliyotolewa katika paja la huyo mtu mliyemfanyia upasuaji ilikuwa na maelekezo ya mahala lilipo sanduku jeusi.Tumefuatilia maelekezo hayo na kugundua kwamba ni nje ya jiji la Arusha.Tunaamini ndani ya sanduku hilo jeusi kuna kitu muhimu sana ambacho magaidi wanakitafuta.Tayari makachero kutoka SNSA Arusha wamekwenda huko kuwahi kabla watu watakaotumwa na magaidi hawajafika.Tukifanikiwa kuwakamata watu wao itakuwa hatua kubwa ya kuwafahamu viongozi wao ni akina nani na mahala waliko watoto.Msihofu mko salama na

tutahakikisha tunawaondoa ndani ya ukumbi.Kwa sasa, bado tunawahitaji muendelee kuwepo ndani ya hilo jengo. Je, kuna chochote mmekipata kuhusu Fabrice Kayembe?”Ruby aliuliza .Gosu Gosu akakohoa mara mbili kuasharia kwamba hataweza kuzungumza kwa wakati ule.

Wakati SNSA wakiendelea kuifuatilia *drone* ya pili ambayo ilielekezwa mahala lilipo sanduku jeusi,Ruby akaitumia nafasi hiyo kuwasiliana na Jenerali Pius.

“Ruby, kuna taarifa zozote mmezipata huko?” Rais Pius aliuliza.

“Ndiyo, Mheshimiwa Rais,” alisema Ruby.Akamuelezea Rais kile ambacho walikipata.

“Hongereni sana.Hatua hii mliyoifikia ni kubwa.Huyo mtu ambaye alikuwa na hiyo diski mweko ni nani? Hawajamtambua?” aliuliza Rais Pius

“Hapana.Hawajaweza kumtambua.Ni wazi lengo la magaidi kutaka madaktari lilikuwa si kuwahudumia majeruhi bali kumpasua huyo mtu,” alisema Ruby.

“Sawa,Ruby endeleeni na mipango yenu mtanijulisha kila mtakachokipata” alisema Rais

SNSA Dar es salaam waliyaelekeza macho yao katika runinga iliyokuwa inaonesha picha kutoka katika *drone* ikionesha mahala lilipo sanduku jeusi.Ni sehemu iliyokuwa nje ya jiji la Arusha na kulionekana kama jangwa.Hakukuwa na

miti zaidi ya vichaka vya miiba.Kulionekana nyumba moja ya tembe ambayo ilikuwa na nyufa nyingi na majani yaliota kuizunguka.Pembeni yake kidogo kulikuwa na zizi la mifugo.Lakini lilionekana kuu kuu na muda mrefu hakukuwa na mifugo iliyofungwa ndani ya zizi hilo.

Wakati SNSA wakizipata picha za mahala ambako kulikuwa na sanduku jeusi,ndani ya ukumbi wa KICC,Gosu Gosu na Agai walikaribia kumaliza kushona sehemu waliyoipasua.Yule jamaa waliyempasua alikuwa anagugumia kwa maumivu huku akizungumza lugha ya Kifaransa akisisitiza kurejeshewa diski.Gosu Gosu

akatamani kuzungumza naye lakini wale magaidi walikuwa makini.

“Hii ni nafasi ambayo hatupaswi kuipoteza hata kidogo.Hawa magaidi wawili hawawezi kutushinda lazima wadhibitiwe haraka sana kabla ya wenzao hawajarejea humu.Nataka kumfahamu mtu huyu ni nani,anaonekana ana siri kubwa,” aliwaza Gosu Gosu.Akainua kichwa akamtazama Agai.Macho yao yalipogongana,Agai akaelewa kile ambacho Gosu Gosu alitaka wakifanye.Mmoja wa magaidi alipoona Agai na Gosu Gosu wanatazamana akahisi kuna kitu hakiko sawa.Akawasogelea.

“Kuna nini hapa mbona ha……” alisema gaidi lakini hakumaliza sentensi yake mkono wa Gosu Gosu uliinuliwa kwa kasi ya umeme na kuzamisha mkasi katika koo lake mara tatu. Kilikuwa kitendo cha ghafla,damu zikaruka.Kwa mikono yenye nguvu, akakikamata kichwa cha yule gaidi na kuivunja shingo. Kwa utaratibu na ustadi mkubwa, akamlaza chini.

Wakati akimlaza chini yule gaidi,Agai naye alikuwa amemaliza kazi ya kumkata pumzi yule gaidi mwingine. Kilikuwa ni kitendo cha haraka mno ambacho wale magaidi hawakuwa wamekitegemea.Hawakujua kama madaktari wale walikuwa watu hatari.Upesi wakazinyakua silaha za

wale magaidi.Wakatulia kwa sekunde kadhaa. Wakamakinika zaidi kusikiliza kama kuna watu nje ya kile chumba.Kimya kilitawala. Hakukusikika hatua zozote za mtu.

Gosu Gosu akamfuata yule jamaa waliyempasua paja. Hakuwa na nguvu.Alikuwa amefumba macho. Akamtikisa kisha akamsemesha kwa lugha ya Kifaransa.

“Wewe ni nani? Niambie tafadhali tuko hapa kuwaokoa,” alisema Gosu Gosu.Yule jamaa akafumbua jicho la kulia.Jicho la kushoto lilikuwa limevimba.Halikuweza kufunguka kabisa.

“Wewe ni nani?” Gosu Gosu aliuliza huku akimchungulia.

Jamaa akajitikisa kidogo. Akaonekana kutafuta maneno.

“Fa..fa.” akanyamaza. Alionekana kabisa pumzi zake hazina ushirikiano. Akakohoa kidogo.

“Fabrice Kayembe,” hatimaye alisema yule jamaa kwa sauti ya chini sana.

“Rudia tena unaitwa nani?” Gosu Gosu alihimiza.

“Fabrice Kayembe,” alitamka tena yule jamaa.Gosu Gosu akalazimika kumtazama mara mbili kama kweli ni yeye.Sura ya Fabrice Kayembe ambayo aliiona katika picha na ile ya mtu aliyekuwa mbele yake zilikuwa tofauti.Alikuwa ameumizwa sana.

“SNSA mnanipata?” Gosu Gosu aliuliza.

“Ndiyo tunakupata, Gosu Gosu.Tumesikia purukushani hapo.Nini kilitokea?”Ruby aliuliza.

“Mambo yameiva.Tumeamua kuchukua hatua.Tayari tumewaua magaidi wawili waliobaki kutulinda ndani ya hiki chumba.Ni nafasi pekee tumeipata, tumeitumia ipasavyo,”alisema Gosu Gosu.

“Ahsanteni kwa kazi nzuri.Hatukutegemea kama ingekuwa mapema namna hii.Kwa kuwa mambo yameanza humo ndani, tunapaswa kuanza mikakati ya kutuma vikosi kuingia humo.Tunamjulisha Rais ili aweze kuwajulisha viongozi wa vyombo

vya ulinzi na usalama.Gosu Gosu, ili vikosi viweze kuingia, tunawategemea ninyi kutupa taarifa namna magaidi walivyojipanga.” alisema Ruby.

“Tutafanya hivyo,Ruby.Lakini kuna kitu kingine nataka kuwajulisha.Mtu ambaye tumempasua paja na kutoa diski mweko ndiye Fabrice Kayembe.”

“What? Fabrice? Umejuaje?”Ruby alimaka.

“Nimemwuliza yeye ni nani.Akakiri kuwa yeye ni Fabrice Kayembe.”

“Mungu wangu!”Ruby alisema.Yamkini mshangao ulimchapa vyema mtimani.

“Ruby,ile taarifa kuhusu Fabrice Kayembe kuwa muhimu kwa magaidi ni ya kweli.Inaonekana magaidi walimtesa

sana huyu Fabrice.Wakafahamu kuhusu uwepo wa ile diski katika paja lake ndipo wakamuomba Rais Pius atume madaktari kwa ajili ya kutoa huduma ya kwanza kwa mateka.Lakini lengo lao kubwa lilikuwa kumpasua Fabrice, ili waipate diski,”alisema Gosu Gosu.

“Gosu Gosu hakikisheni mnamlinda Fabrice kwa namna yoyote ile.Msikubali akauawa na magaidi kutokana na umuhimu wake.Wakati huo huo tunasubiri taarifa kutoka kwenu mtueleze namna vikosi vitakavyoweza kuingia ndani,” alisema Ruby.

Gosu Gosu akazungumza na Agai.Wakakubaliana Agai aendelee kuangalia usalama wa eneo

walilolidhibiti huku yeye akiendelea kumuhoji Fabrice Kayembe.

“Fabrice unanisikia?” Gosu Gosu aliuliza.

“Ninakusikia!” Fabrice alijibu kwa sauti dhaifu huku akionekana kuwa katika maumivu makali.

“Nahitaji kuthibitisha kama kweli wewe ndiye Fabrice Kayembe.Nitakuuliza maswali machache.Nataka kujua unafanya kazi gani?” Gosu Gosu aliuliza.

“Mimi ni profesa katika chuo kikuu cha sayansi cha Paris,” alijibu Fabrice kwa sauti dhaifu.

“Unafahamu hapa uko wapi?”

“Niko Tanzania kwa ajili ya mkutano wa Afrika Asili Yangu” Fabrice

alijibu kwa tabu mno,hakuwa na nguvu tena.Akashindwa hata kufumbua jicho.

“Fabrice! Fabrice!” Gosu Gosu aliita mfululizo lakini Fabrice hakuitika.

“SNSA, hali ya Fabrice si nzuri kabisa.Amepoteza damu nyingi. Hatupaswi kumpoteza mtu huyu ni muhimu sana.Tunahitaji kumtoa humu akiwa mzima,” alisema Gosu Gosu akihema kwa kasi.

“Gosu Gosu, tayari tumezungumza na Rais.Vikosi viko tayari tunasubiri muongozo kutoka kwenu .Tunahitaji kujua kuna magaidi wangapi na namna walivyokaa.*Can you do something please*?”Ruby alisema kwa umakini zaidi.

“Ngoja tuone nini tutafanya halafu nitakujulisha,” Gosu Gosu alijibu.

7

Magari mawili kutoka SNSA Arusha yaliwasili mahala ambako maelekezo yalionesha kulikuwa na sanduku jeusi.Kama ilivyoonekana kupitia *drone*,mahala pale palionekana hapajakaliwa na watu kwa muda mrefu.Walisimamisha magari katika

vichaka vya miiba umbali wa mita kadhaa kabla ya kuifikia ile nyumba.Kwa kutumia kiona mbali,wakaichuguzakiustadi kabisa.Makachero wanne wakatoka ndani ya kile kichaka upesi upesi wakaelekea katika ile nyumba wakiwa katika tahadhari kubwa.

Walipoikaribia, walihisi harufu kali ya uozo wa kitu. Wakazidi kuisogelea. Walipoifikia harufu ile ikawa kali zaidi.Nzi walionekana wakitoka na kuingia kupitia matobo ya ile nyumba.Mlango dhaifu ulioliwa na mchwa ukasukumwa.Ukafunguka bila tabu. Wakaingia ndani ambako walipokelewa na nzi wengi.

Bila kujali harufu au nzi, wakaanza kutafuta kile kilichowapeleka mahala pale yaani sanduku jeusi.Sebuleni hakukuwa na kitu chochote. Oscar aliyekuwa ametangulia mbele, akalisogeza pazia kuukuu.Wakaingia chumbani ambako nzi walikuwa wengi zaidi kuliko walikotoka.Japo kulikuwa na matobo mengi yaliyopenyeza mwanga, lakini iliwalazimu kuwasha tochi na kumulika. Hamaki ikawashika.Walishuhudia mwili wa mtu akiwa amelala katika kitanda cha kamba.Umeharibika vibaya mno na hakuweza kutambulika. Nzi walipita kila tundu la mwili huo. Kwa hakika walifurahia chakula chao.

Pembeni ya kitanda kulikuwa na mkoba mdogo mweusi.Wakaufungua.Wakakuta kuna nyaraka za kusafiria,pakiti nane za biskuti,pakiti mbili za sigara,kiberiti na chupa ya maji ya kunywa.Ghafla wakasikia kama kitu kinajivuta chini ya kitanda.Wakarudi nyuma nukta chache. Wakamulika tochi wakakutana na joka kubwa likijikunjua.

Hawakuwa na muda wa kulisubiri joka lile mpaka lijikunjue, kwa kutumia bunduki iliyofungwa kiwambo cha kuzuia sauti, wakalimiminia risasi.Wakasambaratisha kichwa chake.Kazi ikaendelea, wakakisogeza kitanda na kuliondoa joka lile. Chini yake, wakaliona shimo ambalo ndani

kulikuwa na sanduku dogo jeusi. Wakalitoa kisha wakawajulisha SNSA kwamba wamekipata kile kisanduku cheusi.Waliondoka na kurejea katika magari yao wakalihifadhi lile sanduku halafu wakarejea kujificha karibu na ile nyumba wakiwasubiri magaidi watakaotumwa kwenda kuchukua kisanduku kile.

“Gosu Gosu,tayari makachero wa SNSA wamekipata kisanduku cheusi. Sasa tunawasubiri ninyi mtupe taarifa ili tuweze kutuma vikosi,” alisema Ruby.

Gosu Gosu na Agai waliwavua vitambaa wale magaidi waliowaua.Wakazifunika sura zao kama walivyofanya magaidi.Wakavaa pia zile fulana zao za mabomu.

“Sasa tunaonekana kama wao licha ya vitambaa hivi kuchafuka damu” alisema Gosu Gosu aliyekuwa akikiweka sawa kivazi cha kigaidi.

“Gosu Gosu,hatuwezi kutoka wote humu ndani.Mimi ninakwenda kufanya uchunguzi,wewe utaendelea kumlinda Fabrice,” alisema Agai.

“Una hakika,Agai?”

“Ndiyo, Gosu Gosu.Fabrice ni muhimu sana kwetu hivyo lazima tumlinde kwa namna yoyote ile,” alisemaAgai.

“Sawa. Kila la heri,” alisema Gosu Gosu.Agai akaufungua mlango, akatoka.Hakukuwa na mtu yeyote karibu na kile chumba.Akiwa amerandana kimavazi na magaidi, alitembea kwa

tahadhari kubwa.Jengo lilikuwa kimya.Kwa mbali aliweza kusikia sauti za magaidi wakizungumza.Alivipita vyumba kadhaa.Akakukutana na vidato vya ngazi.Ukutani kulikuwa na kibao kikimuonesha alikuwa ghorofa ya tano.

“Gosu Gosu, tuko ghorofa ya tano.Ninapanda juu!” alisema Agai akipanda ghorofa ya sita.

“Kwa mbali ninawaona magaidi wawili wakiwa nje ya chumba katika ghorofa ya sita.Ninaelekea ghorofa ya saba,” alisema Agai akipanda juu zaidi. Hakukutana na gaidi yeyote yule.

“Ghorofa ya saba kuko kimya. Sioni gaidi yeyote,” alisema Agai.Akapanda vidato vya ngazi haraka haraka kuelekea ghorofa ya nane.Pindi alipotokea katika

ghorofa ya nane ambayo ndiyo ya mwisho, akakutana na gaidi mmoja akitokea katika sehemu ya juu kabisa ya jengo.Alipomuona Agai akiwa na nguo iliyochafuka damu, akasimama.Akamsemesha Agai kwa lugha ya Kiarabu.Agai hakufahamu Kiarabu. Akajifanya anakohoa mfululizo halafu akapiga kifua ishara hawezi kuzungumza. Kwamba anaumwa kifua.Huku akikohoa, akafuata njia ambayo alitokea yule gaidi ambaye bado alisimama akimshangaa.

“Gosu Gosu, tuna tatizo.Nimekutana na gaidi mmoja ambaye ameonyesha wasi wasi.Ninaeleeka juu kabisa kwenye paa,” alisema Agai.Akapanda ngazi na kuingia katika chumba chenye mlango

wa kutokea sehemu ya paa.Akachungulia akawaona magaidi watatu.Wawili walikuwa na bunduki za udunguaji na mmoja akiwa amebeba kombora la RPG.

“Ninawaona magaidi watatu upande wa juu,” alisema Agai.

“Unaweza ukafanya chochote?” Gosu Gosu aliuliza.Kabla ya kujibu swali la Gosu Gosu, Agai akasikia hatua za mtu akipanda ngazi kuelekea kule juu.Mlango ukafunguliwa. Alikuwa yule gaidi aliyepishana naye muda mfupi uliopita ambaye aliamua kurejea juu.Agai akakaa chini na kujifanya amezidiwa.Akaanza kukohoa mfululizo .

Yule gaidi akamfuata na kumsemesha Kiarabu lengo likiwa kutaka kujua ni kitu gani

kilichomsibu.Kufumba na kufumbua Agai akaruka kama kima,akamtandika kichwa kizito.Kabla gaidi hajakaa sawa,akapigwa ngumi mbili mfululizo.Akajibamiza ukutani.Agai akamkaba kabali matata sana. Gaidi akapaparika kujinasua katika kabali ile, lakini mikono ya Agai ilikuwa na nguvu na migumu mithili ya chuma.Taratibu gaidi akapoteza pumzi.Akafa kimya kimya.Agai akamvuta hadi katika chumba kilichokuwa na mipira na vifaa vya kuzimia moto.Akavua mavazi aliyoyavaa yaliyokuwa yamechafuka damu, akavaa ya yule gaidi aliyemuua.

“Gosu Gosu,nimemuondoa gaidi mmoja” alisema Agai.

“Kazi nzuri,Agai.Je, unaweza ukawaondoa hao wengine watatu waliobaki ili tudhibiti sehemu ya juu?” Gosu Gosu aliuliza.Agai akatoka katika kile chumba. Akapanda ngazi zaidi za kutokea upande wa juu. Akapiga mbinja na kuwafanyia ishara wale magaidi kwamba wanahitajika wawili.Waliamini ni mwenzao anawaita.Wakamuacha mmoja aliyekuwa na bunduki kubwa ya udunguaji wakamfuata Agai.Walishuka ngazi haraka haraka huku wakizungumza.Ghafla bila kutegemea akajitokeza Agai akiwa na shoka lenye rangi nyekundu mkononi.

Kwa nguvu na kasi kubwa,shoka likatua katika kichwa cha gaidi aliyekuwa ametangulia mbele.Mwenzake

aliyebaki nyuma akabonyea chini akikwepa shoka lile.Kabla hajainuka,Agai akachomoa kisu kikali alichokuwa amekifutika kiunoni.Kwa kasi ya ajabu, mkono wake wa kulia ukatua katika shingo ya yule gaidi ikabaki inaning'inia.

Haraka haraka,akawavuta na kuwaficha katika chumba alimomficha gaidi yule wa mwanzo.

"Nimewaondoa wawili bado mmoja," alisema Agai.

"Maliza wote upande huo wa juu ili watu wetu watumie upande huo kuingia ndani ya ukumbi," alisema Gosu Gosu.Agai akajitokeza tena upande wa juu. Akapiga Mbinja na kumuita yule jamaa aliyebaki.Jamaa alitembea haraka

haraka kuelekea ndani.Mara tu alipoingia ndani ya kile chumba chenye ngazi za kushukia chini,Agai akamvuta. Akamgeuza kwa haraka na kukipitisha kisu kikali katika shingo ya gaidi. Akaanguka chini huku damu zikimwagika kama bomba.

“SNSA, upande wa juu nimemaliza kazi. Hakuna gaidi yeyote upande huu”

“Kazi nzuri,Agai.Sasa tunatakiwa kumtoa Fabrice humu ndani na kumpeleka katika paa kwa ajili ya kumuondoa kwa haraka mahala hapa,” alisema Gosu Gosu.

“Niliona magaidi wawili nje ya chumba kimoja ghorofa ya sita.Hatuwezi kumpitisha Fabrice hapo bila kuonekana.Ninatakiwa kuwaondoa

kwanza wale magaidi pale," alisema Agai.

"Are you sure?" Gosu Gosu aliuliza.

"Lazima nifike hapo, nifahamu kuna nini ndani ya kile chumba na niwaondoe wale magaidi," alisema Agai kwa msisitizo.Akaichukua bunduki ya udunguaji ya mmoja wa wale magaidi aliowaua.Ilikuwa imefungwa kiwambo cha kuzuia sauti.Akashuka ngazi kuelekea ghorofa ya sita.Akachungulia na kuwaona wale magaidi wawili wakiwa bado wamesimama nje ya chumba kimoja.Kwa kutumia bunduki ya udunguaji, akamlenga wa kwanza.Akaachia bunduki yake akaanguka chini.Mwenzake akashtuka.Akageuka naye akajikuta

akifumuliwa kichwa kwa risasi na kwenda chini mithili ya kiroba cha nazi.Agai akatoka sehemu alikojificha.Akatembea kwa kasi kuelekea katika kile chumba walichokuwa wamesimama wale magaidi wawili.

Kishindo cha muanguko wa wale magaidi wawili kikazua taharuki kwa waliobaki ndani ya chumba. Mlango ukafunguliwa. Akatoka gaidi mmoja kuchungulia kuna nini.Kidole cha Agai kilikuwa chepesi sana.Akaizinga bunduki kwa ufundi mkubwa , risasi ikatua kichwani kwa gaidi akaanguka katikati ya mlango.

Agai akasogea karibu na kile chumba.Akachungulia ndani pengine

kulikuwa na mtu mwingine. Kulikuwa tupu. Hakukuwa na mtu mwingine.Akawavuta kwa ndani wale magaidi aliowaua. Kitendo kilichopelekea kutambua kwamba mmoja wa wale aliowaua ni mkuu wa kikosi cha magaidi.

“Gosu Gosu nimewaondoa wale magaidi wawili pamoja na mkuu wao aliyekuwa anatusimamia wakati tukimpasua Fabrice,” Agai alihitimisha.

“Agai, huu si wakati wa mzaha!” Gosu Gosu alisema akiwa haamini kile alichoelezwa na Agai.

“Ninasema ukweli Gosu Gosu.Nimewamaliza wale jamaa wawili pamoja na kiongozi wao,” alisema Agai. Akatoa tabasamu. Akiwa humo

chumbani, akaona meza ina vitu vingi . Agai akaenda mezani ambako kulikuwa na kompyuta mbili.Zote zilikuwa zikionyesha picha kutoka katika kamera mbali mbali zilizokuwamo ndani ya lile jengo.

“Kuna kompyuta mbili humu ndani ya hiki chumba. Zote zinaonyesha picha kutoka katika kamera mbali mbali zilizomo ndani ya hili jengo,” alisema Agai.

“Ninamtoa Fabrice Kayembe humu ndani na kumpandisha juu.SNSA,huu ni wakati wa kutuma vikosi tayari tunalidhibiti eneo la juu. Vile vile tunaweza kutazama kamera zote za ukumbi.Agai, mpekue huyo mkubwa wao tuipate ile diski ambayo aliichukua

kutoka kwa Fabrice Kayembe," alisema Gosu Gosu,akambeba Fabrice na kumuweka begani.Akausogelea mlango, akaufungua kwa umakini mkubwa,akaanza kupanda vidato vya ngazi za kuelekea juu huku akiwa na bunduki yake mkononi.

Njiani wakati akipanda kuelekea katika paa,akakutana na damu iliyotapakaa chini. Akatabasamu kisha akaendelea na safari akijisemea.

"Nashukuru tumepata nguvu mpya katika timu yeu.Huyu Agai ni mtu anayetufaa sana.Nimependa ufanyaji kazi wake."

"Agai, tunahitaji kuzirudisha kamera zote katika mfumo wetu ili tuweze kuona kila kinachoendelea humo ndani.Hii

itawapa urahisi vikosi vya makomando wetu wanaokuja kuwakomboa mateka.Nitakupa malekezo ya namna ya kufanya,”Ruby alimwambia Agai,akaanza kumpa maelekezo namna ya kufanya ili mfumo wa usalama wa jengo lile urudishwe katika hali yake ya kawaida na kuwapa SNSA fursa ya kufuatilia kamera zote kujua kinachoendelea ndani ya jengo hilo.

****

Gari aina ya Landcruiser ambalo hutumiwa kwa shughuli za utalii, lilionekana kupitia *drone* ya SNSA likielekea katika nyumba iliyohifadhiwa sanduku jeusi.Taarifa zikawafikia

makachero wa SNSA waliokuwa wamejificha karibu na ile nyumba ili wajiandae.

Gari likaegeshwa mita kadhaa kutoka ile nyumba. Wakashuka watu wanne.Wawili wakiwa wamejifunika mashuka mekundu ambayo hupenda kutumiwa sana na kabila la Maasai.Ndani ya mashuka walikuwa wameficha bunduki.Wakaizunguka nyumba nukta hadi nukta.Wakaikagua.

Wakaonekana wakijadiliana jambo baada ya kuona alama za viatu.Waliendelea kukagua alama za viatu mwishowe wakaamua kuingia ndani.Wawili ambao hawakuwa na silaha yoyote,wakausukuma mlango.Wakaingia

ndani.Wawili wenye bunduki wakabaki nje wakilinda.

Bunduki za udunguaji za makachero wa SNSA ziliwekwa tayari .Amri ikatolewa.Zikaachiwa risasi wale watu wawili waliokuwa wamebaki nje ya nyumba wakilinda, wakaanguka chini na kufa pale pale .

Salamu ya kishindo cha muanguko ikawafikia waliokuwa ndani. Mmoja akatoka kuchungulia nje kujua kilichotokea, akapigwa risasi ya kichwa.Akaangukia alikotoka ndani.Kutoka katika gari wakatoka watu wengine watatu wakiwa na bunduki.Kiwewe kimewaingia. Wakatimua mbio kuelekea katika ile nyumba bunduki mkononi ili kuwapa

msaada wenzao lakini Makachero wa SNSA walikuwa makini sana.Wakaibuka wakaswashambulia kwa risasi za mbali wale jamaa,wote wakalamba ardhi.Haraka haraka makacherowa SNSA, wakakimbia hadi katika ile nyumba. Gaidi ambaye alibaki ndani akitafuta sanduku jeusi aliposikia vishindo vya watu wakija upande wake,akachungulia kupitia tundu.Akawaona watu asiowafahamu wakiwa na bunduki wakija upande wake. Akatoka upesi ili akimbie.Alichelewa kwani tayari makachero wa SNSA walikuwa mbele yake.Akawekwa chini ya ulinzi.Wakawapekua wale magaidi wengine hawakuwakuta na kitu.Zaidi

walikuwa na pakiti za sigara.Walilikagua gari lao wakakuta lina nembo ya kampuni ya kitalii ya Swala Safari.Wakawajulisha SNSA pamoja na namba za lile gari kisha wakamuingiza yule gaidi waliyemkamata katika gari lao, wakaondoka naye. Gari walilokuja nalo magaidi likaendeshwa na mmoja wa makachero wa SNSA.Wakiwa njiani, wakajulishwa kwamba hakuna kampuni yoyote ya kitalii iliyosajiliwa kwa jina la Swala Safari. Kama haitoshi, hata namba za usajili za gari lile la magaidi ni za bandia.

8

Helkopta tatu za makomando kutoka jeshi la wananchi wa Tanzania ziliwasili katika paa la jengo la KICC.Wakaanza kushuka kwa kamba.Wakakutana na Gosu Gosu aliyekuwa eneo la juu akiwasubiri. Mfumo wote wa kamera tayari ulikuwa chini ya SNSA hivyo waliweza kuwaongoza makomando kuingia ndani ya ukumbi bila taabu.

Gosu Gosu akamuingiza Fabrice katika moja ya helkopta ya makomando.Wakaondoka naye ili kumuwahisha hospitali hali yake haikuwa nzuri kabisa.Gosu Gosu akarudi ndani kumfuata Agai .

Milio ya helkopta iliwashtua magaidi.Gaidi mmoja akajaribu kuwasiliana na mkuu wao kujua

kinachoendelea.Kila alivyojitahidi kuita kupitia redio zao maalum za mawasiliano hakupata majibu.Akawafuata wenzake kwa lengo na kujaribu kuwasiliana na mkuu wao lakini walipojaribu hawakumpata.Gaidi mmoja akatoka kwa lengo la kumfuata kiongozi wao.Hakufika mbali.Alitandikwa risasi ya kichwa kutoka kwa moja ya bunduki ya makomando waliovamia eneo la ukumbi.Kazi ilianza kutoka kwa makomando wa Tanzania.

“Agai, umempekua vizuri huyu kiongozi wao na kuipata ile diski mweko?” Gosu Gosu aliuliza.

“Sijafanikiwa kuipata.Wala sifahamu imefichwa wapi,” Agai alijibu.

“Tulikuwemo ndani ya chumba kile na tukamuona akiiweka ile diski mfukoni akaondoka.Tunatakiwa kuwapekua magaidi wote.Inawezekana kuna mmoja wao amepewa,” Gosu Gosu alisema. Kazi ya kuwapekua magaidi waliowaua ilianza upya. Hata hivyo, hawakupata chochote.

Risasi zilirindima ndani ya jengo.Wakati makomando wakiendelea kupambana na magaidi,vikosi vingine vya jeshi viliingia ndani ya jengo kupitia geti kuu. Lengo likiwa kuongeza nguvu.

****

Iliwachukua dakika thelathini kwa vikosi vya jeshi kuukomboa ukumbi wa

KICC uliokuwa umeshikiliwa na magaidi.Magaidi wote waliokuwa wameuteka ukumbi ule waliuawa na mateka kukombolewa.Ni komando mmoja tu ndiye aliyepoteza maisha wakati akimdhibiti gaidi aliyetaka kulipua bomu alilokuwa amelivaa mwilini.Kwa umahiri mkubwa, komando huyo alimdhibiti gaidi huyo na kuruka naye nje.

Magaidi wote waliouawa wakakusanywa sehemu moja.Watu wote waliokuwa wanashikiliwa mateka wakatolewa nje ya ukumbi na kuingizwa katika magari kwa ajili ya kupelekwa katika hospitali ya rufaa ya mkoa wa Arusha Mount Meru.

Wakati vikosi vya jeshi vikiendelea na zoezi la kutegua mabomu yaliyokuwa yametegwa na magaidi ndani ya ukumbi ule,Gosu Gosu na Agai waliendelea kuwapekua magaidi wote waliokuwa wameuawa.Pamoja na juhudi zote hizo, hawakuweza kuipata ile diski iliyotolewa katika paja la Fabrice.

“Ruby, hapa kazi imemalizika,magaidi wote wameuawa,mateka wote wamekombolewa lakini kuna tatizo.Ile diski ambayo alikuwa nayo kiongozi wa magaidi, haionekani.Tumewapekua magaidi wote hatujaipata,” alisema Gosu Gosu huku akionekana ana jambo linamsumbua kichwani.

“Ruby, nina wazo,” Gosu Gosu aliongeza

“Tukiwa ndani ya kile chumba,yule mkuu wa magaidi aliondoka na ile diski.Lazima imefichwa mahali ndani ya hili jengo au kuna mtu amepewa.Naomba ufuatilie kumbukumbu za kamera ili tujue kama kuna mtu yeyote alitoka nayo.Pengine kuna njia ya dharura.”alisema Gosu Gosu

“Sawa, Gosu Gosu.Ninalifuatilia hilo.Hongereni sana kwa kazi nzuri mliyoifanya.Hakika bila ujasiri wenu ninyi watu wawili, zoezi la kuwakomboa mateka lingekuwa gumu sana.Rais amenituma nifikishe salamu zake

kwenu.Anawashukuru sana kwa hiki mlichokifanya," alisema Ruby.

"Ahsante,Ruby.Sisi tunaondoka hapa tunaelekea hospitali ya rufaa ya mkoa kufuatilia hali ya Fabrice.Alipoondolewa hapa hali yake ilikuwa mbaya sana.Tukitoka hapo tutakwenda katika ofisi za SNSA kumuhoji yule gaidi aliyekamatwa kule katika sanduku jeusi." alisema Gosu Gosu kisha wakaingia katika moja ya magari yaliyokuwapo mahali pale.Wakapelekwa katika hospitali ya Mount Meru.

****

Katika hospitali ya rufaa ya mkoa wa Arusha ya Mount Meru,Fabrice Kayembe aliendelea kupatiwa matibabu.Bado hakuwa na fahamu.Madaktari waliendelea na jitihada za kuhakikisha wanaokoa maisha yake.Gosu Gosu na Agai wakaelekeza makachero wawili kutoka SNSA wabaki pale hospitali kuhakikisha Fabrice anakuwa salama.Wao wakaondoka kuelekea katika ofisi za SNSA Arusha kumuhoji gaidi aliyekamatwa wakati wa zoezi la kulipata sanduku jeusi.

Hawakuwa na muda wa kupoteza,Leon mkuu wa SNSA Arusha akawapeleka akina Gosu Gosu katika chumba alichofungwa gaidi

aliyekamatwa.Gosu Gosu akamtazama gaidi halafu akavuta kiti akaketi.

“Jina lako nani?” Gosu Gosu alimwuliza gaidi. Hakujibu kitu chochote kile. Zaidi alimtazama Gosu Gosu kwa dharau

“Nakuuliza jina lako nani?” Aliongeza Gosu Gosu.Yule gaidi akamtazama Gosu Gosu kisha akainamisha kichwa chini.Gosu Gosu akaghadhibika.Akauendea ubao mfupi uliokuwa chini na kumtandika nao usoni.Akaanguka chini pamoja na kiti alichokuwa amefungwa.Agai akamuinua.Akamtandika ngumi nzito akaanza kutokwa damu puani na mdomoni.

Hakuwajali.

“Jina lako nani?” Gosu Gosu aliuliza tena.Sura yake haikuwa na masihara.

“Nakuuliza jina lako nani?”

Gaidi aliendelea kuwa kimya.Gosu Gosu akainuka.Akaenda katika meza ambayo kulipangwa vifaa kwa ajili ya kutesea.Akachukua koleo dogo. Akamwambia Agai amvue nguo gaidi.Agai akamvua nguo.Gosu Gosu akamsogelea gaidi.Bila huruma akambana gaidi korodani kwa kutumia lile koleo.Gaidi alikumbana na maumivu makali yasiyomithilika.Akapiga kelele kwa maumivu makali aliyoyapata.

“Jina lako nani?” Gosu Gosu aliuliza

“Khalid Mustapha!”

“Khalid sitaki kujua kama umetaja jina la kweli au la. Hayo yatakuja

baadaye lakini kwa sasa kuna kitu kimoja tu, ambacho ninahitaji kukifahamu.Wako wapi watoto mliowateka?” Gosu Gosu aliuliza.

“Sifahamu waliko!”

“Narudia tena. Wako wapi watoto mliowateka?”

“Sifahamu waliko.Ningewaeleza kama ningefahamu.Mimi ni mtaalamu wa kompyuta ninafanya kazi…” Khalid hakumaliza sentensi yake akanaswa kofi zito lililotua shavuni kwake.

“Sitaki hadithi zako. Wako wapi watoto?” Gosu Gosu aliuliza tena.

“Sifahamu waliko!” alisema Khalid.Gosu Gosu akachukua kifaa cha kukatia vitu vigumu akamfuata

Khalid.Akakiwasha.Kikaanza kuzunguka.

“Nakuuliza kwa mara nyingine, wako wapi watoto?” Gosu Gosu alisema huku kile chombo kikizunguka.

“Sifah….” Alisema Khalid kabla hajamaliza alichotaka kukisema Gosu Gosu, akakipeleka kifaa kile katika bega la kulia.Akakata sehemu kubwa ya eneo hilo la begani. Khalid akalia kwa maumivu makali.Gosu Gosu akakiweka chini kile kifaa.Akachukua chupa iliyokuwa na dawa. Akaimimina katika sehemu aliyoikata.Khalid akapiga kelele kubwa.Alihisi mwili wote unaungua moto baada ya kumwagiwa dawa mahala penye jeraha.

“Wako wapi watoto mliowateka? Gosu Gosu aliuliza tena. Khalid bado aliendelea kulia akijinyonga nyonga kwa maumivu makali aliyoyapata.

“Wako wapi watoto? Gosu Gosu alifoka.Akamshika Khalid shingoni.

“Khalid,mateso hayatapungua bali yataongezeka kadiri unavyozidi kuwa kiburi.Nataka uniambie wako wapi watoto mnaowashikilia mateka?Nielekeze waliko watoto nikutoe katika mateso makali ambayo utaendelea kuyapata.”

“Sifahamu!”alisema Khalid huku akitetemeka baada ya kumuona Gosu Gosu ameshika kisu kikubwa kikali.

“Ni nani alikutuma uende katika ile nyumba ulikokamatwa?” Gosu Gosu

aliendeleza maswali yake. Khalid akawa kimya.

“Nakuuliza tena ni nani aliyekutuma uende katika nyumba ambako ulikamatwa?”Gosu Gosu aliongeza. Lakini bado Khalid aliendelea kuwa kimya,hali ambayo ilimghadhibisha Gosu Gosu.

“Khalid, bado hujanifahamu vizuri.Mimi ni mkatili kuliko wakatili unaowafahamu.Ili kukuonesha ukatili wangu, nitakuondoa uume wako na…” alisema Gosu Gosu akinyoosha mkono uliokuwa na kisu kikali. Khalid akapiga kelele.

“Usinikate tafadhali. Nitaongea!”alisema Khalid.

“Sema haraka! Ni nani alikutuma katika ile nyumba? Ulitumwa nini na watoto wako wapi?” Gosu Gosu aliunguruma kama simba.

“Nilitumwa na Sultan Jabir!”

“Sultan Jabir?”

“Ndiyo!”

“Ni nani huyo?”

“Ni mfanya biashara mkubwa wa madini hapa Arusha.Mimi ni mfanyakazi katika kampuni yake inayojishughulisha na kutengeneza program mbalimbali za kompyuta,” alisema Khalid akitetemeka.

“Alikutuma nini katika ile nyumba?”

“Nilitumwa kwenda kuchukua sanduku jeusi. Akanipa watu niende nao ambao siwafahamu. Tukaenda katika ile

nyumba na ndipo nikakamatwa.”alijibu Khalid

“Alikueleza sanduku hilo jeusi lina kazi gani?”

“Hapana.Hakunieleza.Alitaka nikalichukue kisha tuje kulifanyia kazi,” alijibu Khalid.

“Watoto wako wapi mnaowashikilia?” Gosu Gosu alirudia swali lake la msingi. Khalid akabaki kimya kwa mara nyingine tena. Gosu Gosu hakuchoka.

“Nakuuliza watoto wako wapi?”

Khalid bado akaendelea kukaa kimya.

Gosu Gosu akamtandika ngumi. Kama haitoshi, akaukamata uume wake barabara akauinua mkono wake ulioshika

kisu kikali juu tayari kuukatia mbali. Khalid akapiga kelele .

“Nyumbani kwa Sultan!”

“Nyumbani kwa Sultan!”

“Nyumbani kwa Sultan!”

“Sultan ndiye kiongozi wenu?” Gosu Gosu alihoji. Khalid akawa kimya.

“Nakuuliza tena Sultan ndiye kiongozi wenu?” Gosu Gosu aliuliza.Khalid akainua kichwa juu. Akamtazama Gosu Gosu kwa jicho la huruma. Akitweta, akasema.

“Abdulkareem Fadil Ghedi ndiye kiongozi wa magaidi.”

Gosu Gosu ambaye tayari alikwisha kitoa kifaa cha mawasiliano sikioni, akatoka ndani ya kile chumba na kwenda katika chumba cha mawasiliano.Akapiga

simu makao makuu ya SNSA Dar es Salaam.

“Watoto wako katika nyumba ya Sultan Jabir.Mfanya biashara wa madini hapa Arusha.Narudia tena watoto wako katika nyumba ya Sultan Jabir mfanya biashara wa madini hapa Arusha. Hii ni kwa mujibu wa gaidi ambaye tunamshikilia hapa SNSA Arusha.Kiongozi mkuu wa magaidi hao anaitwa Abdulkhareem Fadil Ghedi.” Gosu Gosu alihitimisha.

“Kazi nzuri Gosu Gosu.Tunawasiliana na mkuu wa operesheni hiyo ambaye ni mkuu wa jeshi la polisi nchini ili aweze kutuma vikosi mahala hapo haraka sana kwenda

kuwakomboa watoto waliotekwa," alisema Maurine Kyaso.

"Sawa. Mtatujulisha kama watafanikiwa kuwapata watoto hao na kuwakamata viongozi wa magaidi," alisema Gosu Gosu.

9

Rais Pius aliendelea kupokea salamu za pongezi kutoka kwa watu mbali mbali na marais wa nchi nyingine hasa za Afrika kufuatia kufanikiwa kuwadhibiti magaidi na kuwakomboa mateka

waliokuwa wanashikiliwa katika ukumbi wa mikutano wa kimataifa wa KICC.Akiwa simuni akizungumza na mmoja wa watu waliompigia,katika simu yake ya mkononi ikaingia simu ya mkuu wa jeshi la polisi.Akalazimika kukata ile simu na kupokea simu ya IGP.

“IGP!” alisema Rais Pius.

“Mheshimiwa Rais,nimekupigia ili kukupa taarifa kwamba tumefanyia kazi taarifa tulizozipata kutoka SNSA.Tumevamia makazi ya Sultan Jabir yaliyoko nje ya jiji la Arusha, eneo la Tengeru. Kwa bahati mbaya tumechelewa,hatujakuta mtu yeyote mahala hapo. Lakini tumefanikiwa kukuta miili ya wasichana wawili waliochinjwa asubuhi na magaidi ikiwa

imeachwa. Inaonekana ni kweli wasichana wale walikuwepo mahala hapo, lakini wameondolewa.Hatujui wamepelekwa wapi.Tayari msako wa kuwatafuta unaendelea.Njia zote za kuingia na kutoka jijini Arusha zimefungwa kwa sasa.”alisema mkuu wa jeshi la polisi

“Kazi nzuri.Fikisha salamu zangu kwa vijana wote.Ninataka kazi iendelee usiku kucha hakuna kupumzika na hadi kufika asubuhi, basi muwe mnafahamu mahala walipo magaidi na wasichana waliotekwa nyara.Nataka uongeze askari mara mbili ya sasa.Ikiwezekana kagueni nyumba kwa nyumba hadi muhakikishe mmewapata magaidi.”

“Nimekuelewa, Mheshimiwa Rais.Ninakuhakikishia tumejipanga vizuri.Hadi kufika asubuhi tutakuwa tumepiga hatua kubwa sana.Kwa hakika tutakuwa aidha tumewapata au tupo karibu na kuwapata,” alisema mkuu wa jeshi la polisi.Akaagana na Rais Pius. Rais akampigia simu Maurine Kyaso.

“Mheshimiwa Rais!” akasema Maurine Kyaso

“Maurine kuna jambo nataka ulifanyie kazi,” Rais Pius akanyamaza kidogo.

“Ninataka kuanzia sasa mumfuatilie sana Ruby lakini kwa siri bila yeye kujua,”alisema Rais Pius.

“Kuna tatizo lolote, Mheshimiwa Rais?”Maurine aliuliza.

“Kuna kitu ambacho hukifahamu,Maurine.Sina hakika kama Ruby amekueleza kuwa taarifa ile ya Fabrice Kayembe kuwa mtu muhimu kwa magaidi ilitoka kwa Mathew Mulumbi.”

“Mathew Mulumbi?”Maurine alishangaa.

“Ndiyo!”

“Ni Mathew huyu aliyekuwa katika ndege iliyopotea ambaye tunamtafuta au Mathew mwingine?” Maurine aliendelea kushangaa

“Duniani kuna Mathew Mulumbi mmoja tu!” alijibu Rais Pius

“Mheshimiwa Rais, jambo hili linawezekanaje? Mathew alikuwemo katika ndege iliyopotea.Tena tunaamini

watu wote waliokuwamo katika ndege hiyo inayohisiwa imeanguka baharini watakuwa wamefariki dunia. Iweje Mathew awe hai? Je, hakuwemo ndani ya ndege?" Maurine aliongea kwa msisitizo.

"Maurine, hilo ndilo hasa linalonipelekea nitoe maelekezo haya kwamba Ruby afuatiliwe mawasiliano yake.Ana ukaribu mkubwa na Mathew.Ninaamini lazima Mathew atampigia tena ili kufahamu kama tumefanikiwa kumpata Fabrice Kayembe au la.Nataka uweke watu wa kufuatilia mawasiliano ya Ruby kwa saa ishirini na nne.Pindi Mathew Mulumbi akipiga simu, basi tuhakiki kama kweli ni yeye na yuko wapi ili tuanze mchakato wa

kumsaka. Yeye ni mtu mwenye majibu sahihi kuhusu ndege yetu iliyopotea," alisema Rais Pius na kutulia kidogo.

"Maurine, jambo hili ni siri.Weka mtu unayemuamini alishughulikie.Hakikisha Ruby asifahamu chochote kile kinachoendelea dhidi yake," alihitimisha Rais Pius.

"Nimekuelewa, Mheshimiwa Rais tutafanya hivyo," alijibu Maurine.Akaagana na Rais.

ARUSHA

Papi Gosu Gosu na Agai Sempa waliondoka katika ofisi za SNSA Arusha na kwenda hospitali ya rufaa ya mkoa kufuatilia maendeleo ya Fabrice

Kayembe.Bado Fabrice alikuwa katika chumba cha upasuaji.Ikawalazimu kukaa nje kusubiri .

“Agai, umefanya kazi ya kishujaa sana leo hii.Ni wewe uliyefungua njia kwa vikosi vya uokozi kupita kwa kuwaua wale magaidi juu ya paa” alisema Gosu Gosu.

“Nashukuru,Gosu Gosu.Mimi ndiye ninayepaswa kukupongeza wewe kwa maamuzi yako ya kuwamaliza wale magaidi wawili waliokuwa wanatulinda ndani ya kile chumba. Njia ilianza kufunguka pale.Nimefurahi kukufahamu Dr. Gosu Gosu!” alisemaAgai. Kwa pamoja wakaangua kicheko.

“Kitendo cha kuamua kuingia ndani ya jengo linaloshikiliwa na magaidi na

kujifanya daktari kilikuwa cha kishujaa sana.Kama mimi ningekuwa Rais,basi ningekutunuku nishani ya ushujaa.Hakuna ambaye angekubali kuhatarisha maisha yake kiasi kile.Nimejifunza kitu kikubwa kutoka kwako Bwana Gosu Gosu. Na ndiyo maana nikaweza hata kupambana na wale magaidi nikawaua," alisema Agai.

“Rais alitueleza ulikuwa kizuizini.Ulifanya kosa gani?” Gosu Gosu aliuliza.Agai akatulia kidogo. Akaonekana kama aliyetaka kughairi kusema, lakini baadaye akashusha pumzi na kusema.

“Niliharibu misheni moja muhimu sana.Kuna mwanamke tulikuwa tunamfuatilia nikalazimika kuanzisha

mahusiano naye ili kupata taarifa.Badala yake, nikajikuta nimempenda.Yamkini sikutaka akamatwe. Hivyo nikamsaidia kutoroka. Hatimaye misheni ikaharibika.Nilipogunduliwa, nikawekwa kizuizini hadi nilipotolewa leo na Rais.Kwa bahati nzuri nikakutana na kazi hii. Vipi kuhusu wewe?Uko SNSA kwa muda gani?" aliuliza Agai

"Hapana.Siko SNSA.Mimi na Ruby tunafanya kazi Shirika la UjasusiTanzania,"Gosu Gosu alijibu.Agai akatabasamu.

"Hata mimi pia ninafanya kazi katika shirika hilo," Agai alijibu.Simu ya Gosu Gosu ikaita. Hakuwa tena na kifaa cha sikioni.Alikiondoa walipokuwa

katika ofisi za SNSA Arusha “Ruby!” alisema Gosu Gosu.

“Gosu Gosu tumepata taarifa kwamba jeshi la polisi limevamia nyumbani kwa Sultan lakini hawajakuta mtu. Wamefanikiwa kuipata miili ya watoto waliokuwa wamechinjwa mchana wa leo.Hii pekee inathibitisha kwamba ni kweli watoto walikuwepo katika nyumba hiyo na wameondolewa kabla jeshi halijafika.Mbaya zaidi,haijulikani mahala walipo.Ninahisi yawezekana magaidi walipata taarifa kwamba tayari tumegundua mahala walipo ndiyo maana wakakimbia. Hata hivyo bado wangali ndani ya jiji la Arusha.Hivi ninavyokwambia, polisi bado wanaendelea na msako,” alisema Ruby.

“Ahsante sana Ruby kwa taarifa hiyo.Umefuatilia ile kamera kama nilivyokuomba?” Aliuliza Gosu Gosu.

“Ndiyo.Nimepitia kumbu kumbu za kamera ndani ya ukumbi wa KICC.Kuna kitu nimekigundua.Wakati ninyi mkiwa katika kile chumba muda mfupi kabla ya kutujulisha kuwa mmewaua magaidi wawili,mtu mmoja aliingizwa katika ukumbi ambao mateka walikuwa wamekusanywa.Alikuwa anavuja damu usoni.Kwa kutumia progamu ya utambuzi wa sura, nimeweza kumtambua pia kupata taarifa zake anaitwa Jamal Hassan Mkeka.Huyu ni mfanyakazi wa ukumbi huo ambaye ni mkuu wa kitengo cha umeme.Nikaenda mbali zaidi kwa kufuatilia mawasiliano yake ya simu

nikagundua asubuhi ya leo aliwasiliana na Sultan Jabir.Si leo tu, kwa muda wa siku saba Sultan amekuwa mtu ambaye amewasiliana naye mara nyingi zaidi.Katika mazungumzo yao leo asubuhi,Sultan alimuuliza Jamal kama kila kitu kimekamilika.Jamal akamjibu kwamba kila kitu kimekamilika.Gosu Gosu, tunaamini magaidi hawakuwa na uhakika wa kutoka salama hivyo kuna uwezekano mkubwa walimpa yule jamaa diski halafu akajichanganya na mateka wengine ili watakapokombolewa aweze kutoka nayo na kuikabidhi kwa akina Sultan.Gosu Gosu, tunahitaji kumpata huyu jamaa!”alisema Ruby.

“Ahsante Ruby kwa taarifa hii.Kwa kuwa tuko hapa hapa hospitali

tunakwenda kufuatilia wagonjwa wote walioletwa kutoka KICC.Nitumie picha ya huyo jamaa katika simu yangu tafadhali," alisema Gosu Gosu huku akiinuka. Wakaanza kukimbia kuelekea katika jengo walikopelekwa watu waliokuwa wanashikiliwa mateka katika ukumbi wa KICC.Kabla ya kulifikia jengo hilo, ukaingia ujumbe katika simu ya Gosu Gosu. Ruby alikuwa amemtumia picha ya Jamal Hassan Mkeka.Gosu Gosu alishangaa sana kwa kuiona picha ile kwani alikuwa ni yule mtu aliyekuwa akitafsiri lugha ya kiarabu wakati akizungumza na mkuu wa magaidi

Walipita kitanda kimoja baada ya kingine wakikagua, lakini hawakumuona

Jamal.Wakarudia kwa mara ya pili kukagua kwa umakini mkubwa sana lakini hawakumuona Jamal.Wakaenda katika ghorofa ya juu.Wakatafuta wakamkosa.Gosu Gosu akamfuata mmoja wa madaktari aliyekuwa akiendelea kutoa huduma.Akamuuliza kama kuna watu ambao tayari wameruhusiwa kutoka.Daktari akamthibitishia kwamba katika watu wote waliowapokea pale hospitali hakuna hata mmoja aliyeruhusiwa kuondoka hadi pale watakapopatiwa huduma.Gosu Gosu akampigia simu Ruby.

“Ruby, Jamal hayumo miongoni mwa wale watu waliokombolewa kutoka KICC,”alisema Gosu Gosu.

“Tumechelewa.Ametoroka.Hata hivyo, lazima tumpate!” alisema Ruby.

“Ruby, watu wote waliotolewa KICC waliletwa hapa na hakuna aliyepelekwa hospitali nyingine au kushushwa njiani.Kama ametoroka, basi alitoroka akiwa hapa hapa hospitali.Kuna kamera ya ulinzi katika geti kuu la kuingilia na kutokea hapa hospitali.Unaweza ukarejea kumbukumbu zake tuone namna alivyoondoka hapa hospitali?” Aliuliza Gosu Gosu.

“Nipe dakika mbili,” alisema Ruby.Akakata simu.

“Magaidi hawa wametumia akili nyingi.Walijua ile diski ni muhimu sana.Uwezekano wa wao kutoka salama

ndani ya ukumbi ulikuwa mdogo hivyo wakampa yule jamaa diski akajichanganya na wale mateka,ikionekana kama vile walimkuta akiwa amejificha ndani ya jengo.Lazima tuipate ile diski ni muhimu sana," alisema Gosu Gosu.Baada ya kupita dakika mbili,Ruby akampigia Gosu Gosu.

"Ulikuwa sahihi Gosu Gosu.Jamal ameonekana akitoka katika geti dakika tano tu baada ya mateka kufikishwa pale hospitalini. Kulikuwa na hekaheka nyingi pale hospitalini.Akaitumia nafasi hiyo kuweza kutoroka na diski.Kamera inamuonyesha akitoka nje ya geti.Akaingia katika gari yenye rangi nyeupe iliyokuwa nje kandoni mwa

barabara.Sikuweza kupata namba zake,”alisema Ruby.

“Ruby, natakiwa kumpata huyo Jamal usiku huu na kuipata hiyo diski.Nahitaji kujua anakoishi Jamal tumfuate na kuichukua hiyo diski,” alisema Gosu Gosu.

“Gosu Gosu, nipe dakika chache nitafute mawasiliano ya mkurugenzi wa ukumbi.Lazima atakuwa anamfahamu vyema Jamal,” alisema Ruby na kukata simu.Gosu Gosu akamueleza Agai kile alichoelezwa na Ruby.

“Agai, kwa namna yoyote ile usiku huu wa leo lazima tuhakikishe tumeipata ile diski aliyonayo Jamal.Ni muhimu sana.Tumsubiri Ruby atafute mawasiliano ya mkuu wa KICC ili

atueleze mahala anakoishi Jamal," alisema Gosu Gosu.

Dakika tano baadaye,Ruby akampigia simu Gosu Gosu akamfahamisha kwamba tayari amefanya mawasiliano na mkurugenzi wa KICC.Amuelekeza mahala anakoishi Jamal ambako ni Njiro karibu na baa ya Lukio.Bila kupoteza muda, Gosu Gosu na Agai wakaingia garini na kuelekea mahala walikoelekezwa.

Mitaa mingi ya jiji la Arusha usiku huo haikuwa na watu. Hata barabarani magari yalikuwa machache sana.Watu wengi walisalia majumbani mwao kama walivyoelekezwa na vyombo vya ulinzi.Gosu Gosu aliyekuwa katika usukani aliendesha gari lile kwa mwendo

mkali.Kutokana na barabara kukosa magari hawakuchukua muda mrefu kuwasili Njiro.Walitafuta baa ya Lukio.Wakaegesha gari lao katika sehemu ya maegesho ya baa.Kulikuwa na magari kadhaa mahala pale.Licha ya kutokea kwa shambulio lile la kigaidi, lakini katika baa hiyo ya Lukio watu walikuwa wanaendelea kupata vinywaji kana kwamba hakuna kilichotokea.Agai akaenda kaunta.Akanunua chupa mbili za maji ya kunywa halafu wakaondoka.

Nyumba waliyoelekezwa na Ruby kwamba ndiyo aliyokuwa akiishi Jamal haikuwa mbali na baa hiyo ya Lukio.Ni hatua chache tu wakafika katika nyumba hiyo.Ilikuwa nyumba ya ghorofa moja.Ndani giza totoro.Hakukuwa na taa

inayowaka.Ishara kwamba hakukuwa na mtu yeyote ndani.Getini kulikuwa na kufuli kubwa.

“Inaonekana hakuna mtu humu ndansi.” alisema Gosu Gosu. Agai akachomoa kitu mfano wa waya mgumu kutoka katika mkanda wake.Akaukunja kisha akaanza kulichokonoa lile kufuli.Haikuchukua sekunde nyingi kufuli likafunguka.

“Huyu jamaa matendo yake ni kama Mathew.Mimi nilikuwa nafikiria kulisambaratisha kufuli kwa risasi lakini kumbe kuna njia ya kuweza kulifungua kwa urahisi kama alivyofanya.Hawa majasusi wanafahamu mambo mengi sana,” aliwaza nafsini Gosu Gosu.Agai

akalifungua geti.Wakaingia ndani wote wakiwa na bastola mkononi.

Walitembea kwa tahadhari kubwa kuelekea katika mlango mkuu wa kuingilia ndani ya nyumba ya Jamal.Kulikuwa na ukimya mkubwa.Waliufikia mlango wa kuingilia sebuleni. Agai akakinyonga kitasa cha mlango.Ulikuwa umefungwa kwa funguo.Akachukua ule waya mgumu mwembaba aliotumia kufungulia kufuli.Akaanza kuchokonoa kitasa.Baada ya muda, akaguna.

“Kuna nini,Agai?” Gosu Gosu aliuliza baada ya kusikia mguno.

“Kitasa kigumu.Hakitaki kufunguka,” alisema Agai akiendelea kuchokonoa kitasa. Gosu Gosu akamtaka

asogee pembeni, akarudi nyuma hatua mbili.Akaruka teke moja zito mlango ukafunguka.Wakaingia ndani.Akawasha taa ya sebuleni.Wakaangaza angaza hawakupata chochote.Wakaingia katika chumba cha chakula. Walikuta kuna vikombe vitatu vya chai vilivyotumika muda mrefu.

“Dhahiri walitumia vikombe hivi asubuhi,” alisema Gosu Gosu huku akitupia jicho kila upande wa eneo la chakula. Hawakukuta kinachotoa shauku kuendelea kubaki eneo hilo.Wakaangalia vyooni nako hakukuwa na mtu. Wakaingia katika vyumba viwili vya kulala vilivyokuwa sehemu ya chini lakini hawakupata chochote zaidi ya vichungi vya sigara.

Taratibu wakaanza kupanda ngazi kuelekea ghorofani.Wakaingia katika chumba cha mapumziko.Walikuta kuna meza ya kioo juu yake kulikuwa na makaratasi kadhaa, kalamu ya risasi na sahani yenye vichungi vya sigara.

“Inaonesha humu ndani kulikuwa na mtu zaidi ya mmoja,” alisema Gosu Gosu huku akiyapekua yale makaratasi yaliyokuwa mezani.Kulikuwa na karatasi nane zikionyesha ramani ya jengo fulani.Akalitazama vizuri, Gosu Gosu akasema.

“Hii ni ramani ya jengo la KICC.Ukitazama vizuri utaona sehemu hii ya chini kuna ukumbi mkubwa wa wazi ambako ndiko walikokuwa wamekusanywa mateka wote.Kuna

mduara mwekundu katika karatasi hii yenye namba sita na upo mshale unaoelekezwa katika ule mduara mwekundu uliochora ukiwa na maandishi '*Communication room*," alisema Gosu Gosu.

"Ramani hii inaonesha namna walivyokuwa wameandaa shambulio.Chumba hiki ghorofa ya sita ndiyo kile ambacho kulikuwa na kompyuta mbili na walikuwa wanakitumia kwa mawasiliano.Hakuna shaka kwamba huyu jamaa naye ni gaidi," alisema Gosu Gosu.

"Ghorofa ya pili kuna chumba kimeandikwa umeme halafu wakazungushia mduara mwekundu na kuweka mshale wenye maandishi

chumba cha silaha," alisema Agai ambaye naye alikuwa ameishika karatasi iliyoandikwa namba tatu.

"Picha imekuja.Kwa mujibu wa maelezo ya Ruby ni kwamba huyu jamaa ndiye mkuu wa kitengo cha umeme pale KICC.Inaonekana silaha ziliingizwa mapema kisha zikafichwa katika chumba cha umeme," alisema Gosu Gosu akachukua simu.Akampigia Ruby.Akamueleza kile walichokikuta katika kile chumba.Wakatoka katika kile chumba cha mapumziko,wakaingia katika chumba cha kulala.Ndani kulikuwa na kitanda kikubwa,kabati la nguo,na meza ndogo kwa ajili ya vipodozi.

Katika mojawapo ya droo za meza ya vipodozi, akakuta karatasi kubwa alipoikunjua ilikuwa ramani.Akaiweka kitandani.Akaanza kuipitia taratibu.Katika baadhi ya sehemu ndani ya ramani ile ziliwekewa alama na kalamu nyekundu.

“Ramani hii inaonesha mipango yote ya mashambulio ya magaidi.Ukiitazama utaona kuna alama ambazo zimewekewa namba,”alisema Gosu Gosu.

Hawakupata kitu kingine cha kuwasaidia.Wakaondoka kurejea katika ofisi za SNSA zilizokuwa hapo hapo Njiro.Bila kupoteza muda, ramani ikawekwa mezani.Wakaanza kuipitia.

“Hii ni ramani ya jiji la Arusha” alisema Leon mkuu wa SNSA Arusha baada ya kuitazama ramani ile

“Magaidi wameweka namba katika ramani.Alama hizi za namba ni vituo kwani kuna namba moja hadi nne.Ukitazama namba moja, ni kituo cha kuhifadhi malikale ambako ndiko shambulio la kwanza la kigaidi lilifanyika na watoto wa shule wakatekwa.Namba mbili, ni ukumbi wa mikutano wa KICC.Ukitazama namna matukio yalivyotokea,utaona kwamba namba hizi zimepangwa kwa mfululizo wa matukio.Lilianza tukio la kutekwa watoto, halafu likafuata la kuteka ukumbi.Kuna namba tatu na namba nne pia.Naamini namba hizi hazijawekwa

katika ramani hii kimakosa. Lazima kuna kitu kinachotarajiwa kufanyika katika maeneo haya yaliyowekewa namba.Tunatakiwa kuyafahamu maeneo haya ni wapi ili tuweze kuyafuatilia kwa haraka na kuzuia kama kuna shambulio lolote limepangwa kufanyika katika sehemu hizo," alisema Leon akanyamaza baada ya simu yake kuita.Alizugumza na aliyempigia halafu akawajulisha akina Gosu Gosu kuwa Fabrice ametolewa katika chumba cha upasuaji.Amelazwa chumba P5.

Gosu Gosu akampa maelekezo fulani Leon halafu akaelekea katika chumba cha mazungumzo ya moja kwa moja kwa njia ya video ili kuwasiliana na SNSA Dar es Salaam.Pembeni ya

runinga kubwa kulikuwa na runinga nyingine tatu na katika moja wapo alionekana Ruby akiwa na Maurine.

“Habari zenu Dar es Salaam,” alisema Gosu Gosu.

“Huku salama.Mnaendeleaje huko? Nini kinaendelea hapo kwa sasa?”Ruby aliitikia salamu na kupachika swali papo hapo.

“Kwa sasa tuko hapa ofisi za SNSA Arusha.Ni baada ya kutoka nyumbani kwa Jamal.Katika chumba chake cha kulala, tuliipata ramani ya jiji la Arusha ambayo nimemuelekeza Leon awatumie,” alisema Gosu Gosu.Ramani ikaonekana katika runinga kubwa.Gosu Gosu akaisogelea

“Hii ndiyo ramani tuliyoipata.Katika ramani hii, mtaona kuna sehemu zimewekewa alama nyekundu na namba moja hadi nne.Ukitazama hapa namba moja, ni nje ya jiji ambako shambulio la kwanza lilifanyika na watoto wakatekwa.Namba mbili, ni hapa jijini ambako lilifanyika shambulio la pili katika jengo la KICC.Namba tatu na nne, bado hatufahamu ni maeneo gani lakini tunaamini kwa kuwa yamewekewa alama katika ramani hii, basi lazima yana umuhimu kwa magaidi.Watu wetu hapa Arusha wanaendelea kutafuta maeneo haya ili kuyatambua. Hiyo itatuwezesha kuyafanyia uchunguzi wa haraka na kuzuia kama kuna kitu chochote magaidi wamepanga kukifanya,” alisema Gosu

Gosu. Akaweka tuo kusikiliza upande wa pili.

“Kuna kila dalili kwamba bado magaidi wana mipango ya kufanya mashambulio zaidi.Gosu Gosu,hatuwezi kuruhusu mashambulio mengine yatokee.Vile vile lazima tuhakikishe ile diski inapatikana,” alisema Ruby. Punde, Leon akaingia ndani. Akampa Gosu Gosu karatasi.Ruby akanyamaza..

“Ruby, tayari vijana wetu wameipata sehemu iliyowekwa alama ya namba tatu.Ni hoteli kubwa ya kitalii iliyoko eneo la Usa river inaitwa Hotel Green.Inaonekana kuna kitu kinatakiwa kufanyika katika hoteli hiyo.Tunaelekea huko sasa hivi.Wakati tukielekea huko,naomba muwajulishe jeshi la polisi

ili watume askari haraka sana eneo hilo la hoteli.Wazuie watu wasiingie katika hoteli hiyo.Uchunguzi ufanyike kubaini kile ambacho magaidi wanakusudia kukifanya," alisema Gosu Gosu.Upesi wakaingia katika gari safari kuelekea Usa river ikaanza.

"Nini magaidi wanakusudia kukifanya katika hoteli hiyo?" Agai aliuliza kidadisi.

"Naamini kuna shambulio wanataka kulifanya mahala hapo.Hotel Green ni moja ya hoteli ambazo walifikia wageni wengi wa mkutano wa Afrika Asili Yangu," alisema Leon mkuu wa SNSA Arusha ambaye ndiye alikuwa dereva.

Taarifa ya Hotel Green kulengwa na magaidi ilifika kwa haraka sana kwa

jeshi la polisi.Kutoka katika kituo cha polisi Usa River, zikatoka gari tatu zikiwa zimejaza askari waliojihami kwa silaha kwa lengo la kukabiliana na tukio lolote la kigaidi.Wakaondoka kwa haraka kuelekea eneo la hoteli.

Mara tu magari ya askari polisi yalipoingia katika barabara kuu, kikasikika kishindo kikubwa cha mlipuko wa bomu. Katika sehemu ya maegesho ya Hoteli Green, lililipuka bomu lililotegwa katika gari.Sekunde chache baadaye, mabomu mengine mawili yakalipuka ndani ya Hoteli.Wakati watu wakikimbia ovyo kuokoa uhai wao,wakatokea watu wanne wenye bunduki na kuanza kuwamiminia watu risasi ovyo kisha wakafunga

milango ya hoteli na kuanza kuua kila waliyemkuta.

Akina Gosu Gosu wakiwa eneo la Makumira wakajulishwa kwamba Hotel Green tayari imeshambuliwa.Kama haitoshi, magaidi bado walikuwemo ndani ya hoteli wakiwashikilia mateka baadhi ya watu.

“Tumechelewa!”alisema Gosu Gosu kwa hasira.

Ving’ora vya magari ya polisi na zimamoto vilisikika,magari hayo yakielekea Usa River kulikotokea tukio lingine la kigaidi.

Akina Gosu Gosu walifika Usa River lakini njia ya kuelekea Hotel Green ilikuwa imefungwa.Walioruhusiwa kwenda huko

ni vikosi vya ulinzi na usalama pekee.Leon alijitambulisha kwa askari walioweka kizuizi.Wakawafungulia.Wakapita na kuelekea katika hoteli hiyo ambayo iko ndani ya msitu.Askari waliizunguka hoteli yote kwa nje huku maandalizi ya kuingia ndani kuwadhibiti magaidi yakiendelea.

Wakiwa bado wangali Hotel Green, simu ya Leon ikaita.Kutazama jina juu ya kioo akaona alikuwa mmoja wa watu wake.Akaipokea.Akazungumza naye kisha akawageukia akina Gosu Gosu.

“Vijana wamefanikiwa kuipata namba nne. Ni sehemu nje ya Usa River ambako kuna bustani ya wanyama inaitwa Usa Garden,” alisema Leon.

“Kuna nini katika hiyo bustani?”Agai aliuliza.

“Tutakwenda kujua huko huko.Tuondokeni mahala hapa.Tuviachie vikosi husika viendelee na majukumu yao.Usa Garden kwa sasa kunatuhusu,” alisema Gosu Gosu .Wakaondoka kwa kasi eneo lile.Kabla hawajafika barabara kuu,Ruby akapiga simu.

“Hallow,Ruby!” alisema Gosu Gosu.

“Gosu Gosu, tumepata taarifa ya kutokea kwa shambulio la bomu katika hospitali ya rufaa ya mkoa wa Arusha ya Mount Meru muda mfupi uliopita.Tunataka kufahamu, je, Fabrice Kayembe yuko salama? Tuna hofu kwamba yawezekana shambulio hilo

lililotokea katika hospitali hiyo lilimlenga yeye," alisema Ruby.

"Tuna watu wetu pale hospitali ambao tuliwaweka kumlinda Fabrice.Ngoja tuwasiliane nao ili tufahamu kuhusu Fabrice.Jambo lingine Ruby, ni kwamba SNSA Arusha wamefanikiwa kuipata sehemu ya nne kwa mujibu wa ile ramani.Ni nje kidogo ya Usa River. Sehemu yenyewe ni bustani ya wanyama inaitwa Usa Garden.Tuko njiani kwa sasa tunaelekea huko," alisema Gosu Gosu.

"Gosu Gosu, unadhani kuna ulazima wa kuwajulisha polisi jambo hilo ili wakawahi kuzuia kama kuna shambulio lolote la kigaidi?"Ruby aliuliza.

“Hapana.Msiwajulishe kwanza hadi tutakapofika mahala hapo na kujua kinachoendelea. Tumewajulisha kuhusu Hotel Green kabla hawajafika likatokea shambulio.Nahisi hawa magaidi wanapata taarifa haraka sana.Kuanzia sasa, tutatoa taarifa pale itakapohitajika tu,” alisema Gosu Gosu.

“Nimekuelewa, Gosu Gosu.Chukueni tahadhari kubwa na mtatujulisha kile kinachoendelea,” alisema Ruby.Bila kupoteza muda,Leon akawapigia simu vijana wake waliokuwa katika hospitali ya mount Meru wakimlinda Fabrice.Simu zao ziliita bila kupokelewa.

“Hii inanipa wasiwasi.Simu zao wote wawili hazipokelewi,” alisema

Leon akionekana kuchanganyikiwa.Akampigia daktari mmoja ambaye alikuwa anafahamiana naye.Akamtaka amsaidie kujua maendeleo ya Fabrice Kayembe ambaye amelazwa chumba namba P5 katika hospitali ya Mount Meru.

Walivuka bango linaloonesha bustani ya wanyama ya Usa iko umbali wa kilomita nne kutokea pale kwenye kibao.Muda mfupi baada ya kukivuka kibao ,daktari aliyepigiwa simu na Leon akapiga simu.Akamfahamisha Leon kwamba walinzi wawili waliokuwa wakilinda chumba P5 pamoja na mgonjwa waliyekuwa wakimlinda wote wameuawa kwa kupigwa risasi.

Ilikuwa taarifa iliyowashtua sana akina Gosu Gosu. Akawapigia simu akina Ruby kuwapa taarifa hiyo.

“Gosu Gosu,misheni yetu ilikuwa kumpata Fabrice.Tumefanya kila tuliloweza hadi tukafanikiwa kumpata lakini magaidi nao wamejitahidi wakamuua.Kuna mambo ambayo hawataki tuyafahamu kutoka kwa Fabrice ndiyo maana wakauchukua uhai wake.Kitu muhimu kwa sasa ni kuhakikisha kwa namna yoyote ile, diski aliyokuwa nayo Fabrice tunaipata.Naamini itakuwa na mambo ya muhimu sana.Ndiyo itakayotuwezesha kumfahamu Fabrice ni nani na kwa nini akawa lengo la magaidi,”alisema Ruby kwa hasira.

“Nimekuelewa Ruby,tutajitahidi kufanya kila lililo ndani ya uwezo wetu kuipata hiyo diski,” alisema Gosu Gosu.Akakata simu.Akaigonganisha mikono yake kwa hasira.

“*Guys*, kitu pekee tunachokihitaji kwa sasa ni ile diski.Ni ile pekee ndiyo itakayotupa picha kamili Fabrice Kayembe ni nani. Najua hii ni misheni ya hatari, lakini lazima tufanye kila tuwezalo kuhakikisha tunaipata diski,” alisema Gosu Gosu.Safari ikaendelea.

Walikaribia kufika katika geti la kuingilia katika bustani ya wanyama kwa mbali wakiwa katika kilima, waliona mataa mengi yakiwaka kama mji mdogo.

“Nani wanaishi huku?Mbona unaonekana mji mzuri

sana.Kinachofanyika huku, je, ni bustani tu ya wanyama au kuna shughuli nyingine?” Gosu Gosu alimuuliza Leon.

“Sifahamu chochote.Hata mimi hii ni mara yangu ya kwanza kuja huku.Sikujua kama kuna mji mzuri namna hii,” alijibu Leon.Walipolikaribia geti, wakakutana na kibao kikielekeza kupunguza mwendo wa gari.Baada ya muda mfupi, wakaanza kuliona geti la kuingilia katika bustani hiyo na walinzi watatu wakaonekana mmoja wao akiwa na bunduki.

Mlinzi mmoja akasimama na kunyoosha kibao kilichoandikwa STOP. Leon aliyekuwa dereva akapunguza mwendo wa gari.Akasimama karibu kabisa na mlinzi huyo.Mlinzi

akawasogelea. Leon akashusha kioo.Wakasalimiana.

“Mnaelekea wapi ndugu?”Mlinzi aliuliza.

“Sisi ni wageni.Tunatafuta hoteli. Tumeelekezwa tushuke huku chini kuna hoteli nzuri,” alisema Leon.

“Ni kweli hapa kuna hoteli lakini kwa sasa huduma zimesimama.Rudini Usa river kuna hoteli nyingi kule mkiuliza mtaelekezwa,” alisema mlinzi.

“Nini sababu ya kufunga kutoa huduma?” Gosu Gosu aliuliza.

“Sifahamu sababu.Sisi tumepewa maelekezo hayo kwamba hakutakuwa na huduma yoyote ya hoteli kwa sasa.Hivyo tusiruhusu mgeni yeyote isipokuwa labda yule anayekuja kutazama wanyama.Tena

kwa muda huu huwa haturuhusu watu kuingia bustanini," alijibu mlinzi.

"Samahani ndugu yangu.Naweza kupata sehemu ya kujisaidia haja ndogo? Nimebanwa sana!"Alisema Gosu Gosu.Mlinzi akamtaka ashuke ili akamuoneshe kilipo choo.Walivuka mlango mdogo pembeni ya geti halafu wakafuata ujia mdogo.Wakavuka kichaka cha maua nyuma yake kulikuwa na choo kizuri sana kwa ajili ya walinzi na wageni wengine.

Mlinzi akamuonesha Gosu Gosu choo cha wanaume.Akaugeuka nyuma akimsubiri.Gosu Gosu akapiga hatua moja kisha kwa kasi ya umeme, akageuka akamvuta yule mlinzi na kumtandika vichwa viwili vya

adabu,akamgeuza na kumkaba kabali kali mlinzi.

Kilikuwa kitendo cha ghafla ambacho yule mlinzi hakukitarajia.Taratibu mlinzi akalegea. Gosu Gosu akamlaza chini.Upesi akamvua sare zake na kuzivaa.Alipomaliza kuzivaa, akamuinua mlinzi na kumfungia bafuni kisha karejea getini.

Wale walinzi wengine walipomuona walidhani ni mwenzao amerejea.

“Jamaa umemuacha peke yake?” Aliuliza mmoja wa wale walinzi lakini Gosu Gosu hakujibu kitu.

“Jamaa umemuacha wapi?” Akauliza tena yule mlinzi. Gosu Gosu aliendelea kukaa kimya bila kumjibu

kitu.Yule mlinzi akaendelea kumsogelea ndipo waliposhtuka kuna utofauti. Mlinzi mwenzao hakuwa mnene kama Gosu Gosu. Mlinzi mwenye bunduki akaupeleka mkono wake begani ili kuishusha bunduki yake.Gosu Gosu alikuwa mwepesi sana kabla mlinzi hajaitoa bunduki yake begani,Gosu Gosu aliruka juu na teke zito likatua usoni pa mlinzi.Akapepesuka.Kabla hajakaa sawa,likatua teke lingine la kifua.Jamaa akaenda kuipa salamu ardhi.

Gosu Gosu akachomoa bastola.Akamuelekezea yule mlinzi mwingine ambaye alikuwa anataka kutimua mbio.Akamuonya asithubutu kukimbia.Alikuwa anatetemeka.Agai baada ya kugundua yule jamaa aliye

katika sare za ulinzi ni Gosu Gosu, akashuka haraka garini.Wakawachukua wale jamaa hadi katika kichaka karibu na choo.Wakawafunga mikono kwa nyuma na kuwapigisha magoti.

“Tunaomba mtusamehe!Msituue jamani.Sisi ni walinzi tu hapa hatuna fedha!”alisema mmoja wa wale walinzi.

“Sikilizeni.Sisi hatuna haja na ninyi.Tunajua hamuhusiki na chochote lakini tunachohitaji kutoka kwenu ni ukweli tu, basi.Tunataka kufahamu je kuna shughuli yoyote inayoendelea hapa usiku huu? Kuna gari zozote au kuna watu wamekuja hapa?” Gosu Gosu aliuliza.

Leon aliyekuwa getini akawafuata.Akawajulisha kwamba kuna

gari zinakuja.Gosu Gosu akamfanyia ishara Agai,wakavua sare za wale jamaa. Katika kuwadhibiti wale walinzi, Agai akawawekea matambara mdomoni ili wasiweze kupiga kelele. Wakawafunga mikono kwa nyuma na kuwafungia bafuni.Haraka haraka wakarejea getini huku wakionekana kama walinzi.Wakajiweka tayari wakiyasubiri yale magari yaliyokuwa yanashuka mlima kwa kasi.

****

Gari mbili zilishuka kwa kasi zilipokaribia geti,Leon akajitokeza na kibao kilichoandikwa STOP.Akasimama mbele kidogo ya geti na magari yale

yakapunguza mwendo.Yalipokaribia geti yakasimama.Leon akalisogelea gari la mbele aina ya Harrier.Dereva akashusha kioo Leon akamsalimu na kuchungulia. Ndani kulikuwa na watu wawili mwanaume na mwanamke.

“Habari zenu,” alisema Leon.

“Nzuri tu.Habari yako,”alijibu yule dereva mwanadada.

“Mnaelekea wapi?

“Fungua geti tunakwenda ndani,” alijibu dada kwa hamaki.

“Hakuna huduma yoyote inayotolewa hotelini kwa sasa.Kila kitu kimefungwa,”alisema Leon.Mlango wa upande wa pili wa gari ukafunguliwa.Akashuka jamaa aliyekuwa na mwanamke

garini.Akamfuata Leon. Walivyohisi hali si shwari, Gosu Gosu na Agai nao wakaanza kupiga hatua kuwasogelea.

“Wewe ni mgeni hapa?” Jamaa aliyeshuka garini aliuliza kwa hasira.

“Kwa nini kaka?” Leon aliuliza.

“Ni nani aliyekupa maelekezo ya kuzuia gari hili? Jina lako nani?”Aliuliza kwa ukali yule jamaa. Gosu Gosu aliyekuwa amefika eneo lile, akamtambua yule jamaa.

“Oh my God.Ni Jamal!” aliwaza nafsini Gosu Gosu huku akimsogelea.

“Kuna nini hapa?” Aliuliza Gosu Gosu.Sauti yake ikamshtua Jamal.Akamtazama vizuri Gosu Gosu.Akamgundua.

“Huyu ni yule daktari aliyekuja ukumbini kufanya upasuaji.Kumbe si daktari!” Jamal aliwaza nafsini mwake akiwa katika mshtuko.Ni baada ya kumuona Gosu Gosu.Upesi aliupeleka mkono wake iliko bastola lakini kabla hajaigusa alipigwa teke zito la mbavu akaanguka chini.Jamal alikuwa mwepesi,akageuka haraka na kuichomoa bastola yake aliyoifutika kiunoni.Kabla hajaitumia Leon akamuwahi na kumpiga risasi katika mkono ule wa kulia.Jamaa aliyebaki katika gari la nyuma alipoona purukushani akafungua mlango na kuanza kutimua mbio vichakani.Agai hakumpa nafasi.Akaizinga bastola yake na kuachia risasi mfululizo.Jamaa akaanguka chini.Agai akamfuata.

Wakati Gosu Gosu akiwa tayari amemdhibiti Jamal,mwanamke aliyekuwa anaendesha gari la mbele akaliondoa kwa kasi kubwa. Almanusura amgonge Leon,lakini aliruka pembeni upesi kisha akaanza kuachia risasi mfululizo. Ghafla kikasikika kishindo kikubwa.Gari lilikosa uelekeo na kugonga ukuta.Leon akalisogelea gari lile kwa tahadhari kubwa.Alimkuta yule mwanamke akigugumia kwa maumivu makali.

“Nisaidieni!”

“Nisaidieni!” alilia yule mwanamke.Leon akamsogelea karibu.Akamtazama.Akaona alikuwa anavuja damu katika bega la kushoto.Akaifutika bastola yake

kiunoni.Akaanza zoezi la kumtoa yule mwanamke ndani ya gari.

Agai alimfuata yule jamaa aliyempiga risasi.Akamgeuza na kumtazama usoni.Akashtuka.

“Huyu ni yule gaidi aliyekuwa anashikiliwa pale SNSA.Amewezaje kutoroka?” Agai alijiuliza.Akamtikisa.

“Hey!”

“Hey!” alisema Agai lakini jamaa alikuwa anakata roho.Risasi kadhaa alizotandikwa na Agai ziliusambaratisha uti wake wa mgongo.Agai akamuacha na kwenda kumsaidia Gosu Gosu.Wakamfunga Jamal miguu na mikono halafu wakamfuata Leon aliyekuwa anahangaika kumtoa yule mwanamke ndani ya gari.Wakasaidiana

na hatimaye kufanikiwa kumtoa.Wakamlaza chini.Alikuwa ameumia miguu na sehemu ya kifua.Bega la kulia lilikuwa linavuja damu.

“Jina lako nani?” Gosu Gosu aliuliza.

“Nipelekeni hospitali nakufa!”Hakujibu swali, badala yake akatoa ombi huku akitoa machozi.

“Tutakupeleka hospitali lakini tueleze kwanza jina lako ni nani?”

“Ninakufa.”alilia

“Nisaidieni!”Alizidi kulia yule mwanamke.

“Utakufa kweli kama hautatueleza ukweli!”alisema sAgai.

“Lilian.Jina langu ni Lilian!” Alisema huku akilia kwa uchungu.

Gosu Gosu akaelekeza yule mwanamke aingizwe katika nyumba ya walinzi.Yeye akamfuata Jamal.Akampekua kila mahali, lakini hakuipata diski.

“Jamal nataka uniambie diski uliyopewa ndani ya ukumbi wa KICC iko wapi?” Gosu Gosu aliuliza kwa ukali.

“Go to hell!” Jamal alijibu kwa karaha.

“Nakuuliza tena. Jamal ile diski ulipewa ndani ya ukumbi wa KICC iko wapi?”

“Sifahamu.Sina diski yoyote!” alijibu Jamal. Gosu Gosu akamvuta

akamuingiza katika nyumba ya walinzi.Akamtaka Leon akae getini kuangalia kama kuna mtu yeyote atatokea.Akamweka Jamal kitini akaanza kumsaili kuanzia juu mpaka chini. Kisha akasema.

“Jamal kwa mara ya mwisho nakuuliza ile diski iko wapi?”

“Sina diski!” Jamal alitoa jibu lake lile lile. Gosu Gosu akapandwa na hasira.Akamuelekezea bastola Lilian.

“We’ mwanamke umekuwa na huyu jamaa .Nataka unieleze diski aliyokuwa nayo iko wapi?” Gosu Gosu aliuliza kwa ukali. Lilian akaendelea kumtazama.

“Nakuuliza diski aliyokuwa nayo huyu jamaa iko wapi?” Gosu Gsou aliongeza. Lilian aliendelea kuwa

kimya.Gosu Gosu akampiga risasi ya paja Jamal, akapiga yowe la uchungu.

“Lilian nitaendelea kumpiga risasi huyu mwenzako hadi apoteze maisha.Tueleze mahala ilipo diski aliyopewa ndani ya ukumbi wa KICC ili kuokoa maisha yake!” Gosu Gosu alifoka.

“Sifahamu chochote kuhusu diski,” Lilian alijibu. Gosu Gosu haridhika na jibu lake. Akampiga tena Jamal risasi nyingine ya mguuni.Kilio kikaendelea kutoka kwa Jamal mithili ya mtoto mdogo.

“Where is the disc?” Gosu Gosu alibadilika kabisa

“I don’t know! Iswear I don’t know!” Lilian alipiga yowe.Gosu Gosu

akakishika kiganja cha mkono wa kushoto wa Lilian.Akakipiga risasi.Lilian akalia kwa maumivu makali.

“Diski iko wapi?” Aliuliza Gosu Gosu lakini Lilian aliendelea kulia akigaragara chini.

“Leo nitawaonesha ukatili mkubwa sana hadi mtakapoamua kusema ukweli mashetani wakubwa nyie!" Gosu Gosu alifoka. Akamwinua Lilian.

“Lilian Diski iko wapi?" Gosu Gosu aliendelea kufoka.

“Nieleze ukweli tafadhali!”

“Si…si...sifa...” Gosu Gosu hakusubiri Lilian amalize alichotaka kukisema.Akamtandika Jamal risasi mbili mguuni.

“Nitamuua mwenzako kwa risasi. Nataka unieleze ukweli.Iko wapi diski?"

“Sifahamu!"

“Leo utasema ukweli!" Gosu Gosu alisema huku akiuma meno yake.Akakishika kiganja kingine cha mkono wa Lilian. Akaelekeza bastola juu yake.Akavuta pumzi ili atandike risasi. Kabla ya kupiga, ghafla nadhari ya Lilian ikaamka. Akapiga kelele.

“Nitasema!"

"Nitasema!" Lilian alipiga kite.

Gosu Gosu akiwa bado ameendelea kukishikilia kiganja cha Lilian, akamtazama kwa hasira.

“Usinipige risasi! Nitasema ukweli!" Lilian alisema.Gosu Gosu akauacha

mkono wa Lilian.Akamkata jicho kali sana kisha akamwuliza.

“Diski iko wapi?"

“Kwa Sultan!"

“Sultan yuko wapi?" Gosu Gosu aliunguruma kama simba. Lilian hakuweza kuhimili mateso ya Gosu Gosu. Akawaeleza kila kitu kwamba yeye ndiye aliyemchukua Jamal kutoka hospitali ya Mount Meru akampeleka kwa Sultan.Akampatia ile diski.Akawaambia kuwa magaidi walipewa taarifa na mtu kuwa wanafuatiliwa,hivyo wakawahamisha watoto.Aliendelea kueleza kuwa Jamal alipewa taarifa na mtu kuwa sanduku jeusi liko katika ofisi za SNSA Arusha na wakavamia ofisi hizo wakaua watu

wote waliowakuta.Wakalichukua sanduku jeusi wakamuokoa na mwenzao ambaye alikuwa anashikiliwa hapo SNSA.Lilian aliendelea kukiri kwamba, ni wao waliofanya shambulio katika hospitali ya Mount Meru na kumuua Fabrice Kayembe.Mwisho akaweka wazi kuwa watoto waliotekwa walikuwa pale Usa Garden.

“Lilian,tutakwenda kukupatia matibabu, lakini kabla ya kufanya hivyo nataka unihakikishie kwamba hayo yote uliyotueleza ni ya kweli.Na kwamba wasichana waliotekwa wako hapa Usa Garden,”alisema Gosu Gosu

“Nimewaeleza ukweli mtupu.Wasichana wote wako hapa Usa Garden,” Lilian alijibu. Gosu Gosu

akamuelekeza Leon kuangalia katika magari kama ataliona sanduku jeusi.Baada ya muda mfupi, Leon akarejea akiwa amebeba sanduku jeusi ambalo lilikuwa limehifadhiwa katika ofisi za SNSA Arusha.

Gosu Gosu akamtazama kwa hasira Jamal.

“Sura yako haifanani na roho yako. Una roho mbaya zaidi ya shetani, Jamal.Umeshiriki katika kuratibu mashambulio ya leo ya kigaidi katika ukumbi wa KICC.Mmeua watu wasio na hatia hasa wale wanafunzi.Mmeua wenzetu pale SNSA na bado mmemuua hadi Fabrice Kayembe.!" Gosu Gosu akamtazama kwa uchungu sana kisha akamwambia.

"Ukiua kwa upanga, nawe utakufa kwa upanga!"

Ghafla akachomoa kisu kidogo akakizamisha katika sehemu ya juu ya jicho la kulia la Jamal.Hakuridhika na hilo, akaingiza vidole na kutoka na jicho.Jamal alilia kwa sauti kubwa mno.Gosu Gosu hakumjali.Akamuondoa pia jicho lililobaki.

“Unastahili kufa kifo cha kikatili sana nyau wewe!"alisema Gosu Gosu halafu akakipitisha kisu kile kikali katika shingo ya Jamal.Damu nyingi ikaanza kumwagika.

“*Guys*, ni wakati wa kukamilisha misheni yetu.Kama alivyosema Lilian kwamba watoto wako hapa.Vile vile diski tunayoitafuta iko hapa anayo

Sult…….” Wote wakageuka baada ya mlio wa risasi kusikika.

“Get down!" Leon alipiga ukelele akawarukia Gosu Gosu na Agai.Akawaangusha chini.Milio ya risasi ikaendelea kusikika.Agai akatambaa kwa tumbo na kwenda nyuma ya sofa lililokuwa ndani ya nyumba ile ya walinzi.Akachungulia.Akawaona jamaa wawili wakiwa na bunduki karibu na ile nyumba ya walinzi.Hakupoteza muda.Kwa kutumia bastola yake, akawadungua mmoja mmoja.Mara kukawa kimya.

“Gosu Gosu!”Agai aliita. Ni baada ya kuhakikisha kuko salama. Gosu Gosu alikuwa amelaliwa na Leon. Aliposikia sauti ya Agai, akamsukuma Leon.Ndipo

alipogundua kwamba Leon hakuwa na uhai tena.Alikuwa amepigwa risasi nyingi. Gosu Gosu akajaribu kuinuka akahisi maumivu makali katika mguu wake wa kushoto.Alikuwa amepigwa risasi.

“Leon!”

“Leon!”

Agai aliita lakini Leon hakuwa na uhai. Alikuwa na matundu mengi ya risasi.Agai akapiga chini kwa hasira.

“Nisaidie kunyanyuka wamenipiga risasi mguu wa kushoto!”alisema Gosu Gosu.Agai akamsaidia kusimama na kumuingiza katika gari lao.

“Sikiliza, Agai,sasa tumepata jibu kuwa magaidi wako hapa.Yule mwanamke aligonga ukuta makusudi ili

wenzao wasikie kishindo kile na wafuatilie kujua kuna nini.Ile milio ya risasi kutoka kwa wale jamaa tayari imetuma taarifa kwa wenzao kuwa wamevamiwa.Kuna uwezekano mkubwa tusiweze kuwapata wale wasichana.Hatuwezi kupambana na hawa jamaa sisi peke yetu lazima tupate msaada wa jeshi la polisi," alisema Gosu Gosu.

Alitulia kidogo kisha akampa simu Agai ili ampigie Ruby kwa minajili ya kuwatuma polisi waje haraka sana katika eneo la tukio kuwadhibiti wale magaidi na kuwakomboa watoto wanaoshikiliwa mateka.

"Gosu Gosu!"Ruby aliita baada ya kupokea simu.

“Ruby, mimi ni Agai,” Agai alisema.Ruby akashtuka.

“Agai, Gosu Gosu yuko wapi?”Ruby aliuliza.Dhahiri hofu ilimtanda.

“Ruby,tunahitaji msaada wa jeshi la polisi.Tayari tumekwisha fahamu mahala walipo magaidi na watoto waliowateka.Haraka sana vikosi vinatakiwa vifike hapa Usa Garden ndiko waliko magaidi na watoto wote waliowateka,” alisema Agai.Ruby akasikika akitoa maelekezo kwa mtu aliyekuwa naye karibu kuwasiliana na polisi haraka ili waweze kufika mara moja mahala pale.

“Agai, tunafanya mawasiliano na jeshi la polisi.Watafika hapo muda si

mrefu.Gosu Gosu yuko wapi? Diski mmefanikiwa kuipata?”Ruby aliuliza maswali mfululizo.Kabla Agai hajajibu, ukasikika mlio wa risasi.Haraka akaupeleka mkono wake ilipo bastola, lakini kabla hajaitoa akamuona jamaa mmoja akianguka chini.

Gosu Gosu aliyekuwa garini alisimama nje ya mlango akiwa na bastola yenye kiwambo cha sauti.Aliweza kumfumua gaidi kwa risasi mara tu alipojitokeza.Agai akampa simu Gosu Gosu azungumze na Ruby. Yeye akawafuata wale magaidi waliowaua.

“Ruby kama alivyokueleza Agai tunahitaji msaada wa haraka sana.Tunakabiliana na magaidi.Wamemuua Leon mkuu wa

SNSA Arusha. Mimi nimepigwa risasi mbili mguuni. Mbaya zaidi, watu wote katika ofisi ya SNSA Arusha wameuawa hiyo ni kwa mujibu wa mmoja wa magaidi tuliyemuhoji," alisema Gosu Gosu. Ruby alishtuka sana kwa taarifa hiyo.

"Vipi kuhusu diski tayari mmeipata?"Ruby aliuliza.

"Hapana. Bado. Inasemekana ipo kwa Sultan ambaye yuko ndani ya moja ya majengo ya hapa Usa garden," Gosu Gosu alijibu. "Mmezipata wapi taarifa hizo?" Ruby aliuliza.

"Tulimhoji kwa kibano kikali mmoja wa magaidi akatueleza hivyo"alisema Gosu Gosu kisha akanyamaza baada ya mlio wa ndege

kusikika.Ilipita chini sana ishara kuwa ilitoka katika kiwanja kidogo kilichokuwa eneo hilo.

“Gosu Gosu!”Ruby aliita.

“Ruby, tutazungumza baadaye kidogo.Waelekeze askari polisi wafike haraka sana mahala hapa!”alisema Gosu Gosu na kukata simu.Agai akarejea akiwa amembeba Lilian begani.

“Alijaribu kutoroka akashindwa.Nimemkuta vichakani akiwa hajiwezi.” alisema Agai.Akamuingiza Lilian katika gari lao.

“Agai,ile ndege iliyopaa muda mfupi uliopita imenipa wasiwasi sana magaidi wametoroka.Yawezekana polisi wakachelewa kufika hapa na tukawapoteza hawa jamaa. Ninashauri

twende sisi wenyewe tukaanze mashambulizi.Tuhakikishe tunaipata diski tunayoihitaji.” alisema Gosu Gosu.

“Gosu Gosu, ni hatari sana kwenda huko sisi wawili.Hatujui magaidi wako wangapi na wamejihami vipi.Isitoshe tayari umeumia mguu,” Agai alijibu.

“Usihofu kuhusu mimi.*I’m a soldier*.Si mara ya kwanza kupigwa risasi.Naomba kamba ngumu au waya,” alisema Gosu Gosu.Agai akamletea kamba.Akafunga mahali alikopigwa risasi.

“Naomba kisu!”alisema Gosu Gosu.

“Unataka kufanya nini Gosu Gosu?”

“Give me a knife!” Gosu Gosu alisema kwa ukali.Agai akafungua sehemu katika gari lao akatoa sanduku la

huduma ya kwanza.Gosu Gosu huku akiuma meno kwa maumivu, akapasua mahala alikopigwa risasi.Agai aliendelea kumshangaa.Akigugumia kwa mamivu makali, Gosu Gosu akamtaka Agai kuugandamiza ule mguu wake.Akaingiza vidole viwili mahala alipopasua na kuisaka risasi.Akaitoa.

“Aaagghhh!”Gosu Gosu aligugumia maumivu.Akaanguka katika kiti.

“Gosu Gosu, hiki unachokifanya ni hatari sana.Subiri msaada unakuja sasa hivi,” Agai alisihi.

“We don’t have time to wait.Funga hilo jeraha haraka sana!”alisema Gosu Gosu akiwa amefumba macho.Agai akamwagia dawa katika lile jeraha halafu

akalifunga kuzuia damu isiendelee kumwagika.

“Sijawahi kukutana na mtu wa aina hii katika maisha yangu!”Aliwaza Agai wakati akimaliza kufunga jeraha la Gosu Gosu.

“Bado risasi moja imebaki!”alisema Gosu Gosu.

“Gosu Gosu!”Agai aliita kwa wasiwasi

“Agai, fanya ninavyokuelekeza!”Alifoka Gosu Gosu.Agai akaushika barabara mguu wake.Gosu Gosu akakishika kisu na kupasua mahala ilikoingia risasi ya pili.Akafanya kama alivyofanya mara ya kwanza na kuitoa ile risasi.Jasho lilikuwa

linamtiririka kama amemwagiwa ndoo ya maji.

“Nashukuru nilipitia mafunzo magumu sana msituni kwani mambo kama haya hayawezekani kwa mtu ambaye hajayapitia. Sisi tulikuwa tunayafanya na mapambano yanasonga mbele,” aliwaza Gosu Gosu.Mwili wote ulikuwa katika maumivu makali.Akachukua chupa ya dawa ya kutuliza maumivu.Akatoa vidonge kadhaa, akatafuna.

“*Agai, we need to go*.Hatujui muda gani watafika hapa polisi.Hawa jamaa tayari wamekwisha jua wamevamiwa,” alisema Gosu Gosu.Akafungua sehemu ya kuhifadhia silaha ndani ya lile gari

lao.Akachukua bunduki.Agai akawasha gari, wakaelekea ndani zaidi.

“Kuna uwanja wa ndege mahala hapa.Tunatakiwa tukadhibiti kwanza eneo hilo ili wasiweze kuondoka.Nadhani pale panapowaka taa nyingi utakuwa ni uwanja wao wa ndege,” alisema Gosu Gosu.Akamuelekeza Agai azime gari.

“Kuna nini, Gosu Gosu?”Agai aliuliza, Ghafla, mbele yao wakatokea watu wanne wakiwa na silaha.Wakaanza kumimina risasi katika gari la akina Gosu Gosu.Kilichowasaidia ni magari yote yanayotumiwa na SNSA hayapenyi risasi.Gosu Gosu akafungua sanduku la silaha na kutoa mabomu mawili ya

kutupa kwa mkono halafu akafunua sehemu ya juu ya gari.

“*Agai Cover me*!”alisema Gosu Gosu.Agai akafungua mlango kidogo.Akatoa mkono.Akaachia risasi na kuwalazimu wale jamaa kutulia kwa muda.Hiyo ikawa nafasi kwa Gosu Gosu.Akasimama kwa mguu mmoja katika kiti.Kupitia ile sehemu ya juu ya gari, akarusha mabomu yale ya kutupa kwa mkono na kuwasambaratisha wale jamaa wote wanne.

“Tutembee kwa mguu hadi uwanjani,” alisema Gosu Gosu.

“Gosu Gosu, niache mimi nitangulie.Wewe utakuja na gari.Tunatakiwa kulilinda sanduku letu,” alisema Agai.Akachukua bunduki na

kushuka garini.Akaanza kutembea kwa tahadhari kuelekea mahala kulikowaka taa nyingi.

Kama walivyokuwa wamehisi.Ni kweli mahala pale ulikuwa ni uwanja wa ndege uliozungushiwa uzio wa wavu.Agai akakata uzio.Akapenya ndani ya uwanja.Karibu na jengo moja lililokuwamo mle uwanjani, akaiona ndege moja imeegeshwa taa ndani zimewashwa. Nje kulikuwa na wasichana wachache waliovaa sare za shule huku watu wanne waliokuwa na bunduki wakiwahimiza kupanda haraka haraka ndani ya ndege.Injini za ndege tayari zilikuwa zimewashwa kiashiria kwamba muda wowote ndege ingeweza kuondoka.

“Gosu Gosu alikuwa sahihi hatuwezi kuwasubiri askari polisi wafike kwani hawa jamaa wanaondoka.Nimepata wazo!” aliwaza Agai huku akiizinga bunduki yake.Akamlenga mmoja wa wale jamaa waliokuwa wanasimamia wasichana kuingia ndegeni.Akaanguka.Bunduki ile haikuwa na kiwambo cha kuzuia sauti ikawashtua. Wote wakageuka.

Agai akaitumia vyema nafasi hiyo akaanza kuwaangusha mmoja baada ya mwingine.Akabaki gaidi mmoja.Akapanda ngazi haraka na kuingia ndegeni.Agai akakimbia mbio kuelekea katika ile ndege.Alipoikaribia akawaona magaidi zaidi ya sita wakitoka ndani ya jengo moja wakikimbia

kuelekea iliko ndege.Mkononi wakiwa na bunduki.Akaachia risasi kadhaa, lakini wale magaidi wakaendelea kumuelekezea mashambulizi.Akaruka na kujificha nyuma ya ngazi ya ndege. Ghafla, likatokea gari moja kwa kasi kubwa na kufunga breki za ghafla kisha sehemu ya juu ikafunuliwa.Akajitokeza mtu akiwa na bunduki kubwa.Akaanza kuwamiminia risasi magaidi wale waliokuwa wanamfuata Agai.

“Ahsante Gosu Gosu,” alisema Agai.Akashtuka baada ya kuziona ngazi za ndege zikipanda taratibu. Ishara kwamba mlango unafungwa.Agai akaruka kama mshale na kuingia ndani ya ndege.Mlango ukafungwa huku ndege tayari ikiwa imeanza kuondoka.

Agai alipoingia ndegeni akapigwa na kitu kizito kwa nyuma ya kichwa.Fahamu zikampotea. Muda huohuo magari ya polisi yakawasili uwanjani hapo yakiwa yamejaza askari.Wakaanza kuikimbiza ile ndege kwa lengo la kuitungua.

“Kwa namna yoyote ile,hakuna kusimamisha ndege tunaendelea na safari!"alisema mmoja wa magaidi waliokuwamo mle ndegeni.Aliwaambia marubani wake. Ndege ikaongeza kasi taratibu ikaanza kupaa.

Huku akichechemea mguu, Gosu Gosu akashuka garini na kuwakimbilia askari akiwataka wasiishambulie ile ndege kwani ndani kuna wasichana wengine.Kamanda wa polisi mkoa wa

Arusha aliyeongoza operesheni ile akawataka askari wake kuiacha ndege iondoke.Akazungumza na mkuu wa jeshi la polisi na kumjulisha juu ya kile kilichotokea.

Magaidi wote waliokutwa pale uwanjani waliuawa na jumla ya wasichana arobaini waliokolewa.Gosu Gosu akamfuata kamanda wa polisi wa mkoa wa Arusha akamuomba wazungumze pembeni kidogo.

“Magaidi ni hawa hawa tu waliopatikana au kuna wengine wamehifadhiwa sehemu nyingine?" aliuliza Gosu Gosu

“Tuliofanikiwa kuwaua ni hawa wachache lakini upekuzi unaendelea hivi sasa kubaini kama kuna wengine

wamejificha au la," alijibu kamanda wa polisi.

"Tumechelewa.Kuna ndege nyingine imeondoka awali kabla ya hii.Nina imani viongozi wao waliondoka na ile ndege ya kwanza," alisema Gosu Gosu.

"Tayari zimetumwa ndege vita mbili hivi sasa zinaifuatilia ile ndege iliyoondoka na magaidi kujua inakoelekea," alisema kamanda wa polisi wa mkoa wa Arusha.Punde akatokea askari na kumueleza tayari kuna mwanafunzi mmoja anaweza kuzungumza.Wakaongozana na Gosu Gosu kuelekea katika chumba alimo huyo binti.Wakaanza kumuhoji maswali.Binti akawaeleza kisa chote

tangu walivyotekwa hadi walivyofikishwa mahali hapo.

“Mlikuwa sabini wengine wako wapi?" Gosu Gosu aliuliza.

“Wamechukuliwa na ndege.Kwanza waliwachukua wenzetu nane, wakachagua watoto wa viongozi akiwamo mtoto wa Rais wakaondoka nao.Baada ya muda, wakaja kuwachagua tena wengine ishirini wakaondoka nao.” alisema msichana aliyeokolewa.

“Walisema wanawapeleka wapi? Hamkusikia chochote" Gosu Gosu aliuliza.

“Walikuwa wanazungumza kwa lugha ya Kiarabu!” alijibu yule msichana.Simu ya Gosu Gosu

ikaita.Alikuwa Ruby.Akatoka nje na kuipokea.

“Hallow!” Gosu Gosu alisema.

“Gosu Gosu, poleni sana.Tumepata taarifa muda mfupi uliopita kutoka kwa Rais kwamba misheni imekamilika na watoto arobaini wameokolewa,” Ruby alisema.

“Ni kweli ,Ruby tumefanikiwa kuwakomboa watoto arobaini lakini tumechelewa.Viongozi wa magaidi wamefanikiwa kutoroka.Wameondoka na watoto ishirini na nane hivyo misheni bado inaendelea.Kamanda wa polisi mkoa wa Arusha ameniambia kwamba tayari ndege vita mbili zinaifuatilia ile ndege ya magaidi kujua inaelekea wapi.Misheni tutaikamilisha baada ya

kuwapata watoto wote kutoka mikononi mwa magaidi,” alisema Gosu Gosu.

“Gosu Gosu vipi wewe hali yako.Unaendeleaje?”

“Nilitoa zile risasi mbili mguuni.”

“Ulifanya nini?!” Ruby alishangaa

“Usishangae,Ruby.Nilitoa mwenyewe zile risasi mguuni.”

“Gosu Gosu, umefanya kitu cha hatari sana.Tafadhali wahi kwa daktari akuangalie huo mguu.”

“Usihofu,Ruby.Mambo kama haya tumeyazoea wakati nikiishi msituni.Kuna jambo lingine kubwa limetokea hapa,Ruby.”

“Jambo gani?”Ruby aliuliza Gosu Gosu akamueleza kuhusu Agai.

“Agai amefanya kitu cha hatari sana,” alisema Ruby.

“Nadhani lengo lake lilikuwa kuisimamisha ile ndege.Lakini sijui nini kilitokea, ndege ikapaa na kuondoka.Kwa hiyo kwa sasa tuna kazi ya kuwatafuta watoto na Agai.” alisema Gosu Gosu.Akanyamaza baada ya kamanda wa polisi mkoa wa Arusha kutoka ndani ya kile chumba.

“Ruby, nitakupigia tena baada ya muda,” alisema Gosu Gosu akakata simu,akamfuata kamanda wa polisi mkoa.Akamueleza kuna mwanamke aliyekuwa anashirikiana na magaidi yumo katika gari lake anahitaji matibabu ya haraka kwani bado SNSA wanahitaji kuendelea kumuhoji.Lilian akatolewa

upesi kutoka katika gari la Gosu Gosu na kuingizwa katika gari la wagonjwa.Likaondoka kwa kasi kubwa kumuwahisha hospitali huku askari wakilisindikiza.

Simu ya Gosu Gosu iliita.Akaitazama namba iliyokuwa inapiga. Akaelekea katika gari lake. Akaipokea.

“Hallow!”alisema Gosu Gosu.

“Gosu Gosu,naamini uko peke yako,”ilisema sauti ya upande wa pili ambayo Gosu Gosu aliitambua mara moja.

“Ndiyo.Unaendeleaje,Mathew?”

“Niko vizuri.Nimepata taarifa magaidi wamedhibitiwa na mateka wote wamekombolewa.”

“Ndiyo,Mathew.Tumefanikiwa kuwakomboamateka wote. vilevile tumefanikiwa kuwakomboa watoto zaidi ya arobaini waliokuwa wametekwa na magaidi,” alisema Gosu Gosu.

“Kazi nzuri sana.Vipi kuhusu Fabrice Kayembe?”Mathew aliuliza.

“Tulifanikiwa kumpata Fabrice Kayembe lakini tumempoteza dakika za mwisho kabisa,” Gosu Gosu alimweleza Mathew kila kitu kilichotokea hadi kuuawa kwa Fabrice.

“Utatusamehe,Mathew kwa hiki kilichotokea.Hata hivyo,tumejitahidi sana.Hatukutarajia kama tungempoteza Fabrice katika dakika za mwisho,” alisema Gosu Gosu kwa masikitiko.

“Usijali,Gosu Gosu.Mambo kama haya yanatokea.Huu si mwisho.Bado tuna kazi ya kufanya,” alisema Mathew.

“Nakusikiliza,Mathew!”

“Kwanza kabisa,nataka hilo sanduku jeusi litunzwe kwa gharama yoyote ile.Lihifadhiwe sehemu salama.Lisitoke katika mikono yako na asifahamu mtu kama unalo.Pili kuanzia sasa, msifanye mashirikiano yoyote na SNSA,”alisema Mathew.

“Kuna nini ndani ya sanduku hilo,Mathew?”

“Ni la muhimu sana.Tena tafadhali lihifadhi vyema. Kama haitoshi,asijue mtu yeyote mahala lilipo.Kesho hakikisha unafika nalo Dar es Salaam.Nitakupa maelekezo mengine

zaidi utakapokuwa Dar ” alisema Mathew.Akakata simu.

“Natakiwa kutibiwa huu mguu.Bila kufanya hivyo sitaweza kuendelea na misheni nyingine,” aliwaza Gosu Gosu.Akampigia simu Ruby.

“Gosu Gosu, tayari umepata matibabu?”Ruby aliuliza.

“Ruby, nilikwambia awali kwamba magaidi walifanikiwa kuvamia ofisi za SNSA Arusha wakamtorosha yule jamaa tuliyekuwa tunamshikilia,aliyetuelekeza mahala waliko watoto nyumbani kwa Sultan.Hata hivyo,tumefanikiwa kumuua.Changamoto iliyopo mpaka sasa hatujui mahala lilipo sanduku jeusi,” alisema Gosu Gosu.

“Japo kumekuwa na mafanikio makubwa katika misheni ya leo, lakini misheni kubwa kuliko zote imeshindwa kufanikiwa.Tumempoteza Fabrice Kayembe,tumeipoteza diski na mwisho kabisa sanduku. *We have nothing*,” alisema Ruby.

“Ruby, unaweza kwenda pembeni kidogo, mahali kusiko na watu tukateta kidogo?”Gosu Gosu aliuliza.

“Sawa.Nipe sekunde chache,” alisema Ruby.Akakata simu.Baada ya sekunde kadhaa, akapiga.

“Unasemaje, Gosu Gosu?”Ruby aliuliza.

“Ruby, nimewasiliana na Mathew Mulumbi.” alisema Gosu Gosu.

“Mathew? Amekupigia simu?”Ruby aliuliza kwa mshituko.

“Ndiyo.Amenipigia simu.Alitaka kufahamu kama misheni imefanikiwa au la.Nikamjulisha kilichotokea, namna tulivyompoteza Fabrice na ile diski,”alisema Gosu Gosu.

“Alisema nini baada ya kumueleza tumeshindwa kufanikiwa kumpata Fabrice Kayembe?”Ruby aliuliza kidadisi.

“Amesikitika sana.”

“Amekupa maelezo yoyote kuhusu Fabrice Kayembe kwamba ni nani?Na kwa nini akawa muhimu kwa magaidi?”Ruby aliendeleza ufukufuku wa taarifa.

“Hakusema chochote.Lakini amesema kesho atatoa tena misheni nyingine,” Gosu Gosu alijibu.

“*Again?*”Ruby aliuliza kwa mshangao.

“Ndiyo,Ruby!”

“Gosu Gosu, *I’m done*.Sitaki tena misheni nyingine yoyote ya Mathew Mulumbi!”Ruby alisema kwa hamaki.

“Ruby!”Gosu Gosu aliita kwa utulivu.

“Gosu Gosu, I’m done with Mathew.Sitaki kusikia tena kitu chochote kuhusu Mathew.Tumetekeleza misheni aliyoitoa bila kutoa maelezo yoyote kuhusu Fabrice Kayembe. Bado anataka kutoa tena misheni nyingine? Gosu Gosu, ninaanza kupoteza imani na

Mathew Mulumbi.Hukumuuliza kuhusu lile suala la yeye kuwepo katika ndege iliyopotea? Hukumuuliza yuko wapi?”Ruby aliongea mfululizo.

“Hakunipa nafasi,” Gosu Gosu alijibu.

“Gosu Gosu, mimi nadhani tumemaliza.Sitaki tuingie tena katika misheni nyingine ya Mathew Mulumbi ambayo hatujui chimbuko lake.Kwa sasa jitahidi upate matibabu kesho utarejea Dar es Salaam na kila kitu kitaishia hapo.Sehemu iliyobaki wataendelea SNSA,” alisema Ruby.Akakata simu.

Gosu Gosu akashusha pumzi,akashuka garini akaelekea katika hema ambako kulikuwa na madaktari waliokuwa wanatoa

huduma.Akajitambulisha kwamba amepigwa risasi mbili na akazitoa mguuni.Madaktari walibaki wanamtazama kwa mshangao halafu wakamlaza katika kitanda na kuanza kuyashughulikia majeraha yake.Wakati akiendelea kupatiwa matibabu, akatokea kamanda wa polisi mkoa wa Arusha.Akawataka madaktari wampe nafasi anataka kuzungumza na Gosu Gosu.

“Gosu Gosu, nimepigiwa simu na Ruby anataka kuzungumza nawe.”

“Ruby?” Gosu Gosu alishangaa.

“Ndiyo.Amesema nikupe simu yangu anataka kuzungumza nawe” alisema kamanda wa polisi wa mkoa.Akampa simu Gosu Gosu.

“Hallow,Ruby!”Alisema Gosu Gosu.

“Gosu Gosu, nimetumia simu nyingine kumpigia kamanda wa polisi wa mkoa ili utumie simu yake tuzungumze.Kuna mambo ambayo yanaendelea hapa SNSA kwa sasa nataka uyafahamu.”

“Kuna nini ,Ruby?”Gosu Gosu aliuliza kwa mshtuko.

“SNSA hawajui uchawi wangu katika mambo haya ya teknolojia.Nimegundua wamekuwa wakifuatilia simu yangu.Wanachunguza mawasiliano yangu.Wanasikiliza kila simu ninayopiga au kupigiwa.Nadhani wanafanya hivi kwa sababu ya lile suala la Mathew Mulumbi. Wanajua sisi tuna

ukaribu naye na wanataka sana kufahamu mahala alipo ndiyo maana wananichunguza.Uliponipigia nilizungumza kwa ukali namna ile ili kuwapoteza wale wanaotufuatilia, lakini siku maanisha yale niliyoyasema.Ninamuamini sana Mathew Mulumbi.Tunatakiwa kufanya kila tuwezalo kuhakikisha tunatimiza maelekezo yake.Nataka unieleze kwa kina alikueleza kitu gani Mathew alipokupigia?" Ruby aliuliza.

"Kuna jambo alielekeza.Anataka tulihifadhi lile sanduku jeusi sehemu ambako hakuna mtu atajayejua mahala lilipo.Amesisitiza tusishirikiane tena na SNSA"alisema Gosu Gosu.

“Hukumueleza kama sanduku nalo tumelipoteza?”Ruby aliuliza.

“Ruby,sanduku bado tunalo.Ni kweli magaidi walikuwa wamelichukua, lakini kwa sasa liko mikononi mwetu,”

“Ahsante kwa taarifa hii, Gosu Gosu.Nilifadhaika sana uliponiambia magaidi wamelichukua.Kama alivyoelekeza Mathew, hakikisha sanduku linafika salama Dar es Salaam ili tulihifadhi.Kuna ndege ya jeshi inaondoka usiku huu inakuja Dar es Salaam.Tayari nimekwisha fanya mpango.Utaondoka na ndege hiyo.Kamanda wa polisi Arusha atakupa maelekezo,” alisema Ruby.

“Ahsante,Ruby.Vipi kuhusu yule mwanamke Lilian? Tunamuacha?Yule

anaweza akatusaidia sana katika kuufahamu mtandao wa hawa magaidi ili tuweze kufuatilia na kufahamu alipo Agai" Aliuliza Gosu Gosu.

"Huyo ataendelea kuwa katika mikono ya jeshi la polisi.Watambana atawaeleza kila kitu.Sisi misheni yetu imemalizika.Jitahidi kwa kila uwezavyo sanduku jeusi liweze kufika salama," alisema Ruby.Akaagana na Gosu Gosu kisha akamrejeshea simu kamanda wa polisi mkoa wa Arusha.

"Naamini tayari,Ruby amekupa maelekezo," alisema kamanda wa polisi mkoa wa Arusha.

"Ndiyo.Amenipa.Saa ngapi tunaondoka?"Gosu Gosu aliuliza.

“Ndani ya saa moja kutoka sasa ndege itaondoka,” kamanda alijibu huku akiitazama saa yake.Gosu Gosu akaendelea kupatiwa matibabu.

10

DAR ES SALAAM.
OFISI ZA SNSA
(SECRET NATIONAL SECURITY AGENCY)

“Maurine,misheni yetu mimi na Gosu Gosu imemalizika.Tulihitaji kumuokoa Fabrice Kayembe,lakini tumeshindwa kufanikisha misheni hiyo.Fabrice ameuawa,tumeikosa diski muhimu na sanduku jeusi pia.Mimi na Gosu Gosu kwa hapa tulipofika tunakabidhi kila kitu kwenu SNSA.Mtaendelea kumalizia kile kilichobaki.Bado kuna mengi ambayo

SNSA mnatakiwa kuyafanya.Tunawashukuru sana kwa ushirikiano wenu," alisema Ruby.

"Ruby, sina cha kusema japo ninatamani sana muendelee kushirikiana nasi," alisema Maurine.

"Maurine, hapa ni nyumbani.Muda wowote tukihitajika tutakuja, lakini kwa sasa jukumu letu limemalizika tunawaachia ninyi muendelee." alisema Ruby.

"Ruby,tumejifunza mengi kutoka kwenu.Bila ninyi yawezekana muda huu tusingewapata wasichana arobaini.Imekuwa siku ya mafanikio makubwa kwetu.Japo tumewapoteza watu wetu, lakini tumefanikiwa kuwakomboa mateka.Hivi sasa tayari

nimetuma timu inaelekea Arusha.Kila kitu kitakaa sawa,”alisema Maurine.

“Ahsante sana,Maurine.Kabla sijaondoka, nataka kuwasiliana na Rais nimuage,” alisema Ruby.Maurine akampigia simu Rais kwa kutumia simu yake.

“Maurine,” Jenerali Pius alisema.

“Mheshimiwa Rais, ni mimi Ruby!”

“Aah, Ruby!Nilikuwa najiandaa nije SNSA usiku huu kuwashukuru kwa kazi kubwa mliyoifanya leo.Hongereni sana kwa kufanikiwa kuwakomboa mateka.”

“Mheshimiwa Rais, ni kweli kazi imefanyika kubwa, lakini bado pia kazi iliyobaki ni kubwa.Kama ulivyosikia watoto ishirini na nane bado wanaendelea kushikiliwa na

magaidi.Mimi na mwenzangu Gosu Gosu tumekamilisha misheni yetu.Nimekupigia simu hii kukushukuru kwa kutuamini na kutupa nafasi.Sehemu iliyobaki itaendelea kufanywa na SNSA na idara nyingine" alisema Ruby.

"Ruby, mimi ndiye ninayepaswa kuwashukuru kwa kazi kubwa mliyoifanya.Hasa kwa kushirikiana kwenu na SNSA na vyombo vingine.Japo misheni ya kumuokoa Fabrice imeshindikana, lakini tumefanikiwa kuwaokoa watoto wetu na mateka waliokuwa wanashikiliwa na magaidi katika ukumbi wa KICC. Hilo si dogo hata kidogo.Kesho, Gosu Gosu, ataletwa Dar es Salaam kupatiwa matibabu.Nitapenda kuonana naye

kumshukuru kwa ushujaa wake wa kukubali kuingia katika jengo lile.Kuhusu Agai, tunaendelea kufuatilia ndege aliyopanda.Kwa taarifa tuliyoipata hivi punde ni kwamba ndege hiyo kwa sasa inaonekana inaelekea nchini Kenya.Ndege za jeshi zinaifuatilia ndege hiyo kwa umakini mkubwa.Tutahakikisha tunamuokoa Agai na watoto wote walioko ndani ya ndani ya ndege.” Alisema Rais Pius

“Ninashukuru sana,Mheshimiwa Rais.Nakutakia usiku mwema,” alisema Ruby.Akaagana na Rais.Maurine alimsindikiza Ruby hadi nje katika gari lake.Akaondoka rasmi katika ofisi hizo.Dakika mbili baada ya Ruby kuondoka, kukatokea mlio fulani katika

simu yake.Chapchap akaweka kifaa sikioni,Akabonyeza sehemu katika simu yake na kuanza kusikiliza mazungumzo.

“Maurine, nipe taarifa!” ilisikika sauti ya Rais Jenerali Pius.

“Mheshimiwa Rais, tayari Ruby amekwisha ondoka.Nimepokea taarifa kutoka kwa watu wangu niliowaweka kumfuatilia Ruby kama ulivyoelekeza,” alisema Maurine.Ruby akashtuka.

“Kumbe Rais ndiye aliyeelekeza tuchunguzwe,” Ruby alishangaa.

“Wamepata nini watu wako?”Jenerali Pius aliuliza.

“Ruby na Gosu Gosu walizungumza usiku huu,” alisema Maurine.Akacheza mazungumzo ya Ruby na Gosu Gosu kupitia spika zilizopo katika mitambo ya

mezani katika ofisi za SNSA. Rais akayasikia.

“Kazi nzuri sana,Maurine. Endeleeni kuwafuatilia tutagundua mengi,” alisema Jenerali Pius.

****

Ikulu jijini Dar es Salaam,Rais Pius alikuwa na kikao kizito na mkuu wa majeshi pamoja na wakuu wa vikosi mbali mbali vya jeshi.Wakati kikao kikiendelea,mkuu wa majeshi akapigiwa simu.Akaipokea na kuzungumza na yule aliyempigia halafu akamgeukia Rais.

“Mheshimiwa Rais,nimetaarifiwa kwamba ndege vita zetu zilizokuwa zinaifuatilia ile ndege iliyowatorosha

magaidi zinakaribia kufika katika anga la Kenya.Kiitifaki, hawataweza kuingia katika anga la nchi nyingine bila kibali.Hivyo tunakuomba uzungumze na Rais wa Kenya aweze kutoa kibali cha kuruhusu ndege zetu ziendelee kuifuatilia ndege hiyo ya magaidi" alisema mkuu wa Majeshi.Jenerali Pius hakuchelewa.Akachukua simu yake na kumpigia Rais wa Kenya Bwana Daniel Mwangi.

"Mheshimiwa Rais, habari za usiku huu," alisema Jenerali Pius.Ni baada ya Rais Daniel Mwangi kupokea simu.

"Nzuri Jenerali Pius.Poleni na yale yanayoendelea huko Tanzania.Pia hongereni kwa kufanikiwa kuwadhibiti magaidi," alisema Rais Daniel.

“Ahsante,Mheshimiwa Rais.Tumefanikiwa kuwadhibiti magaidi na kuwakomboa wasichana waliokuwa wametekwa. Bahati mbaya, viongozi wa magaidi hao wamefanikiwa kutoroka huku wakichukua baadhi ya wasichana.Hivi tuzungumzavyo ndege waliyopanda iko angani inakaribia kuingia katika anga la Kenya.Ndege vita mbili kutoka kikosi chetu cha anga zinaifuatilia ndege hiyo waliyopanda magaidi.Pindi itakapoingia katika anga la Kenya, ndege zetu zinazoifuatilia ndege hiyo hazitaweza kuingia.Hivyo nimekupigia kuomba ruhusa ndege zetu za vita ziruhusiwe kuingia katika anga la Kenya kwa minajili niliyokueleza,” alisema Jeneral Pius.

“Jeneral Pius, si rahisi kutoa maamuzi ya haraka katika jambo hili.Kama unavyojua zipo taratibu za kufuata ili kuruhusu ndege hizo ziweze kuingia kaika anga la Kenya na kuendelea na operesheni yake,” alijibu Rais Daniel Mwangi.Akakatishwa na Jeneral Pius.

“Mheshimiwa Daniel, sioni ugumu wowote katika suala hili.Kinachofanywa na ndege zetu ni kuifuatilia tu ndege hiyo na kujua inakoelekea.Hakuna operesheni yoyote ya kijeshi itakayofanyika naomba unielewe kwa hilo.”

“Nimekuelewa, Jenerali Pius.Lakini bado jambo hili si rahisi linahitaji muda zaidi.Ninachokushauri kwa kuwa ndege hiyo inaelekea katika anga la Kenya,

tuachie sisi jukumu hilo.Vikosi vya anga vya jeshi la Kenya vitaendelea kuifuatilia ndege hiyo na kujua inakoelekea,”alisema Rais Daniel.

“Mhemshimiwa Rais Daniel, ndani ya ndege hiyo kuna wasichana waliotekwa na magaidi.Hatujui wanapelekwa wapi.Tunahitaji kuifutilia ndege hiyo, tafadhali, ”alisisitiza Jenerali Pius.

“Mheshimiwa Rais, ndege hiyo itakapoingia katika anga la Kenya litakuwa jukumu la vikosi vya Kenya kuifuatilia na kujua inakoelekea. Na kama ikiwezekana, basi tutawaokoa watoto wote waliomo katika ndege hiyo.Ninaomba uwe na imani na vikosi

vyetu vitaifanya kazi hiyo," alisema Rais Daniel.

"Mheshimiwa Rais Daniel, kuna ugumu gani kuruhusu ndege zetu zifanye kazi ya kuifuatilia ndege hiyo? Au unataka niziingize kwa nguvu ndege zetu katika anga la Kenya?"Jenerali Pius aliuliza kwa ukali.

"Mheshimiwa Rais Pius, naomba nikuweke wazi kwamba ndege za vita za Tanzania zitakapoingia katika anga la Kenya bila ruhusa utakuwa ni uvamizi na zitatunguliwa!"

"Hamuwezi kutungua ndege zetu!"alisema kwa ukali Jenerali Pius.

"Mheshimiwa Rais, ninakueleza ukweli usijaribu kutumia nguvu katika suala hili.Tuachie sisi jambo hili pale

ndege hiyo itakapoingia katika anga letu itakuta tayari vikosi vimejipanga vyema na wataanza kuifuatilia hatimaye kuwaokoa watoto.Naomba mheshimiwa Rais tusilifanye jambo hili kuwa kubwa," alisema Rais Daniel Mwangi.

"Sawa,Mheshimiwa Rais.Maafisa wetu wa jeshi la anga watawasiliana na wenzao wa Kenya ili zoezi la kuifuatilia ndege hiyo liendelee pale itakapoingia Kenya," alisema Jenerali Pius.

"Ahsante sana, Jenerali Pius.Nitakujulisha kila kinachoendelea," alisema Rais wa Kenya na kukata simu.Jenerali Pius akiwa ameikunja sura yake, akamtazama mkuu wa majeshi.

"Amekataa ndege zetu zisiingie katika anga la Kenya kuwafuata magaidi.

CDF nini ushauri wako?” Jenerali Pius aliuliza

“Alichokisema Rais Mwangi ni sahihi kabisa.Hatuwezi kuingiza ndege zetu za vita ndani ya anga lao bila kufuata taratibu.”

“Lakini tunawafuatilia magaidi ambao wamekuwa wakiendesha mashambulio hata nchini Kenya kwenyewe,” Jenerali Pius alisema kwa hamaki.

“Pamoja na hayo,Mheshimiwa Rais, lakini hatuwezi kutumia nguvu katika suala hili.Tunaweza kuanzisha mgogoro mwingine mkubwa.Tufanye kama alivyoshauri kwamba tuviachie vikosi vya Kenya viendelee kuwafuatilia.

Halafu watupe taarifa," alisema mkuu wa majeshi.Kikao kikaendelea.

****

Ndege vita za kikosi cha anga cha Tanzania zilizokuwa zinaifuatilia ndege iliyowabeba wasichana waliotekwa na magaidi,ziligeuza baada ya ndege ile kuingia katika anga la Kenya.Hakukuwa na ndege nyingine yoyote iliyoifuata ndege ile ya magaidi ilipoingia Kenya.

Ndani ya ndege,Agai alizinduka na kujikuta akiwa amefungwa pingu katika chuma ndani ya chumba kidogo.

"Nahisi bado tuko angani.Lazima nitafute namna ya kufanya kujiokoa.Endapo ndege ikitua hawa

magaidi hawataniacha hai," aliwaza nafsini.Akakohoa mfululizo.Mlango wa kile chumba ukafunguliwa.Wakaingia magaidi wawili.

"Umeamka! Ungeomba fahamu zikupotee milele usizinduke.Maana unachokwenda kukutana nacho ni kitu ambacho hukuwahi kukishuhudia katika maisha yako.Tumekushuhudia ukiua wenzetu na sasa ni zamu yako nawe tutakutoa uhai kama ulivyowatoa wenzetu. Kwako itakuwa tofauti kidogo.Utakufa kwa mateso makali zaidi!"alisema mmoja wa magaidi.Akamlamba Agai kofi zito la usoni.

"Wewe si nd'o unajifanya shujaa wa Tanzania? Siku zote mashujaa hufa

kwanza.Endelea kuvuta pumzi ya mwisho muda wako wa kuivuta hewa hii safi unakaribia kumalizika," alisema kwa kejeli na maudhi gaidi mwingine.

"Naombeni maji ya kunywa!"alisema Agai kwa sauti dhaifu.Magaidi hawakujali. Zaidi wakaangua kicheko kikubwa.

"Tangu lini maiti akaomba maji?" Alijibu mmoja wa magaidi. Wakaendelea kucheka kisha mmoja akafungua zipu ya suruali yake na kumjolea Agai usoni.Alipomaliza, wakaufunga mlango, wakaondoka.

"Hawa jamaa wanamaanisha kile wanachokisema. Kama nisipojitajidi wataniua.Lazima nitafute mbinu ya kujiokoa na kuwaokoa wale wasichana,"

aliendelea kuwaza Agai.Akaanza kukohoa tena mfululizo.Mlango ukafunguliwa.Akaingia gaidi mmoja.Akamuona Agai akitetemeka, akadhani anakata roho. Hilo likamzubaisha gaidi.Akamfuata na kumfungua pingu alizokuwa amefungwa mikononi.Ghafla,Agai akageuka kama mbogo.Akamtandika gaidi kichwa kizito, akapepesuka.Hakumpa nafasi, akamuongeza tena ngumi mbili mfululizo.Gaidi akahisi kizunguzungu.Kwa kasi ya ajabu, akamgeuza na kumkaba kabali nzito.Gaidi akajitahidi kufurukuta, lakini taratibu akaanza kulegea.Agai akamuachia,gaidi akaenda chini kama furushi.

“Ahsante Mungu” alisemaAgai na kuichukua bastola ya gaidi aliyemuua.Taratibu akaufungua mlango na kuchungulia nje, akawaona magaidi wawili wakiwa wamesimama wakizungumza.Hawakuwa na wasiwasi wowote.Hawakujua kama mwenzao tayari ameuawa.

Agai akaufungua mlango zaidi na kutoka.Akatazama upande mwingine, hakukuwa na pilika. Akarejesha jicho lake tena kwa wale magaidi halafu akawashtua.Wakageuka. Ghafla wote wakapeleka mikono yao zilipo bastola zao, lakini haikusaidia kitu.Agai alikuwa mwepesi sana, akaizinga bastola haraka na ikasikika milio ya risasi.Wale magaidi wawili wakaanguka chini.Akawafuata na

kuwaongezea risasi kadhaa. Ikiwa ni kuhakikisha wote wamekufa.

Wanafunzi walipiga kelele baada ya kusikia milio ile ya risasi.Akawatuliza na kuwahakikishia kwamba yuko pale kwa ajili ya kuwaokoa.Akawauliza magaidi walikuwa wangapi mle ndani ya ndege wakamjibu walikuwa watatu.Moja kwa moja Agai akawafuata marubani.

“Tunageuza ndege kurejea tulikotoka,” alisema Agai akiwaelekezea bastola.

“Mafuta yaliyomo ndegeni ni kidogo sana hayawezi kutufikisha kokote.Ili tuweze kurejea tulikotoka, tunapaswa kuongeza mafuta.Upo uwanja wa karibu na hapa tulipo.Tunaweza kutua na kuongeza mafuta halafu tutarejea

tulikotoka," alisema mmoja wa marubani.

Agai hakuwa na jinsi. Ilibidi tu akubali maana hakuwa na utaalamu wowote kuhusu masuala ya ndege.Akabariki kishingo upande ushauri wa wale marubani kwamba ndege itue katika uwanja mdogo wa chuo cha kujifunzia urubani na ufundi wa ndege kilichopo Mombasa.

Agai akawafuata wanafunzi na kuwahakikishia kwamba watakuwa salama. Ndege itatua kwa muda mfupi kujaza mafuta halafu watarejea Tanzania.Baada ya kuwapa moyo wale wanafunzi, akawafuata marubani na kuwataka wampatie simu.Mmoja wa marubani akatoa simu na

kumpa.Kichwani kwa Agai kulikuwa na namba moja tu aliyoikumbuka.Ni namba ya idara ya ujasusi Tanzania alikokuwa akifanya kazi hapo awali.Akaiandika katika ile simu iliyokuwa inatumia mtandao wa Kenya.Akapiga.

“Naomba Mungu namba hii iwe bado inatumika,” Agai aliwaza wakati akijaribu kupiga simu.Simu ikaanza kuita.

“Ahsante Mungu!” alisema Agai. Haikuchukua muda, simu ikapokelewa.

“Hallow!”

“Hallow, hapo ni Shirika la UjasusiTanzania?”

“Ndiyo.Nikusaidie nini?”

“Naitwa Agai Sempa.Nimewahi kufanya kazi hapo.Ninataka kuzungumza

na mkurugenzi tafadhali.Ni muhimu sana na haraka," Agai alisema upesi.

"Subiri kidogo!" alisema mwanadada aliyepokea simu.Baada ya sekunde chache, ikasikika sauti ya kiume,

"Hallow!"

"Hallow, mkurugenzi!"

"Mkurugenzi hayupo nipo mimi badala yake.Unasemaje?"aliuliza jamaa aliyepokea simu. Hakujitambulisha jina lake.

"Niko katika ndege ya magaidi.Kuna wasichana ishirini ndani ya ndege hii wametoroshwa na magaidi nimefanikiwa kuwaua magaidi wote, lakini ndege haina mafuta ya kutosha kurudi Tanzania.Nataka umjulishe Rais wa

Tanzania kuwa niko salama wa salmini.Cha muhimu azungumze na rais mwenzake wa Kenya. Amjulishe kwamba tunakaribia kutua katika uwanja mdogo wa ndege wa chuo cha kufundisha urubani na ufundi wa ndege Mombasa kwa ajili ya kujaza mafuta.Tunaomba ulinzi na kama ikiwezekana tupatiwe ndege nyingine tuweze kuwarejesha nyumbani wanafunzi hawa.”

“Sawa,Agai.Tunamjulisha Rais sasa hivi,” alijibu jamaa kutoka idara ya ujasusi.Wakati huo, tayari ndege ilianza kutua katika uwanja mdogo wa Mombasa,uliokuwa na taa za kuwezesha ndege kutua hata usiku.

Mara tu ndege ilipotua, marubani wakashuka kwa ajili ya kwenda kushughulikia suala la mafuta.Ghafla yakatokea magari sita yaliyokuja kwa kasi.Kutoka katika magari yale, wakashuka watu wenye silaha nzito.Wakakimbia kuelekea ndegeni.

“Oh my God! Kumbe ulikuwa mtego! Alisema Agai.

“Wako wengi na wana silaha kali siwezi kupambana nao,” Agai aliendelea kuwaza. Magaidi wakaingia ndani ya ndege.Agai akaweka chini bastola yake.Wakamfunga pingu na kumshusha chini.Wasichana wote nao wakashushwa chini,wakawaingiza katika magari halafu wakaondoka kwa kasi sana eneo lile.Wakati Agai akishushwa, aliwaona

wale marubani wakizungumza na mmoja wa watu waliokuja na yale magari kisha akawakabidhi bahasha ambayo mmoja wa marubani akaifungua.Akatoa bunda la noti.Akaanza kuzihesabu kisha wakaingia katika mojawapo ya gari.

Jenerali Pius alipopata taarifa za Agai kutoka Shirika la Ujasusi, hakupoteza muda.Akampigia simu Rais Daniel Mwangi, lakini simu haikupokelewa.Akajaribu zaidi ya mara nne bila mafanikio.

“Hataki kupokea simu kwa kuwa anajua kitu alichokifanya.Alikataa ndege zetu zisiingie nchini Kenya kwa ajili ya kufuatilia ndege ya magaidi.Akatoa ahadi bandia ya vikosi vya Kenya vingefuatilia ndege hiyo kumbe

alinidanganya na hakufanya hivyo," alisema Rais Pius kwa hasira.Akainamisha kichwa chini.Akazama mawazoni kwa sekunde kadhaa, halafu akainua kichwa.Akawatazama majenerali wake wa jeshi.

"Tunakwenda kuwakomboa watoto wetu.Agai amefanya kazi kubwa ya kuwaua magaidi na kuidhibiti ndege yao.Rais wa Kenya, ambaye kwa hakika angeweza kutupa msaada wa haraka, hapokei simu.Hivyo nimefanya maamuzi magumu kama amiri jeshi mkuu. Sasa rasmi ninapeleka wanajeshi nchini Kenya kuhakikisha usalama wa watoto wetu," alisema Jenerali Pius.

“Mheshimiwa Rais sidhani kama hilo ni wazo zuri,” alisema mkuu wa majeshi.

“Hatuna namna ya kufanya.Ni lazima tupeleke wanajeshi haraka sana kuokoa watoto wetu.Agai amekwisha idhibiti ndege ya magaidi na yuko peke yake anawalinda watoto.Tunatakiwa kumpa msaada wa haraka sana.Kama tukichelewa, tunaweza kuwapoteza watoto.Nataka ndani ya muda mfupi ujao vikosi vya jeshi kutokea Tanga vielekee Mombasa mahala waliko watoto wetu na kwenda kuwachukua.Sijali kitakachotokea.Ninachohitaji ni kuwapata watoto wetu tu, basi.Kama kutaibuka mgogoro wowote na Kenya, basi nitashughulika nao,” alihitimisha

Rais Pius kwa sauti yenye amri.Mkuu wa majeshi akasimama na kupiga saluti. Ikiwa ishara ya kuyapokea maelekezo yale ya Rais wake.

11

DAR ES SALAAM

Ndege ya jeshi iliwasili jijini Dar es Salaam saa tisa za usiku ikitokea jijini Arusha.Ruby alikuwepo katika uwanja wa ndege wa jeshi akimsubiri Gosu Gosu aliyekuwemo ndani ya ndege hiyo.Lango la nyuma la ndege lilifunguliwa na maafisa wa jeshi wakaanza kushuka mmoja baada ya mwingine. Gosu Gosu naye akashuka taratibu akiwa na mkoba wake begani huku nyuma yake mwanajeshi mmoja akimsaidia kubeba sanduku jeusi.

“Gosu Gosu!”Ruby aliita huku akimfuata.Gosu Gosu hakuamini kama

Ruby alikuwepo uwanjani pale akimsubiri. Hasa nyakati hizo za usiku mnene.Kwa furaha tele, wakakumbatiana.

“Pole sana, Gosu Gosu!”

“Ahsante,Ruby!Sikutarajia kama ungekuwepo hapa uwanjani muda huu,” alisema Gosu Gosu.

“Tutazungumza baadaye.Liko wapi sanduku?”Ruby aliuliza.Gosu Gosu akageuka nyuma yake. Kulikuwa na mwanajeshi amelibeba lile sanduku.Ruby akalifuata na kulichukua.Akalipeleka katika gari lake. Kwa hadhari na umakini mkubwa, akalifungia katika buti la gari yake halafu akawashukuru maafisa wa jeshi

waliokuja na Gosu Gosu kisha wakaondoka pamoja.

“Vipi maendeleo yako, Gosu Gosu?”Ruby aliendelea kumjulia hali Gosu Gosu.

“Nilipatiwa matibabu, lakini bado nahitaji kuonana na daktari.Maumivu ningali nayahisi ni makali mno.Ninatembea kwa sababu tu, mimi ni mwanajeshi sipaswi kulalamika,”alisema Gosu Gosu.

“Pole sana.Ilikuwa misheni ya hatari.Maadam umerejea salama, ni jambo la kumshukuru Mungu.Huku nilikuwa ninasali kimya kimya kumuomba Mungu utoke salama ndani ya ukumbi ule. Maana si jambo dogo

kuingia ndani ya mdomo wa Mamba,”alisema Ruby.

“Ni kweli,Ruby.Ilikuwa misheni ya hatari sana. Japo haikwenda kama tulivyotarajia, lakini mafanikio yapo. Si haba. Tumempoteza Fabrice na ile diski. Bado tumewakomboa mateka na watoto arobaini.Haya ni mafanikio makubwa yanayostahili kupigiwa makofi. Hata hivyo, inaonekana kazi ndiyo kwanza imeanza.Mbele yetu, kuna kazi kubwa imebaki,” alisema Gosu Gosu.

“Laiti kama tungefahamu Fabrice Kayembe alikuwa nani, na nini mahusiano yake na magaidi ingeweza kutufumbua macho.Gosu Gosu, bado tuna maswali mengi ya kujiuliza na kuyatafutia majibu sisi wenyewe kabla

ya Mathew hajatupa majibu yake.Kwanza ni kuhusiana na hili sanduku.Lina nini ndani yake? Kwa nini likawa muhimu sana kwa magaidi?Ile diski ina kitu gani ndani yake? Kwa nini shambulio kubwa kama lile ambalo limemwaga damu ya watu wasio na hatia iwe ni kwa ajili ya vitu hivi viwili diski na hili sanduku?”Ruby aliuliza maswali mengi mfululizo. Katika hali ya kutafuta jibu sahihi kwa Ruby,Gosu Gosu akakumbuka kitu.

“Kuna kitu nimekumbuka,Ruby.Makachero wa SNSA waliokwenda kulichukua hili sanduku walikuta maiti ya mtu.Ndani ya hiyo nyumba,walimolikuta sanduku,kulikuwa na mkoba mdogo

pembeni ya kitanda.Ndani yake kulikuwa na nyaraka za kusafiria.Ilikuwa kama bahati tu, niliwahi kuuchukua mkoba huo mapema katika ofisi za SNSA Arusha.Nimekuja nao hapa," alisema Gosu Gosu.Akaufungua mkoba wake.Ndani yake akatoa mkoba mdogo mweusi.Akampa Ruby.

"Kuna uwezekano mkubwa kwamba mkoba huu ni wa huyo mtu aliyekutwa amefariki ndani ya hiyo nyumba.Nini kilimuua mtu huyo?"Ruby akazua swali.

"Hakuna anayejua hadi uchunguzi ufanyike.Lakini wanadai walikuta joka kubwa ndani ya chumba hicho.Yawezekana kabisa pengine mtu huyo aliumwa na nyoka na hatimaye kupoteza maisha," Gosu Gosu alijibu.

“Hiyo ni sehemu nzuri ya kuanzia uchunguzi wetu, Gosu Gosu.Huyo mtu kwa namna yoyote ile, lazima alikuwa na mahusiano na hili sanduku jeusi.Pengine yawezekana alifika hapo kwa ajili ya kulichukua au kuna kitu alikwenda kukifanya.Tukishamfahamu ni nani, ametokea wapi tunaweza kupata mwanga kuhusiana na Fabrice na hili sanduku jeusi.Tukienda taratibu tutaipata picha kamili ya kile kinachoendelea hapa nchini.Kitu pekee kinachokula akili yangu kwa sasa ni kuhusiana na ndege iliyopotea ambayo inadaiwa Mathew Mulumbi alikuwemo ndani yake.Je, ni kweli alikuwemo ndani ya ndege hiyo? Kama alikuwemo. ndege iko wapi? Haya maswali ni magumu sana.Mtu pekee

anayeweza kutupa majibu ni Mathew ambaye kwa sasa hatujui mahala aliko," alisema Ruby.Akapunguza mwendo wa gari kidogo halafu,akacheza mazungumzo ya simu ya Rais Pius na Maurine Kyaso. Gosu Gosu akatahayari sana. Hakuamini alichokisikia.

"Nataka ufahamu tu kwamba hatuko salama.Jamaa wanatufuatilia.Wakiona wameshindwa kupata kitu katika mawasiliano yetu, basi wataweka watu wa kutufuatilia kila tunachokifanya.Ndiyo maana nataka tufanye haraka sana kufanya uchunguzi wa hili suala na tupate majibu yake haraka sana tujue ni nini kinaendelea," Ruby alisema.

****

Walifika nyumbani kwa Ruby,Gosu Gosu akakaribishwa ndani.Sebuleni walikumta mwanadada mmoja aliyekuwa amejilaza sofani.

“Maria samahani sana kwa kukuweka hadi muda huu.Ndege ilichelewa kuondoka Arusha,” alisema Ruby kwa unyenyekevu akimwambia yule mwanadada waliyemkuta sebuleni.

“Usijali,Ruby! Huyu ndiye mgonjwa mwenyewe?”Maria aliuliza.

“Ndiye.Anaitwa Papi Gosu Gosu,” Ruby alisema kwa kutia nakshi kidogo. Maria likamponyoka cheko kidogo.

“What a name.Gosu Gosu!” Maria alisema kwa kulitaja jina la Gosu Gosu. Yamkini alistaajabishwa na jina hilo. Kicheko kilitamalaki usoni pake. Ikawa zamu ya Ruby kumtambulisha Maria mbele za Gosu Gosu.

“Gosu Gosu, huyu ni rafiki yangu anaitwa Dr Maria.Yuko hapa hapa kwa ajili ya kuhudumia jeraha lako,” Ruby alisema.

“Ahsante sana,Ruby.Nashukuru kukufahamu Dr. Maria,” Gosu Gosu alitoa kauli. Ruby akamuongoza katika chumba walichokuwa wamekiandaa. Dr. Maria akaanza kulichunguza jeraha la Gosu Gosu. Wakati Gosu Gosu akipatiwa matibabu,Ruby akaingia katika ofisi yake.Akaketi kitini.

“Nimechoka sana, lakini bado tuna kazi kubwa ya kufanya,” aliwaza huku akiufungua ule mkoba mdogo aliopewa na Gosu Gosu.Ndani yake kulikuwa na hati ya kusafiria yenye jina la Amos Jackson Ntuyahaga.Raia wa Rwanda.Hati yake ya kusafiria ilionesha alikuwa amesafiri katika nchi mbali mbali za Ulaya.Nchi ya mwisho kutembelea kabla ya kuingia Tanzania ilikuwa Ufaransa.

Ruby akaingia kazini kutafuta taarifa za Amos Ntuyahaga.Taarifa alizozipata kuhusu Amos ni kwamba, aliingia nchini akitokea Ufaransa.Aliwasili nchini kwa ndege ya shirika la ndege la Ethiopia. Akashukia katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Kilimanjaro.Hiyo ilikuwa

mwezi mmoja kabla ya kufanyika kwa mkutano wa *Afrika Asili Yangu*.

“Je, mtu huyu ana mahusiano yoyote na hili sanduku jeusi? Nini kilimleta hapa nchini? Ana mahusiano yoyote na Fabrice Kayembe?”Ruby alijiuliza maswali.Akaendelea kupekua nyaraka alizozikuta katika ule mkoba aliopewa na Gosu Gosu,akakutana na karatasi ndogo iliyokuwa na namba ya simu.

“Hii namba si ya Tanzania.Ni namba ya mtandao wa Amanicom wa Rwanda,” Ruby aliwaza huku akifuatilia ile namba.Akagundua ni ya Joseph Nahimana.

“Joseph Nahimana.Ni nani huyu mtu?” aliendelea kujiwazia akilini.

Akaachana kwanza na suala

lile,akatoka na kumfuata Gosu Gosu.Alimkuta Dr. Maria akimalizia kumfunga jeraha lake.Ruby akaenda chumbani kwake na kurejea na bahasha iliyotuna ikiwa na fedha ndani.Akampatia Dr. Maria kisha akamshukuru.Akamtaka arudi tena siku inayofuta kuja kuangalia maendeleo ya Gosu Gosu.Dr. Maria akawaaga, akaingia katika gari lake na kuondoka.

“She’s very pretty!”alisema Gosu Gosu huku akichanua tabasamu mwanana.

“Gosu Gosu, tafadhali usianze mambo yako.Tuna kazi kubwa inatukabili mbele yetu,” alisema Ruby akionesha uzito wa jambo lenyewe.Wakaenda ofisini kwake.

“Kuna nini ndani ya sanduku hili?”Gosu Gosu aliuliza.Akaenda kulitazama sanduku kwa umakini zaidi.

“Magaidi walifanya shambulio lile wakimlenga Fabrice Kayembe na lengo kuu likiwa ni kulipata sanduku hili.Lina nini dani yake?Bomu?”Gosu Gosu aliuliza.Ruby akasimama na kwenda kulitazama sanduku.

“Ni sanduku la aina yake.Sijawahi kuliona sanduku kama hili,” alisema Ruby akiendelea kulichunguza.

“Hakuna mahala pa kufungulia.Lina sehemu moja tu, ya kuchomeka diski.Nadhani ndiyo ile diski mweko aliyokuwa nayo Fabrice Kayembe.Pengine ndiyo funguo ya sanduku.Bila ile, hatuwezi

kulifungua.Hivyo tukitaka kulifahamu sanduku hili basi lazima tuipate ile diski" alisema Ruby.

"Ruby, wewe ni mchawi wa mambo haya ya teknolojia.Huwezi ukafanya chochote tukaweza kulifungua sanduku hili?"Gosu Gosu aliuliza

"Ningejaribu kama ningekuwa nalifahamu sanduku hili ni la kitu gani.Lakini siwezi kufanya chochote bila kufahamu kile ninachokifanya.Gosu Gosu,hili sanduku lazima linafunguliwa kwa program maalum iliyomo katika ile diski.Kwa namna yoyote ile, lazima tuipate ile diski ni muhimu sana," alisema Ruby kwa msisitizo.

"Gosu,tayari ni usiku mwingi sasa. Naomba tupumzike kwa muda huu

mfupi, kabla ya mapambazuko ili tuendelee na majukumu yetu.Kitu kikubwa tumelifikisha salama sanduku kama alivyoelekeza Mathew.Utalala hapa hapa katika chumba cha wageni.Huna haja ya kurudi nyumbani kwako," alisema Ruby.Akamsindikiza Gosu Gosu kwenda katika chumba cha wageni.

MOMBASA - KENYA

Helkopta nne za jeshi la wananchi wa Tanzania ziliwasili katika chuo cha mafunzo ya urubani na ufundi wa ndege jijini Mombasa,Kenya.Wanajeshi walishuka kwa tahadhari kubwa.Wakazingira eneo lote la uwanja

wa ndege wa chuo hicho.Baada ya kuhakikisha hakuna hatari yoyote,mkuu wa kikosi akiwa ameongozana na wanajeshi kadhaa, wakaelekea katika ndege iliyokuwa pale uwanjani ambayo mlango wake ulikuwa wazi.

Wakaingia ndani ya ndege kwa hadhari kubwa.Wakaipekua, lakini hawakukuta mtu yeyote.Zaidi walikuta damu zikiwa zimetapakaa ndani ya ndege.Ishara ya kwamba kuna watu walijeruhiwa au kuuawa ndani ya ndege hiyo.

Kiongozi wa kikosi kile,akaamuru wanajeshi wake waanze upekuzi katika baadhi ya ndege zilizokuwepo pale uwanjani na katika majengo.Wakati zoezi likiendelea, ghafla ikasikika milio

ya magari.Dakika chache baadaye gari kadhaa za jeshi la Kenya zikiwa zimesheheni wanajeshi waliojihami kwa silaha zikafika katika uwanja ule.Kiongozi wa wanajeshi wa Tanzania akatoa maelekezo kwa wanajeshi wake kusimamisha kwa muda zoezi la upekuzi.Wakajiweka tayari kwa mapambano iwapo yangetokea.Wanajeshi wa Tanzania walipewa amri ya kujisalimisha,kwani walikuwa wamezingirwa kila upande.Jenerali Pius akajulishwa haraka kile kilichokuwa kimetokea.Pia alitakiwa kutoa maelekezo nini kifanyike baada ya kadhia ya wanajeshi wa Kenya.Jenerali Pius akampigia tena simu Rais wa Kenya, lakini matokeo yalikuwa yale

yale.Hakupokea simu.Akampigia simu balozi wa Tanzania nchini Kenya.

“Mheshimiwa Rais, shikamoo!” alisema balozi Perpetua Kibaha.

“Mheshimiwa Balozi, kuna jambo linalohitaji kufanyiwa kazi haraka sana iwezekanavyo.Hivi tuzungumzavyo, wanajeshi wetu wamezingirwa na wanajeshi wa Kenya jijini Mombasa ambako wanawafuatilia magaidi waliofanya mashambulizi jijini Arusha leo.Kama tusipochukua hatua za haraka, basi wanaweza wakashambuliana.Nataka kuzungumza haraka sana na mkuu wa majeshi wa Kenya au waziri wa ulinzi!”alisema Rais Pius.Balozi akamtumia namba za simu za waziri wa

ulinzi wa Kenya.Bila kupoteza muda Rais Pius, akampigia waziri huyo.

“Hallow!”

“Hallow, unazungumza na Rais Pius Mawingu wa Tanzania.”

“Shikamoo,Mheshimiwa Rais.”alisema waziri wa ulinzi wa Kenya

“Marahaba!Mheshimiwa Waziri, ninahitaji msaada wako wa haraka.Wanajeshi wangu waliokuwa wanawatafuta magaidi waliotoroka na watoto na kukimbilia Mombasa, wamezingirwa na wanajeshi wa Kenya.Naomba mviondoe vikosi vyenu haraka sana au muwape wanajeshi wangu ushirikiano katika kuwatafuta magaidi waliotoroka hapa

nchini.”alisema Rais Pius kwa sauti yenye amri

“Mheshimiwa Rais,hiki kilichofanywa na jeshi lako si sawa hata kidogo.Hiki ni kitendo cha uvamizi na wanajeshi hao wanapaswa kabisa kushikiliwa kwa kosa la kuvamia nchini yetu.”alisema waziri wa ulinzi wa Kenya

“Mheshimiwa Waziri,ninatoa onyo endapo mwanajeshi wangu yeyote atarejea hapa nchini akiwa hata na mkwaruzo kutoka kwa wanajeshi wa Kenya,hatua nitakazozichukua zitakuwa kubwa sana.Nataka ndani ya dakika chache zijazo vikosi vya Kenya vilivyowazingira wanajeshi wangu ambao wanawasaka magaidi wondoke mara moja.Wawaache vijana wangu

wafanye kazi iliyowapeleka huko ya kuwasaka magaidi.”

“Mheshimiwa Rai…”

“Waziri,sitaki siasa.Inua simu sasa hivi na piga kwa makamanda wako wa jeshi waondoe wanajeshi wenu mahala hapo haraka.Nataka ndani ya dakika tano kutoka sasa nipate taarifa kuwa wanajeshi wa Kenya wameondoka!”alifoka Jenerali Pius na kukata simu.

“Kwa nini Rais Daniel alinidanganya kwamba atailinda ndege hiyo ya magaidi itakapoingia Kenya na hakufanya hivyo?Kwa nini amekuwa na kigugumizi katika mapambano dhidi ya ugaidi? Tanzania hatuna ajizi na magaidi.Tutawafumua mahala kokote

kule watakakojificha.Yeyote atakayethubutu kutaka kutuwekea vizingiti, tutakabiliana naye vikali," aliwaza Jenerali Pius huku akitazama saa yake.

Kabla ya dakika tano alizozitoa kupita, akapigiwa simu na mkuu wa majeshi,Akajulishwa kuwa tayari vikosi vya Kenya vimesogea pembeni na kuwaacha wanajeshi wa Tanzania wamalize kazi yao.

"Nataka kuzungumza na kiongozi wa wanajeshi wetu waliokwenda Mombasa," alisema Rais Pius.Baada ya muda mfupi, akaunganishwa na kiongozi wa wanajeshi wa Tanzania waliokuwa Mombasa Kenya.

"Mheshimiwa Rais!"

“Kamanda, nataka unihakikishie, je, ni kweli vikosi vya Kenya vimesogea pembeni na kuwapa nafasi ya kutekeleza jukumu lenu la kuwasaka magaidi?”Aliuliza Rais

“Ndiyo Mheshimiwa Rais.Wametupa nafasi.Kwa sasa tunashirikiana nao katika kufanya upekuzi mahala hapa.”

“Upekuzi? Hamjawakuta magaidi wala watoto mahala hapo?”Rais aliuliza kwa ukali kidogo.

“Ndiyo, Mheshimiwa Rais.Tumeikuta ndege ambayo ilitumiwa na magaidi, lakini hakuna mtu yeyote ndani ya ndege.Inaonekana kulifanyika uvamizi mahala hapa kwani kuna watu wameuawa waliokuwa katika jengo la

kuongozea ndege usiku huu.Vile vile walimu na wanafunzi sita waliokuwa katika mafunzo wakijiandaa kwa somo la usiku.”

“Hamjajua bado kama waliofanya tukio hilo ni magaidi au la?”

“Tunaendelea na uchunguzi mheshimiwa Rais.Kwa sasa baada ya jeshi la Kenya kuanza kutoa ushirikiano, tutapata majibu tu. Tutakujulisha baada ya kumaliza, Mheshimiwa Rais.”

“Sawa.Hakikisheni mnapata majibu mahala walikopelekwa watoto wetu,” alisema Rais na kukata simu.Akiwa amefura, sura kaikunja, akagonga meza kwa hasira.

“Namlaumu sana Rais Daniel.Yote haya yasingetokea kama angeruhusu

ndege zetu kuwafuatilia magaidi.Au hata kama angetuma vikosi vya Kenya kuifuatilia ndege hiyo.”Aliendelea kuwaza Rais Pius.Akatuliza akili kidogo kisha akampigia simu Ruby.

“Shikamoo Mheshimiwa,Rais” Ruby alitoa salamu baada ya kupokea simu.

“Marahaba,Ruby!Samahani kwa kukuamsha asubuhi hii.”

“Bila samahani,Mheshimiwa Rais.”

“Ruby, nilikwambia kwamba nataka kuonana na Gosu Gosu baadaye leo lakini nataka mje wote” alisema Rais Pius.

“Kuna tatizo lolote,Mheshimiwa Rais?”Ruby aliuliza kwa upole.

“Hakuna tatizo,Ruby.Kuna mambo ya muhimu nataka kuzungumza nanyi.Hasa ni kuwashukuru kwa kazi kubwa mliyoifanya jana.”

“Sawa,Mheshimiwa Rais.Tutafika!” alijibu Ruby.Rais akakata simu.Ruby akatoka chumbani kwake na kwenda kumfuata Gosu Gosu.Akampatia ujumbe ule wa Rais.

“Kitu gani Rais anataka kuzungumza nasi?”Gosu Gosu alihoji.

“Amegusia kidogo tu kwamba anataka kutushukuru kwa kazi tuliyoifanya jana,” alijibu Ruby.

“Nina wasi wasi kama hilo ndilo lengo lake.Kwa nini atake kutushukuru sisi wawili peke yetu wakati tulioshiriki

katika zoezi lile tuko wengi? Hapa kuna kitu kingine,Ruby!” alisema Gosu Gosu.

“Tutajua tukifika huko.Kwa sasa nina kazi ya kutafuta taarifa za Joseph Nahimana” akasema Ruby na kwenda katika ofisi yake akaanza zoezi la kutafuta taarifa za Joseph Nahimana mtandaoni.

Taarifa aliyoipata ni kuwa Joseph Nahimana ni mtoto wa Rais wa Rwanda.Ni mtu mwenye kuheshimika sana kwanza kwa sababu ya cheo cha baba yake,pili kwa sababu ya utajiri wake.Ni mmoja wa vijana wenye utajiri mkubwa sana Rwanda.Anamiliki kampuni kadhaa za kutengeneza vifaa vya elektroniki kama kompyuta na simu.

Baada ya kupata taarifa ile Ruby akamfuata Gosu Gosu

“Joseph Nahimana ni mtoto wa Rais wa Rwanda,” Ruby alimwambia Gosu Gosu

“Hiki ni kisiki kingine tumekutana nacho.Kuwachunguza hawa watu wanaotoka kwenye familia za marais huwa ni kujiingiza katika mgogoro mkubwa na watawala,” alisema Gosu Gosu.

“Lakini tayari ameingia katika ubao wetu.Namba yake ya simu imekutwa kwa yule jamaa aliyefariki Arusha hivyo lazima wana mashirikiano.Lazima tumchunguze hata kama anatokea katika familia ya rais,”alisema Ruby.

“Tutamchunguzaje huyu Joseph?Yeye yuko Rwanda na sisi tuko hapa Tanzania,” alisema Gosu Gosu.

“Nitakwenda Rwanda.Nitamfuata huko huko aliko kutafuta majibu,”alisema Ruby.

“Huwezi kwenda mwenyewe.Kama ni kwenda Rwanda, basi tutakwenda sote.”

“Hapana, Gosu Gosu!Wewe tayari umeumizwa mguu.Vilevile tuna sanduku hapa ambalo tunapaswa kulilinda kwa gharama zozote zile.Nitakwenda mwenyewe.Wewe utabaki hapa Dar es Salaam,”Ruby alisisitiza.

“Ruby, hawa jamaa ni mtandao mrefu sana.Hadi magaidi wameingia ndani yake, hivyo siwezi kukuacha

ukaenda huko peke yako.Nitakwenda nawe ili nihakikishe unakuwa salama.”

“Vipi kuhusu sanduku?” Ruby aliuliza.

“Tutaliweka sehemu salama,” Gosu Gosu alijibu.Ukapita ukimya kisha Ruby akasema.

“Fine!Nitashughulikia suala la usafiri ili leo hii hii tuondoke kwenda Rwanda.”

****

Rais Pius alipigiwa simu na mkuu wa majeshi, akajulishwa kwamba upekuzi katika chuo cha mafunzo ya urubani na ufundi wa ndege huko jijini Mombasa ulimalizika.Hakukuwa na

gaidi wala mtoto aliyepatikana.Kitu cha kushangaza mara tu wanajeshi wa Tanzania walipomaliza kufanya upekuzi wao katika chuo hicho wakawekwa chini ya ulinzi tena.Jenerali Pius hakupoteza muda.Akampigia simu Rais wa Kenya, Daniel Mwangi.

“Mheshimiwa Rais,” alisema Rais Daniel baada ya kupokea simu yake.

“Rais Daniel, habari za asubuhi!”

“Habari si nzuri, Jenerali Pius.Ninataka maelezo kwa nini vikosi vya Tanzania vimevamia nchini Kenya?” Aliuliza kwa ukali Rais Daniel.

“Kilichofanyika si uvamizi,Mheshimiwa Rais, bali wanajeshi wangu wako katika operesheni ya kuwasaka magaidi wanaoendelea

kuwashikilia watoto wetu waliowateka. Hilo limetokea baada ya wewe kushindwa kutimiza ahadi yako ya kuifuatilia ndege ya magaidi.Daniel, nilikuomba uruhusu ndege zetu zilizokuwa zinawafuatilia magaidi ziingie katika anga la Kenya na kuendelea kuwafuatilia magaidi hao.Lakini ulikataa katakata. Ukaenda mbali zaidi kwa kuahidi utatuma vikosi vyako kuifuatilia, lakini hukufanya hivyo.Unaweza ukanieleza sababu ya kutokufuatilia ndege hiyo mheshimiwa Rais?”Jenerali Pius aliunguruma.

“Hiyo ndiyo sababu ya kuingiza wanajeshi wako kuvamia nchini Kenya?”Rais Daniel aliuliza

“Bado hujajibu swali langu,Mheshimiwa Rais.Kwa nini hukutuma vikosi vyako kuifuatilia ile ndege? Unanipa mashaka,Mheshimiwa Daniel kama kweli una nia ya dhati ya kupambana na ugaidi. Laiti kama ungekuwa na nia hiyo ya dhati, basi usingeshindwa kuwaokoa watoto waliotekwa na magaidi.Mmoja wa watu wangu ambaye alikuwa anashikiliwa mateka katika ndege hiyo, alijitahidi kupambana, akawadhibiti magaidi.Lakini ndege haikuwa na mafuta ya kutosha kurejea Tanzania.Hivyo ikalazimika kutua katika uwanja wa ndege wa chuo cha mafunzo ya urubani huko mjini Mombasa.Nimekupigia simu zaidi ya mara nne, lakini hukupokea.Hii

inadhihirisha kwamba hukuwa tayari kutusaidia kuwaokoa wale watoto hadi wakachukuliwa na magaidi.Tuyaweke hayo kando tutaendelea kuyazungumza.Nimejulishwa muda mfupi uliopita kwamba wanajeshi wangu wamezuiliwa katika chuo hicho.Sitaki ugomvi nawe Daniel.Sitaki ugomvi na nchi ya Kenya.Nataka nitakapomaliza kuzungumza nawe simuni,wanajeshi wangu waruhusiwe kuondoka. Kinyume na hapo, tusilaumiane, Daniel“! Jenerali Pius alisema

“Unanitisha, Jenerali Pius?” Rais Daniel aliuliza kwa ukali.

“Sikutishi, Daniel.Ninakwambia ukweli mtupu!Ninapokata simu hapa,nitawasiliana na wanajeshi wangu

kujua kama bado wanazuiliwa au la. Na ikitokea bado, ndipo utakaponifahamu vizuri mimi ni mtu wa aina gani!”alisema Jenerali Pius,akakata simu kwa hasira.

“Mimi si mwanasiasa na wala sina lugha laini ya kubembeleza.Mimi ni mwanajeshi na jeshini hatuna lugha laini.Ni kutoa amri na kuhakikisha inatekelezwa.Hivi ndivyo itakavyokuwa kuanzia sasa katika urais wangu bila kufanya hivyo itaniwia ugumu kuongoza nchi hii.Nilichomwambia Rais Daniel, ndicho ninachokimaanisha.Kama wanajeshi wangu hawataachiwa nchini Kenya, basi nitachukua maamuzi magumu sana ambayo hawataamini,” aliwaza Rais Pius.. Akainua simu yake

na kumpigia mkuu wa majeshi.Akamtaka amjulishe ndani ya muda wa dakika kumi kama bado wanajeshi wa Tanzania wanaendelea kushikiliwa jijini Mombasa.

MOMBASA – KENYA

“Nilifanya kosa kubwa kuwaamini wale marubani.Sikupaswa kuwaamini waliponiambia ndege haina mafuta ya kutosha kurejea Tanzania.Kumbe mahala pale ndipo walipoelekezwa kutua.Magaidi walikuwepo pale wakiwasubiri.Ninajilaumu sana kwa kosa hili nililolifanya kwa sababu tayari nilikwisha idhibiti ndege,” Agai aliwaza akiwa ndani ya gari la magaidi yeye na

watoto wakipelekwa mahala kusikojulikana.Wote walikuwa wamefungwa vitambaa usoni mwao ili wasiweze kuona mahala wanakopelekwa.

“Nilituma taarifa nyumbani ili Rais Pius amuombe rais mwenzake wa Kenya vikosi vya ulinzi,kama watakuja baada ya sisi kuchukuliwa,pengine wanaweza kujaribu kufuatilia na hatimaye kujua mahala tunakoelekea.Huko wanakotupeleka, sina hakika kama wataniacha hai kwa kuwa nimeua wenzao wengi.Kabla hawajaniua, nitajitahidi kwa kila uwezo nilionao kupambana nao kwa minajili ya kujiokoa.Sitakubali kuchinjwa kama kuku,” Agai aliendelea kuwaza.Akainua

kichwa kuwatazama wale watoto. Akainama tena.

Magaidi walikwenda hadi katika nyumba moja kubwa mithili ya hoteli iliyokuwa pembezoni mwa bahari.Wasichana wote wakashushwa na kutolewa vitambaa usoni.Wakaingizwa ndani ya lile jumba.Wakawekwa katika sebule kubwa huku wakilindwa na watu wawili wenye bunduki.Agai akiwa amefungwa pingu,akawekwa pamoja na wale wasichana.

“Msiogope mabinti.Tutakuwa salama tu.Tayari nimetuma ujumbe nyumbani kuwajulisha mahala tulipo.Nina uhakika mkubwa hivi sasa wanatufuatilia,” alisema Agai kwa sauti ndogo akiwaambia wale wasichana

kuwapa moyo.Kwa hakika walijawa na wasiwasi mkubwa. Macho yao yalijaa machozi na walionekana kukata tamaa.Gaidi mmoja aliyekuwa anawalinda alimuona Agai akizungumza na wale wasichana akamfuata,akamtandika teke zito la uso.Akamtaka akae kimya.Damu ilianza kumtoka mdomoni.Hata hivyo,hakukuweza kufanya chochote kwa kuwa mikono yake ilifungwa kwa nyuma.Msichana mmoja akainuka.

"Sit dow!"aliamuru mmoja wa magaidi.

*"I'm going to help him.The man is bleeding!"*alisema yule msichana kwa ujasiri huku machozi yakimtoka.

“*Please let me help him.He’s bleeding.Please, sir!*”alisema tena yule msichana.Yule gaidi akamfanyia ishara ya kichwa kwamba akamsaidie.

“Thank you!” alisema yule msichana.Akamfuata Agai na kuanza kumpatia huduma ili kuzuia damu kuvuja.

“Jina lako nani?”Agai aliuliza kwa sauti ndogo.

“Perpetua Pius Mawingu!” Alijibu msichana. Agai akabaki akitahayari.

“President’s daughter!” alisema Agai.

“Ndiyo!” alijibu Perpetua

“Kwa nini unahatarisha maisha yako?”Agai aliuliza.

“Kwa sababu ninaamini ni wewe utakayeturejesha nyumbani.Hivyo basi lazima uwe salama,” Perpetua alijibu

“Siku nyingine usifanye kama ulivyofanya.Hawa jamaa ni watu wabaya sana wanaweza wakakuua,” Agai alionya.

“Hawawezi.Wanafahamu mimi ni mtoto wa Rais Pius.Hivyo basi, hawawezi kunigusa.Kwa kila hali, bado ningali na faida kwao,” Perpetua alijibu kwa ujasiri mkubwa.

“Wewe ni binti shujaa sana.Tafadhali wape moyo wenzako wasikate tamaa, tutarudi nyumbani salama,” alisema Agai. Ghafla wakaingia watu wanne mle ndani wakiwa wameongozana na jamaa mmoja mnene

aliyevaa kanzu ya rangi ya kahawia.Pindi alipomkuta Perpetua akimsaidia Agai, akaanza kuwafokea wale magaidi wawili kwa kutumia lugha ya Kisomali.

Yule gaidi aliyempiga Agai alionekana kama vile akiomba msamaha halafu maelekezo yakatolewa.Muda huohuo mateka wote wakatakiwa kusimama.Wakaelekezwa njia ya kupita na kutokea nje ya lile jumba.Huko nje wakakuta kuna njia inaelekea baharini.Wakaanza kutembea katika njia ile wakakuta gati na boti moja kubwa likiwa limeegeshwa.Wakaingizwa ndani,wote wakafungwa tena vitambaa usoni.Boti likawashwa, safari ikaanza hawakujua mahala wanakoelekea

12

DAR ES SALAAM –TANZANIA
ASUBUHI

Rais Pius alijulishwa kwamba tayari mkuu wa majeshi ameshafika na amepelekwa katika chumba cha mikutano kama alivyokuwa

ameelekeza.Bila kupoteza muda, Rais akamfuata.Wakasalimiana.Muda huo huo runinga iliyokuwa ukutani mbele yao ikawashwa,akaonekana mkuu wa jeshi la polisi akiwa jijini Arusha.

“Habari za asubuhi ndugu zangu.Kabla ya kikao chetu nataka tumshukuru tena Mungu kwa kutuwezesha kuiona siku ya leo na tumuombe aendelee kutupigania ili tuweze kuifanikisha mipango yetu.Tutumie dakika mbili kila mmoja aombe kwa imani yake kabla ya kikao kuanza,” alisema Jenerali Pius na kufumba macho kuomba.Baada ya dakika mbili, akafumbua macho.Kikao kikaanza rasmi.

“Nataka kwanza kupata taarifa wapi tumefikia katika matukio ya jana? CDF tuanzie kwako,” alisema Jenerali Pius.Mkuu wa majeshi akalifungua faili lililokuwa mbele yake kisha akasema.

“Kwanza kabisa ni kama nilivyokujulisha Mheshimiwa Rais kwamba wanajeshi wetu waliokwenda Kenya wote wako salama na wamerejea nyumbani,” alisema mkuu wa majeshi na kuweka tuo. Akavuta pumzi kidogo kisha akaendelea kuelezea hatua mbali mbali ambazo zinafanywa na jeshi ili kuimarisha ulinzi katika mipaka na sehemu nyingine muhimu. Lengo likiwa kuhakikisha mashambulio mengine ya magaidi hayatokei.

“CDF naomba uwape shukrani kwa niaba yangu wanajeshi wote waliotoka Kenya.Japo hatukufanikiwa kuwahi kuwakomboa watoto, lakini walifanya kazi nzuri sana.Ilikuwa misheni ya hatari,” alisema Jeneral Pius.Mkuu wa majeshi akasimama na kupiga saluti ishara kuwa maagizo yamepokelewa.

“IGP, kuna nini kwa upande wako? Jiji la Arusha limeamkaje leo hii?”Aliuliza Rais.IGP aliyekuwa anaonekana katika runinga akasema.

“Mheshimiwa Rais,kwanza kabisa jiji la Arusha liko salama wa salmini kwa sasa.Tumeendelea na doria kali usiku kucha.Tulifanikiwa kuwaua magaidi wote waliovamia hoteli ya Green ambao jumla yao walikuwa watatu.Idadi ya

watu waliofariki katika shambulio hilo ni kumi na tisa.Katika hospitali ya rufaa ya mkoa wa Arusha, waliouawa ni watu nane.Kwa upande mwingine, jeshi la polisi linamshikilia mwanamke mmoja aliyekuwa akishirikiana na magaidi hao.Kwa sasa amelazwa katika hospitali ya rufaa ya mkoa ya Mount Meru.Hali yake inaendeea vizuri. Tunaamini huyu atatueleza mambo mengi sana kuhusiana na mtandao huo wa magaidi.Nimepokea pia taarifa kutoka kwa kiongozi wa kikosi cha jeshi kilichokwenda Mombasa Kenya kwamba, ndege ambayo magaidi waliitumia kutorokea ni mali ya kampuni moja kubwa ya utalii nchini Kenya.Ndege hiyo ilipelekwa katika chuo cha mafunzo ya urubani na ufundi

wa ndege kwa ajili ya matengenezo ya kawaida.Hapo ndipo ikachukuliwa na magaidi wale kuja Tanzania,ikatumika kuwatorosha watoto na magaidi.Inadaiwa kwamba walioendesha ndege hiyo si marubani wa chuo hicho bali walikodiwa na magaidi.Bado tunaendelea kuwasaka hadi hivi sasa.Taarifa zinadai kwamba walinzi,walimu na wanafunzi waliokuwepo chuoni hapo usiku huo waliuawa na magaidi.Kwa sasa jeshi la polisi la Kenya linaendelea kuwasaka magaidi hao kwa nguvu zote. Nimewasiliana muda mfupi uliopita na mkuu wa polisi wa Kenya na amenihakikishia kwamba,magaidi hao lazima watakuwa bado wako

Mombasa.Njia zote za kuingia na kutoka Mombasa zimewekwa vizuizi huku zoezi la kuwasaka likiendelea.” alisema mkuu wa jeshi la polisi ambaye ndiye kiongozi wa operesheni ya kupambana na magaidi waliofanya shambulio jijini Arusha.

Kikao kiliendelea wakijadili mambo mbali mbali kuhusu usalama wa nchi. Ghafla ukaingia ujumbe katika simu ya Rais Pius. Umekutoka kwa Ruby akimjulisha kwamba tayari wamewasili Ikulu.Jenerali Pius akawataka wakuu wale wa vyombo vya ulinzi na usalama wakayafanyie kazi yale yote waliyoyazungumza kisha wakutane baada ya saa nne kwa kikao kingine kujua utekelezaji ulivyokwenda.

Baada ya kutoka katika chumba cha mkutano, Rais akaelekea moja kwa moja katika sehemu ya wageni walikokuwako akina Ruby.

“Pole na hongera sana Gosu Gosu kwa kazi kubwa na ya hatari uliyoifanya jana.Vipi unaendeleaje, lakini?”Rais Pius aliuliza.

“Ninaendelea vyema kabisa mheshimiwa Rais,” alijibu Gosu Gosu.Rais akawataka waende katika chumba kingine ili wazungumze kwa kirefu.

“Ninawashukuru sana kwa kufika.Nimewaiteni hapa kuna mambo ya msingi sana nataka kuzungumza nanyi,” alisema Rais Pius na kushusha

pumzi.Alionekana kuwa na mzigo mkubwa wa mawazo.

“Kwanza kabisa, niwashukuru kwa kazi kubwa na nzuri tena ya kishujaa na kizalendo mliyoifanya jana.Gosu Gosu, sina maneno mazuri ya kukushukuru wewe na mwenzako Agai kwa ujasiri wenu mkubwa mliouonesha.Ninyi mliweza kufungua njia kwa wanajeshi wetu kuweza kuingia ndani ya jengo lililokuwa linashikiliwa na magaidi.Mliyatoa maisha yenu kwa ajili ya Watanzania na wote waliokuwa wameshikiliwa mateka katika jengo lile.Nafahamu ni watu wengi walioshiriki katika operesheni ile, lakini ninyi watatu Ruby,Gosu Gosu na Agai ambaye hayuko hapa tumuombee huko aliko awe

salama,mlifanya kazi ya kutukuka kabisa.Ninapenda niwape shukrani za kipekee kabisa.Mlikuja na taarifa ambayo sisi sote hatukuwa nayo.Gosu Gosu ninakupa pongezi za kipekee kwa sababu, pale ambapo magaidi walipohitaji daktari,bila kujiuliza mara mbili ukajitolea.Sina hakika kama tungeweza kumpata daktari ambaye angejitolea kuhatarisha maisha yake na kuingia katika ukumbi ule uliokuwa unashikiliwa na magaidi.Huu ni ushujaa uliopitiliza.Kwa niaba ya Watanzania, napenda niwashukuru sana," alisema Rais Pius.

"Tunashukuru Mheshimiwa Rais kwa kuwa sehemu ya watu waliotoa

mchango katika kufanikisha misheni ile ngumu,” alisema Ruby.

“Ninajivunia kuwa rais wa taifa lenye vijana wazalendo kama ninyi ambao mko tayari kumwaga damu yenu kwa ajili ya kulipigania taifa lenu.Magaidi wametuchokoza na tumewaonesha kuwa Tanzania si mahala ambako unaweza ukafanya ugaidi na ukatoka salama.Japo bado wanaendelea kuwashikilia watoto wetu, lakini naamini tutafanikiwa kuwapata tu.”alisema Rais Pius

“Je,kuna maendeleo yoyote mpaka sasa juu ya kufahamu mahala walikokimbilia magaidi?”Ruby aliuliza.Rais akawaeleza kile kilichokuwa kimetokea.

“Kwa nini Rais wa Kenya hakuweza kutuma vikosi vifuatilie ndege ya magaidi? Naamini hivi sasa tayari tungekwisha wapata watoto wetu pamoja na Agai,” alidakia Gosu Gosu huku akionekana kuwa na hasira.

“Sifahamu kwa nini alifanya vile, lakini nimeshaamua kwa gharama zozote zile, lazima watoto wetu wapatikane!”alisema Rais huku akiuma meno. Akanyamaza baada ya simu yake kuita. Mpigaji alikuwa ni mkuu wa jeshi la polisi.

“IGP, unasemaje?”Rais aliuliza.

“Mheshimiwa Rais, kuna taarifa nimeipata muda si mrefu kutoka kwa mkuu wa jeshi la polisi Kenya.”

“Ndiyo anasemaje?”

“Anadai kwamba jeshi la polisi nchini humo limebaini kuwa magaidi hawako jijini Mombasa.Wameelekea nchini Somalia kwa boti.Ameelekeza tuombe msaada kwa mamlaka nchini Somalia waweze kutusaidia kufuatilia baharini na kuchunguza boti zote zinazoelekea huko zikitokea upande wa Kenya” alisema mkuu wa jeshi la polisi.

“Nakushukuru sana, IGP, kwa taarifa hiyo.Nitarudi tena kwako baada ya muda mfupi nikiwasiliana na mamlaka za Somalia,” alisema Rais Pius na kukata simu.Akabonyeza laini namba mbili.

“Vera, nataka kuzungumza na balozi wa Somalia hapa nchini haraka sana,”

alisema Rais na kukata simu.Akawageukia akina Ruby.

“Nimejulishwa na mkuu wa jeshi la polisi kuwa,amepata taarifa kutoka kwa mwenzake wa Kenya, magadi tunaowatafuta wamekimbilia nchini Somalia.Ninataka kuzungumza na balozi wa Somalia kuhusiana na suala hili na kuiomba serikali ya Somalia iweze kutoa msaada,” alisema Rais Pius.

“Mheshimiwa Rais,hawa magaidi wana mbinu nyingi na wamejiandaa kikamilifu kukamilisha ajenda yao.Hauwezi kumpigia simu Rais wa Somalia moja kwa moja ukazungumza naye suala hili na maamuzi ya haraka yakafanywa kuliko kumtumia balozi?” aliuliza Gosu Gosu.

“Sina mahusiano mazuri na Rais wa Somalia tangu nilipoingiza majeshi nchini mwake tukamkamata Mahmoud Fadil Ghedi baba yake na kiongozi wa magaidi waliofanya mashambulizi ya jana.Naamini hatapokea simu yangu nikimpigia,ndiyo maana ninataka kumtumia balozi wao hapa nchini.Wakati tukimsubiri balozi,nataka kufahamu Gosu Gosu umerejea saa ngapi Dar es Salaam?”Rais alijibu swali la Gosu Gosu na kuhitimisha na swali.

“Nilirejea jana usiku na ndege ya jeshi,” Gosu Gosu alijibu.

“Ouh!Sikulifahamu hilo.SNSA wanahangaika kukutafuta Arusha kumbe tayari uko Dar.Karibu sana kwa mara nyingine.Dhumuni la kuwaiteni hapa

moja ni kama nilivyowaeleza ni kuwashukuru kwa kazi kubwa mliyoifanya jana.Lakini sababu kuu ni kutaka kuzungumza nanyi masuala muhimu sana.Kwanza kabisa, ninataka kuwaomba samahani kuna jambo nililifanya ambalo baada ya kulifikiria sana nikagundua nilikosea," alisema Rais na kunyamaza kwa sekunde chache kisha akaendelea.

"Mliponieleza kuwa Mathew Mulumbi ndiye aliyepiga simu na kutoa maelekezo kuhusu Fabrice Kayembe,nilistukasana.Nilijiuliza maswali mengi wapi alipo Mathew Mulumbi hadi akajua kuwa Fabrice ndiye lengo la magaidi kufanya shambulizi lile? Papo hapo mkumbuke

kuwa Mathew Mulumbi alikuwemo katika ndege yetu iliyopotea, hivyo nilihitaji sana kufahamu mahala alipo.Ikanilazimu kumpa maelekezo Maurine Kyaso tuchunguze mawasiliano ya Ruby ili kujua mahala alipo Mathew" akanyamaza na kuwatazama akina Ruby.Akaendelea.

"Mtanisamehe sana,Ruby na Gosu Gosu.Nilielekeza mawasiliano ya Ruby yadukuliwe ,lengo likiwa ni kumtafuta Mathew Mulumbi," Rais alisema.Ruby akatabasamu.

"Usihofu,Mheshimiwa Rais," alisema Ruby. Akatabasamu tena kisha akasema.

"Tayari tulikwisha lifahamu jambo hilo." Alisema Ruby

“Mnalifahamu?Maurine amewaeleza?”Rais aliuliza kwa mshtuko mkubwa.

“Hapana.Maurine hajatueleza chochote.Mheshimiwa Rais, mimi nina uwezo mkubwa sana wa kucheza na teknolojia.Hivyo basi niling’amua mapema sana kuwa mawasiliano yangu yanadukuliwa.”alisema Ruby huku akitabasamu tena.

“Ruby I’m so s..... ”

“Usijali,Mheshimiwa Rais,” alisema Ruby na ukimya ukatawala.Rais akaendelea.

“Nimetafakari sana na kugundua kuwa ninapaswa kushirikiana nanyi badala ya kuwazungukeni.Hivyo nimewaiteni hapa vijana wangu ili

tuweze kuanza upya.Nimeuona umuhimu wa Mathew Mulumbi na nimeyaamini maneno aliyoyasema Ruby jana mchana kuwa, yawezekana Mathew Mulumbi akawa katika misheni.Nataka tusahau haya yaliyotokea na tufungue ukurasa mpya.Naona kuna mambo makubwa ambayo yanaendelea hapa nchini na anayefahamu ni Mathew Mulumbi pekee.Hivyo basi kila anachokielekeza,kuna ulazima mkubwa kifanyiwe kazi haraka sana bila kusita," alisema Rais.Ruby na Gosu Gosu wakatazamana.

"Nafahamu itakuwa vigumu kwenu kuniamini,lakini naombeni mniamini kwani nimewaeleza ukweli."

“Tunakuamini,Mheshimiwa Rais wala usihofu.Hakuna shaka katika kushirikiana nawe,” alisema Ruby.

“Nashukuru kwa hilo.Nataka kujua, je, mmewasiliana tena na Mathew Mulumbi? Kuna maelekezo mengine ameyatoa?”Rais aliuliza

“Mheshimiwa Rais, Mathew alimpigia simu Gosu Gosu jana usiku.Alitoa maelekezo kwamba lile sanduku jeusi lililopatikana kwa msaada wa ile diski kutoka kwa Fabrice Kayembe, asikabidhiwe mtu yeyote bali lihifadhiwe sehemu salama.”alijibu Ruby

“Subiri kwanza Ruby.Nilipewa taarifa kuwa magaidi wameondoka na

hilo sanduku pamoja na ile diski," alisema Rais Pius.

"Hapana,Mheshimiwa Rais,Sanduku tunalo tumelihifadhi sehemu salama,"alijibu Ruby.

"Dah!Endelea!"alisema Rais

"Mheshimiwa Rais, hili suala ni pana na tayari tumeanza kulifanyia uchunguzi ili tuipate picha ya kile kinachoendelea kabla ya Mathew hajatueleza kwa kina ni kitu gani kinachoendelea.Makachero wa SNSA walipokwenda katika nyumba iliyokuwa na sanduku jeusi, walikuta maiti na pembeni yake kulikuwa na mkoba mdogo mweusi ambao ndani yake kulikuwa na nyaraka kadhaa za kusafiria.Kwa bahati nzuri, Gosu Gosu

aliweza kuupata mkoba huo akaja nao Dar es Salaam.Mtu aliyekuwa na mkoba huo,tunaamini ndiye aliyekutwa amekufa mle ndani anaitwa Amos Jackson Ntuyahaga. Ni raia wa Rwanda. Amos aliingia nchini akitokea Ufaransa kama hati yake ya kusafiria inavyoonesha.Aliwasili nchini kwa ndege ya shirika la ndege la Ethiopia. Akashukia katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Kilimanjaro.Hiyo ilikuwa mwezi mmoja kabla ya kufanyika kwa mkutano wa *Afrika Asili Yangu*.Ukiacha hati ya kusafiria, katika mkoba huo tulipata pia karatasi iliyokuwa na namba ya simu ya Joseph Nahimana.Huyu ni mtoto wa Rais wa Rwanda," alisema

Ruby.Rais akamtazama Ruby kwa macho makali ya mshangao.

“Ruby,nataka unihakikishie kuwa haya unayonieleza ni mambo ya kweli!”

“Ni kweli kabisa,Mheshimiwa Rais,tunaamini huyo mtu aliyekutwa amekufa ndani ya nyumba hiyo ni Amos Ntuyahaga na alikuwa na karatasi yenye namba ya simu ya Joseph Nahimana” Ruby alisema.

“Nataka unieleze kila mlichofanikiwa kukipata mpaka sasa,” Rais aliongeza.

“Mheshimiwa Rais,kupatikana kwa ile namba ya simu ya Joseph katika ile nyumba moja kwa moja inatufanya tuhisi kuwa ana mahusiano na lile sanduku jeusi ambalo magaidi walilihitaji kutoka

kwa Fabrice Kayembe.Kwa sasa tunachoendelea kukichunguza ni kujua huyu Amos alikuja nchini kufanya nini?Pia tunataka kujua mahusiano yake na Joseph Nahimana.Tayari nimekata tiketi mbili za ndege.Mimi na Gosu Gosu jioni ya leo tunakwenda Kigali kumchunguza Joseph" alisema Ruby.

"Hakuna haja ya kwenda Kigali.Joseph Nahimana yuko hapa Tanzania,"alisema Rais Pius.

"Yuko hapa Tanzania?"Gosu Gosu aliuliza kwa mshangao

"Ndiyo.Yuko hapa Tanzania.Ni mmoja wa watu waliokuwa wanashikiliwa mateka na magaidi katika ukumbi wa KICC," alisema Rais.Ruby na Gosu Gosu wakatazamana.

“Rais wa Rwanda alinipigia simu akanijulisha kuwa mtoto wake ni mmoja wa watu wanaoshikiliwa na magaidi katika ukumbi wa KICC,” alisema Rais Pius.

“Mheshimiwa Rais, huyu ni mtu muhimu mno katika hili suala.Kama yuko hapa nchini, tunatakiwa kumpata haraka iwezekanavyo,”alisema Ruby.

“Nina uhakika mkubwa yuko hapa nchini.Lakini ili kupata uhakika zaidi, tuipitie orodha ya majina ya watu waliokuwemo katika ukumbi wa KICC wakati magaidi wanauteka,” alisema Rais.Akatoka pale alipoketi akaifuata simu iliyokuwa mezani pembeni.Akawapigia wasaidizi wake akaomba kuletewa orodha ya watu

waliokuwa wanashikiliwa mateka na magaidi jijini Arusha.

“Baada ya mateka kukombolewa,Rais wa Rwanda amekupigia tena simu kuuliza kuhusu mwanaye?”Gosu Gosu aliuliza.

“Alinipigia kunipongeza.Aniuliza kuhusu mwanaye, nikamwambia nitafuatilia.Ndiyo maana nikaomba orodha ile itumwe ili nijue kama ni mmoja wa watu waliokuwa wanashikiliwa na magaidi au la,” alisema Rais Pius.Punde, mlango ukagongwa.Akaingia mlinzi wa Rais na kumpatia faili ambalo alimkabidhi Ruby.

“Haya ni majina ya watu waliokuwemo ndani ya ukumbi wa KICC ulipotekwa na magaidi.Litafuteni

jina la Joseph kama litakuwepo," alisema Rais.Ruby akaanza kuyapitia majina yale moja baada ya lingine. Kimya kikapita kisha akasema.

"Ni kweli.Joseph Nahimana alikuwemo katika ukumbi wa KICC wakati magaidi wanavamia na kuuteka," Ruby alisema.

"Tuna uhakika mkubwa sasa kuwa alikuwemo ndani ya ukumbi.Vilevile tuna uhakika alitoka mzima kabisa na watu wote walipelekwa katika hospitali ya mkoa wa Arusha kwa ajili ya kupatiwa matibabu.Tunahitaji kuipata orodha ya watu wote waliopelekwa pale hospitali ili tuone kama jina la Joseph Nahimama nalo lilikuwamo," Gosu Gosu alisema.

Bila kupoteza muda, Rais akachukua simu na kumpigia mkuu wa mkoa wa Arusha.Akamtaka amtumie ndani ya dakika tatu orodha ya watu wote waliopelekwa katika hospitali ya rufaa ya mkoa wakitokea katika ukumbi wa KICC baada ya kukombolewa.

“Wakati tunasubiri orodha hiyo nataka…” akanyamaza Rais baada ya simu ya Gosu Gosu kuita.

“Excuse me. I need to take this call,”alisema Gosu Gosu na kutoka nje ya kile chumba kwa ajili ya kuipokea simu.

“Hallow,” alisema Gosu Gosu.

“Gosu Gosu, ni mimi Mathew.Uko sehemu salama?”

“Ndiyo,Mathew.Habari yako? Unaendeleaje?”

“Mimi ni mzima kabisa.Kuna kazi nyingine ninataka kukupa ambayo nataka ifanywe kikamilifu sana,” alisema Mathew.

“Ninakuahidi Mathew,nitafanya kila linalowezekana kuikamilisha kazi hiyo,” alisema Gosu Gosu.

“Kuna mwanamke mmoja anaitwa Carmelita Michael, atawasili leo saa mbili usiku jijini Dar es Salaam akiwa na mwanaye wa miaka minne kwa ndege ya shirika la ndege la Emirates akitokea Dubai.Umeandaliwa mpango ya kumuua yeye na mwanaye hivyo basi kazi yako ni kumuokoa na kumpeleka mafichoni

hadi nitakaporejea mwenyewe," alisema Mathew.

"Unarudi nyumbani?" Gosu Gosu aliuliza.

"Ndiyo.Ninakuja nyumbani,hivyo fanya juu chini kuhakikisha Carmelita anakuwa salama."

"Akina nani hao wanaotaka kumuua na kwa nini?" Gosu Gosu aliuliza.

"Gosu Gosu, nimekupa kazi ya kufanya sihitaji maswali.Wewe ni mwanajeshi unafahamu namna mambo yanavyokwenda jeshini.Ukipewa kazi ya kufanya, hakuna kuhoji.Ifanye kwanza halafu kama kuna maswali utauliza baadaye.Ikamilishe kazi hiyo kikamilifu na nitakaporejea nyumbani nitakuja kuwaeleza kila kitu," alisema Mathew.

“Sawa,Mathew.Nahitaji kuipata picha ya mwanamke huyo na taarifa zake nyingine za muhimu.Atafikia hoteli ipi hapa Dar es Salaam?”Aliuliza Gosu Gosu.

“Atafikia Saafin Hotel.Kitu cha muhimu hakikisha hafiki katika hoteli hiyo kwani ndiko wamepanga wamuue.Baada tu ya kukata simu nitakutumia picha yake” alisema Mathew.

“Sawa,Mathew.Nitafanya hivyo,”alisema Gosu Gosu.Mathew akakata simu.Sekunde chache baadaye,ukaingia ujumbe katika simu ya Gosu Gosu.Akaufungua na kukutana na picha ya mwanamke mrembo sana.Gosu

Gosu akaitazama akatabasamu halafu akarejea ndani ya kile chumba.

“Mambo yamekwendaje humu?"Aliuliza.

“Tumeipata ile orodha ya wagonjwa waliofikishwa hospitali wakitokea katika ukumbi wa KICC, lakini Joseph Nahimana hayupo!”

“Haonekani katika orodha?"Gosu Gosu aliuliza kwa mshtuko.

“Ndiyo haonekani,” Ruby alijibu.

“Watu wote kutoka KICC walipelekwa hospitali ya Mount Meru, hivyo kama ni kuondoka, basi lazima aliondokea akiwa pale.Unakumbuka hata Jamal naye aliondoka mara tu baada ya kufikishwa hospitali,” alisema Gosu Gosu.

“Nimejaribu kupitia kamera, lakini sijamuona akitoka kama alivyotoka Jamal,” alisema Ruby.

“Vipi kuhusu hotelini alikofikia?"Gosu Gosu aliuliza.Ruby akamgeukia Rais.

“Mheshimiwa Rais, tunaomba uongozi wa mkoa wa Arusha watusaidie kutafuta huyu Joseph Nahimana alifikia katika hoteli gani jijini Arusha,” alisema Ruby.Rais akampigia simu mkuu wa mkoa wa Arusha,akamtaka apitie taarifa za wageni wote waliohudhuria mkutano wa Afrika Asili Yetu ajue Joseph Nahimana kutoka Rwanda alifikia hoteli gani.

“Wakati tukisubiri majibu kutoka Arusha, kuna jambo la muhimu sana

ambalo mnatakiwa kulifahamu,” alisema Gosu Gosu na kuwatazama Rais na Ruby.

“Aliyenipigia simu muda mfupi uliopita ni Mathew Mulumbi,” alisema Gosu Gosu.Rais akashusha pumzi.

“Amesemaje,Mathew Mulumbi?"Rais aliuliza.

“Ametoa kazi nyingine,” Gosu Gosu alijibu kisha akawaeleza kuhusiana na ile kazi nyingine aliyoitoa Mathew ya kumuokoa Carmelita.

“Kitu cha mwisho alichokisema Mathew ni kwamba, mara tu misheni hiyo itakapokamilika, atarejea nyumbani,” alisema Gosu Gosu.Ukapita ukimya ndani ya kile chumba.

“Hakukueleza mahala alipo?"Rais aliuliza.

“Hapana.Hakusema yuko wapi.Nadhani atakaporejea, atatueleza kila kitu,” alijibu Gosu Gosu.

“Ni misheni kubwa hii, lakini huyu mwanamke ni nani? Kwa nini anataka kuuawa? Kwa nini Mathew anataka asiuawe?"Rais alihoji kidadisi. Mara simu yake ikaita.Akaipokea.

“Hallo, Vera!” alisema Rais.

“Mheshimiwa Rais, tayari balozi wa Somalia amekwisha patikana na yuko katika laini ya video namba mbili,” alisema Vera.

“Sawa.Ninakwenda sasa hivi kuzungumza naye” Rais alijibu na kuwataka akina Ruby waendelee na

kikao yeye anakwenda kuzungumza na balozi wa Somalia nchini Tanzania.

“Kuna kingine chochote ambacho Mathew amekuambia hujakisema?"Aliuliza Ruby.Ni baada ya Rais kutoka.

“Yote aliyonieleza ni hayo niliyowaambia.Mathew ameweka msisitizo mkubwa sana katika misheni hii.Naomba tufanye kila linalowezekana kuhakikisha tunamuokoa huyo mwanamke asiuawe,” alisema Gosu Gosu.

“Ni nani huyu mwanamke?”Aliuliza Ruby na kuichukua simu ya Gosu Gosu, akaitazama picha yake.

“She’s very pretty!”alisema Gosu Gosu.

“Kwa nini mrembo huyu anataka kuuawa? Kwa nini tumuokoe?”Aliuliza Ruby huku akianza kutafuta taarifa za mwanamke yule kwa kutumia programu zake za utambuzi.

Rais Pius aliingia katika chumba cha mawasiliano ya moja kwa moja kwa njia ya video na kuchukua kitanza mbali akakielekeza runingani akabonyeza,balozi wa Somalia akaonekana. “Assalaam alaykum,Mheshimiwa Balozi,” alisema Rais Pius.

“Wa alaykum salaam,” aliitikia balozi.

“Balozi, nimekutafuta, ninahitaji kuzungumza nawe jambo la muhimu sana,” alisema Rais Pius

“Nakusikiliza mheshimiwa Rais” alisema balozi

“Kama unavyojua nchi yetu imeshambuliwa na magaidi siku ya jana.Tulifanikiwa kuwadhibiti magaidi hao lakini wapo wengine waliponyoka wakakimbia.Hawakukimbia peke yao waliwachukua baadhi ya watoto waliowateka wakaondoka nao.Walikimbia hapa Tanzania kwa kutumia ndege ambayo waliiacha jijini Mombasa Kenya.Baada ya hapo, wakapanda boti kuelekea Somalia.Tunahitaji msaada kutoka serikali ya Somalia kuwafuatilia magaidi hawa na ikiwezekana kuwadhibiti kabla hawajapotea kabisa,” alisema Rais Pius.

“Mheshimiwa Rais, nashukuru kwa kunifahamisha jambo hilo.Ninaamini serikali yangu ina dhamira ya dhati ya kuyatokomeza makundi haya ya kigaidi. Ninakuhakikishia nitafikisha taarifa hizi ili hatua za haraka ziweze kuchukuliwa za kuwadhibiti hao magaidi,”alisema Balozi wa Somalia.

“Ahsante sana,Mheshimiwa Balozi.Naomba unijulishe kila utakapopata taarifa kutoka kwa serikali yako kuhusiana na suala hili,” alisema Rais Pius kwa unyenyekevu.Wakaagana na Rais akarejea katika chumba alikowaacha akina Ruby.

“Tayari nimewasiliana na Balozi wa Somalia hapa nchini. Kwa sasa anakwenda kuzungumza na serikali yao

ili waweze kuwafuatilia magaidi hao wanaoelekea Somalia hivi sasa.Vipi hapa kuna maendeleo yoyote?”Rais Pius aliuliza .

“Mheshimiwa Rais, huyu mwanamke ambaye Mathew ametoa maelekezo tumuokoe anaitwa Carmelita Michael Wartbull.Ni mtoto wa bilionea Michael Wartbull ambaye anamiliki kiwanda cha kutengeneza magari ya kifahari aina ya Carmela,” alisema Ruby.

“Huyu Carmelita kwa nini anataka kuuawa?”Rais alihoji.

“Mheshimiwa Rais, nadhani kwa sasa tujielekeze katika kumuokoa huyo mwanamke.Na kama alivyoahidi Mathew Mulumbi kwamba pale misheni hiyo itakapokamilika, basi atarejea

nyumbani.Kwa mujibu wa taarifa alizotoa Mathew, ni kwamba Carmelita atawasili hapa nchini leo saa mbili usiku na ndege ya Emirates akitokea Dubai.Atafikia katika hoteli ya Saafin.Hajaweka wazi anakuja hapa nchini kwa shughuli gani, lakini hayo yote tutayafahamu hapo baadaye," alisema Ruby.

"Ni namna gani mtamuokoa huyo mwanamke? Aliuliza Rais Pius.

"Gosu Gosu, wewe ndiye mzoefu wa mambo hayo.Tunahitaji mawazo yako katika hilo tafadhali," alisema Ruby.

"Tunatakiwa kuushirikisha uongozi wa hoteli ya Saafin ambako atafikia Carmelita," alisema Gosu

Gosu.Walijadiliana kwa dakika kadhaa kuhusu jambo hilo, halafu Rais akachukua simu na kupiga.

“Vera, naomba unitafutie meneja wa hoteli ya Saafin.Ninahitaji kuzungumza naye tafadhali,” alisema Rais.

“Wakati tukiendelea kumsubiri meneja apatikane, tuendelee kujadili kuhusiana na Joseph Nahimana,” alisema Ruby. Rais Pius akachukua simu akampigia mkuu wa mkoa wa Arusha.

“Mheshimiwa mkuu wa mkoa, nilikupa kazi inayohitaji majibu ya haraka.Mbona mpaka sasa sijapata mrejesho wowote?”Aliuliza kwa ukali Rais Pius pindi tu mkuu wa mkoa wa Arusha alipopokea simu.

“Mheshimiwa Rais, samahani sana.Nilikuwa namalizia kukusanya taarifa ndipo nikupigie.Hata hivyo, tayari nimekwisha kamilisha ile kazi uliyonituma.Joseph Nahimana raia wa Rwanda alifikia katika hoteli ya Meru paradise,chumba namba 153” alisema mkuu wa mkoa wa Arusha.

“Ahsante sana,” alijibu Rais na kukata simu.

“Joseph amefikia Meru Paradise hotel,” alisema Rais.Ruby upesi akaitafuta hoteli hiyo mtandaoni akawapigia simu.

“Hallow, Meru Paradise hapa.Tukusaidie nini, tafadhali?”Muhudumu aliuliza.

“Nina mgeni wangu alifikia hapo hotelini kwenu namba ya chumba chake ni 153,anaitwa Joseph Nahimana raia wa Rwanda,je bado yupo?”Ruby aliuliza.

“Naomba dakika moja dada niangalie halafu nitakujulisha,” alisema mwanadada,baada ya sekunde chache,akasema.

“Joseph Nahimana tayari amesharudisha chumba na hayupo tena hapa hotelini.”

“Ahsante.Unaweza ukanisaidia kujua ni lini amerejesha chumba?”Ruby aliuliza.

“Jana usiku,”alijibu muhudumu.Ruby akakata simu.

“Jana ndiyo siku ambayo Joseph amerudisha chumba” alisema Ruby.Rais

Pius hakutaka kupoteza muda.Papo hapo akampigia simu Rais wa Rwanda.

“Mheshimiwa Rais,” alisema Alpha Nahimana Rais wa Rwanda.

“Mheshimiwa Alpha, habari za Kigali?” aliuliza Rais Pius

“Huku kwema.Mnaendeleaje huko Tanzania?”

“Huku kwema pia tunaendelea vyema, japo bado tunawasaka magaidi waliofanikiwa kutoroka na watoto zaidi ya ishirini.”

“Mheshimiwa Rais, kama kuna kitu chochote Rwanda inaweza ikasaidia usisite kunitaarifu.” Alisema Rais Alpha

“Nakushukuru sana,Mheshimiwa Rais Alpha.Vipi mwanao Joseph uliwasiliana naye?” rais Pius aliuliza

“Ndiyo!Alinipigia simu na kunijulisha kuwa tayari wamefanikiwa kukombolewa na yuko salama.Ninashukuru sana,Mheshimiwa Rais kwa jitihada mlizozifanya kuwakomboa wale mateka akiwemo na mwanangu.” Alisema Rais Alpha

“Ninataka kukuhakikishia,Mheshimiwa Alpha, kuwa mwanao atakuwa salama salimini kwa muda wote atakaokuwa hapa Tanzania.Ninataka kutuma walinzi maalum wa kuhakikisha anakuwa salama wakati huu akiwa nchini Tanzania.Je, bado yuko Arusha?”Rais Pius aliuliza kimtego.

“Ndiyo bado yuko, Arusha!” alijibu Rais Alpha.

“Unaweza ukanipa namba yake ya simu anayotumia ili niweze kuwasiliana naye nimpe pole na kumuhakikishia kwamba yuko salama?”Aliuliza Rais Pius.

“Hakuna tatizo kabisa, Mheshimiwa Rais.Nitakutumia namba anayotumia sasa hivi.”alijibu Rais Alpha

“Nashukuru sana,Mheshimiwa Alpha.” alisema Rais Pius.

Sekunde chache baadaye, ukaingia ujumbe mfupi wa simu katika simu ya Rais.Akaufungua.Ilikuwa namba ya simu ya mtandao wa Amanicom ambayo anaitumia Joseph Nahimana.Hii ilikuwa tofauti na ile ambayo Ruby aliikuta katika mkoba wa Amos Ntuyahaga

Ruby aliipiga ile namba, lakini haikupatikana.Akajaribu tena kwa mara ya pili. Majibu yakawa ni yale yale.

“Simu yake haipatikani!” alisema Ruby.

“Mbona anaanza kuleta wasiwasi huyu kijana? Je,naye ameuawa?”Rais aliuliza.

“Kwa kuwa tayari tunayo namba yake ambayo anaitumia basi tutampata tu.Nitakachofanya ni kujua amewasiliana na namba zipi za hapa Tanzania halafu nitaingia katika hifadhi ya SNSA ambao wanahifadhi mawasiliano ya simu zote za hapa nchini na tutajua hao aliowasiliana nao wamezungumza nini.” Ruby alisema.

“Unaweza kuingia katika mfumo wa SNSA? Aliuliza Rais Pius

“Ndiyo mheshimiwa Rais.Kwa muda mfupi niliokaa pale siku ya jana nimeusoma mfumo huo na ninaweza kuingia nikafanya chochote” alijibu Ruby

“Mhn ! Rais aliguna

“Mheshimiwa Rais tunasubiri ruhusa yako” alisema Gosu Gosu

“Tafuta haraka!” alisema Rais Pius. Ruby akaingia katika mfumo wa SNSA wa kutunza kumbu kumbu za mawasiliano ya simu kwa kutumia utundu wake wa kuinyanyasa teknolojia.Rais alibaki akimtazama kwa mshangao namna Ruby alivyokuwa

akicheza na kompyuta yake kama ana vidole sita katika kila mkono

“Nimeyakubali maneno ya Mathew Mulumbi.Huyu mwanamke ni mchawi wa teknolojia” aliwaza Rais.Baada ya muda Ruby akasema

“Joseph amewasiliana na namba moja tu hapa Tanzania ambayo imesajiliwa kwa jina la Mwasi Jumbe,” alisema Ruby huku akiendelea kubofya kompyuta yake.

“Mara ngapi wamewasiliana?”Rais Pius aliuliza.

“Wamewasiliana mara mbili.Mara ya mwisho ilikuwa jana saa tano usiku.”alijibu Ruby

“Good.Unaweza kwenda mbali zaidi ili tufahamu walichokizungumza pindi

walipowasiliana?”Rais aliuliza.Ruby akaendelea kubofya kompyuta, sekunde chache baadaye, yakaanza kusikika mazungumzo yao.

“Thirteen,one,seven,” ilisema sauti ya mwanamke.

“One,four,seven,zero,” ilisema sauti ya mwanaume ambayo waliamini ni sauti ya Joseph.

“Two,” alisema mwanamke.

“Two,” alisema pia Joseph na simu ikakatwa.

Wote wakabaki wanatazamana.Rais likamtoka cheko kidogo la mshangao.

“Haya mbona maajabu. Ni nini wamekizungumza? Mbona wamekuwa wanataja namba tu?” Rais aliendelea kuuliza huku akistaajabu.

“Haya maajabu kweli kweli!” alisema Gosu Gosu.Ruby akacheza mazungumzo ya mwisho ya Joseph na Mwasi.

“Fifty five,twelve,nine,Twenty,” alisema Joseph.

“Sixty,two hundred,eighty seven,two,” alijibu Mwasi na simu ikakatwa.Safari hii wote wakajikuta wanaangua kicheko tena.

“Jamani haya mbona malimwengu.Haya ni mawasiliano ya namna gani?”Rais Pius aliuliza.

“Mheshimiwa Rais, ninaamini hii ni namna yao ya kuwasiliana na wenyewe wanajua kile wanachokimaanisha kwa kutaja hizo namba.Mawasiliano ya namna hii, mara nyingi hutumiwa na

majasusi waliobobea ili mazungumzo yao yasiweze kujulikana,” alisema Ruby.

“Inawezekana Joseph akawa ni jasusi?”Rais aliuliza kidadisi huku akimtazama Ruby.

“Sina hakika sana.Lakini huko nyuma ya hizo namba kuna kitu kikubwa kinafichwa kisijulikane” alisema Ruby kwa msisitizo.

“Nadhani kuna ulazima wa kumtafuta huyu Mwasi ni nani na yuko wapi.Nina uhakika tukifanikiwa kumpata, basi tutakuwa tumempata Joseph,” alisema Gosu Gosu.Ruby akaisakama tena kompyuta kuzitafuta taarifa za Mwasi. Baada ya muda mfupi akasema.

“Taarifa zinaonesha Mwasi Jumbe ni mtumishi wa ofisi ya mkemia mkuu wa serikali,” Ruby alijibu huku akiinua kichwa kuwatazama Rais na Gosu Gosu.

“Mimi nitamfuata Mwasi ofisini kwake nikazungumze naye,” alisema Gosu Gosu.

“Gosu Gosu,” Ruby alitaka kusema kitu lakini Gosu Gosu akamzuia.

“Ruby, hatuna muda wa kupoteza.Lazima tumtafute Joseph kwa haraka sana na kujua mahala aliko,” alisema Gosu Gosu.

“Analosema Gosu Gosu ni sawa kabisa.Hata hivyo, hautakwenda peke yako.Nitakupa vijana wangu wawili utakwenda nao huko kwani huwezi jua kitu unachoweza kukutana nacho.Hivyo

lazima kuchukua tahadhari kubwa," alisema Rais. Akapiga simu, akazungumza na mtu fulani na kutoa maelekezo.

Haukupita muda mlango ukafunguliwa.Akaingia jamaa mmoja, Rais akamtaka Gosu Gosu amfuate.Mara tu Gosu Gosu alipotoka, simu ya Rais ikaita.Akaipokea.

"Vera, unasemaje?"

"Mheshimiwa Rais, tayari meneja wa hoteli ya Saafin yuko katika laini ya simu namba sita."

"Ahsante, Vera!" alisema Rais na kukata simu.Akaenda katika simu iliyokuwa mezani.Akabonyeza laini namba sita.

"Hallow!"

“Hallow!” ikasema sauti ya upande wa pili.

“Unazungumza na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hapa.” Alisema Rais Pius

“Shikamoo,Mheshimiwa Rais.”

“Marahaba.Unaitwa nani ndugu?”

“Naitwa Ramesh Chopra. Ni meneja mkuu wa Saafin Hotel.”

“Nimefurahi kukufahamu, Ramesh!”

“Mimi pia,Mheshimiwa Rais.Sikutarajia kama ungeweza kunipigia simu.”

“Ramesh, nina mazungumzo nawe muhimu sana.Ninatuma wasaidizi wangu watakuja kukuchukua hapo mahala ulipo watakuleta hapa Ikulu!”

“Hakuna tatizo,Mheshimiwa Rais!”

“Ahsante sana,” alijibu Ramesh.Rais akakata simu kisha akatoa maelekezo kwa wasaidizi wake kwenda Saafin Hotel kumchukua Ramesh.Pindi anaweka simu ya mkonga chini, ujumbe mfupi ukaingia katika simu yake ya kiganjani.Akausoma kisha akatoa kauli kwa Ruby.

“Ruby, endelea kufukua zaidi suala hili na pindi utakapopata kitu chochote, utanijulisha.Ninakwenda ofisini mara moja” alisema Rais na kutoka.

****

Meneja wa hoteli ya Saafin aliwasili Ikulu kufuatia wito wa Rais. Hii ndiyo mara yake ya kwanza kufika

Ikulu.Alionekana kuwa mwenye wasi wasi mwingi.Alipokewa na katibu wa Rais, akakaribishwa ndani kwenda kukutana na Rais.

“Mheshimiwa Rais, shikamoo!” alisema meneja.

“Marahaba.Karibu sana bwana Ramesh,” alisema Rais na kumuelekeza kiti aketi.

“Nimefurahi kukufahamu bwana Ramesh.Naamini hii ni mara ya kwanza tunaonana.”

“Ndiyo,Mheshimiwa Rais. Hii ni mara ya kwanza pia kufika hapa Ikulu,” alisema Ramesh.

“Karibu sana, Ramesh.Ikulu ni nyumba yenu,ni nyumba ya Watanzania

hivyo basi unapofika hapa umefika nyumbani.”

“Nashukuru sana,Mheshimiwa Rais,” alisema Ramesh, lakini bado uso wake uliendelea kuonesha woga.Rais akampa maelekezo mmoja wa walinzi wake kwenda kumchukua Ruby.

“Ramesh, sitaki kuchukua muda wako mwingi.Kuna suala la muhimu nimekuitia hapa na nitahitaji sana msaada wako.”

“Ndiyo,Mheshimiwa Rais,” alisema Ramesh.Ruby akaingia, Rais akamtambulisha kwa Ramesh kisha akamtaka Ruby aendelee.

“Ramesh, kuna mgeni anatarajia kuwasili leo saa mbili usiku na ndege ya shirika la ndege la Emirates akitokea

Dubai.Mgeni huyo anaitwa Carmelita Michael Wartbull.Taarifa zinaonesha kuwa atafikia katika hoteli yako.Nataka tuanzie hapo, je, ni kweli mgeni huyo atafikia katika hoteli yako?”Ruby aliuliza.

“Ni kweli.Tunamtegemea mgeni huyo siku ya leo kuanzia saa mbili atawasili.” Alijibu Ramesh.

“Ahsante, Ramesh.Nataka kufahamu namna mlivyojiandaa kumpokea mgeni huyo” alisema Ruby.

“Kwa kawaida wageni ambao hutoka nje ya nchi huwa tunawapokea moja kwa moja uwanja wa ndege.Tuna magari yetu ya hadhi mbalimbali kutokana na aina ya mgeni.Yapo magari ya kawaida, lakini yapo pia magari ya

hadhi ya juu kwa ajili ya wageni wale maalum kama mabilionea na watu wenye majina makubwa.Kwa Carmelita, tumemuandalia gari la kifahari na tutampokea yeye na watu wake uwanja wa ndege”alisema Ramesh.

“Vizuri sana.Ramesh, dhumuni la kukuita hapa ni kukupa taarifa muhimu kuhusiana na mgeni huyo.Kutoka katika vyanzo vyetu, tumepata taarifa za kiintelijensia kwamba kuna mpango wa kumuua mgeni huyo pindi atakapofika hapa Tanzania,” alisema Rais akimtazama mgeni wake.Ramesh akashtuka sana.

“Nani wanaotaka kumuua?”Aliuliza kwa hamaki.

“Hatujui ni akina nani, lakini tumekuita hapa ili kwa pamoja tuweze kushirikiana namna ya kuweza kumuokoa mgeni huyo asiweze kuuawa.Usihofu,Ramesh kila kitu kitakaa sawa.Tunachohitaji ni ushirikiano wako tu,”alisema Rais.Ramesh akatikisa kichwa kuashiria kukubaliana na maelezo ya Rais. Wakaendelea na majadiliano kuhusu mpango wa kumuokoa Carmelita asiuawe.Ramesh akaagana na Rais akaondoka.

13

Gosu Gosu, aliwasili katika jengo la ofisi ya mkemia mkuu wa serikali.Akashuka na mmoja wa wale walinzi wa Rais, wakaelekea mapokezi.Wakajitambulisha kuwa ni wageni wa Mwasi Jumbe.Wakaombwa kusubiri katika sofa nzuri za rangi nyeusi.Baada ya dakika kumi,aliwasili mwanamama mmoja mnene wastani aliyevaa suti ya kijivu.Wahudumu wa mapokezi wakamuelekeza kwa akina Gosu Gosu, akawafuata.

“Habari zenu,” alisema Mwasi huku akitabasamu.

“Salama kabisa,” alisema Gosu Gosu akisimama.Akampa mkono.

“Nimeambiwa ninyi ni wageni wangu,” alisema Mwasi.

“Ndiyo.Tunaweza kuzungumza nje tafadhali?”Aliuliza Gosu Gosu.Mwasi akawaongoza hadi katika sehemu ya mgahawa.Wakatafuta sehemu iliyotulia, wakaketi.

“Najaribu kuvuta kumbu kumbu, lakini nashindwa kukumbuka kama tunafahamiana au tumewahi kukutana sehemu,” alisema Mwasi.

“Ni kweli, Mwasi, hatufahamiani.Hii ni mara ya kwanza tumekutana.”alisema Gosu Gosu

“Mimi mmenifahamuje?”

“Mwasi, awali ya yote, ningependa kujitambulisha.Ninaitwa Papi Gosu Gosu na mwenzangu anaitwa Damian.Tunatokea Ikulu,” alisema Gosu Gosu.Mwasi akashindwa kuuzuia

mshtuko wake.Gosu Gosu akamtolea ishara Damian akatoa kitambulisho na kumuonesha Mwasi.

“Kuna nini? Mbona mnaniogopesha namna hiyo?”Mwasi aliuliza kwa tahayari.

“Usihofu, Mwasi.Tumekuja hapa kuna jambo tunahitaji msaada wako,” alisema Gosu Gosu kwa upole.

“Niwasaidie nini?”

“Kulifanyika shambulio la kigaidi jana jijini Arusha.Ninaamini taarifa hizo unazo,” alisema Gosu Gosu

“Ndiyo ninafahamu kuhusu jambo hilo,”alisema Mwasi huku akijimakinisha zaidi.

“Miongoni mwa watu waliokuwa wanashikiliwa mateka na magaidi katika

ukumbi wa KICC, ni Joseph Nahimana.Mtoto wa Rais wa Rwanda ambaye ni rafiki mkubwa wa Rais wetu.Baada ya kukombolewa,hatujui Joseph mahala aliko na Rais Pius anahitaji kuhakikisha anakuwa salama.Katika harakati za kumtafuta na kujua mahala alipo,tukagundua kuwa wewe uliwasiliana naye jana usiku.Hivyo basi tumekuja hapa kwa lengo moja tu,kufahamu Joseph yuko wapi.Ni kwa ajili ya usalama wake," alisema Gosu Gosu.

"Umesema Joseph Nahimana?" Mwasi aliuliza kwa mshangao,

"Ndiyo.Tunahitaji kujua mahali alipo," alijibu Gosu Gosu.

“Simfahamu na wala sijawahi kuwasiliana na mtu anayeitwa Joseph.Hata katika simu yangu hii hapa nikikuonesha majina hakuna mtu anayeitwa Joseph,” alisema Mwasi,Akaiweka simu yake mezani.

“Yawezekana mmechanganya majina na mkamuacha muhusika mkanifuata mimi.Simfahamu kabisa huyo Joseph,” Mwasi aliongeza kwa msisitizo.

“Wewe si Mwasi Jumbe?”Gosu Gosu aliuliza.

“Ndiyo,Ni mimi, lakini si mimi niliyewasiliana na huyo Joseph,”Mwasi alijibu kinagaubaga.

“Mwasi, tumekuja hapa baada ya namba yako ya simu kuonekana ikiwa

imewasiliana na Joseph jana usiku.Tusingekufuata kama hatuna uhakika kuwa umewasiliana naye.”

“Jamani, haya mbona maajabu? Hiyo simu imejipiga yenyewe au vipi? Nakwambia ukweli kaka yangu tazama orodha ya watu niliowasiliana nao jana,’ alisema Mwasi na kumpa Gosu Gosu simu.Akatazama watu ambao Mwasi aliwasiliana nao siku iliyopita.Mara akashtukia kitu.

“Una laini ngapi za simu?” Gosu Gosu alimuuliza.

“Nina laini moja tu ambayo ndiyo hii ninayoitumia katika simu,” alijibu Mwasi.Gosu Gosu akaingiza mkono mfukoni na kutoa karatasi iliyokuwa na

namba ya simu ambayo iliwasiliana na Joseph Nahimana.Akampa Mwasi.

“Namba hii si ya kwako?”Aliuliza Gosu Gosu.Mwasi akaitazama namba ile kisha akasema.

“Namba hii si ya kwangu!”

“Mbona imesajiliwa kwa jina lako?”Gosu Gosu alihoji kwa ukali huku akimtazama Mwasi kwa macho yake ya kazi.

“Ngoja niwaeleze ukweli kaka zangu.Hii ni namba ya simu ya mdogo wangu anaitwa Nicole, sisi tumezoea kumuita Nicki.Yeye anaishi nje ya nchi.Amekuja nchini kwa mapumziko akaniomba nimsajilie laini ya simu kwa kutumia kitambulisho changu cha taifa ili aweze kuitumia kwa siku hizi chache

atakazokuwa hapa nchini.Nilikubali.Nikamsajilia laini mpya kwa jina langu na kumpa akaanza kuitumia.Na hii ndiyo namba yake.Huyu ndiye aliyewasiliana na huyo Joseph.Kama mkionana naye anaweza akawaeleza mahala aliko huyo Joseph," alisema Mwasi kwa upole huku akimtazama Gosu Gosu kwa wasiwasi.

"Ahsante kwa kutueleza ukweli.Huyo mdogo wako Nicki anaishi nchi gani?"Aliuliza Gosu Gosu.

"Ufaransa,"alijibu Mwasi.

"Anafanya kazi gani huko?"Aliuliza Gosu Gosu.

"Alikwenda kusoma na baada ya kumaliza masomo yake, hakurudi Tanzania.Aliendelea kutafuta maisha

huko huko na.Hajawahi kuweka wazi kazi yake” alisema Mwasi huku chozi likimlenga.

“Tunaweza kumpata wapi, Nicki?”Aliuliza Gosu Gosu.

“Akija hapa nchini mara nyingi huwa ni mtu wa starehe na marafiki zake na anaweza akamaliza hata wiki nzima hajaonekana nyumbani.Nina siku ya tatu leo sijamuona nyumbani,” alisema Mwasi na kuchukua simu yake. Akampigia mmoja wa marafiki wa Nicki, akamwuliza kama yuko kwake.Akamkosa.Aliwauliza marafiki wanne wakubwa wa Nick anaowafahamu,lakini wote hawakufahamu mahali alipo.

“Hawa niliowapigia simu ndiyo marafiki zake wakubwa akija Tanzania,ukimkosa nyumbani, basi lazima utamkuta kwa mmoja kati ya hao.Ila leo inashangaza wote hawajui mahali alipo.Mbona ninaanza kupatwa na wasiwasi!”alisema Mwasi.

“Usihofu!Mdogo wako ni mzima na wala hajapatwa na tatizo lolote.Naweza kuipata picha yake tafadhali,” alisema Gosu Gosu.Mwasi akamtumia picha tatu za Nicole katika simu.

“Katika hao marafiki zake uliowapigia simu, ni yupi hasa rafiki yake mkubwa?”Gosu Gosu aliuliza.

“Rafiki yake mkubwa sana ni Zaituni.Ambaye naye nimempigia lakini hafahamu alipo,” alisema Mwasi.

“Naomba tafadhali unielekeze mahala anakopatikana huyo Zaituni.Ninahitaji kuzungumza naye!” alisema Gosu Gosu.Mwasi akamuelekeza mahali anakoishi Zaituni.Gosu Gosu akampa Mwasi namba yake ya simu.

“Kama utapata taarifa zozote kuhusiana na Nicole, utanijulisha kwa kutumia namba hiyo,” alisema Gosu Gosu.Wakaondoka kuelekea katika gari lao huku Mwasi akiwa bado amesimama akiwatazama.

Gosu Gosu na Damian waliingia garini wakaondoka.Gosu Gosu akampigia simu Ruby.

“Nipe habari Gosu Gosu.Kuna chochote umekipata huko?”Ruby aliuliza

kwa shauku.Gosu Gosu akamueleza kile alichofanikiwa kukipata kutoka kwa Mwasi.

“Una uhakika na hicho alichokisema huyo mwanamke?”Ruby aliuliza.

“Amesema kweli hajadanganya.Ninakutumia picha za huyo mdogo wake uendelee kutafuta taarifa zake wakati sisi tunaelekea nyumbani kwa rafiki yake, Zaituni!” alisema Gosu Gosu.Akamtumia Ruby zile picha za Nicki.

“Nicole Jumbe! Ni nani huyu mwanamke? Kwa nini hajawahi kuwaeleza ndugu zake kile anachokifanya nchini Ufaransa? Kitu gani anakificha?”Alijiuliza Gosu Gosu.

“Kuna picha nyingine hapa inajitengeneza.Amos alitokea Ufaransa ndipo akaja Tanzania,Fabrice Kayembe naye pia ametokea Ufaransa,Nicole Jumbe naye pia anatokea Ufaransa.Kuna nini huko Ufaransa?”Gosu Gosu aliendelea kujiuliza maswali rundo kichwani mwake.

“Bado fumbo ni gumu, lakini tutalifumbua tu!”

****

Gosu Gosu aliwasili katika nyumba aliyoelekezwa na Mwasi kuwa anaishi Zaituni rafiki mkubwa wa Nicole.Ni nyumba iliyozungukwa na biashara kadhaa.Kulikuwa na maduka na saluni kubwa ya wanawake.Gosu Gosu na Damian wakashuka garini na kuelekea katika saluni kubwa wakamfuata muhudumu mmoja, wakamwulizia Zaituni.

“Dada kuna wageni wako!” alisema muhudumu na mwanadada mmoja aliyevaa suruali nyeusi ya *jeans* iliyombana na shati jekundu akawafuata.

“Karibuni!Niwasaidie nini?”Zaituni aliwakaribisha na kutupia swali papo hapo.

“Samahani kwa kukuvamia kazini kwako bila hodi.Tunaweza kuzungumza kidogo hapo nje?”Aliuliza Gosu Gosu.Zaituni akafungua mlango uliokuwamo mle ndani ya saluni, wakatokea katika varanda ndogo.

“Karibuni!”alisema Zaituni huku akiongoza njia.Wakaelekea ndani hadi katika sebule moja nzuri yenye mapambo mengi.

“Niwasaidie kinywaji gani?”Aliuliza Zaituni aliyeonekana kuwa dada mkarimu sana.

“Tunashukuru sana.Tunaomba tusikusumbue,”alisema Gosu Gosu.

“Sawa! Haya, niwasaidie nini kaka zangu?”

“Awali ya yote, ingekuwa vyema tukajitambulisha kwako.Mimi naitwa Gosu Gosu,mwenzangu ni Damian.Sisi tunatokea Ikulu!”

“Wow ! Ikulu?”Zaituni aliuliza huku akitoa kicheko kidogo.

“Hii ni neema leo.Nimefuatwa na watu wa Ikulu.Hebu niambieni, nimeteuliwa na Rais?Mimi uongozi siuwezi ila nikipewa siukatai”Zaituni aliuliza kwa utani.Hali iliyopelekea wote kutoa kicheko.

“Zaituni, nadhani umelisikia tayari tukio lililotokea jana Arusha!”

“La wale magaidi?”

“Ndiyo!”

“Lilikuwa tukio baya sana.Tuvipongeze vyombo vyetu vya

ulinzi kwa kufanikiwa kuwadhibiti.Tunapaswa kuwaheshimu sana hawa watu wetu wanaotulinda usiku na mchana na kuhakikisha tunakuwa salama," alisema Zaituni.

"Ahsante kwa kulifahamu hilo.Watu wetu waliomo katika vyombo vya ulinzi na usalama wanastahili heshima ya pekee kabisa"alisema Gosu Gosu

"Kweli kabisa.Hawalali usingizi wakitulinda sisi tuwe salama" alisema Zaituni

"Katika ukumbi uliotekwa na magaidi kule Arusha,alikuwemo pia mtoto wa Rais wa Rwanda anaitwa Joseph Nahimana.Baada ya magaidi kuuawa, watu wote waliokuwa wanashikiliwa mateka na hao magaidi

walipelekwa katika hospitali ya rufaa ya mkoa ya Mount Meru.Walivyofikishwa hospitalini hapo, ikagundulika watu kadhaa hawaonekani na mmoja wao ni Joseph Nahimana.Rais wa Rwanda amemuomba Rais wa Tanzania kumsaidia kumtafuta mwanaye.Baada ya uchunguzi kufanyika, ikabanika kuwa simu ya Joseph imetumika jana usiku na aliwasiliana na mtu anaitwa Nicole Jumbe.Kwa sasa tunamtafuta Nicole ili tujue mahali alipo Joseph Nahimana.Dada wa Nicole ametuelekeza kwako kuwa wewe ndiye rafiki yake mkubwa.Tumekuja hapa utusaidie ni wapi tunaweza kumpata Nicole" alisema Gosu Gosu.

“Mhh! Haya sasa mbona makubwa tena” alisema Zaituni akionekana kuanza kuingiwa na woga.

“Usihofu, Zaituni! Nicole hana tatizo lolote.Tunachotaka ni kuzungumza naye ili tufahamu mahali alipo Joseph.Tunataka kujua kama yuko salama” alisema Gosu Gosu.

“Tatizo ni kumpata Nicki.Hapa ni kama nyumbani kwake na ukitaka kumtafuta mara nyingi utamkuta hapa.Ajabu leo siku ya pili sijaonana naye na sijui yuko wapi kwa kweli.Nicki ana marafiki wengi.Yawezekana amekwenda kwa marafiki zake wengine.Akija Tanzania, kazi yake kubwa huwa ni kutumia tu.Tunaweza

kumtafuta kumbe yuko Zanzibar anakula upepo,” alisema Zaituni.

“Kwani anafanya kazi gani huko nje ya nchi anakoishi?”Aliuliza Gosu Gosu.

“Sifahamu!Ila yule ni mpambanaji.Kazi yoyote anaweza kufanya,” alijibu Zaituni.

“Wewe ni rafiki yake mkubwa sana na unamfahamu vyema.Sehemu gani nyingine huwa anapenda kwenda? Naamini unazifahamu sehemu zote,” alisema Gosu Gosu.

“Nyinyi watu wa Ikulu,n’nataka mniweke wazi, je, shoga yangu yuko matatizoni? Kama kuna hatari yoyote, niwekeni wazi tafadhali,” alisema Zaituni kwa masikitiko.

“Usiogope,Zaituni!Hakuna tatizo lolote kwa Nicki.Tunachohitaji ni kupata taarifa za mahali alipo Joseph ambaye waliwasiliana jana usiku.”alisema Gosu Gosu

“Mmh! Ngoja nikachukue simu yangu nijaribu kuwasiliana na watu kadhaa ili kujua kama kuna aliyemuona mahali,” alisema Zaituni.Akatoka kwenda kuchukua simu yake, halafu akarejea sebuleni alikowaacha akina Gosu Gosu.Akaanza kupiga simu kwa watu mbali mbali huku akiwauliza kama wamemuona Nicki.Wakati Zai akiendelea kufanya mawasiliano, simu ya Gosu Gosu ikaita.Akaipokea.

“Hallow!” alisema Gosu Gosu.

“Ni mimi, Mwasi.Tayari umefika kwa Zaituni?”Aliuliza Mwasi.

“Ndiyo tayari tuko hapa kwa Zai!”

“Kuna mtu nimewasiliana naye ni mmoja wa marafiki wa Nicki, ameniambia kuwa jana jioni alikuwa naye lakini akamuaga kuwa anakwenda kuonana na Mau.Huyo Mau ni mmoja wa marafiki zake pia.Mimi simfahamu, lakini kama ukimuuliza Zai anaweza kumfahamu,” alisema Mwasi.

“Mwasi, nakushukuru sana kwa taarifa hiyo.Kama utafanikiwa kupata taarifa nyingine, tafadhali naomba unijulishe!” alisema Gosu Gosu.

“Sawa!Nitafanya hivyo!”alijibu Mwasi ,akakata simu .Gosu Gosu akamfuata Zai aliyekuwa nje ya kile

chumba.Akamfanyia ishara,Zai akakata simu, akamfuata.

“Unamfahamu, Mau?”

“Mau yupi?”

“Rafiki wa Nicki.Nimepewa taarifa kuwa Nicki alikwenda kwake jana jioni.”alisema Gosu Gosu

“Ndiyo, ninamfahamu!Lakini mimi na yeye hatuna mawasiliano na wala sifahamu anaishi wapi.Simpendi ana dharau.Ni dada mmoja ana pesa nyingi. Yeye na Nicki wamefahamiana siku nyingi tangu wakiwa Ulaya.Kila Nicki ajapo Tanzania huenda kuonana naye,” alisema Zaituni.

“Anafanya kazi gani huyo Mau?”Gosu Gosu aliuliza.

“Sifahamu kitu chochote kuhusu huyo Mau.Mimi si mtu wake wa karibu.Nimemjua kwa sababu ya Nicki,” alisema Zaituni,

“Unayo picha yake?” Aliuliza Gosu Gosu.

“Ndiyo!Ninayo picha yake katika simu.Kuna siku tulikutana katika sherehe ya kuzaliwa ya mmoja wa marafiki zetu na Nicki, akamualika huyo dada, tukapiga picha ya pamoja,” alisema Zaituni huku akiifungua simu yake sehemu ya kuhifadhia picha.Akaanza kuitafuta.

“Nina picha nyingi sana humu.Mimi ni mpenzi wa picha,” alisema Zaituni. Punde akaipata picha aliyokuwa akiitafuta.Akamwonesha Gosu Gosu.

“Picha yenyewe ni hii hapa!” alisema Zaituni.Ghafla,Gosu Gosu akahisi kama miguu inataka kumuisha nguvu.

“Ninaweza kuipata picha hii?”Gosu Gosu aliuliza.

“Bila shaka!” alijibu Zai na kumtumia Gosu Gosu picha nne za Mau akiwa na Nicki halafu wakaagana,wakaondoka.Hadi wanaingia ndani ya gari, bado Gosu Gosu alihisi mwili wake ungali unamtetemeka.Hakujua ni hofu au ni kwa nini alipatwa na hali ile baada ya kuitazama ile picha ya Mau akiwa na Nicki.

“Sikumwelewa Mathew aliposema tusishirikiane kwa namna yoyote ile na

SNSA, lakini sasa nimemuelewa.Kumbe Maurine Kyaso Mkurugenzi wa SNSA ni rafiki mkubwa wa Nicki.Sikutegemea kabisa!” Gosu Gosu aliwaza.

“Sitaki kuhitimisha haraka haraka kuwa Maurine naye ana mahusiano na Joseph hadi pale tutakapofanya uchunguzi wa kina na kujiridhisha.Maurine ni mtu mkubwa anaongoza idara nyeti ya usalama wa nchi.Hivyo unapotaka kumjumuisha katika suala kubwa kama hili, ni lazima uwe na ushahidi wa kutosha!” aliendelea kuwaza Gosu Gosu.

****

Baada ya kutoka kwa Zaituni, walirejea Ikulu.

“Nini kimetokea wakati sipo?”Gosu Gosu aliuliza.Ruby akamueleza kuhusiana na taarifa ile aliyopewa Rais kuwa bado vikosi vya Somalia vilikuwa vinaendelea kuwatafuta magaidi,lakini hawajafanikiwa kuwapata.

“Kwa upande wako, nini umekipata?”Ruby aliuliza.

“Ruby, suala hili ni kubwa!” alisema Gosu Gosu akumueleza Ruby kila kitu.

“Gosu Gosu, huyo mwanamke ametudanganya!” alisema Ruby.

“Hapana,Ruby!” alisema Gosu Gosu na kumuonesha Ruby zile picha alizopewa na Zaituni.

“Hapa sasa patamu! Alisema Ruby kwa sauti ndogo “Nadhani sasa umeelewa kwa nini Mathew alisisitiza kuwa tusiwashirikishe SNSA kuhusiana na lile sanduku.Lazima anafahamu kuna kitu kinachoendelea pale.Huyu Nicole anashirikiana na Joseph, wakati huohuo ana urafiki mkubwa na Maurine.Jana walikuwa wote.Huoni kunaweza kuwa na kitu hapo Ruby?”Gosu Gosu aliuliza.

“Kuna ulazima wa kumfanyia uchunguzi huyu Maurine.Tumfahamu vyema nyendo zake.Gosu Gosu, tumshirikishe Rais suala hili.” Alisema Ruby

“Unadhani ni wazo zuri?”Gosu Gosu aliuliza.

“Ndiyo.Lazima afahamu kile kinachoendelea.Afahamu pia kuwa tunamchunguza Maurine!” alisema Ruby na kumpigia simu Rais Pius.Akamjulisha kuwa wanamuhitaji kuna dharura.Wakati wakimsubiri Rais,Ruby akamueleza Gosu Gosu kuhusiana na ule mpango wa kumtorosha Carmelita walioupanga wakishirikiana na meneja wa hoteli ya Saafin.

Mlango wa ofisi ukafunguliwa.Akaingia Rais Pius.

“Kuna kitu gani?” Rais aliuliza.

“Mheshimiwa Rais, kuna kitu Gosu Gosu amekipata.Tumeona ni vyema kama utakifahamu,” alisema Ruby.Gosu Gosu akamueleza Rais kila kitu alichokipata.Halafu akamuonesha zile

picha za Maurine Kyaso akiwa na Nicki, akazitazama kwa umakini mkubwa sana.

“Una hakika picha hizi ni za kweli? Teknolojia imetanuka sana zama hizi Watu wanaweza wakatengeneza picha kama hizi.” Alisema Rais Pius

“Mheshimiwa Rais, kila kitu ni cha kweli kabisa na hakuna shaka hata kidogo kwamba Maurine na Nicki ni marafiki!”alisema Gosu Gosu.

“Nini ushauri wenu?”Rais Pius aliuliza.

“Tunataka kumchunguza Maurine.Tunataka kwenda nyumbani kwake kufunga kamera za siri kwa lengo la kumfuatilia nyendo zake.Yawezekana tukagundua mambo mengi zaidi,”

alisema Ruby huku akimtazama Rais atasemaje.

“Mna uhakika hawezi akagundua kama anachunguzwa?” Rais aliuliza

“Hapana!Hataweza kugundua chochote.Tunahitaji ruhusa yako mheshimiwa Rais ili tuweze kulifanya jambo hilo,” alisema Ruby.Rais Pius akainamisha kichwa chini akatafakari kidogo halafu akasema

*“Okay. Do it!”*Rais alisema.

“Ahsante sana,Mheshimiwa Rais, lakini bado tunahitaji utusaidie kitu kimoja zaidi.Wakati tunakwenda kutekeleza mpango huo, tunaomba umuite Maurine hapa Ikulu uwe na mazungumzo naye hadi tutakapomaliza kazi yetu tutakutumia ujumbe

utamruhusu aondoke zake," alisema Ruby.

"Hakuna tatizo katika hilo.Ninachotaka kufahamu ni kwamba, hizo kamera za siri mnazotaka kuzifunga nyumbani kwa Maurine, mnazo?" aliuliza Rais

"Tunazo mheshimiwa Rais."alijibu Ruby

"Vizuri.Nitampigia simu na kumtaka Maurine afike hapa mara moja ili mpate nafasi ya kwenda kuingia nyumbani kwake.Vipi kuhusu mpango wa usiku wa leo?"

"Kila kitu kitakwenda vizuri,Mheshimiwa Rais usihofu!" alisema Ruby kisha wakakusanya vifaa vyao nakuondoka.

****

Ujumbe mfupi wa maandishi uliingia katika simu ya Ruby, akaufungua na kuusoma.Ulitoka kwa Rais Pius.

“Go ahead !” ndivyo ulivyosomeka ujumbe ule.Ruby akatoa tabasamu dogo halafu akasema.

“*We have a green light*!”alimwambia Gosu Gosu aliyekuwa pembeni yake ndani ya gari.Walikuwa mita chache kutoka ilipo nyumba ya Maurine Kyaso.

“Gosu Gosu, mara tu nitakapozima mfumo wa SNSA, tutakuwa na dakika ishirini tu za kumaliza kila kitu

kilichotuleta hapa hivyo basi, tunatakiwa kujitahidi sana kufanya mambo kwa haraka," alisema Ruby.

"Usihofu,Ruby!"alisema Gosu Gosu.Ruby aliyekuwa na kompyuta yake mapajani, akabonyeza kitufe chenye maandishi *ENTER*,program ikaanza kufanya kazi kama alivyotarajia.

"Itachukua muda gani kwa mfumo kuzima?"

"Dakika mbili,"

"Kwa nini idara nyeti kama hii inayohusika na usalama wa nchi ikawa na mfumo kama huu ambao mtu yeyote mwenye ubobevu katika masuala ya teknolojia anaweza akauzima au kuudukua?"Gosu Gosu aliuliza swali fikirishi.Ruby akacheka kidogo.

“SNSA ina mfumo bora kabisa ambao si rahisi kuingiliwa au kudukuliwa.Kwa muda mfupi nilioutumia jana usiku pale SNSA niliweza kuingia hadi ndani ya mfumo wao bila wao kugundua.Kuna kitu nilikifanya katika mfumo wao ili kuniwezesha kufanya chochote katika mfumo huo muda wowote ninaotaka” alisema Ruby.

“Unadhani hawawezi wakagundua kile ulichokifanya?”Gosu Gosu aliibua swali lingine.

“Gosu Gosu, unauliza maswali kama vile hunifahamu vizuri.Usiwe na wasiwasi wowote,” alisema Ruby.

“Ninakuamini,Ruby!” alisema Gosu Gosu.Muda mchache baadaye, katika

komputa ya Ruby kulionekana miduara mingi ya rangi nyekundu.

“Tayari.Twende sasa!” alisema Ruby kisha wakashuka garini huku Gosu Gosu akiwa makini kuchunguza kama wako salama.

Wakati Gosu Gosu na Ruby wakiwa katika harakati za kuingia nyumbani kwa Maurine,simu ya Maurine aliyeitwa Ikulu na Rais ikatoa mlio ambao ulimshtua kidogo.Akaitoa na kuitazama.

“Kuna tatizo lolote?”Rais Pius aliuliza.

“Naomba dakika moja,Mheshimiwa Rais.Nataka kuzungumza na SNSA,” alisema Maurine na kupiga simu ofisini kwake SNSA.

“Shakira, kuna tatizo gani hapo SNSA?”Maurine aliuliza.

“Mkurugezi ,kuna tatizo la kiufundi limetokea.Lakini linaendelea kushughulikiwa”

“Tatizo gani? aliuliza Maurine

“Mfumo umezima ghafla!” alijibu Shakira

“Sawa.Nataka tatizo hilo lishughulikiwe haraka sana na nipate taarifa nini sababu ya mfumo huo kuzima!” alisema Maurine kisha akakata simu.

“Nini kimetokea?”Rais Pius aliuliza.

“Kuna hitilafu ya kiufundi imetokea, lakini wanaendelea kuishughulikia,” alijibu Maurine.

“Sawa!Tuendelee na mazungumzo yetu,” alisema Rais.Wakaendelea na mazungumzo, lakini sura ya Maurine ilionesha wazi kuwa mawazo yake hayakuwepo pale kabisa.Wakati mazungumzo kati ya Rais na Maurine yakiendelea Ikulu,tayari Gosu Gosu na Ruby walikuwa ndani ya nyumba ya Maurine wakiendelea na zoezi la kuweka kamera za siri katika sehemu mbalimbali.

Chumba cha mwisho walichoingia kilikuwa cha kulala.Ruby akamuelekeza mahala pa kufunga kamera.Gosu Gosu hakupoteza muda, akaifunga kisha wakaweka kifaa kingine cha kunasa sauti.Ruby akafanya majaribio na kila kitu kilikuwa vizuri.

“Tumemaliza kazi.Tuondoke!” alisema Ruby kisha wakatoka na kurejea katika gari lao.Ruby akaikunjua kompyuta yake na kuingia katika programnu yake aliyoitumia kuzima mfumo wa SNSA, akaurudisha mfumo tena katika hali yake ya kawaida.

“*Done!*” Ruby alimtumia ujumbe Rais Pius,baada ya kuondoka eneo lile.

“Tunaelekea wapi?” Ruby aliuliza.

“Tunakwenda kuonana na jamaa ambao watatusaidia katika misheni ya usiku wa leo ya kumteka Carmelita,” alisema Gosu Gosu.

Ikulu Rais Pius alipokea ujumbe kutoka kwa Ruby ukimjulisha kuwa tayari wamemaliza kazi.Dakika kumi baadaye, akajulishwa kuwa balozi wa

Somalia hapa Tanzania alikuwa katika laini ya simu akitaka kuzungumza naye.Rais akamtaka Maurine akaendelee na majukumu yake.Maurine akaondoka.

14

AL KUFRAH – LIBYA

Ilikaribia saa kumi na mbili za jioni kwa saa za Libya,ndege moja ilipowasili katika uwanja wa ndege unaotumiwa na kundi la Ansar al Sharia.Mlango ulifunguliwa, wakashuka watu watatu.Hawa walikuwa ni Abdulkhareem Fadil Ghedi akiwa na dada yake Zahra pamoja nao akiwepo Sultan mfanyabiashara mkubwa wa madini jijini Arusha Tanzania.Milio ya risasi ikasikika kutoka kwa wafuasi wa Abdul waliokuwepo uwanjani hapo kumpokea kiongozi wao.Sultan aliingiwa na hofu.

“Usiogope Sultan, hii ni hali ya kawaida ukiwa hapa.Wanafurahi kuniona kiongozi wao nimerejea salama,” alisema Abdul.Akasalimiana na wafuasi wake waliokuwepo uwanjani hapo

kumpokea.Wakati huo huo,watoto wa shule waliotekwa Tanzania, wakashushwa ndegeni na kuingizwa katika gari.

Wa mwisho kushushwa ndegeni alikuwa Agai Sempa.Akiwa amefungwa pingu, akaingizwa katika gari lingine halafu msafara mrefu wa magari ukaondoka kuelekea katika makao makuu au kama wenyewe wanavyopenda kuita ngome kuu.

“Sultan karibu Libya.Hii yote ni himaya yangu.Kwa sasa ninaishikilia miji ya Al Kufrah,Marzuq,Awbari na Sabha.Tunajiandaa kuchukua miji ya Adjabiya,Tubruq,Darnah,Al Jabal,Al Faith na Benghazi.Baada ya hapo tutaanza hatua ya pili ya kuelekea

kuuchukua mji wa Tripoli.Tumechelewa kutokana na upinzani tunaokutana nao kutoka kwa makundi mengine yenye silaha kali lakini kwa sasa baada ya kuanza kuungwa mkono na Marekani InshaAllah tutaikomboa Libya," alisema Abdul huku akimtazama Sultan.

"Karibu katika maisha mapya Sultan.Sahau kuhusu Tanzania.Kila ulichokipoteza kule, hapa utakipata mara kumi zaidi.Pale nitakapofanikiwa kuitawala Libya,utakuwa mmoja wa watu wa juu kabisa katika serikali yangu," alisema Abdul.Lakini Sultan,dhahiri alionekana kuwa mbali sana kimawazo.

Safari iliendelea hadi walipoingia katika ngome kuu ya Abdul.Ulinzi

uliokuwepo mahala hapo haukuwa wa kawaida.Sultan akakaribishwa ndani,akatambulishwa kwa baadhi ya makamanda na watu wa juu wa kundi hilo kisha akapelekwa katika jengo kuu la Abdul kwa ajili ya mapumziko.Lilikuwa kasri zuri mno.

Wanafunzi waliotekwa, wakaingizwa katika chumba kimoja kikubwa.Wakatolewa vitambaa usoni kisha wakaingia madaktari sita wanawake na kuanza kuwahudumia wale waliokuwa wamejeruhiwa.Baada ya hapo, wakapelekwa katika mabafu kuoga kisha wakapewa mavazi mengine na chakula.

Agai Sempa alifungwa katika chumba kisicho na dirisha.Mkono wake

wa kulia ulifungwa katika meza iliyokuwa na chuma katikati huku meza hiyo ikiwa imeshikiliwa na zege imara.

“Tumesafiri umbali mrefu sana.Nahisi tutakuwa tumepelekwa sehemu ya mbali.Tumebadilisha vyombo kadhaa vya usafiri.Tulishushwa katika boti,tukaingia katika magari halafu tukaingia katika ndege na hapa tulipofika sijui kama tutahamishwa tena au ndipo wanapoishi hawa magaidi.Nahisi haya ndiyo makao makuu ya hawa magaidi kwa kuwa nilisikia milio ya risasi na watu wakishangilia mara tu ndege ilipowasili” aliwaza Agai .

Akiwa yungali katika lindi la mawazo,ghafla mlango wa chumba ukafunguliwa, akaingia mtu

mmoja,aliyekuwa ameongozana na watu wengine wanne ambao kwa mwonekano tu, walikuwa walinzi wake.Mtu yule alivuta kiti akaketi.

“Assalam alaykum,” alisema yule jamaa kwa upole, lakini Agai hakujibu kitu.

“Karibu sana.Hapa ni Al Kufrah Libya.Mimi naitwa Abdulkhareem Fadil Ghedi kiongozi mkuu wa Ansar Al Sharia” alisema Abdulkhareem huku akionesha mwonekano wa kijivuni.

“Mna chakula chochote hapa?” Agai akatoa sauti.

“Sisi si watu wabaya au makatili kama tunavyochukuliwa.Sisi ni watu waungwana, lakini tunakuwa wakali na kulazimika kutumia nguvu pale

tunapodai haki.Mleteeni chakula ale halafu apumzike kisha tutazungumza,”alisema Abdul huku akisimama.Akatoka huku akitoa maagizo kwa lugha ya Kiarabu kwa watu waliokuwa wanalinda chumba alimo Agai.

Baada ya kutoka katika chumba alimo Agai, akaenda katika chumba kikubwa walimokuwamo watoto waliowateka.Kulitandikwa magodoro na watoto wote baada ya kula walitakiwa kulala.Mlango ulipofunguliwa,watoto wote wakainuka.

“Poleni sana watoto.Ninaitwa Abdulkhareem Fadil Ghedi.Ni mkuu wa kundi hili lililowachukua Tanzania.Nawaomba msihofu hapa mko

sehemu salama.Tunafanya mazungumzo na serikali ya Tanzania,kama tukikubaliana, basi mtarejeshwa nyumbani.Lakini nawahakikishia kwamba hakuna ambaye atachinjwa tena ila kuondoka kwenu hapa kutategemea na ushirikiano utakaotolewa na serikali ya Tanzania namna watakavyoweza kutimiza madai yetu.Kadiri wakatavyochelewa, ndivyo ninyi mtakavyoendelea kukaa hapa.Na kama wakipuuzia kabisa, basi hamtarejea tena nyumbani kwenu!" alisema Abdul. Kauli iliyozalisha vilio kutoka kwa watoto hao

"Kimyaaa!!"Abdul alisema kwa ukali. Papo hapo wasichana wakaogopa, wakakaa kimya kabisa.

“Mkiwa hapa, mtapata kila mnachokitaka,wakati tunaendelea na mazungumzo na serikali yenu.Tutawaeleza kila hatua inayofikiwa kati yetu na Tanzania,” alisema Abdul kisha akatoka. Nyuma yake aliacha vilio vikirindima.

****

Kwa mara nyingine, mlango wa chumba alimo Agai ukafunguliwa.Akaingia Abdulkhareem.Hakuwa peke yake.Aliongozana na watu wengine wawili na nyuma yao kulikuwa na walinzi.Abdul akavuta kiti akaketi

“Naamini tayari umekwishapata chakula na sasa tunaweza kuzungumza,” alisema Abdulkhareem.Mmoja wa watu aliyeongozana naye mwenye wajihi mfupi na ndevu nyingi, akasogea mezani.

“Tunataka utuambie jina lako,” alisema yule jamaa kwa Kiswahili sanifu kabisa.Agai akamtazama kwa macho makali.

“Naitwa Agai Sempa,”alijibu kibabe

“Agai Sempa, unafanya kazi idara gani? Wewe ni askari polisi?”Jamaa aliuliza maswali mfululizo.

“Wewe jina lako nani?”Agai likamtoka swali badala ya kujibu swali.

“Mimi ndiye ninayekuuliza.Hivyo sitaki uanze kuuliza maswali!”alifoka yule jamaa kwa sauti ya juu.

“Nimekwisha kutajia jina langu. Nawe nitajie lako tuendelee na mazungumzo ama muondoke humu ndani!”alisema Agai kwa msisitizo.Jamaa wakazungumza kwa Kiarabu,kisha aliyekuwa akimuhoji Agai akasema.

“Ninaitwa Sultan.Sasa nijibu swali nililokuuliza.Unatokea idara gani ya usalama?” aliuliza Sultan

“Kumbe ni wewe msaliti mkubwa kwa nchi yako.Kwa nini umeshirikiana na hawa mashetani kufanya uhalifu huu mkubwa? Unapata faida gani kumwaga damu ya Watanzania wenzak…..” Agai alisema kwa hasira, lakini hakumaliza kauli yake,akalambwa kofi zito. Agai

hakushtuka hata kidogo.Akamkata Sultan jicho la dharau.

“Ukweli umekuumiza.Umesaliti nchi yako na Watanzania shetani mkubwa wewe!”alisema Agai bila woga.

“Agai, naomba ujibu kile ulichoulizwa.Unatokea chombo gani cha ulinzi?”Aliuliza Sultan

“Sitokei chombo chochote cha ulinzi.Mimi ni Mtanzania mzalendo ambaye niko tayari kumwaga damu yangu kwa kuipigania nchi yangu,” Agai alijibu kishujaa akimkazia macho Sultan.

“Umeua watu wetu, unafahamu adhabu inayokukabili?”Abdul aliuliza kwa Kingereza.

“Ndiyo.Najua adhabu yangu ni kifo!”alijibu Agai

“Watu uliowaua ni makamanda wangu niliowaamini sana.Adhabu inayokukabili ni kifo, lakini tunaweza kukuondolea adhabu hiyo, endapo utakubali kushirikiana nasi.” Alisema Abdul

“Siwezi kushirikiana nanyi kwa namna yoyote ile.Tanzania na Watanzania hata siku moja hatufanyi makubaliano na magaidi.Jukumu letu sisi ni kuwaangamiza magaidi wote na kuwapeleka wanakostahili.Nataka kuwahakikishia kwamba mtaniua mimi, lakini hautakuwa mwisho wa mapambano haya.Watanzania wazalendo na imara wako wengi,watawafikia hapa

mlipo na kuwakomboa watoto mnaowashikilia!!alisema Agai kwa ghadhabu.Hali iliyomfanya Abdulkhareem atoe kicheko kidogo.

“Unajidanganya,Agai. Mosi, hakuna mtu anayefahamu uko hapa.Pili,hakuna Mtanzania anayeweza kufika mahala hapa. Tatu, hakuna muujiza unaoweza ukafanyika kuja kukuokoa wewe na wasichana tunaowashikilia,” alisema Abdulkhareem akichanua tabasamu la kejeli.

“Kwa nini mnawashikilia wale wasichana wadogo?Wamekosa nini? Kama mnataka makubaliano yoyote na mimi, lazima mkubaliane na masharti yangu!”alisema Agai.

“Nini unakitaka,Agai?”aliuliza Abdulkhareem

“Ili tufanye mazungumzo yoyote, mimi nanyi nataka kwanza wasichana wote waachiwe warudi nyumbani.Kama hamuwezi kufanya hivyo, sintafumbua tena mdomo wangu kuzungumza nanyi chochote kile,” Agai alisema akiwatazama usoni

”Mnakubaliana na sharti hilo?”Agai aliuliza.Abdulkhareem akabaki kimya akimtazama Agai.Ghafla akaangua kicheko cha maudhi kilichojaladiwa na dharau kwa juu.

“Agai! Agai! Agai!” Abdul alisema huku akitikisa kichwa. “Agai nimeupenda sana ujasiri wako.Umetuonesha ni namna gani

unawajali na kuwathamini wasichana wale hadi kuuweka uhai wako hatarini.Utajisikiaje pale utakapowaona wasichana wale wakiingiliwa kimwili mmoja baada ya mwingine?”Kauli ya Abdulkhareem ikaleta wingu la mtanziko katika sura ya Agai.Akabadilika kabisa.

“Msithubutu kufanya kitu kama hicho.Ninawaapia,nitawafanya kitu kibaya sana hamnifahamu mimi ni nani” Agai alitamba.

“Sikiliza Agai.Tunafahamu kila kitu kuhusu wewe.Tunajua ulikuwa umefungwa gerezani na ukatolewa leo na Rais Pius.Wewe na mwenzako mkatumwa katika ukumbi wa KICC, mkijifanya ni madaktari na unajua kile mlichokifanya mle ndani.Ninyi wawili

ndio mliowaua watu wangu ukumbini," alisema Abdulkhareem bila sura ya utani.Agai kijasho kikamtoka.

"Hawa jamaa wana mtandao mpana sana.Wamewezaje kupata taarifa hizi zote?"Agai alijiuliza.

"Agai unajiuliza tumewezaje kuyafahamu hayo yote?Tulikuuliza maswali machache ili kukupima, lakini tunafahamu kila kitu.Kuna kitu kimoja tu ambacho endapo utatueleza ukweli, basi tutawaachia watoto tunaowashikilia kama ulivyoomba.Kuna watu wawili tu, ambao mnafahamu mahala lilipo sanduku jeusi ambao ni wewe na yule mwenzako Gosu Gosu.Nataka utuambie sanduku liko wapi?" alisema

Abdulkhareem na kuzidi kumshangaza Agai.

“Sanduku liko sehemu salama na kamwe hamtaweza kulipata!”alisema Agai kikakamavu.

“Agai, hatuhitaji masihara katika hili.Tunataka kufahamu mahala lilipo hilo sanduku!”alisema Abdulkhareem

“Mimi si mgeni wa mambo haya, hata nikiwaeleza najua mtaniua,hivyo niko tayari kuuawa, lakini si kuwaeleza mahala lilipo sanduku hilo!”Agai alisimamia msimamo wake.Abdulkhareem akapiga meza kwa hasira.

“Nitakuharibu haribu,Agai.Hebu tueleze mahala lilipo sanduku!”Abdulkhareem alifoka.

“Siwezi kuwaeleza chochote!”

“Waleteni wasichana wawili humu ndani haraka sana!”alifoka Abdulkhareem.

“Umeyatoa maisha yako kwa ajili ya kuwaokoa wasichana hawa, lakini utajisikiaje pale utakapoona wasichana hao wakiingiliwa kimwili mbele yako?” Abdulkhareem alisema.Agai akainuka, lakini kabla ya jitahada zozote, akaelekezewa bunduki,akarudi chini.

“Msithubutu kuwafanyia chochote wasichana hao!”alisema Agai.

“Ni wewe ambaye unaweza ukawasaidia hawa wasichana kwa kutueleza mahali liliko sanduku.Tueleze tafadhali liko wapi?”

“Siwezi kuwaeleza chochote niko tayari mnipige risasi nife, lakini si kuwaeleza lilipo sanduku hilo!” alisema Agai.

“Hautaipata tena nafasi nyingine kama hii.Tafadhali tueleze lilipo sanduku hilo au utashuhudia ukatili mkubwa sana kwa wasichana hao ambao umewapigania hadi hatua hii,” alisema Abdulkhareem. Mara mlango ukafunguliwa, wakaingizwa wasichana wawili wakilia.

“Ee Mungu, mimi si mkamilifu, lakini naamini katika nguvu na uwezo wako.Ninakuomba usiruhusu watoto hawa wafanyiwe udhalilishaji.Hawastahili kufanyiwa

unyama kama huu!”Agai aliomba kimya kimya.

“Agai, ninakupa nafasi ya mwisho kabla hujashuhudia wasichana hawa uliowapigania kutaka kuwakomboa wakifanyiwa kile ambacho hawastahili kufanyiwa. Bado ni wadogo,lakini kama kweli una dhamira ya dhati ya kutaka kuwasaidia, basi tueleze mahala lilipo lile sanduku tunalolitafuta,” alisema Abdulkhareem.

“Aaaggh!!”alisema Agai kwa hasira.

“Sanduku liko wapi.Agai?”Sultan aliuliza.Agai akawa kimya. Abdulkhareem akawaelekeza walinzi wake kumvua msichana mmoja nguo.

“Subiri!”alisema Agai,zoezi likasimama.

“Uko tayari kueleza ukweli mahala lilipo sanduku?”Aliuliza Sultan.

“Mvalisheni mtoto mavazi yake!” Alisema Agai.Abdulkhareem akawaelekeza walinzi kumvalisha yule msichana nguo zake.

“Tueleze mahala lilipo sanduku!”alisema Sultan.Agai akavuta pumzi ndefu.

“Agai, tueleze tafadhali mahala lilipo sanduku ama .....” Abdulkhareem akafoka, ghafla msaidizi wake mkuu Gamil, akaingia.Akamnong’oneza kitu,Abdulkhareem akaonekana kushtuka.

“Zoezi lisimame kwanza.Warudisheni hawa wasichana

chumbani kwao, tutaendelea baadaye kidogo!” alisema Abdulkhareem huku akimtazama Agai.

“Nitarejea baada ya muda mfupi.Elewa kwamba, sitahitaji masihara.Nataka unieleze mahali lilipo sanduku!”Abdul alisema kisha akatoka na watu wake.

“Kuna nini, Abdul? Mbona tumesimamisha zoezi?” aliuliza Sultan

“Nimeambiwa mwanangu Fahad amefika!”

“Fahad?” Sultan aliuliza kwa mshangao.

“Ndiyo” alijibu Abdul

“Nakumbuka mara ya mwisho uliniambia Fahad alikuwa amefungwa gerezani nchini Ujerumani kwa kosa la

kukutwa na silaha bila kuwa na kibali," alisema Sultan.

"Ndiyo.Tulikuwa katika mgogoro mkubwa nikamtengenezea ile kesi ya kukutwa na silaha akafungwa gerezani.Ninashangaa amewezaje kutoka gerezani.Nimeshtuka sana.Nataka nimsikilize na kujua amewezaje kutoka gerezani halafu tutaendelea na zoezi letu," alisema Abdulkhareem.

Moja kwa moja wakaelekea katika jumba kubwa la kifahari.Walipoingia sebuleni, wakamkuta Fahad,akasimama alipomuona baba yake.Akamfuata,wakakumbatiana.

"Karibu nyumbani, Fahad!"alisema Abdulkhareem.

“Nashukuru baba!” alisema Fahad,kisha akasalimiana na Zahra, shangazi yake pamoja na Sultan.Baada ya salamu, Abdulkhareem akaomba watoke wakazungumze faragha.

“Fahad, nimefurahi sana kukuona tena mwanangu.Sikutarajia kama ungerejea nyumbani siku kama ya leo.Umewezaje kutoka gerezani?”Abdulkhareem aliuliza kwa upole.Fahad akatoa machozi.

“Baba!” Alisema Fahad kisha akaweka tuo. Chozi liliendelea kushuka kidogo kidogo kisha akaendelea.

“Kwa nini ulinitelekeza na kuniacha nikafungwa gerezani wakati unafahamu kabisa kuwa kesi ile iliyokuwa inanikabili haikuwa ya kweli na zile

silaha walizonikuta nazo nilibambikiwa?”Chozi la uchungu likaumbwa na Fahad.

“Utanisamehe sana, Fahad!Nilijitahidi sana kuzungumza na watu mbali mbali nchini Ujerumani ili wakusaidie, lakini wote waliniambia kwamba kesi inayokukabili ni mbaya na hakuna namna nyingine ya kuweza kukusaidia.Najua nimekukosea mwanangu, naomba unisamehe!” alisema Abdulkhareem.Fahad akatoa sigara, akaiwasha, akavuta mikupuo kadhaa na kupuliza moshi mwingi.

“Hayo yamekwishapita baba, kitu cha muhimu ni kwamba nimetoka gerezani na nimerejea tena nyumbani.”

“Karibu tena nyumbani, Fahad.Uliwezaje kutoka gerezani?”

“Watu wenye huruma na mapenzi na mimi walinisaidia nikaweza kutoka gerezani.Kitu kikubwa kwa sasa ni kuangalia maisha ya mbeleni baada ya kurejea nyumbani.Mambo yanakwendaje hapa?”

“Mambo yanakwenda vizuri.Tunaendelea kupata ushindi japo tunakumbana na upinzani mkali kutoka kwa vikosi vya serikali na vile vya waasi ambao kwa sasa wameunganisha nguvu ili kupigana nasi.Lakini tutashinda na kuikomboa tena Libya.Umekuja wakati mzuri sana, kwani leo hii nimerejea kutoka Tanzania” alisema Abdul

“Baba nimeamua kurejea nyumbani kuja kuungana nawe tena katika ukombozi wa Libya.Nataka unishirikishe katika mapambano haya,” alisema Fahad.Abdulkhareem akainuka na kumkumbatia mwanaye.

“Ninajivunia sana kuwa na kijana kama wewe.Ahsante kwa maamuzi haya makubwa uliyoyafanya.Kwa pamoja tutaikomboa ardhi hii na utashika nafasi ya juu ya uongozi katika serikali nitakayoiunda,” alisema Abdulkhareem.

“Nilipofika, niliambiwa kuna mateka ulikuwa unawahoji.Umetoka nao Tanzania?”Fahad aliuliza.

“Ndiyo.Kuna watu kadhaa nimetoka nao Tanzania.Kuna jasusi nilikuwa

namuhoji anieleze lilipo sanduku tunalolitafuta!”

“Sanduku lipi hilo?”

“Nitakueleza kila kitu usihofu.Kuna mpango mkubwa sana unaendelea hivi sasa,” alisema Abdulkhareem.

“Huyo jasusi amesema chochote? Ameonesha lilipo hilo sanduku?” aliuliza Fahad

“Tulipopata taarifa za ujio wako,tulikuwa katika harakati za kumuhoji,alikuwa anataka kufunguka kwani tulitishia kuwaingilia kimwili wasichana tuliowateka!”

“Mmeteka na wasichana?”Fahad aliuliza kwa mshtuko.

“Ndiyo!Tumeteka wasichana kadhaa akiwamo mtoto wa Rais wa

Tanzania.Hawa tunataka kuwatumia katika kuilazimisha serikali ya Tanzania kutekeleza madai yetu.”

“Safi sana.Naweza kuruhusiwa kuwaona wasichana hao?”Fahad aliuliza.

“Fahad, umekuja leo pumzika.Sisi tutaendelea na kazi!”

“Baba, usihofu.Nimekuja kufanya kazi, hivyo nataka nikusaidie nawe upumzike.Nioneshe walipo wasichana hao tafadhali halafu unipeleke alipo huyo jasusi nishughulike naye hadi atakapofunguka,” alisema Fahad.

“Ni wasichana wadogo, lakini wazuri sana.Unataka kuchagua mmoja wa kupitisha naye usiku wa leo? Au hata wa kuoa kama utataka,” alisema Abdulkhareem huku akiangua kicheko.

“Kwa sasa masuala ya kuoa nimeyaweka pembeni baba” alijibu Fahad.

“Yule mwanamke wako mmewasiliana? Mwanao anaendeleaje?” Abdul aliuliza

“Nilikata mawasiliano nao kama ulivyonitaka, hivyo sifahamu walipo na wanaendeleaje,” alijibu Fahad.

“Ulifanya vizuri sana Fahad, kukata mawasiliano nao.Ulikosea mwanangu kuingia katika mahusiano na yule mwanamke.Kwanza si wa dini yetu,vile vile ni mtu mweusi na kibaya zaidi Mmarekani ambao ni maadui zetu na kamwe hatupaswi kuchanganya nao damu.Fahad, tulia na utampata mwanamke ambaye atakufaa,mwenye

maadili mema ya dini na anatokea aidha hapa Libya au katika nchini za Kiarabu," alisema Abdulkhareem.

"Ujana ulikuwa unanisumbua baba, lakini baada ya kugundua kosa nililolifanya,nikakata mawasiliano nao," alisema Fahad.Wakainuka na kurejea sebuleni. Wakaongozana na akina Sultan kuelekea katika chumba walimokuwamo wasichana waliotekwa.

"Hawa ndio wasichana tuliowatoa Tanzania," alisema Abdulkhareem.Wakatoka katika kile chumba cha wasichana, wakaelekea katika chumba alimokuwamo Agai.

"Huyu ndiye yule jasusi kutoka Tanzania ambaye anafahamu lilipo sanduku tunalolitafuta.Anaitwa Agai

Sempa,” alisema Abdulkhareem.Fahad akamtazama.

“Naombeni bastola.Nataka nimfungue huyu aseme kila kitu!”alisema Fahad.Baba yake akatabasamu akatoa bastola yake,akampatia.Fahad akaikagua,akaikuta na risasi za kutosha.Akamfuata Agai alipo.

“Mfungueni pingu!”alisema Fahad.Agai akafunguliwa pingu, Sultan akabaki akishangaa.

“Nitahesabu mpaka tano, nataka kabla sijamaliza kuhesabu, unieleze mahala lilipo sanduku.Umenisikia?”Fahad akauliza kwa ukali huku akikiinua kichwa cha Agai kwa bastola.

“Moja!”Fahad alianza kuhesabu.

“Fahad, unataka kufanya nini? Huyu mtu ana taarifa muhimu sana!”alisema Sultan kwa wasiwasi.

“Fahad anajua anachokifanya!” alisema Abdulkhareem hakuwa na hofu yoyote.

“Mbili!” Fahad aliendelea kuhesabu huku Agai akimtazama machoni. Kuna ishara fulani aliisoma machoni kwa Fahad.

“Abdulkhareem, ni vyema kama tukitumia njia ile tuliyoitaka kuitumia ya kuwaingilia wale wasichana kuliko hii anayotaka kuitumia Fahad,” Sultan alisema kwa kihoro.

“Mwanangu ni mwanajeshi.Anajua anachotaka kukifanya.Tumpe nafasi,” alijibu Abdulkhareem.

“Tatu!”alisema Fahad huku macho yake ameyaelekeza kwa Agai.

“Nne!”Fahad aliendelea kuhesabu.

“Abdul, sina imani na Fah…..” alisema Sultan.Fahad akahesabu tano,ghafla kukasikika kishindo kikubwa cha bomu.Eneo lote likatetemeka.Agai akaitumia taharuki ile mle ndani akamrukia mmoja wa walinzi wa Abdulkhareem, akamtandika kichwa kizito na kumnyang’anya bunduki.Akageuka nayo kwa haraka na kuizinga, akaachia risasi mfululizo zilizowalambisha sakafu walinzi wa Abdulkhareem waliokuwa wameduwaa

kufuatia mlipuko ule mkubwa wa bomu.Walinzi wawili wakaingia, lakini wote walikaribishwa na mvua ya risasi kutoka kwa Agai.

Mara moja Abdulkhareem akajua mambo yameharibika.Akaruka na kuanza kukimbia kuelekea mlangoni, lakini Fahad aligeuka kwa kasi ya ajabu na kumpiga risasi mbili mguuni, akaanguka chini.Milio ya risasi na mabomu viliendelea kusikika nje.

“Fahad! Fahad! Alilia Abdulkhareem kwa uchungu akimtazama mwanaye.Wakati huo huo,Agai akiwa amewaelekezea bunduki Sultan na Zahra waliokuwa wanatetemeka.

“Fahad, nimekukosea nini hadi ukanifanya hivi?”Abdulkhareem akauliza kwa ukali.

“Baba, nimekuja kuhitimisha enzi yako.Ukatili ulioufanya umetosha,”alisema Fahad kwa ukali.

“Nani amekudanganya, Fahad? Nani wameingia ndani ya kichwa chako na kukufanya ukanisaliti hata mimi baba yako?”Aliuliza Abdulkhareem kwa ukali

“Nimeamua kwa hiari yangu kuja kukuondoa.Nina hasira nawe sana kwa mambo uliyonifanyia.Mambo uliyowafanyia watu wa Libya na sehemu nyingine.Wewe huna tofauti na baba yako aliyeko gerezani. Ninyi nyote ni makatili mliopindukia!”alisema Fahad

huku akiendelea kumtazama baba yake kwa hasira.

Ghafla Zahra akakurupuka kutaka kumvaa Fahad, lakini Agai alikuwa mwepesi mno, akaachia risasi kadhaa kuelekea upande ule, Zahra akaanguka chini.

“Safi sana!”alisema Fahad akainama,akaiokota bunduki ya mmoja wa walinzi wa Abdulkhareem, akammiminia baba yake risasi nyingi huku akipiga kelele hadi risasi zilipokwisha.Mwili wa Abdulkhareem haukuwa ukitazamika kwa jinsi ulivyochakazwa na risasi.

“Fahad, imetosha!”alisemaAgai.

“Bado nina hasira sana na huyu mtu.Natamani niendelee kummiminia

risasi!”alisema Fahad akiutazama mwili wa baba yake kwa hasira.

“Haya ni malipo ya uovu wako!”alisema Fahad,akamgeukia Agai.

“Muue na huyo aliyebaki ” alisema Fahad.

“Huyu tumuache tusimuue.Tunahitaji kufahamu mahali ilipo diski,” alisema Agai.Ghafla bin vuu, mlango ukafunguliwa,Agai alikuwa mwepesi tayari alikwisha ielekeza bunduki mlangoni akidhani ni watu wa Abdulkhareem.Akataka kuachia risasi, lakini Fahad akamuwahi.

“Usipige risasi! Usipige risasi!”alisema Fahad.Watu wawili waliovaa fulana za kujikinga risasi wakiwa na bunduki nzito, wakaingia mle

ndani.Huko nje bado milio ya risasi na mabomu ya kurusha kwa mkono viliendelea kusikika.

“Uko salama, Fahad?”Aliuliza mmoja wa wale jamaa walioingia mle ndani.

“Niko salama kabisa.Ahsante sana,Mathew Mulumbi kwa kutekeleza mpango kwa wakati kama tulivyopanga” alisema Fahad.Agai akashtuka.

“Mathew Mulumbi, ni wewe?”Agai aliuliza asiyaamini macho yake kama mtu yule aliye mbele yake ni Mathew Mulumbi

“Hello,Agai !”alisema Mathew huku akimpa mkono Agai.

“Umenifahamuje?”Agai aliuliza.

“Huu ni mpango mkubwa sana Agai.Tulikuwa tunafuatilia kila kilichokuwa kinaendelea hapa ndani.Kumefungwa kamera za siri sehemu mbali mbali kuzunguka ngome hii.Agai, hatuna muda wa mazungumzo ila hongera umefanya kazi kubwa” alisema Mathew.

“Ahsante sana Mathew.Vipi kuhusu wasichana?” Fahad aliuliza.

“Tayari wote washakombolewa. Pia wameondolewa katika eneo hili,” alijibu Mathew.

“Wote wako salama?”Agai aliuliza.

“Wote wako salama kabisa!” alijibu Mathew.

“Tuondokeni hapa kabla vikosi vingine vilivyoko karibu havijafika.Kuna

kambi nyingine si mbali na hapa.Naamini baada ya kusikia milio ya mabomu, watafika mara moja,”alisema jamaa aliyeongozana na Mathew.

“Ahsante sana, Gamil, kwa msaada huu mkubwa.Una hakika hakuna aliyekuona unashirikiana na vikosi vya serikali?”Fahad aliuliza.

“Hakuna anayefahamu,” Gamil alijibu.

“Gamil ulikuwa msaidizi mtiifu wa baba, lakini kwa sasa baada ya baba kuuawa kundi hili la Ansar al Sharia limesambaratishwa rasmi.Kila kitu alichokuwa nacho baba, kinabaki mikononi mwako.Utajiri wote wa baba ni wako,” alisema Fahad.

“Fahad, baba yako ni tajiri sana.Siwezi kuuchukua utajiri wote peke yangu,” alisema Gamil.

“Sihitaji mali yoyote ya baba.Nilichokuwa nakihitaji ni kumuua ili niwe huru kuendelea na maisha yangu.Chukua kile unachoona kitakutosha kuanzisha maisha mapya uondoke” alisema Fahad.

“Sawa, Fahad.Twendeni niwatoe humu kabla vikosi vingine havijafika,” alisema Gamil.Fahad akatoa simu yake,akaipiga picha miili ya Abdulkhareem na dada yake Zahra.

“Huyu jamaa ni nani?”Mathew alimuuliza Agai.

“Anaitwa Sultan.Ndiye aliyesaidiana na magaidi kuandaa mashambulio ya

Arusha.Nimemuacha hai kwa kuwa anafahamu mahali ilipo diski mweko aliyokuwa nayo Fabrice Kayembe," alisema Agai.Mathew akamfuata Sultan.

"Diski iko wapi?"Mathew aliuliza kwa Kiswahili.

"Sifahamu ilipo" alijibu Sultan.

"Mpekue!" Mathew alimuelekeza Agai, akampekua, lakini hakuwa na diski.

"Mpekue na yule kiongozi wao" alisema Mathew,Agai akampekua Abdulkhareem,naye hakuwa na diski.

"Tuoneshe tafadhali diski iko wapi?"Mathew alimuuliza Sultan kwa upole, lakini hakujibu kitu.

"Agai hebu mshughulikie huyu mtu mara moja afunguke mahala iliko diski"

alisema Mathew kisha yeye,Fahad na Gamil wakatoka nje.Baada ya dakika kadhaa wakarejea ndani wakamkuta Sultan akiwa hatazamiki usoni.Alikuwa amechafuka damu

“Huyu Agai, mambo yake ni kama Gosu Gosu.Ndani ya kipindi hiki kifupi tayari jamaa hatazamiki,”aliwaza Mathew.

“Amefunguka mahala iliko diski?”Mathew aliuliza.

“Ndiyo!”Agai alijibu.

“Amesema diski iko wapi?”Mathew aliuliza.

“Iko Tanzania!”

“Una hakika anasema ukweli?”

“Ndiyo!”

“Iko Tanzania sehemu gani?”

“Hajasema bado ni sehemu gani.”

“Good!Atatueleza mbele ya safari.Tuondokeni mara moja,” alisema Mathew.Wakamchukua Sultan na kutoka mle ndani.Gamil akawaongoza katika njia ya siri,wakatokea nje ya ile ngome kuu ya Abdulkhareem ambayo iliendelea kusambaratishwa.

Helkopta ikashuka taratibu, akina Mathew wakaingia,Fahad akaagana na Gamil ambaye bado aliendelea kushirikiana na vikosi vya serikali.Helkopta ikapaa kuelekea katika uwanja mdogo wa ndege wa Al Kufrah ambao tayari ulikuwa chini ya vikosi vya serikali.Pale uwanjani walikuta ndege ikiwasubiri, wakaingia.Ndani yake,waliwakuta wasichana wote

waliowakomboa wakiwa ndegeni.Wakashangilia sana baada ya kumuona Agai.Bila kupoteza muda, ndege ikapaa na kuondoka.

“Ahsante sana,Mathew Mulumbi!” alisema Agai wakiwa angani.

“Agai, tutapata muda wa kushukuru pale tutakapofika katika ardhi ya nyumbani, lakini kwa sasa tuna safari ndefu kidogo kuelekea Tripoli hivyo tukiwa safarini, tuendelee kumuhoji yule jamaa atueleze mahali ilipo diski,” alisema Mathew.Akatoka katika chumba walichokuwamo.Akafunua pazia, akaingia katika sehemu walimokuwamo watoto.

“Habari zenu, mabinti!” Mathew aliwasalimu wasichana.Waliposikia

lugha ya Kiswahili, wote wakainua vichwa na kumuitikia.

“Jina langu naitwa Mathew Mulumbi.Ni Mtanzania.Kwa sasa tumeshawaondoa katika mikono ya wale magaidi,tunaelekea Tripoli ambako tutachukua ndege kurejea nyumbani.Nawasihi msiwe na hofu tena mko salama kabisa.Kuna yeyote ambaye ameumizwa na anahitaji matibabu?”Mathew aliuliza lakini hakuna aliyehitaji matibabu

“Pumzikeni.Tutapata nafasi ya kuzungumza pale tutakapokuwa tumefika Tripoli,” alisema Mathew.Akamfuata Fahad aliyekuwa katika chumba kidogo peke yake akiwa na sanduku la rangi ya fedha lenye

komyuta na vifaa mbali mbali vya mawasiliano.Mathew akamtaka ampatie simu ili aweze kumpigia Gosu Gosu.

“Hallow!” Gosu Gosu aliitikia simu.

“Gosu Gosu, nataka kufahamu kama misheni ya kumuokoa Carmelita imekwenda vizuri na imekamilika,”alisema Mathew huku Fahad akimtazama kwa macho yaliyojaa wasiwasi.

“Mathew, kila kitu kimekwenda vizuri.Calmerita na mwanaye wote wako salama,” alisema Gosu Gosu.

“Gosu Gosu, ahsante kwa kazi kubwa mliyoifanya.Kama nilivyoahidi nitarejea nyumbani.Nitakupigia tena simu kukupa maelekezo” alisema Mathew.Akakata simu.

“Fahad, ninapaswa kukushukuru kwa maamuzi magumu uliyoyafanya.Kupitia kwako, tumeweza kuwapata wasichana wetu waliokuwa wametekwa vile vile kumuondoa Abdulkhareem Fadil Ghedi kiongozi wa kundi la kigaidi la Ansar al Sharia ambaye ni baba yako.Kundi hili limeshamwaga damu nyingi ya watu wasio na hatia”alisema Mathew akarejea katika chumba alikomuacha Agai ambaye aliendelea kumtesa Sultan.

“Amesema mahala ilipo diski?”Mathew aliuliza.

“Anakuwa mgumu kueleza chochote!”

Mathew akamsogelea Sultan.

“Sultan, jina langu naitwa Mathew Mulumbi.Naamini umewahi kulisikia jina hilo.Una bahati mbaya umekutana nami leo hii.Nataka unieleze mahali ilipo diski nchini Tanzania kabla hatujafika Tripoli.Maana kitakachokukuta ni kisanga kikubwa sana!”alisema Mathew akitazamana na Sultan.

“Sultan, kama una kitu chochote cha kunieleza muda ni huu.Usisubiri mpaka tutakaposhuka, utatamani mtoa roho aje aichukue roho yako lakini haitachukuliwa!” alisema Mathew.Sultan aliendelea kubaki kimya bila majibu yoyote yale.

“Agai, naomba koleo nimuoneshe huyu jamaa anazungumza na mtu wa aina gani,” alisema Mathew.Agai

akampa koleo dogo.Wakamfunga Sultan mikono na miguu kwa waya, halafu wakamvua suruali.Sultan jicho likamtoka.

“Mnataka kunifanya nini?”Sultan alisema kwa woga.Mathew akaidaka korodani moja na koleo, akaanza kuiminya. Yowe la uchungu likamponyoka Sultan. Alikuwa akipitia maumivu yasiyomithilika.

“Diski iko wapi?”Mathew aliuliza.Sultan akatukana kwa Kiarabu.Mathew akaibana tena kwa nguvu zaidi.

“Diski iko wapi?”Mathew aliuliza huku akimtazama Sultan ambaye tayari macho yake yalijaa machozi.

“Hapa ninakuonesha utangulizi wa kile kinachokwenda kukutokea pindi tutakapofika Tripoli. Kwa mara nyingine tena, iko wapi diski?”Mathew alifoka.

“Diski...!” alisema Sultan akivuta pumzi ndefu.

“Ndiyo!Iko wapi?”

“Iko kwa Omega!”

“Omega ni nani?”

“Ni mfanyakazi wangu!”

“Sultan, naomba usitutanie.Tulielezwa kila kitu na mmoja wa watu wenu kwamba baada ya kupewa diski katika ukumbi wa KICC. Jamal aliwasiliana nanyi na akaja katika makazi yako, akakukabidhi hiyo diski, nawe ukampatia Abdulkhareem.Tunafahamu

mchezo mzima ulivyokwenda.Tueleze mahali diski ilipo," alisema Agai.

"Ninawaambia ukweli.Diski hatukuja nayo huku.Ilibaki Tanzania.Alipewa Omega ili aipeleke katika hoteli ya Meru Paradise amkabidhi dada mmoja anaitwa Rebeca Anderson."

"Huyo Rebeca ni nani?"Mathew aliuliza.

"Simfahamu!Ila ndiye tulipewa maelekezo ya kumpatia hiyo diski."

"Nani aliwapa maelekezo hayo?"Mathew aliuliza, Sultan akakaa kimya.

"Nakuuliza, Sultan.Nani aliwapa maelekezo ya kumpatia diski, Rebeca?"

“Sifahamu.Ni Abdulkhareem pekee aliyekuwa anafahamu,”alisema Sultan.Mathew akamtazama halafu akatoka, akamfuata Fahad, akachukua simu kutoka katika sanduku la mawasiliano, akampigia Gosu Gosu.

“Gosu Gosu, kuna jambo nataka lifanyiwe kazi mara moja.Nataka mumtafute mtu anaitwa Rebeca Anderson, anafanya kazi Meru Paradise Hotel.Chunguzeni kila kitu,mawasiliano yake,washirika na nyendo zake.Mpe Ruby hiyo kazi, wewe nataka usibanduke mahali hapo alipo Carmelita,” alisema Mathew,akakata simu.

****

Ndege waliyokuwamo akina Mathew ilitua katika uwanja wa ndege wa kijeshi jijini Tripoli.

“Tumefika Tripoli, tutalala hapa,kesho tutaanza safari kuelekea nyumbani Tanzania” Mathew aliwaambia wasichana.Nyuso zao zilionesha tabasamu.Wote wakashangilia,Perpetua akawataka wenzake wakusanyike pamoja,wakashikana mikono akaongoza maombi ya kumshukuru Mungu kwa ukombozi,kwani hawakutarajia.Baada ya maombi kukoma, wakashuka ndegeni na kuingia katika magari yaliyokuwepo pale uwanjani.Hakuna aliyejua mahala wanakoelekea.

Kutoka katika uwanja wa ndege wa jeshi,msafara ulioongozwa na gari la jeshi, ulielekea moja kwa moja katika jumba moja kubwa la ghorofa nne,lenye ulinzi mkali wa wanajeshi.Wasichana wakashushwa na kuingizwa ndani.

“Agai, tafadhali pata mapumziko.Hapa ni sehemu salama sana, hivyo usihofu.Mimi kuna sehemu natakiwa kwenda muda huu,baadaye nitakuja kuungana nanyi,tutazungumza kirefu.” Alisema Mathew

“Mathew, kama kuna kazi nyingine, mimi niko tayari kukusaidia!” alisema Agai.

“Kwa hapa Libya kazi imemalizika.Ninakwenda kumuaga Rais wa Libya!”

“Sawa,Mathew!” alisema Agai akielekea ndani.Mathew akarejea garini,tayari kwa safari ya kuelekea Ikulu kuonana na Rais wa Libya.

****

.

Mathew na Fahad walifika katika makazi ya Rais wa Libya. Walipokewa vizuri na kukaribishwa katika sebule maalum kabisa.Baada ya muda, Rais Fakhr al din Hussein akatokea,wote wakasimama,wakasalimiana naye kwa kushikana mikono.

“Karibuni sana vijana shupavu.Siwezi kuelezea furaha niliyonayo baada ya kusikia Abdulkhareem Fadil Ghedi ameuawa.Ni mtu ambaye alikuwa anatuumiza vichwa vyetu sana.Hatukujua ni namna gani tungeweza kumuondoa yeye na kundi lake.Kupitia kwenu vijana hodari kabisa, hatimaye leo hii tumehitimisha rasmi uhai wa kundi la Ansar al Sharia nchini Libya.Leo kila mahali katika nchi ya Libya ni furaha tupu.Muda mfupi kabla ya ninyi kufika hapa,kupitia ukurasa wangu wa Twitter nimeitangazia dunia ushindi mkubwa baada ya kumuua Abdulkhareem.!” alisema Rais Fakhr.

“Mheshimiwa Rais,” alisema Mathew.

“Itapendeza sana kama usiku wa leo utakuwa mwanzo wa Libya mpya.Tumeshuhudia baada ya kuibuka kwa Abdulkhareem na kundi lake la Ansar al Sharia,hata wababe wengine wa vita walidiriki kuunganisha makundi yao kupigana na kundi hilo ambalo walidai si la ukombozi wa Libya bali ni kwa maslahi ya mabeberu.Hii ni ishara kuwa Libya mkiamua kumaliza mapigano haya yanayoendelea nchini mwenu mnaweza.Wewe,Mheshimiwa Rais, unatakiwa uwe kinara wa kutafuta suluhu ya kudumu ya mgogoro wa Libya.Ninyi viongozi ndiyo mnaoukuza mgogoro huu kwa tamaa ya madaraka, lakini pale ambapo mtazinduka kutoka usingizini na kulitupa pembeni blanketi mlilofunikwa

na nchi kubwa mtalia machozi kwa mambo mnayowatendea watu wa Libya" alisema Mathew huku akimtazama Rais Fakhr kwa makini.

"Mheshimiwa Rais, katu msitegemee kwamba amani ya Libya italetwa na watu wa kutoka nje.Amani ya Libya italetwa na Walibya wenyewe pale watakapoamua kuacha kutumiwa na mabeberu kwa maslahi yao na kuamua kuweka silaha chini kuijenga nchi yao.Mtapungukiwa nini kama mkiamua kukaa meza moja na kujadili hatima ya nchi yenu? Hili ninakwambia wewe na viongozi wengine wa bara hili la Afrika ambao bado wamefunikwa na blanketi la mabeberu.Amkeni na mpigane vita dhidi ya mabeberu.Wazee wetu akina mzee

Nyerere na wengineo walipambana kutuondoa katika ukoloni na bara zima la Afrika sasa liko huru.Lakini wakoloni wale wale kwa sasa wanarejea tena kwa kasi kubwa wakiwatumia watawala wetu,wanasiasa,asasi za kijamii na kadhalika.Hawana huruma, wanachukua raslimali zetu tena mchana kweupe bila aibu.Wanachukua madini yetu huku jamii zetu zikiendelea kubaki masikini.Kabla ya kuja kwa ukoloni, jamii za Afrika zilikuwa na tamaduni zao nzuri, lakini sasa tunalazimishwa kufuata tamaduni za kigeni kama vile mapenzi ya jinsia moja na kadhalika.Mimi ni Mkristu,japo si mbobezi sana katika maandiko matakatifu,ila naamini hakuna sehemu katika kitabu chetu kitukufu

ambako kumeandikwa mwanaume atamuacha baba na mama yake na kumuoa mwanaume mwenzake vivyo hivyo kwa mwanamke.Kwa miaka ya hivi karibuni, tumeanza kuzishuhudia tamaduni hizo katika nchi zetu.Tunalazimishwa kuzikubali kwa kigezo cha haki za binadamu.Mko wapi viongozi wetu? Kwa nini hamsimami imara na kukemea mambo kama haya? Mnahofia nini? Mnahofia kunyimwa misaada ambayo chanzo chake ni rasilimali kutoka katika nchi zenu wenyewe?Naomba niishie hapa,Mheshimiwa Rais,nina hasira sana na hawa mabeberu.Ninaamini ujumbe umekufikia na utaufanyia kazi.”Mathew Mulumbi alisema.

“Ahsante sana,Mathew Mulumbi kwa nasaha hizo.Nimekuelewa.Nasema Afrika ina bahati sana kwa kuwa na vijana wazalendo kama wewe.Haya yote uliyonieleza ni ya kweli kabisa.Sisi viongozi tumechangia kwa kiasi kikubwa sana kulibomoa bara hili na kulifanya lizidi kuwa masikini kwa tamaa zetu.Viongozi wengi tumekuwa vibaraka wa nchi tajiri ambazo zimekuwa zikiuchota utajiri wetu.Bara hili limejaa utajiri mkubwa,lakini utajiri huo badala ya kutunufaisha sisi, umekuwa ukizinufaisha nchi tajiri na sisi kuendelea kuogelea katika umasikini.Maneno yako yamenipa hamu ya kutaka kuiona Libya mpya,” alisema Rais Fakhr al Din.

“Nashukuru,Mheshimiwa Rais, kwa kunielewa.Kikubwa kilichotuleta hapa kwako usiku huu, ni kukupa taarifa rasmi kuwa ile kazi tuliyokuja kuifanya imemalizika na Abdulkhareem Fadil Ghedi ameuawa.Huyu jamaa ana wafuasi wengi,ana jeshi kubwa hivyo, kazi ya kukiondoa kikundi hicho haitamalizika leo japokuwa ngome kuu tayari imeteketezwa na iko chini ya vikosi vya serikali,” alisema Mathew akanyamaza kidogo halafu akaendelea.

“Mheshimiwa Rais,baada ya kumaliza misheni yetu sasa ni wakati wa kurejea nyumbani.Naamini huu wakati mzuri wa kumfahamisha rasmi Rais wa Tanzania kuhusu jambo hili,” alisema Mathew Mulumbi.Bila kupoteza muda

,Rais Fakhr akachukua simu yake, akaitafuta namba ya Rais wa Tanzania, akampigia.Simu ikaita,ikapokelewa.

“Mheshimiwa Rais Fakhr,” alisema Jenerali Pius Mawingu. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

“Habari za usiku huu,mheshimiwa Rais Pius,” alisema Rais Fakhr.

“Nzuri kabisa habari za huko? Kwanza hongera sana,Mheshimiwa Rais.Muda mfupi uliopita nimeona ujumbe wako wa Twitter,nilikuwa mbioni kukupigia ili nikupongeze.Huyu jamaa aliyeuawa Abdulkhareem Fadil Ghedi kundi lake ndilo lililofanya mashambulizi hapa Tanzania, wakaua watu.Mpaka sasa wanaendelea kuwashikilia mateka wasichana zaidi ya

ishirini na hatujui walikowapeleka.Mnaweza mkatusaidia kufanya uchunguzi katika ngome yake kama kuna wasichana anaowashikilia?” Rais Pius aliomba.

“Mheshimiwa Rais Pius,ahsante kwa pongezi lakini kuna mtu ambaye anastahili pongezi hizo.Yeye ndiye aliyeratibu suala hili lote na hadi kufanikisha kumuua Abdulkhareem Fadi Ghedi.Huyu hapa zungumza naye,” alisema Rais Fakhr,akampa simu Mathew.

“Hallo Mheshimiwa Rais!”alisema Mathew Mulumbi kwa lugha ya Kiswahili kisha akaweka tuo.

“Hallo.Nazungumza na nani?”Rais Pius aliuliza.

“Mheshimiwa Rais, unazungumza na Mathew Mulumbi!” alijibu Mathew kwa upole sana, Jenerali Pius akasikika kupitia spika ya simu akivuta pumzi ndefu.

“Mathew Mulumbi?”Rais Pius aliuliza kwa mshtuko.

“Ndiyo!Mheshimiwa Rais!”

“Mathew Mulumbi, ni kweli hayo anayoyasema Rais Fakhr kwamba wewe ndiye uliyeratibu mpango mzima wa kumuua Abdulkhareem Fadil Ghedi?”Rais Pius aliuliza kwa kiwewe. Hakuna namna aliweza kuibayanisha furaha yake.

“Ndiyo,Mheshimiwa Rais!”

“Mathew Mulumbi, nimekosa neno la kusema!”

“Mheshimiwa Rais, tutapata muda mzuri wa kuzungumza kuna mambo mengi ambayo bado unahitaji kuyafahamu, lakini kwa sasa nataka tu nikujulishe kuwa tumewakomboa wasichana wote waliokuwa wametekwa nyara jumla yao ni ishirini na nane wote wako salama kabisa na wana afya na siha njema,”alisema Mathew.Rais Pius akashusha pumzi.

“Unasema kweli,Mathew?” aliuliza

“Ndiyo,Mheshimiwa Rais.Watoto wote hivi sasa wamekombolewa,wako salama kabisa,”alisema Mathew.Ukimya ukatanda.

“Mheshimiwa Rais,nataka kukujulisha kuwa kesho nitawarejesha watoto wote nyumbani kwa kutumia

ndege yetu mpya iliyokuwa imepotea.Kama utaona inafaa wazazi wa watoto hao wajulishwe ili waweze kufika uwanja wa ndege kuwapokea watoto wao pamoja na kuipokea ndege yetu mpya," alisema Mathew.

"Mathew Mulumbi, haya unayonieleza ya kweli au?" Bado Rais Pius hakuwa akiamini

"Mheshimiwa Rais, ninayokueleza ni ya kweli kabisa.Nitakutaarifu kesho asubuhi muda tutakao ondoka hapa Tripoli."

"Mathew Mulumbi!" Alisema Rais Pius kisha akanyamaza kwa nukta chache halafu akaendelea

"Ahsante sana.Sina maneno mazuri ya kukushukuru kwa hiki ulichokifanya."

“Usijali,Mheshimiwa Rais.Tutazungumza nitakapofika hiyo kesho,” alisema Mathew.Akamrejeshea simu Rais Fakhr.Akaendelea kuzungumza na Rais Pius na hatimaye wakaagana.

“Jenerali Pius ni rafiki yangu sana.Bado hajaamini hiki kilichotokea,” alisema Rais Fakhr.

“Mheshimiwa Rais, ninahitaji kurejea katika makazi yetu kuwaandaa watu wangu kwa ajili ya safari ya kesho,’ alisema Mathew na kuagana na Rais Fakhr.Wakaondoka kurejea katika makazi yao.

15

DAR ES SALAAM – TANZANIA

Ni saa saba za usiku,Ruby hakuwa amefunga jicho.Bado alikuwa chumbani kwake akiendelea na zoezi la kufuatilia kamera walizofunga nyumbani kwa Maurine Kyaso.Akiwa ameyaelekeza macho yake katika kompyuta yake akapigiwa simu na Rais.

“Mheshimiwa Rais!” alisema Ruby.

“Ruby,naamini tayari umekwisha pata taarifa za kuuawa kwa Abdulkhareem Fadil Ghedi usiku huu nchini Libya”

“Ndiyo,Mheshimiwa Rais!.Tayari taarifa hiyo imesambaa mtandaoni”alisema Ruby

“Kuna jambo lingine muhimu ninataka kukufahamisha.Nimezungumza na Mathew Mulumbi muda mfupi uliopita.”alisema Rais Pius

“Mathew amekupigia?”aliuliza Ruby

“Ndiyo, amenipigia simu akiwa katika Ikulu ya Libya.”

“Mathew yuko Libya?”Ruby alishangaa.

“Ndiyo, yuko Libya.Mathew ndiye aliyeratibu na kuongoza operesheni ya kumuua Abdulkhareem Fadil Ghedi akishirikiana na vikosi vya serikali ya Libya” alisema Rais

“Mungu wangu!”alisema Ruby kwa mshangao tena.

“Amesema hivyo yeye mwenyewe?”Ruby aliuliza.

“Hakuishia kumuua Abdulkhareem pekee, bali pia amewakomboa na wasichana wote waliokuwa wametekwa na magaidi.Kesho watoto wote watarejea nyumbani, tena na ndege yetu tuliyodhani imepotea!”

“Ndege yetu imepatikana?”Ruby aliuliza.

“Ruby, ninapaswa kukushukuru sana.Ni wewe ndiye uliyeniasa niwe na subira kuwa Mathew Mulumbi yuko katika misheni.Sikuweza kukuamini haraka kwa kuwa sikumfahamu vyema Mathew Mulumbi ni kiumbe wa aina gani.Nimepata furaha kubwa sana leo isiyoelezeka”alisema Rais.

“Tangu mwanzo niliamini lazima kuna jambo linaloendelea.Tumsubiri hiyo kesho atakaporejea, atatufumbulia fumbo hili gumu.Ni yeye pekee mwenye majibu ya kila kitu kilichotokea!” alisema Ruby.Akaagana na Rais kwa miadi ya kuonana naye asubuhi yake.

“Nimekuwa na Mathew Mulumbi kwa muda mrefu sasa tukishirikiana katika misheni mbali mbali lakini

nadhani bado sijamfahamu huyu ni mtu wa aina gani.Sikutegemea kabisa kama angeweza kuibukia Libya.Hakuna aliyehisi kama magaidi wangewapeleka watoto wetu Libya.Kuna mengi ambayo tutahitaji kuyafahamu kutoka kwake.Tumuombee aweze kurejea salama nyumbani!" aliwaza Ruby halafu akampigia Gosu Gosu akampa taarifa ile.

****

Saa tisa na dakika ishirini na tisa usiku, bado Ruby hakuwa ameufunga ukope.Alikuwa akiendelea na kazi.Mara kamera ya sebuleni ikaonesha mlango ukifunguliwa.Watu watatu wakaingia.Wote walikuwa wamevaa

mavazi meusi na waliziba nyuso zao zisionekane.Muonekano wao,ulijidhihirisha kulikuwa na wanawake wawili na mwanaume mmoja.

“Tumalize maandalizi ya chumba mara moja halafu shughuli ianze! alisema mmoja wao.Ruby alisikia sauti zao kufuatia vile vinasa sauti vya siri walivyoviweka ndani ya nyumba ile ya Maurine.Aliitambua sauti ile ni ya Maurine Kyaso.

“Wale wengine ni akina nani?”Ruby alijiuliza.

Watu wale wakaelekea katika stoo ya kuhifadhia vitu, wakatoa meza moja na viti.Wakaviingiza katika chumba ambacho akina Ruby hawakuweka

kamera kwani kilikuwa kitupu na kilionekana hakitumiki.

“Wanataka kufanya nini ndani ya kile chumba? Sisi tulikiona kiko tupu hivyo hatukufunga kamera yoyote mle kumbe tulikosea.Chumba kile kinaonekana ni kwa ajili ya kazi maalum,” Ruby aliendelea kujipa tafakuri.Baada ya dakika saba, wakatoka katika kile chumba, wakaelekea nje,

Dakika chache baadaye, wakarejea ndani wakiwa wamemtanguliza mbele mtu mmoja aliyekuwa amefungwa mikono kwa nyuma.

“Ramesh!”alisema Ruby kwa mshangao.

“Huyu ni Ramesh Chopra, meneja wa hoteli ya Saafin ambayo alitakiwa

kufikia Carmelita.Inaonekana kama vile wamemteka.Kwa nini wamemleta hapa?”Ruby alijiuliza.

“Lazima kuna kitu wanataka kukifanya hawa watu!” Aliwaza Ruby.

Ramesh aliingizwa ndani ya kile chumba ambacho hakikuwa na kamera.

“Ninapatwa na wasi wasi hawa jamaa hawana nia nzuri,” tafakuri ya Ruby iliendelea. Ikaamsha nadhari yake, akachukua simu, akampigia Gosu Gosu.

“Ruby hujalala bado?”Gosu Gosu aliuliza.

“Hakuna kulala, Gosu Gosu, hadi tutakapolifumbua hili fumbo,” alisema Ruby.

“Mimi pia niko hapa naendelea kumlinda Carmelita kama alivyoelekeza

Mathew.Kuna habari yoyote kwa upande wako?”Aliuliza Gosu Gosu.

“Kuna kitu kinaendelea nyumbani kwa Maurine!” alisema Ruby.Akamueleza Gosu Gosu kila kitu alichokishuhudia kupitia kamera.

“Kwa nini wakamteka Ramesh na kumpeleka mahala hapo? Je ni SNSA ndiyo waliofanya hivyo?”Aliuliza Gosu Gosu.

“Hilo ndilo swali ambalo hata mimi nimekuwa najiuliza.Gosu Gosu, ninapata mashaka sana.Wale jamaa wanaweza wakamfanya kitu kibaya Ramesh,”alisema Ruby.

“Unadhani sababu inaweza kuwa ni hili tukio la kupotea kwa Carmelita?” Gosu Gosu aliuliza.

“Sina hakika sana, lakini inawezekana kwa sababu Ramesh aliufahamu mpango wetu wa kumteka Carmelita na kumpeleka sehemu salama,” alisema Ruby.

“Yawezekena labda SNSA wanafanyia uchunguzi suala la kupotea kwa Carmelita.Pengine wamempeleka Ramesh mahala hapo kumuhoji,” alisema Gosu Gosu.

“Kama ni SNSA, basi wasingemleta mahala hapa.Wangeweza kumpeleka katika ofisi yao kuu au katika nyumba zao wanazotumia kuwahoji watu.Gosu Gosu, suala hili halina uhusiano wowote na SNSA” alisema Ruby akanyamaza

“Gosu Gosu, tulikosea sana kutokuweka kamera katika kile chumba

tukidhani hakitumiki.Kwa nini tusiende tukavamia kujua kile kinachoendelea mle ndani na kumuokoa Ramesh?”Ruby aliuliza.

“Ruby, hatuwezi kufanya hivyo kwa sasa.Kwanza mimi niko hapa kumlinda Carmelita.Siruhusiwi kuondoa mguu wangu hapa.Pili…..” alisema Gosu Gosu kabla Ruby kumkatisha.

“Gosu Gosu, suala hili litachukua muda mfupi tu kisha utarejea kuendelea kumlinda Carmelita!”

“Huo muda mfupi ndio wanautafuta wale wanaotaka kumuua Carmelita.Ruby sikiliza,hatuwezi kuvamia nyumbani kwa Maurine kwa sababu bado tunaendelea kumchunguza.Kama tukimvamia leo, tutaharibu kila kitu na atajua

anachunguzwa.Anaonekana ni mtu mwenye siri nyingi.Kwanza anashirikiana na Nicki ambaye tunamtafuta ili tujue mahala alipo Joseph Nahimana. Pili, ameshiriki katika utekaji wa meneja wa hoteli ya Saafin ambako alitakiwa kufikia Carmelita,"alisema Gosu Gosu.

"Ni vipi kama lengo lao ni kumuua Ramesh?.*Are we gong to let them kill him?*"Ruby aliuliza.

"Ruby, hakuna tunachoweza kukifanya kwa sasa.Tafadhali usifanye chochote.Maurine ni mtu wa muhimu,lazima tumchunguze, tumfahamu vyema.Kama wana mpango wa kumuua Ramesh, *let them do it!*"alisema Gosu Gosu.

“*I can’t believe this!”*alisema Ruby.

“Ruby, tafadhali kwa namna yoyote ile, usijaribu kufanya kitu ambacho kinaweza kuharibu misheni yetu.Tuliweka kamera zile kwa ajili ya kumchunguza Maurine na ndivyo tunatakiwa kufanya,” alisema Gosu Gosu.Ruby akakata simu kwa hasira.Akainama,akawaza,akachukua simu, akampigia Rais.Akumueleza kile alichokishuhudia nyumbani kwa Maurine.

“Mheshimiwa Rais, ninahisi kuna kitu kibaya wale jamaa wanataka kumfanyia Ramesh.Naomba tufanye kitu kumuokoa tafadhali” alisema Ruby.

“Umezungumza na Gosu Gosu kuhusu jambo hili?”Aliuliza Rais

Pius.Ruby akamueleza kile alichokisema Gosu Gosu.

“Gosu Gosu yuko sahihi.Hatuwezi kufanya chochote kwa sasa.Tusubiri tuone kile ambacho wanataka kukifanya.Endeleeni kumfuatilia kila anachokifanya.Umenielewa,Ruby?”

“Nimekuelewa,Mheshimiwa Rais!”alijibu Ruby.Akakata simu, akazama mawazoni.

“Kwa namna wale jamaa walivyomuingiza Ramesh mle ndani, ni wazi anaonekana ametekwa.Kuna jambo wanamtaka aliseme.Ninapata mashaka yawezekana suala la Carmelita ndilo lililopelekea akatekwa. Kwa nini Rais na Gosu Gosu hawataki kunielewa?”Alijiuliza huku akiendelea

kufuatilia zile kamera. Bahati mbaya, hakuonekana mtu yeyote nje. Wote walikuwa ndani ya kile chumba, kama haitoshi, hakujua kilichokuwa kinaendelea ndani kwa sababu hakukuwa na kamera.

Ilipita saa moja na dakika kumi na saba ndipo mlango wa kile chumba walimoingia Maurine na wale watu wegine wawili, ukafunguliwa.Akatoka mtu mmoja akionekana kufoka kwa hasira.Akavua ile kofia ya kufunika uso akaitupa chini kisha akageuka.Akarejea tena katika mlango wa kile chumba akifoka.Upesi Ruby akaichukua sura yake, akaikuza na kupatwa na mshangao mkubwa.

“Nicole!”Ruby alisema huku akihisi mwili ukimtetemeka.

Watu wengine wawili wakatoka ndani ya kile chumba,wakaonekana wakizungumza huku wakimsihi Nicole kupunguza hasira.Nicole akaiokota ile kofia yake ya kuficha sura, akaivaa.Wakaonekana wakijadiliana jambo.Hakukuwa na kinasa sauti mahala pale hivyo Ruby hakuweza kusikia walichokizungumza.Baada ya dakika nne, wakaingia tena ndani ya chumba. Wakaufunga mlango.Zilipita dakika chache tena, mlango ukafunguliwa.Wakatoka wakiwa wamembeba Ramesh ambaye alikuwa ametapakaa damu mwili mzima.Hakuwa na fahamu.

“Oh my God!”alisema Ruby kwa mshangao.

“Nilijua tu kitu kinachokwenda kutokea!”aliwaza Ruby.Watu wale wakamtoa Ramesh na kwenda naye nje.Ruby hakuweza kuona kilichoendelea nje kwani hawakuwa wameweka kamera yoyote kwa nje.

“I must do something!”aliwaza na kuchukua simu.Akampigia Rais Pius.

“Hallo,Ruby!” alisema Rais Pius.

“Mheshimiwa Rais, nakuomba umpigie Maurine simu.Jitahidi kumuweka katika laini kwa dakika tatu”

“Kuna kitu gani kinaendelea,Ruby? Kuna chochote umekipata?”Aliuliza Jenerali Pius.

“Nitakueleza,Mheshimiwa Rais, lakini kwa sasa naomba unisaidie kufanya hivyo nilivyokuomba,”alisema Ruby.

“Sawa,Ruby!” alijibu Rais.Ruby akabonyeza kompyuta yake haraka haraka,akaenda kabatini akachukua bastola.Akaifutika kiunoni, akachukua na baadhi ya vifaa vyake akatoka mbio kuelekea katika gari,akaingia na kuondoka kwa kasi.Akiwa ameuweka mkono wake wa kulia katika usukani wa gari, alikuwa akihesabu sekunde,katika kompyuta yake kukatokea mlio.Akasimamisha gari,akatazama katika kompyuta yake, akaisoma ramani iliyoonekana katika program halafu akawasha gari tena akaendelea na

safari.Tayari program yake ilikwisha anza kumfuatilia Progaramu Maurine

Gari la akina Maurine lilikwenda hadi ufukwe wa Makego,likasimama.Bado Ruby aliendelea kuwafuatilia.

“Naamini lazima wanakwenda kumtupa Ramesh ufukweni mwa bahari!”aliwaza Ruby.

Kama alivyokuwa amewaza Ruby, ndivyo ilivyokuwa.Gari la akina Maurine liliposimama, mlango ukafunguliwa.Wakashuka, wakakamshusha na Ramesh pia. Wakamtupa,wakarudi tena garini na kuondoka kwa kasi.Wakiwa katika mwendo mkali, wakapishana na gari la Ruby ambaye naye alikuwa anaelekea

kule ufukweni.Ruby alifika hadi ufukweni, akasimamisha gari, akashuka akiwa na bastola yake mkononi,Akawasha tochi na kuanza kufuatilia alama za matairi ya gari.

Fukwe ya Makego usiku huo kulikuwa na kiza totoro. Hakukuwa na hoteli yoyote mahala hapo.Kilichosikika ni sauti za mawimbi ya bahari pekee.Ruby hakuogopa, akafuata matairi ya gari yalikoenda.Mara akaona alama ya mburuzo wa kitu, akaifuata.Hatua kadhaa mbele, akauona mwili wa mtu ukiwa umelala.

“Ramesh!”aliita huku akimkimbilia.Hakukuwa na mtu yeyote wa kumpa msaada mahali pale.Akammulika Ramesh, alikuwa

ametapakaa damu mwili mzima.Alitumia sekunde kadhaa kumchunguza,akagundua Ramesh hakuwa amekufa.

Bado mapigo yake ya moyo yalikuwa yakidunda japo kwa mbali.Ruby hakuwa na uwezo wa kumbeba, mbaya zaidi hakukuwa na mtu wa kumsaidia.Akarudi mbio hadi katika gari lake, akaliwasha na kurejea mahala pale, akajitahidi kutumia nguvu zake zote akamuingiza Ramesh garini.Akafanikiwa, akaondoa gari kwa kasi.

Akiwa garini, akampigia simu Dr. Maria.Akamtaka aende nyumbani kwake kuna mgonjwa wa dharura.

****

Ruby aliwasili nyumbani kwake na kumkuta Dr. Maria tayari amefika.Dr. Maria haishi mbali na makazi ya Ruby.

“Karibu ndani, Dr. Maria!” alisema Ruby huku akifungua geti.Wakaingiza magari ndani.Wakasaidiana kumshusha Ramesh na kumuingiza ndani.Dr. Maria hakuhoji chochote kuhusu mgonjwa.Papo hapo akaanza kumpima kujua kama bado yuko hai au la.Hali yake haikuwa nzuri.

“Is he alive?”Ruby aliuliza.

“Ndiyo.Bado yuko hai” alisema Dr. Maria haraka haraka huku akilifungua sanduku la huduma ya kwanza alilokuja nalo.Akatoa dawa na baadhi ya vifaa.

“*Will he be okay*?”Ruby aliuliza kwa kihoro.

“Tuombe Mungu!”alijibu Dr Maria.Ruby akatoka nje akampigia simu Gosu Gosu.Akamjulisha kile kilichotokea.

“Dah!”Kama walitaka kumuua Ramesh, basi lazima ipo sababu.Ruby, nahisi sababu kuu yaweza kuwa ni kutoweka kwa Carmelita.Yawezekana walikuwa wanataka awaeleze mahali Carmelita alipo,” alisema Gosu Gosu.

“Gosu Gosu, tutapata majibu yote baada ya Ramesh kupata nafuu.Tumuombee aweze kupata ahueni na kutueleza kisa chote kwa nini wakataka kumuua”alisema Ruby.akarudi ndani, breki ya kwanza katika ofisi yake,

akatazama kamera zao zilizofungwa nyumbani kwa Maurine.Katika kamera iliyofungwa katika chumba cha kulala ilimuonesha Maurine akiwa amekaa katika sofa lililo chumbani mwake akizungumza na simu.

“She’s back.Huyu mwanamke ni nyoka mwenye vichwa viwili.Nitamfuatilia hadi nitampata tu!”alisema Ruby huku akikaa katika kompyuta yake akaanza kutafuta taarifa za Rebeca Anderson.

****

Ruby alihisi uchovu mwingi ukibisha hodi.Akaenda chumbani kwake kujipumzisha kwa muda mfupi.Akiwa

ametopea katika usingizi, mlango wake ukagongwa.Akaamka na kwenda kuufungua.Akakutana na mtumishi wake ambaye alimjulisha kuwa anaitwa na Dr Maria.Ruby akaenda haraka haraka katika chumba kile alimolazwa Ramesh huku akiwa na wasiwasi mkubwa.Alipoingia, akakuta Dr Maria akizungumza na Ramesh.Akashusha pumzi nzito.

“Ruby,mgonjwa wetu ameamka. Sasa unaweza ukazungumza naye,” alisema Dr. Maria.

“Unajisikiaje sasa hivi?”Ruby aliuliza.

“Nina maumivu makali sehemu zote za mwili!”alijibu Ramesh.

“Pole sana.Hutajali kama nikikuuliza maswali machache?”Ruby aliuliza kwa upole.

“Uliza!”

“Nataka kulifahamu jina lako nani?”

“Naitwa Ramesh Chopra.”

“Ramesh, unafanya kazi gani?”

“Ni meneja wa hoteli ya Saafin.”

“Good.Huu ni mwezi gani?”

“Huu ni mwezi wa tatu.”

“Safi sana.Unamfahamu Rais wa nchi hii?”

“Ndiyo.Ni Jenerali Pius Mawingu,” alisema Ramesh halafu akafumbua macho.

“Nimekukumbuka.Ninakufahamu.Ni likuona Ikulu,” Ramesh aliongeza. Moyo wa Ruby ukayatupilia mbali mashaka

yake. Badala yake akachanua tabasamu kubwa huku akimtazama Dr. Maria.

“Kumbu kumbu zake ziko sawa!” alisema Ruby.Dr. Maria akatoka ili kumpa nafasi ya kuweza kuzungumza na Ramesh.

“Ramesh, pole sana!Ni kweli mimi na wewe tulikutana Ikulu.Unaweza ukawakumbuka wale waliokufanyia hivi?”Ruby aliuliza.

“Walitaka kuniua!”alisema Ramesh. Akaanza kulia.

“Usilie, Ramesh!”

“Walitaka kuniua.Walinipiga sana hadi nikapoteza fahamu!”

“Ramesh, nataka kujua.Je, unawafahamu watu wale waliokufanyia hivi?”Ruby aliuliza

“Hapana!Siwafahamu.Walikuwa wamezificha sura zao sikumtambua hata mmoja wao,” alijibu Ramesh.

“Unaweza ukaniambia ulifikaje mikononi mwao?”

“Nilitoka kazini, nikapita supermarket kununua mahitaji.Wakati nikipakia vitu nilivyonunua katika buti ya gari, nikahisi kuna watu nyuma yangu.Kabla sijageuka, nikajikuta nimekabwa na kuwekewa kitambaa fulani puani, nikakosa hewa nikapoteza fahamu.Nilipozinduka nilijikuta katika gari ambalo ndani yake kulikuwa na watu watatu wakiwa wamezificha nyuso zao!” alisema Ramesh,akanyamaza.

“Walikuhoji mambo gani?”

“Walichotahitaji kujua ni mahala alipo Carmelita.Walinitesa mno na kudai kuwa ninafahamu kila kitu kilichotokea kuhusu Carmelita.”alisema Ramesh

“Watu waliomteka Carmelita hawajulikani,kwa nini wakakufuata wewe na kudai unafahamu kile kilichotokea? Kuna mtu yeyote ulimueleza kuhusu mpango wetu ule tuliokubaliana Ikulu?”Ruby aliuliza.

“Hapana!Sikumueleza mtu yeyote.”

“Unadhani kwa nini walitaka kukuua?”Ruby aliuliza

“Sifahamu!”

“Ramesh, naomba unieleze ukweli.Watu waliokuteka si wajinga hadi wakawaacha watu wote na kukuteka

wewe peke yako.Lazima ipo sababu," alisema Ruby kwa msisitizo.

"Hata mimi najaribu kutafakari, lakini sijapata jibu kwa nini waniteke?"

"Ramesh, ni mimi niliyekuokota ufukweni walikoenda kukutupa baada ya kudhani tayari umekufa.Nilihatarisha maisha yangu kwa ajili ya kuokoa uhai wako.Laitani ningekuacha pale, hivi sasa tayari ungekwisha poteza maisha yako.Hivyo naomba unieleze ukweli mtupu kwa nini wale watu wakakufuata kwa minajili ya kufahamu mahali alipo Carmelita? Naamini walikufuata wakijua kabisa kuna kitu unakifahamu.Nieleze ukweli ili niweze kukusaidia.Fahamu kuwa wale jamaa watakapogundua hujafa, wataendelea kukusaka kila kona

hadi wakuue.Hatari si kwako tu, bali hata familia yako iko hatarini hivi sasa!”

“Tafadhali, naomba unisaidie!”alisema Ramesh kwa kihoro.

“Ramesh, unafahamu niko karibu na Rais, hivyo uwezo wa kukusaidia ninao, lakini nataka unieleze ukweli wote!” alisema Ruby.Ramesh akafumba macho, akapitisha kimya kwa uchache. Kwa unyonge akasema.

“Kama wiki mbili zimepita, nilifuatwa na watu wawili,” Ramesha alisema,akanyamaza.

“Walitaka nini watu hao?”Ruby aliuliza.

“Waliniambia kuwa wana mpango wa kumuondoa mmoja wa wageni atakayefikia katika hoteli

yetu,wakamtaja jina kuwa ni Carmelita.Walikuwa na taarifa zake zote.Hawakunieleza sababu, ila wakafungua sanduku walilokuja nalo lililokuwa limejaa fedha, wakaniambia yale ni malipo yangu!" Ramesh akanyamaza tena.Akafumba macho.

"Nini kilifuata?" Ruby aliuliza

"Nilizichukua zile fedha na kwenda nazo nyumbani."

"Kwa nini hukuripoti suala hilo polisi?"

"Walinitisha kuwa nikiwaeleza polisi wao watafahamu.Na wataiteketeza familia yangu!"

"Hukuamini kama jeshi la polisi wanaweza wakakulinda wewe na familia

yako dhidi ya hao watu?”Ruby aliuliza,Ramesh akabaki kimya.

“Endelea,” alisema Ruby huku akijiweka vyema.

“Kesho yake, wakanifuata tena.Wakanieleza kwamba kuna mtu ambaye ataautekeleza mpango huo. Hivyo basi natakiwa kumuajiri kama mmoja wa wafanyakazi wa hoteli.’

“Anaitwa nani huyo mtu?”

“Selina Kambazi,”alijibu Ramesh.

“Endelea” alisema Ruby

“Nilifuata maelekezo yao na kumuajiri huyo mwanamke katika hoteli.Nilielekezwa yeye ndiye apangiwe kumuhudumia Carmelita pale atakapowasili,” Ramesh akanyamaza tena.

“Endelea!” alisema Ruby.

“Nilipoitwa na Rais Ikulu, mkanieleza kuhusu mpango ule wa kumuokoa Carmelita, niliogopa sana.Nilitamani niwaeleze kile kinachoendelea, lakini nikawahofia wale jamaa wakijua wangeweza kuiteketeza familia
yangu.Nilichokifanya,nikaendelea kushirikiana na wale jamaa hadi pale Carmelita alipotekwa na kupelekwa sehemu salama.Baada ya hapo ndipo nilipotekwa na kwenda kuteswa.Huo ndio ukweli wa kile kilichokuwa kimetokea.Naomba unisaidie tafadhali!” alisema Ramesh.

“Ramesh, kwanza ulikosea sana kwa kuuficha ukweli huu hadi mambo

yamefika hapa yalipofika.Hata hivyo, njia pekee ya kukusaidia ni kwa kuwapata watu hao waliotaka kumuua Carmelita. Nataka kufahamu je,uliwaeleza chochote kuhusiana na wewe kuitwa Ikulu na Rais?" Ruby aliuliza.

"Hapana!Sikuwaeleza kitu chochote.Ndiyo maana wakanipiga sana wakiamini kuna kitu ninakifahamu kuhusu kutekwa kwa Carmelita!" alijibu Ramesh.

"Unaweza kuwakumbuka watu hao waliokufuata na kukushirikisha mpango huo wa mauaji?"Ruby aliuliza.

"Walikuwa wanawake wawili,"alijibu Ramesh.

“Ukiona picha zao unaweza kuwakumbuka?”

“Ndiyo!” akajibu Ramesh.Ruby akatoka na kwenda ofisini kwake halafu akarejea na faili lililokuwa na picha.

“Nataka uzitazame picha hizi kwa makini na uzitambue!” alisema Ruby.Akaziweka picha mezani.Moja kwa moja Ramesh akamtambua mmoja wao.

“Huyu hapa!”alisema Ramesh huku akielekeza kidole katika picha ya Nicole.

“Una hakika ni huyu?”

“Ndiyo.Ni huyu.sura yake haiwezi kunipotea,” alisema Ramesh.

Ruby akachukua simu na kumpigia Gosu Gosu.

“Gosu Gosu, nimepata uhakika aliyepanga mpango wa kumuua Carmelita ni Nicole,”alisema Ruby.

“Kazi nzuri sana,Ruby.Kwa sasa ambacho tunatakiwa kukichunguza ni mahusiano ya Maurine na Nicki.Uwepo wake wakati wa kumuhoji Ramesh inaonesha wazi ana mahusiano na mpango wa kutaka kumuua Carmelita.Papo hapo tukumbuke kuwa Nicki ndiye aliyewasiliana mara ya mwisho na Joseph Nahimana.Hivyo lazima anafahamu mahali alipo.Swali ni je,Maurine naye ana mahusiano na Joseph Nahimana?”Gosu Gou aliuliza .

“Tuendelee kumfuatilia Maurine.Tunaweza kugundua mambo mengi zaidi,” alisema Ruby.

16

UWANJA WA NDEGE WA KIMATAIFA WA JULIUS NYERERE - DAR ES SALAAM

Taratibu msafara wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jenerali Pius Mawingu uliingia katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es salaam.Umati mkubwa ulifika uwanjani hapo kwa ajili ya kuipokea ndege mpya ya Tanzania iliyokuwa imepotea pamoja na watoto

waliokombolewa kutoka katika mikono ya magaidi.Asubuhi ya siku ile,msemaji mkuu wa serikali alikutana na wanahabari na kupitia kwao akawahabarisha watanzania kuwa watoto wote waliotekwa na magaidi wamekombolewa na vikosi vya serikali ya Libya,vile vile akawataka wakazi wa Dar es salaam wafike kwa wingi uwanja wa ndege kuipokea ndege mpya ambayo waliamini imepotea.

Mara tu baada ya Rais Pius kuwasili, shughuli zikaanza rasmi.Hotuba kutoka kwa watu mbalimbali zikatolewa wakati wakiendelea kuisubiri ndege iwasili.Hatimaye ikafika zamu ya Rais Pius kuzungumza na umati mkubwa wa Watanzania.Katika hotuba yake,

alivipongeza sana vyombo vyote vya ulinzi na usalama vilivyokabiliana na magaidi na kuwashinda.Kinyume na wengi walivyotarajia Rais Pius hakugusia kabisa kitu chochote kuhusiana na tukio la kupotea kwa ndege waliyokuwa wanaisubiri.Vilevile aligusia kwa uchache sana kuhusu namna watoto walivyokombolewa kutoka katika mikono ya magaidi.Kwa kiasi kikubwa, hotuba yake haikubeba kile ambacho wengi walitamani kukisikia.

Hatimaye saa kumi na mbili za jioni, umati wa watu walikuwepo uwanjani, wakatakiwa kuyaelekeza macho yao angani ambako ndege waliyokuwa wanaisubiri ilikuwa inajiandaa kutua.Uwanja ukalipuka kwa furaha,

watu wakiruka ruka na kushangilia na wengine walishindwa kuyazuia machozi kuwatoka.

Taratibu ndege ilishuka na hatimaye ikagusa ardhi ya Tanzania.Kila aliyekuwepo uwanjani pale alisisimkwa.Ilikuwa furaha ya aina yake.

Ndani ya ndege ilikuwa furaha tu.Watu walipongezana kwa kurejea salama nyumbani.Wanafunzi waliimba kwa furaha na hisia kubwa huku wengi wakibubujikwa machozi.Mambo waliyoyapitia katika kipindi kifupi yalikuwa makubwa.

Ndege ilirejea taratibu, hatimaye ikafika mahala ambako ilipewa heshima ya kumwagiwa maji kama utaratibu ulivyo kwa ndege mpya.Hatimaye ndege

ikasimama.Ngazi ikasogezwa,mlango wa ndege ukafunguliwa.Wakapanda wanausalama na maafisa wengine wawili wa uwanja wa ndege na kuwapa utaratibu namna ya kushuka.

Mathew akaenda kuagana na marubani ambao walianza kushuka na kuvishwa mashada ya maua huku wakishangiliwa.Msisimko ukazidi, watu wakiwa na hamu ya kutaka kuwaona watoto.

Hatimaye kile ambacho watu walikuwa wanakisubiri kwa hamu kubwa kikawadia.Wanafunzi waliokombolewa walianza kushuka ndegeni.Kila aliyeshuka alisalimiana kwanza na Rais na viongozi wengine kabla ya kukabidhiwa kwa wazazi wake.Lilikuwa

tukio la furaha na machozi.Baada ya watoto wote kushuka ndegeni, wakafuata wafanyakazi wa shirika la ndege nao wakashuka.

Wa mwisho kushuka ndegeni walikuwa Mathew Mulumbi,Agai na Fahad.Sultan aliwekwa katika chumba maalum akilindwa hadi pale zoezi litakapokamilika ndipo ashushwe.Akina Mathew waliongozwa na msaidizi wa Rais aliyekuwa na maelekezo maalum.Wakatoka nje ya uwanja ambako aliwaongoza hadi katika gari moja lenye rangi nyeusi.Mlango ukafunguliwa akashuka Ruby.Mathew akajikuta akitabasamu

“Ruby!”alisema Mathew.

“Mathew!”alisema Ruby.wakakumbatiana

“Karibu tena nyumbani,Mathew.Nimefurahi kukuona tena!” alisema Ruby.

“Mimi pia nimefurahi kurejea salama nyumbani!” alijibu Mathew.

“Agai!”alisema Ruby kwa furaha na kumpa mkono Agai.

“Mungu mkubwa,Ruby!Hatimaye tumeonana tena!” alisema Agai.Ruby akatupa jicho mbele zaidi, akamwona Fahad. Akampa mkono.

“Karibu Tanzania!” alisema Ruby.Fahad akatabasamu.Waliingia garini wakaondoka pale uwanjani.Ruby tayari alikwishampa dereva maelekezo

yote mahala wanakoelekea.Haikuwa safari yenye mazungumzo.

Uwanjani baada ya wanafunzi wote kushuka ndegeni na kukabidhiwa kwa wazazi wao,Rais Pius alipanda ndegeni akaikagua, ndege ilikuwa mpya na nzuri.Viongozi wengine wakaungana naye halafu wakashuka ndegeni ikiwa ni ishara kuwa shughuli pale uwanjani zilifikia mwisho.Rais akaelekea katika gari lake, akaingia na kuondoka kurejea Ikulu.

****

Gari walilopanda akina Mathew lilisimama katika nyumba moja na kupiga honi mara tatu haraka haraka.Baada ya muda mfupi, geti likafunguliwa.Gari likaingia ndani.Sura ya Mathew ikaonesha tabasamu baada ya kumuona Gosu Gosu.

“Mathew, karibu tena nyumbani!” alisema Gosu Gosu huku akimpa mkono Mathew.

“Mambo yanakwendaje hapa? Kila kitu kiko shwari?” Mathew aliuliza huku akichanua tabasamu.

“Hapa kila kitu kiko shwari kabisa!” alijibu Gosu Gosu.

“Vizuri sana! Gosu Gosu, kutana na Fahad.Fahad kutana na Gosu Gosu!” Mathew alifanya utambulisho.

“Karibu sana Tanzania, Fahad!” alisema Gosu Gosu halafu akatazamana na Agai.Wote wakatabasamu wakakumbatiana

“Guys!Mtapata nafasi hapo baadaye ya kuzungumza na kupeana michapo.Kwa sasa bado tuna mengi yanatukabili,muda tulionao ni mchache.Tunahitaji kumuona Carmelita!” alisema Mathew.Gosu Gosu akawaongoza kuelekea ndani.Kabla ya kuonana na Carmelita,Gosu Gosu akawaeleza kila kitu namna walivyomchukua Carmelita uwanja wa ndege na maendeleo yake.

“Kazi nzuri sana Gosu Gosu.Sasa mpeleke Fahad katika chumba cha Carmelita!” alisema Mathew.

Gosu Gosu akamuongoza Fahad katika chumba alimo Carmelita.Akagonga mlango,Carmelita akaufungua.Alitaka kusema kitu, lakini ghafla akajikuta akiufunika mdomo wake kwa mshangao baada ya kukutanisha macho na Fahad.

“Fahad!”alisema Carmelita kwa mshangao

“Carmelita!”alisema Fahad.Carmelita akatoka ndani, akamrukia Fahad.Wakakumbatiana.Carmelita machozi ya furaha yakamtoka.Carmelita na Fahad wakaingia chumbani.

“Dady!”alisema Lebron kwa furaha baada ya kumuona baba yake.

“Lebron!”alisema Fahad huku akimuinua Lebron, akamkumbatia.

“Fahad na Carmelita wanafahamianaje?”Ruby aliuliza.

“Ni wapenzi!” alijibu Mathew.

“Wapenzi?”Gosu Gosu aliuliza .

“Ndugu zangu, kuna mengi ambayo mtayafahamu.Hivyo naomba vuteni subira!” alisema Mathew.Ukimya ukatawala huku Mathew akiwa ameyaelekeza macho katika chumba walimo akina Fahad.

“Fahad, mpaka sasa bado siamini macho yangu.Ni wewe kweli au niko ndotoni?”Carmelita aliuliza huku furaha ikimshika barabara.

“Ni mimi, Carmelita.Mnaendeleaje wewe na Lebron? Mko salama kabisa?”

“Nashindwa kuelewa, Fahad, hiki kinachoendelea.Umefahamuje kama tuko hapa? Hawa jamaa ni akina nani?”Carmelita aliuliza kwa kihoro.

“Kuna mengi ya kukueleza mpenzi wangu.Lakini si kwa sasa.Kilichonileta hapa ni kuhakikisha kweli uko salama wewe na Lebron.Nitaondoka kidogo na nitarejea tena baadaye nitakueleza kila kitu!”

“Fahad, hapana hautaondoka humu hadi unieleze kile kinachoendelea.Umefahamuje kama niko hapa? Hawa jamaa ni akina nani? Wameniteka na kunifungia hapa mimi na mwanagu na hatujui hatima yetu.Nini wanakitaka? Fedha?”Aliuliza Carmelita.

“Carmelita!Naomba nikutoe wasiwasi kwamba hamjatekwa.Mmeletwa hapa wewe na mwanangu kwa ajili ya usalama wenu.Hawa waliokuleta hapa si watu wabaya!” alisema Fahad kwa upole.

“Fahad, unazidi kunichanganya.Unafahamu kuhusu jambo hili la mimi na Lebron kutekwa na hawa jamaa?”Aliuliza Carmelita.

“Carmelita, ninarudia tena na kukuhakikishia kuwa haujatekwa.Hapa uko sehemu salama!”

“Unasemaje sijatekwa wakati nimechukuliwa uwanja wa ndege na kuletwa hapa na siruhusiwi hata kutoka nje?”

“Sikiliza Carmelita.Ni mimi niliyeelekeza jambo hili lifanyike!” alisema Fahad.Carmelita akamtazama kama vile amekutana na kitu cha kushangaza.

“Ni wewe?”Aliuliza kwa sauti ya ukali na mshangao ndani yake huku akimsogelea zaidi Fahad.

“Ndiyo!Ni mimi ndiye niliyefanya hivi na ndiyo maana niko hapa.Carmelita kulikuwa na mpango wa kukuua wewe na Lebron na…”

“Nani alitaka kuniua na kwa nini? Naomba unieleze ukweli Fahad sitaki unifiche kitu!” alisema Carmelita.

“Ni baba yangu!”

“Baba yako?”Carmelita alishangaa

“Ndiyo.Kama unavyofahamu mimi naye hatuna maelewano mazuri kwa kuwa tu nimezaa nawe mtoto.Anakuchukia na anamchukia pia Lebron.Ndiyo maana akaandaa mpango wa kukuua hapa Tanzania!”

“Alifahamu ninakuja Tanzania?” Carmelita aliuliza

“Anafahahamu kila kitu kuhusu wewe!” alijibu Fahad na mlango ukagongwa.

“Carmelita kuna sehemu ninahitajika kwenda.Baada ya kutoka huko nitakuja hapa kukuchukua.Naomba uwe na amani usihofu chochote!”alisema Fahad.

“Fahad siwezi tena kubaki hapa.Kama kuna sehemu unakwenda

basi tunakwenda sote.Huwezi kutuacha hapa tena!” alisema Carmelita.

“Mpenzi, usiwe na hofu.Mko salama hapa na nitarejea naomba uniamini!”

“Nimekwisha sema tunakwenda sote huko unakoenda.Sitaki kuendelea tena kukaa mateka ndani ya nyumba hii na sihitaji mjadala katika hilo!”alisema Carmelita kwa ukali.

“Naomba dakika moja!” alisema Fahad na kufungua mlango.Akamfuata Mathew Mulumbi.

“Fahad, muda wa kuzungumza na mpenzio umekwisha!” alisema Mathew.

“Mathew, utaniwia radhi kuna tatizo naomba unisaidie!” alisema Fahad.Akamueleza Mathew kuhusiana na Carmelita kutaka kuongozana naye.

“Hakuna tatizo.Kwani hata mimi nilikuwa nafikiria hivyo.Tutaongozana naye,mwambie ajiandae!” alisema Mathew.Fahad akarejea chumbani, akamtaka Carmelita ajiandae kisha akawafuata akina Mathew sebuleni.

“Fahad, tayari umemuona Carmelita yuko salama.Nimetimiza ahadi yangu ya kuhakikisha anakuwa salama.Sasa ni zamu yako!”alisema Mathew.

“Ninakushukuru sana Mathew na wenzako kwa kazi kubwa mliyoifanya.Usalama wa Carmelita na mwanangu Lebron ndicho kitu pekee ambacho niko tayari kukinunua kwa gharama yoyote ile.Ninashukuru wote wawili wako salama kabisa.Sasa niko

tayari na mimi kutimiza ahadi yangu!” alisema Fahad.

“Safi sana!Tunaelekea Ikulu.Utatueleza kila kitu mbele ya Rais!” alisema Mathew.Fahad akarejea katika chumba alimo Carmelita.Baada ya dakika chache Fahad akatoka akiwa anakokota sanduku la Carmelita.Wakapakia katika gari na kuondoka kuelekea Ikulu.

****

Mathew na wenzake waliwasili Ikulu.Walipokewa na katibu wa Rais, akawakaribisha sebuleni kwa Rais.Baada

ya muda mfupi, Rais Pius akatokea,wote wakasimama.

“Karibuni ndugu zangu.Pale uwanjani hatukupata nafasi ya kusalimiana,hivyo nataka nitumie nafasi hii adhimu kuwakaribisheni tena nyumbani.Hongereni mashujaa wetu na karibuni tena nyumbani!” alisema Rais Pius huku akimpa kila mmoja mkono wa pongezi.Baada ya kuwasalimu wote, akawaelekeza waketi.

“Mheshimiwa Rais, kwanza kabisa kwa niaba ya wenzangu ninakushukuru kwa makaribisho haya.Nataka nitumie nafasi hii kuwatambulisha wenzangu nilio nao hapa!” alisema Mathew na kuwataja majina wote na kila mmoja

akasimama.Wa mwisho kutambulishwa walikuwa Fahad na Calmerita.

“Ninawafahamu wote isipokuwa Fahad na Carmelita.Karibuni sana katika Ikulu ya Tanzania!” alisema Rais Pius,Carmelita na Fahada wakashukuru.Rais akawaongoza akina Mathew kwenda kupata chakula alichokiandaa kwa heshima yao.

****

Baada ya kupata chakula, Rais Pius akawachukua akina Mathew hadi katika chumba maalum cha mazungumzo ya

siri. Carmelita hakuruhusiwa kushiriki mazungumzo yale, hivyo akabaki chumba cha mapumziko yeye na mwanaye wakiwasubiri akina Mathew wamalize mazungumzo.

“Jamani, sasa tunaweza kuanza mazungumzo.Kwa mara nyingine tena karibuni nyumbani.Mathew Mulumbi, ninakushukuru wewe na timu yako yote kwa haya mliyoyafanyia nchi yenu.Huu ndio unaitwa uzalendo.Ninyi mmeyatoa maisha yenu kwa ajili ya kuhakikisha nchi inakuwa salama.Japokuwa wote mmeshiriki katika jambo hili, lakini naombeni mniruhusu nimpe shukrani za pekee kabisa Mathew Mulumbi.Kwani ndiye hasa aliyetufumbua macho juu ya

nini kinachoendelea.Hongera sana,Mathew!” alisema Rais Pius.

“Nashukuru sana,Mheshimiwa Rais!” alisema Mathew.

“Katika kikao hiki, mimi sintakuwa mzungumzaji.Uwanja ni wenu, nataka mnieleze kile mnachotaka kunieleza bila kuacha hata nukta moja!” alisema Rais Pius.

“Mheshimiwa Rais,nitaanzia miezi miwili iliyopita,” alisema Mathew.Akawaeleza Rais na wengine waliokuwamo katika kile chumba namna alivyokutana na Fahad,yale aliyomueleza kuhusu mpango wa kumuua Rais kwa kutumia ile ndege mpya na mashambulio yale ya magaidi.Chumba kilijawa na ukimya mkubwa.Wote walimsikiliza

Mathew kwa makini sana.Aliwaeleza mipango yote waliyoipanga na Fahad.

“Mheshimiwa Rais, nilifanya jitihada za kila namna na hatimaye nikafanikiwa kuonana na Rais wa Libya.Haikuwa rahisi, lakini alinielewa na kuukubali mpango wetu.Tukaanza kushirikiana!” alisema Mathew.

“Wakati tukiendelea na mipango yetu huko nchini Libya,Nilikuwa naendelea na mipango ya kuiteka ndege yetu mpya wakati ikitokea nchini China.Ilinilazimu kuingia katika mahusiano na Silvia Mwalule ambaye ni mmoja wa maafisa wa shirika la ndege,” alisema Mathew.Akawaeleza namna alivyoingia katika mahusiano na Silvia.

“Kupitia Silvia, nilipata tarehe ya kuwasili kwa ndege yetu ikitokea China.Nikalazimika kumshawishi Silvia ili afanye kila linalowezekana apate safari ya kwenda China ambako nilikwenda naye.Mheshimiwa Rais wakati mwingine katika hizi kazi inatulazimu kuumiza mioyo ya watu ili misheni ifanikiwe.Naamini Mungu atanisamehe kwani nilimuumiza sana yule dada ambaye alizama mapenzini na mimi bila kujua kama mwenzake nilikuwa katika misheni.” Alisema Mathew

“Usijilaumu sana Mathew,ninafahamu mambo hayo.Endelea na maelezo yako” alisema Rais Pius

“Ndege yetu mpya ilipoondoka Shanghai, ilipita jijini Guangzhou ambako alikuwepo Silvia na mwenzake pamoja na mimi.Kwa kumtumia yeye, nilipata nafasi ndani ya ndege,nikatekeleza mpango wangu wa kuiteka.Kama tulivyokuwa tumepanga,baada ya ndege kutoweka katika rada, ilibadili uelekeo na kuelekea nchini Libya!”

“Uliwezaje kuiteka ndege hiyo?”Rais Pius aliuliza.

“Kwa sababu ya muda na mambo tuliyonayo ni mengi, usiku huu naomba nisieleze kila kitu kilichotokea,nitakapopata nafasi huko mbeleni, nitawaeleza,Eleweni tu japo

nilifanikiwa, lakini haikuwa rahisi hata kidogo!” alisema Mathew.

“Endelea!” alisema Rais Pius.

“Baada ya kuiteka ndege tulielekea Tripoli.Tukiwa pale, kile kifaa kilichobeba hewa ya sumu kiliondolewa ndegeni na kupelekwa mbali kabisa.kikaharibiwa jangwani.Mheshimiwa Rais, kama ule mpango ungefanikiwa, basi ulikuwa na muda wa saa mbili tu au pungufu ya hizo za kuishi tangu uvute hewa ile ya sumu.Ninayo diski inayoonesha namna kifaa kile kilivyoondolewa ndegeni hadi kilivyoteketezwa!” alisema Mathew huku akitoa diski, akamkabidhi Rais ambaye aliichomeka katika runinga.Picha ya mjongeo iliyorekodiwa

ikaanza kuonekana.Kifaa kilichokusudiwa kupokonya uhai wa Rais kilionekana jinsi kilivyotolewa ndegeni hadi kilivyoteketezwa.

“Inaogopesha.Ilikuwa sumu mbaya mno!” alisema Jenerali Pius kwa kihoro. Mathew akaendelea.

“Toka awali tulifahamu kuwa magaidi wamepanga kuondoka na mateka nchini Tanzania na kuwapeleka Libya ila hatukujua kama mateka hao ni wanafunzi wale wadogo.Abdulkhareem aliporejea akiwa na wasichana aliowateka nyara hakujua kwamba anakwenda kifoni.”Mathew aliwaeleza namna walivyoweza kuingia katika ngome ya Abdulkhareem wakamuua na kuwakomboa watoto. “Dah!”alisema

Jenerali Pius baada ya kupokea maelezo yale kutoka kwa Mathew namna walivyoweza kumuua Abdulkhareem.

“Mathew, nataka kwanza nikushukuru kwa kazi kubwa uliyoifanya.Ahsante sana kwa kuniokoa na kifo.Hakuna aliyefahamu kama kuna mpango wa kuniua.Washenzi hawa walitaka kuniua kitaalamu sana.Ahsante sana Mathew Mulumbi.Ahsante sana Fahad!” alisema Rais Pius.

“Mheshimiwa Rais, ninakushauri kuanzia sasa uongeze zaidi ulinzi.Wameshindwa katika hili,lakini hawajashindwa vita.Wataendelea kujaribu tena na tena,” alisema Mathew.

“Ndiyo maana nikakuteua uongoze Shirika la Ujasusi ili tuweze kung’amua

mambo kama haya.Nafahamu majaribio ya kuniondoa au kunidhoofisha yatakuwepo mengi, lakini kama tutakuwa na shirika imara, basi tutakuwa tukiinasa mipango yao yote wanayoipanga dhidi yetu!”alisema Rais Pius na kuinamisha kichwa chini.Alionekana kuzama katika tafakari nzito.

“Mheshimiwa Rais!”alisema Mathew.Rais akainua kichwa kumtazama.

“Kama nilivyowaeleza kuwa Fahad ndiye aliyenipa taarifa za mipango yote ya mabeberu lengo kuu likiwa ni kuwaokoa kuwaokoa mpenzi wake na mwanae.Mimi naye tulikuwa na makubaliano kwamba kama

ningefanikisha kuwaokoa mpenzi wake Carmelita na mwanae Lebron basi angemalizia kunipa taarifa zaidi za mipango ya mabeberu kwa nchi yetu.Kwa kuwa tayari tumefanikisha kile alichokihitaji yaani kuwaokoa Carmelita na Lebron sasa ni uwanja wake kumalizia sehemu iliyobaki ya taarifa na wote tuwe makini kumsikiliza.Karibu Fahad" alisema Mathew

"Ahsante sana,Mheshimiwa Rais.Ahsante pia Mathew Mulumbi,ahsanteni pia wengine wote.Nawashukuru kwa makaribisho mazuri.Mheshimiwa Rais, kama alivyonitambulisha Mathew, ninaitwa Fahad Abdulkhareem Ghedi.Ni mjukuu wa Mahmoud Fadil Ghedi gaidi ambaye

anashikiliwa katika mahakama ya Afrika.Baba yangu ni Abdulkhareem Ghedi, ambaye ndiye gaidi aliyeongoza mashambulizi ya Arusha na ambaye mimi na Mathew Mulumbi tulifanikiwa kumuua.Tayari Mathew ameshawaeleza kila kitu namna alivyouawa" akasema Fahad na kujipapasa katika mifuko akatoa mkebe

"Mheshimiwa Rais niko chini ya miguu yako naomba univumilie niwashe sigara" alisema Fahad.Rais akamgeukia Mathew

"Let him" alisema Mathew

"Hakuna tatizo washa sigara" alisema Rais

"Ahsante mheshimiwa Rais.Mathew ananifahamu vyema" alisema Fahad

akawasha sigara akavuta mikupuo kadhaa halafu akaendelea

“Mheshimiwa Rais, ninatoka katika familia ya magaidi, lakini mimi si gaidi,ndiyo maana kwa mkono wangu nilimmiminia baba yangu risasi thelathini kwa hasira nilizokuwa nazo kutokana na matendo yake maovu.Si jambo jepesi kumuua baba yako mzazi,lakini mimi nililazimika kufanya hivyo kwani baba alikuwa mtu hatari mno.” Fahad alisema kisha akanyamaza kwa nukta chache akavuta sigara yake

“Mheshimiwa Rais ni kweli nilimuahidi kumpa Mathew taarifa ya mwisho kuhusiana na mipango ya mabeberu kwa Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla.Nitaanza maelezo

yangu mbali kidogo” akanyamaza tena akavuta sigara

“Baada ya majeshi ya Tanzania na Rwanda kukisambaratisha kikundi cha waasi wa jeshi la ukombozi la Congo,na kumuondoa madarakani Rais Jean Francois Kazadi,ulianza mchakato wa siri wa kuyaunganisha mataifa ya Rwanda na Burundi kuwa sehemu ya Tanzania.Naamini wote mliomo humu mnalifahamu jambo hilo.Mpango huo ulikuwa siri kubwa baina ya maraisi wa nchi hizi tatu lakini ndani ya muda mfupi haikuwa siri tena kwani mabeberu walifahamu uwepo wa mpango huo.Hawakuwa tayari mpango huo ufanikiwe kwa sababu ungeharibu kabisa mipango yao ya kinyonyaji hivyo

wakaanza mikakati ya kuhakikisha mpango huo haufanikiwi.Mkakati wao wa kwanza ulikuwa ni kukuondoa wewe mheshimiwa Rais kwani tayari ulikwisha kuwa mwiba kwao.Ulikata mirija yote waliyokuwa wanaitumia kunyonya nchi ya Tanzania.Hili halikuwapendeza hawa wakubwa hata kidogo na ndiyo maana walipanga mkakati wa kukuua kwa ile hewa ya sumu kwa bahati nzuri mpango huo ulishindwa kufanikiwa!" alisema Fahad na kuvuta sigara.

"Ni kweli anayoyasema, Fahad!" alisema Rais Pius.

"Nilipoingia madarakani, nilikuta hali si nzuri kwa namna rasilimali zetu zilivyokuwa zinabebwa na haya mataifa makubwa.Sikufurahishwa na hali ile,

ndipo nilipoanza kuchukua hatua za kuhakikisha tunalinda rasilimali zetu kwa gharama zozote.Kama alivyosema Fahad, ni kweli hawa watu ambao tumewakatia mirija waliyoitumia kunyonyea rasilimali zetu, hawawezi kufurahi hata kidogo.Ndiyo maana wanatumia kila aina ya mbinu kujaribu kunidhoofisha mimi na serikali ninayoiongoza.Hata hivyo bado nimesimama imara kutetea rasilimali za Tanzania ndiyo maana wakaamua kuja na mpango huo wa kuniua.” alisema Rais. Ukimya ukapita kwa sekunde kadhaa.Fahad akaendelea.

“Kupatikana kwa madini ya Kardistone katika mpaka wa Rwanda na Burundi ambayo ni madini adimu kabisa

kumewapa kiwewe mabeberu.Wanapigana vikumbo wao kwa wao katika kuyapata madini hayo.Hiyo ndiyo sababu ya kuundwa kwa kundi la waasi wa jeshi la ukombozi wa Congo na kuivamia Rwanda. Tayari hili mnalifahamu sina haja ya kurudia kulieleza" alisema Fahad akavuta tena mikupuo kadhaa akaizima ile sigara na kuiweka katika kisahani alicholetewa kwa ajili ya kuwekea majivu.Akaendelea "Mabeberu waliingiwa na hofu mno baada ya kupata taarifa za mazungumzo ya kuziunganisha Rwanda na Burundi kuwa sehemu ya Tanzania.Hofu yao kuu ni kuwa kama nchi hizi zingeungana na kuwa nchi moja ile ndoto yao ya kuyapata madini ya Kardistone

isingewezekana tena.Swali la kujiuliza, je, mazungumzo hayo ya siri ya marais kuhusu kuziunganisha nchi za Rwanda na Burundi kuwa sehemu ya Tanzania yaliwezaje kuvuja na kuwafikia mabeberu hao?”Fahad aliuliza.Zikapita sekunde kadhaa akaendelea

“Kuna mtu anaitwa Joesph Nahimana” alisema Fahad.Rais akatazama na Ruby

“Huyu ni mtoto wa Rais wa Rwanda.Amesoma nchini Ufaransa.Akiwa huko, alipatiwa mafunzo ya ujasusi kwa ahadi ya kuitawala Rwanda.Mipango ya Ufaransa ni kumuweka mdarakani kibaraka wao ambaye atawawezesha kunufaika hasa na madini ya Kardistone ambayo

wanayasaka kwa udi na uvumba.Mtaona hawa jamaa namna wanavyofanya mambo yao.Wanawaandaa watu kwa ajili ya kushika nafasi kubwa za uongozi barani Afrika.Walifanya hivyo kwa baba, walimsomesha na baadaye wakamuandaa kwenda Libya kuongoza kundi la waasi kwa lengo la kutwaa uongozi wa Libya ili waweze kunufaika na rasilimali za nchi hiyo.Mimi pia niliandaliwa na Marekani ili niwasaidie katika mpango wao wa kumuondoa baba nchini Libya.Kabla sijafanikisha hilo,mipango yao ilibadilika wakaanza kushirikiana na baba.Nitawaeleza zaidi hapo baadaye.Huyu Joseph naye alisomeshwa kwa ajili ya kwenda kumuondoa baba yake na achukue uongozi wa

Rwanda.Mkitaka kuamini hilo, Joseph ni mtu mwenye jina kubwa sana nchini Rwanda kutokana na namna anavyosaidia watu.Amekuwa akijihusisha sana na kusaidia jamii.Anajenga mashule,mahospitali anasomesha watoto wa masikini, anasaidia watu wasio na uwezo.Ni mtu ambaye kila aendako anaonekana kama mfalme.Kitu ambacho watu wa Rwanda hawajiulizi, je, fedha hizi zote ambazo anatumia kutoa misaada zinatoka katika biashara zake? Jibu ni hapana!Fedha hizo zinatoka nje ya nchi.Wanamuandaa awe Rais na tayari imekwisha anza kampeni kuwa Joseph ndiye Rais ajaye wa Rwanda.Inatumika fedha nyingi kumpamba,kumuandika vizuri katika

magazeti,kumsifu kwa nyimbo na mambo mengine mengi ya kumuinua huyu kijana.Zote hizi ni njama za mabeberu!” alisema Fahad,akanyamaza.

“Baada ya kuufahamu mpango wa Rwanda na Burundi kujiunga na Tanzania na kuunda nchi moja,Ufaransa waliogopa kuwa mpango wao wa kumuweka kibaraka wao madarakani ambaye ni Joseph utashindikana, ndipo walipokuja na mpango mwingine wa kuhakikisha wanaivuruga Afrika Mashariki.Hapo ndipo alipoingia mtu anaitwa profesa Fabrice Kayembe!” Alisema Fahad.Akanyamaza kidogo.Akameza funda la mate kisha akaendelea.

“Fabrice Kayembe ni profesa katika chuo kikuu cha sayansi cha Paris Ufaransa.Ni mbobezi katika sayansi ya virusi.Asili yake ni Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, lakini ameishi Ufaransa tangu akiwa mtoto mdogo.Profesa Fabrice Kayembe alipewa kazi ya kufanya utafiti wa kirusi chenye uwezo mkubwa wa kusambaa kwa binadamu kwa haraka na kuua ndani ya siku chache.Hakuelezwa nini hasa malengo ya utafiti wa kirusi hicho.Hatimaye baada ya utafiti Profesa Kayembe, alifanikiwa kupata kirusi alichokipa jina la Neira 43.Wakati Fabrice akiendelea na zoezi la kutafuta kinga yake,kirusi hicho kikaibwa kutoka mahala kilipokuwa

kimehifadhiwa.Ambacho hawakukifahamu walioiba kirusi hicho ni kwamba,Fabrice Kayembe alifahamu hatari ya kirusi alichopewa kazi ya kukitafiti.Iwapo kingetumika sehemu fulani, basi kingeweza kuleta maangamizi makubwa.Hivyo alichukua tahadhari mapema kwa kukiweka katika kisanduku kidogo alichokiwekea program maalum ya kumuwezesha yeye pekee kukifungua.Ndani ya sanduku,aliweka pia kifaa ambacho kingemuwezesha kufuatilia kirusi hicho na kujua mahala kilipo hata kama kingeibwa!" Fahad alinyamaza tena kidogo.Akanywa maji kulainisha koo lake.

“Kirusi hicho kilitakiwa kusambazwa jijini Arusha ili kutokea hapo kisambae katika eneo lote la Afrika Mashariki.Malengo yao ni ili pale maambukizi yatakapokuwa makubwa basi eneo lote la Afrika mashariki lionekane ni eneo hatarishi.Walitaka watu wafungiwe ndani kuepuka kusambaa zaidi kwa maambukizi na wao wangekuja kwa dhumuni la kutoa msaada lakini lengo lao kuu likiwa ni kuchota madini hasa Kardistone.Mtu aliyetakiwa kukileta kirusi hicho hapa nchini anaitwa Amos Ntuyahaga,” Fahad alisema kisha akavuta pumzi kidogo.

“Amos Ntuyahaga alitakiwa kuonana na Joseph Nahimana pindi atakapofika hapa nchini.Wakati

maandalizi ya kukipokea kirusi hicho yakiendelea,Joseph Nahimana alijulishwa kuwa mipango imebadilika.Kirusi hakitaletwa tena Tanzania.Kuna sababu kubwa hapa kwa nini mipango ilibadilika ghafla”Fahad akanyamaza tena kidogo,halafu akaendelea

“Ufaransa walimuandaa Joseph Nahimana kushika nafasi kubwa ya uongozi wa Rwanda,lakini waligundua kuwa Joseph amekuwa pia akishirikiana na Marekani akiwapa taarifa za mipango yote ya Ufaransa.Baada ya kuligundua hilo, ndipo mipango yao ikabadilika kimyakimya bila kumjulisha Joseph.Amos Ntuyahaga akiwa na kirusi, alifika nchini Tanzania kimya kimya bila

ya Joseph na mtandao wake kufahamu chochote kile.Pindi tu alipofika Arusha, mawasiliano na watu wa Ufaransa yalipotea.Hakuna aliyefahamu ni nini kilimtokea.Wiki mbili baadaye bila mawasiliano yoyote na Amos,walilazimika kumfuata tena Fabrice Kayembe na kumueleza ukweli wote kuhusu kirusi na faida ambazo zingepatikana endapo kingesambazwa katika eneo la Afrika Mashariki.Fabrice akawaeleza ukweli kuwa alitengeneza mfumo maalum wa kukifuatilia kirusi kile na kufahamu mahala kilipo.Akawathibitishia kwamba hata kama wakikipata kirusi hicho, hawataweza kukisambaza bila yeye kutokana na mfumo wote wa

kukisambaza kirusi hicho anao yeye.Fabrice aliahidiwa fedha nyingi mno endapo angefanikisha kupatikana kwa kirusi hicho.Hilo hasa ndilo lililomletaTanzania" Fahad alinyamaza tena

"Marekani kwa kupitia majasusi wao,walipata taarifa za Fabrice kuja nchini Tanzania katika mkutano wa *Afrika Asili Yangu*,na walifahamu kuwa lengo lake kuu lilikuwa ni kukitafuta kirusi hicho.Marekani walikihitaji pia kirusi hicho,ndipo lilipoandaliwa shambulio lile la kigaidi lengo kuu likiwa ni kumpata Fabrice Kayembe ili awaoneshe mahala kilipo kirusi," Fahad akatulia tena kidogo.Akatoa kitambaa na kujifuta usoni.

“Fahad kabla hujaendelea zaidi ninataka kufahamu.Hili kundi la Ansal al sharia lililokuwa linaongozwa na baba yako Abdulkhareem lilikuwa chini ya ufadhili wa Ufaransa.Iliwezekanaje kundi hilo hilo likatumiwa tena na Marekani kufanya shambulio lile la kigaidi la Arusha na kuwasaliti wafadhili wao? Ruby aliuliza

“Jibu ni kwa sababu Marekani wasingeweza kumfikia Fabrice kwa urahisi kwani alikuwa analindwa na majasusi wa Ufaransa waliokuwa wanamfuatilia kila sehemu.Hawakutaka wajulikane kuwa nao wanamfuatilia Fabrice.Njia pekee ya kuweza kumpata kirahisi Fabrice ilikuwa ni kwa kuandaa shambulio lile la kigaidi wakilitumia

kundi la Ansar al Sharia.Wakiongozwa na Abdulkhareem Ansar al sharia walikubali kuwasaliti Ufaransa na kushirikiana na Marekani kwa sababu mbili.Kwanza waliahidiwa kuungwa mkono na Marekani katika harakati za kutwaa uongozi wa Libya kwa kuwapa silaha nzito za kivita.Pili Marekani waliwaahidi kuliondoa kundi hilo kutoka katika orodha ya makundi ya kigaidi duniani.Hizi ndizo sababu za Ansar al sharia kukubali kuwasaliti Ufaransa wakajiunga na Marekani.”Fahad alipumzika kidogo halafu akaendelea

“Magaidi walipewa maelekezo ya kuhakikisha wanaipata diski pamoja na sanduku lenye kirusi na ndipo maandalizi ya shambulio lile

yalipoanza.Walikutanishwa na Joseph Nahimana pamoja na mwanamke mmoja anaitwa Maurine Kyaso.Huyu ni mfanyakazi wa idara nyeti ya serikali ya Tanzania inaitwa SNSA.Huyu ndiye ambaye amekuwa akiwapa mabeberu siri nyingi za serikali.Ni huyu ambaye alifanikisha kuuawa kwa waziri wa mambo ya nje wa Tanzania wakati akitokea Rwanda.Lengo lilikuwa kupata nyaraka muhimu za maendeleo ya mpango wa kuziunganisha Rwanda na Burundi kuwa sehemu ya Tanzania.Hata silaha walizotumia magaidi katika shambulio la Arusha zote ni kwa msaada wa huyu mama.Nilimuonya Mathew kuhusu huyu mtu.Ni mwanamke hatari sana" Fahad akanyamaza.

“Mheshimiwa Rais, na ndugu zangu wengine, japokuwa tumewamaliza magaidi lakini bado kuna kazi kubwa ya kufanya kuhakikisha diski inapatikana, kwa sababu ndiyo yenye program ya kufungulia hilo sanduku kilimo kirusi.Kwa namna yoyote ile, lazima muhakikishe diski inapatikana.Mathew Mulumbi, mimi nimemaliza kile nilichokuahidi kukueleza na sasa mpira ninakuachia wewe.Ninashukuru kile nilichokuwa nakihitaji nimekipata.Mpenzi na mtoto wangu wako salama.Baba ambaye alikuwa hatari kwao hayupo tena.Sasa niko huru kuendelea na maisha yangu bila hofu yoyote ile.Naamini nimejiweka katika hatari kwa kuwapa siri za mipango ya

mabeberu kwa hiyo sintarudi tena Marekani.Ninakwenda mafichoni sehemu salama!” alisema Fahad.Ukimya mfupi ukapita. Mathew akasema.

“Fahad, ninakushukuru sana kwa maelezo yako yaliyotufumbua macho.Sisi bado tunaendelea na mapambano kuhakikisha nchi inakuwa salama.Kama kuna chochote utakipata au kuna msaada tutauhitaji kutoka kwako, basi tutakujulisha mara moja!” alisema Mathew.

“Fahad kwa haya mambo makubwa uliyotueleza umejiweka katika hatari kubwa.Ninaamini Marekani wakijua kuwa ni wewe ndiye uliyevujisha siri zao watakusaka kwa kila njia hadi wakupate.Kwa nini usiamue kuishi hapa

Tanzania? Hapa utakuwa salama” alishauri Rais Pius

“Ahsante sana mheshimiwa rais kwa ushauri wako.Yawezekana nikarejea tena huko mbeleni lakini kwa sasa lazima niondoke” alisema Fahad

Rais alitoa maelekezo kwa wasaidizi wake kuwapeleka Fahad na Carmelita katika moja ya hoteli kubwa kabisa jijini Dar es salaam ambako wangekaa kwa usiku ule kwa gharama za Rais. Baada ya akina Fahad kuondoka akina Mathew wakarejea ndani kuendelea na kikao.

“Karibuni tena.Kikao kinaanza upya!” alisema Rais Pius.

“Tumewasikiliza Mathew na Fahad.Mambo waliyoyaeleza ni mazito mno na sikuyatarajia.Hongereni sana

nyote kwa kazi kubwa mliyoifanya hadi haya yote yakajulikana!” alisema Rais na kufuta jasho usoni.

“Baada ya ya kufahamu kuwa sanduku lile limebeba kirusi hatari kabisa,jukumu letu ni kulilinda kuhakikisha linakuwa salama.Jambo la pili ni kuhakikisha tunaitafuta diski na kuipata kwa gharama zozote zile.Mathew, nina imani kubwa nanyi! Mmeifanya kazi kubwa hivyo nawasihi mfanye kila mnaloweza kuhakikisha mnaimalizia kazi hii ndogo iliyobaki.Naamini diski hiyo bado iko hapa nchini nataka mtumie kila mbinu mnayoweza kuhakikisha diski inapatikana.Nataka pia muhakikishe wale wasaliti wote na mawakala wa

mabeberu ambao wameshiriki kwa namna yoyote ile kusaidia mipango miovu ya mabeberu hapa nchini wanajulikana ili wakamatwe na wafikishwe mbele ya sheria.Mimi nitatoa msaada wa kila aina kuhakikisha mnaikamilisha kazi yenu kwa wepesi na haraka.Jambo lingine mnanishauri nini kuhusu Maurine Kyaso? Amenisikitisha sana yule mwanamke.Sikutegemea kabisa kuwa ni kuwadi wa mabeberu”Rais Pius alisema.

“Maurine Kyaso, kwa sasa hatakiwi kuguswa.Tunataka aendelee na mipango yake na mtandao wake huku sisi tukiendelea kumfuatilia kila anachokifanya.Huyu ndiye atakayetusaidia sana kuufahamu mtandao

wake wote hapa nchini.Vilevile kumpata Joseph Nahimana," alisema Mathew.

"Kabla hatujamaliza kikao hiki, nataka kufahamu kuhusu sanduku lenye kirusi.Mnadhani ni wapi litahifadhiwa ambako litakuwa salama?" Aliuliza Rais.

"Mheshimiwa Rais, kama itakupendeza sanduku hilo linaweza likahifadhiwa hapa Ikulu au sehemu nyingine yoyote ambako wewe utaamua." alisema Ruby.Rais akaonekana kuzama mawazoni kisha akauliza.

"Lengo la mabeberu ni kusambaza kirusi hicho hapa nchini.Kama bado wanayo diski,mnadhani wanaweza wakalifungua sanduku hilo kutokea

mbali na kirusi kikasambaa?”aliuliza Rais Pius akionesha wasiwasi kidogo

“Hilo haliwezekani mheshimiwa Rais.Ili kukisambaza kirusi hicho lazima kwanza walipate sanduku” alijibu Ruby.Rais akashusha pumzi.

“Nataka kirusi kiondolewe hapo nyumbani kwako nitatoa maelekezo mahala pa kukipeleka ambako kitakuwa salama,” alisema Rais Pius.

Kikao kilimalizika,Rais akaagana na akina Mathew, wakaondoka kuelekea nyumbani kwa Ruby huku wakifuatana na gari nyingine mbili za watu ambao Rais Pius aliwatuma kwenda kuchukua sanduku lenye kirusi.

Safari ilikuwa ya kimyakimya hadi walipofika nyumbani kwa Ruby.Sanduku

lenye kirusi likakabidhiwa kwa watu waliokuwa wameambatana nao, wakaondoka nalo kulipeleka mahala walikoelekezwa na Rais Pius.

“Baada ya sanduku kuondoka, sasa tunaanza kazi!” alisema Mathew huku akivua shati na kubaki na fulana.Wakaelekea ofisini kwa Ruby.

“Kazi kubwa tuliyonayo,kwanza ni kuitafuta diski ya Fabrice Kayembe.Kwa mujibu wa Sultan,alidai kuwa baada ya kuipata diski kutoka kwa Fabrice Kayembe, alikabidhiwa mtu anayeitwa Jamal.Naye alikwenda kuwakabidhi akina Sultan.Na wao wakampa mtu anayeitwa Omega ili aipeleke kwa Rebecca Anderson.Rebecca ni mfanyakazi wa hoteli ya Meru

Paradise.Nilitoa maelekezo ya kumtafuta huyu mtu, mmefikia wapi?”Alisema Mathew.

“Mathew, kabla ya kukupa taarifa za Rebecca kuna taarifa fupi nataka kuiwasilisha kwako.Katikamkoba wa Amos Ntuyahaga ambaye kama alivyosema Fahad kuwa ndiye aliyeleta sanduku lenye kirusi hapa Tanzania,tulikuta karatasi yenye namba ya simu ya Joseph Nahimana.Tulimchunguza Joseph,tukabaini aliwasiliana na mtu anaitwa Mwasi Jumbe wa hapa Dar es Salaam.Tulimfuata Mwasi,akatueleza kuwa namba yake iliyotumika kuwasiliana na Joseph inatumiwa na mdogo wake anaitwa Nicole.Tulianza

kumfuatilia Nicole na kugundua ana urafiki mkubwa na Maurine Kyaso.Tulinasa mazungumzo ya Nicole na Joseph, lakini hatukuelewa chochote!" alisema Ruby na kucheza mazungumzo ya Nicole na Joseph.Mathew akayasikiliza kwa makini kisha akasema.

"Huu ni mfumo wa mawasiliano wa kijasusi.Kama tulivyosikia huyu jamaa Joseph ni jasusi na hapa kuna jambo hawakutaka lijulikane ndiyo maana wakatumia mfumo huu."alisema Mathew.

"Baada ya kugundua ukaribu wa Maurine na Nicole, tuliweka kamera za siri nyumbani kwa Maurine na kuanza kumchunguza!" alisema Ruby.Alimweleza Mathew namna

walivyoweza kumteka Carmelita wakampeleka katika nyumba ya siri na namna alivyoweza kumuokoa Ramesh

“Hongereni sana kwa kazi nzuri mliyoifanya.Uchunguzi mlioufanya umerahisisha sana kazi yetu.Kipaumbele chetu kikuu kwa sasa ni kuipata diski.Kuna hawa watu watatu ambao tunaelekeza macho kwao kwa sasa.Maurine Kyaso,Rebeca Anderson na Nicole.Kwa mujibu wa Sultan,diski alipewa Rebecca ila hakusema alipewa aipeleke wapi.Hivyo tunatakiwa kumuhoji zaidi Sultan na kufahamu mipango yao baada ya kuipata hiyo diski.Wakati huo huo tuendelee kumfuatilia kwa karibu sana Maurine,kujua kila anachokifanya,kila

anakoenda na kila anayewasiliana naye.Huyu atatusaidia sana kufahamu mahala alipo Joseph Nahimana!”alisema Mathew

“Katika kumfuatilia Maurine kuna kitu nilikigundua.Maurine ana simu ambayo huitumia kwa siri.Kama tukifanikiwa kuipata, basi itatuwezesha kujua mawasiliano yake yote ya siri.Inawezekana huitumia simu hiyo kuwasiliana na Joseph na washirika wake wengine!” alisema Ruby.

“Hakuna namna unayoweza kuidukua?”Mathew aliuliza.

“Tunatakiwa kuipata namba anayotumia kisha tutaiingiza kwenye mfumo wa kuidukua,” alisema Ruby.

“Kwa sasa Maurine yuko nyumbani kwake?”Aliuliza Mathew.Ruby akatazama kamera za siri walizofunga nyumbani kwa Maurine.

“Hapana!Bado hajarejea,” alijibu.

“Ni vipi mliweza kuingia mle ndani na kuweka kamera za siri?”Aliuliza Mathew,Ruby akamueleza kile walichokifanya.

“Itatulazimu kufanya hivyo tena ili tuweze kuipata hiyo simu na kujua anawasiliana na nani,”alisema Mathew.

“Gosu Gosu, tunakwenda kwanza kumchukua Sultan tumlete hapa kwa mahojiano zaidi.Agai atabaki hapa kuhakikisha Ruby anakuwa salama!” alisema Mathew kisha wakatoka nje kwa ajili ya kuingia katika gari la Ruby ili

waelekee mahala alikopelekwa Sultan.Mara tu walipoingia garini, simu ya Ruby ikaita.Alikuwa Rais, ikamlazimu kuwazuia akina Mathew wasiondoke kwanza.

“Rais anapiga simu.Yawezekana kuna jambo la muhimu anataka kutueleza!” alisema Ruby.Akina Mathew wakashuka garini.

“Mheshimiwa Rais!” alisema Ruby baada ya kuipokea simu.

“Ruby,nahitaji kuzungumza na Mathew Mulumbi, tafadhali!” alisema Rais Pius,Ruby akampatia Mathew simu.

“Mheshimiwa Rais!” alisema Mathew.

“Mathew nimepata taarifa mbaya muda mfupi uliopita.”

“Taarifa gani,Mheshimiwa Rais?”aliuliza Mathew

“Nimetaarifiwa kwamba wale vijana niliowatuma kuchukua sanduku lenye kirusi ili kulipeleka sehemu salama, wamevamiwa njiani na watu wasiojulikana.Wameshambuliwa na sanduku limechukuliwa,” alisema Rais Pius. Akameza funda la mate kisha akasema.

“Mathew, tumekipoteza kirusi!” Mathew alihisi kama jiwe zito limegonga kichwa chake.

“Mathew, unanisikia?”Aliuliza Rais Pius.

“Mheshimiwa Rais, taarifa hiyo imenishtua sana.Walifahamuje kama

moja kati ya magari yale limebeba sanduku lenye kirusi?” Aliuliza Mathew.

“Hilo ndilo swali la kujiuliza namna walivyoweza kujua.Mpaka sasa hakuna taarifa zozote zimepatikana kuonesha nani waliofanya tukio hilo.”alijibu Rais

“Mheshimiwa Rais, hakuna haja ya kuumiza kichwa kuhusu nani waliofanya kitendo hicho.Tunawafahamu watu wanaokitafuta kirusi.Tutakachokifanya ni kuwafuatilia na kuhakikisha tumekirejesha mikononi mwetu.Mheshimiwa Rais, nakuhakikishia mimi na timu yangu tutafanya kila linalowezekana kuhakikisha kirusi hicho kinapatikana” alisema Mathew.

“Mathew unadhani kuna haja ya kutoa tahadhari kwa vyombo vingine ili maandalizi ya kukabiliana na kirusi hicho endapo kitasambazwa yaanze mara moja? Aliuliza Rais Pius

“Mheshimiwa Rais,bado hatujashindwa kukipata kirusi.Tupe muda tuifanye kazi yetu.Pale tutakapoona tumeshindwa tutakujulisha lakini kwa sasa msiwape wananchi taharuki” alisema Mathew

“Mathew, nakuomba tafadhali hakikisheni mnakipata kabla ya jua kuchomoza.Kukipambazuka, tunaweza kuwakosa hawa watu na nchi ikaingia katika hatari kubwa.Mathew hakikisheni wale wote waliohusika katika jambo hili

aidha *wanakamatwa* au *wanauawa*”alisema Rais Pius.

“Sawa,Mheshimiwa Rais.Nitakutaarifu kila hatua tutakayoipiga,” alisema Mathew.

“Kila la heri.Maisha ya Watanzania yanawategemea sana ninyi.Mungu awatangulie katika misheni hii!” alisema Rais Pius na kukata simu.Mathew akavuta pumzi ndefu baada ya simu kukatwa.

“Wamechukua kirusi!”alisema na kuwaeleza wenzake kile alichoelezwa na Rais Pius.

“Wamefahamuje kama kirusi kimo ndani ya yale magari?”Aliuliza Agai.

“Watu ambao wanakitafuta,tunawafahamu hivyo

kilichopo hapa ni kuwatafuta mahala walipo na kukichukua kutoka katika mikono yao.Ndugu zangu, nchi inatutegemea sisi.Kama tukishindwa kukipata kirusi kabla ya asubuhi, hawa jamaa wanaweza wakakisambaza na kazi yote tuliyoifanya itakuwa bure.Tunatakiwa kufanya kila lililo ndani ya uwezo wetu kuhakikisha tunakipata.Rais ametoa ruhusa *this is a capture or kill mission*.Hakuna huruma kwa yeyote ambaye ameshiriki kuweka maisha ya ndugu zetu mashakani.Hivi sasa Watanzania wamelala tusikubali Watanzania wakaamka wakiwa na taharuki kubwa.!" alisema Mathew.

"Tunaanzia wapi?" Aliuliza Agai.

“Tunaanzia kwa Maurine.Ruby unaweza ukatusaidia kujua mahala alipo Maurine?”Alisema Mathew.Ruby akaweka sawa programu yake katika kompyuta halafu akampigia simu Maurine, lakini simu ya Maurine haikupatikana.

“Simu yake haipatikani.*She’s gone dark*!” alisema Ruby.

“Tunakwenda nyumbani kwake.Hatuwezi kukosa kitu cha kutusaidia kujua kuhusu mipango yao.*There is must be something there!*” alisema Mathew kisha bila kupoteza muda wakaingia garini na kuondoka kuelekea nyumbani kwa Maurine.

“Bado najiuliza wamejuaje kama katika yale magari kuna sanduku lina

kirusi? Nina pata mashaka kuwa yawezekana wana mtandao wao hadi kwa watu wanaomzunguka Rais" alisema Gosu Gosu

"Hata kama wana mtandao mkubwa kiasi gani, hakuna jiwe litasalia juu ya jiwe hadi tuhakikishe kirusi kimepatikana!" alisema Mathew.

Walikaribia kufika nyumbani kwa Maurine wakasimamisha gari.

"Ruby, kazi kwako sasa!" alisema Mathew.Ruby ambaye alishaiweka tayari program yake, akabonyeza kitufe *Enter* na baada ya dakika mbili nyumba ya Maurine ikawa giza.Taa zote zilizimika.Nyumba ya Maurine ilikuwa inalindwa na mfumo maalum wa ulinzi wa SNSA.Ili kuingia ndani ya nyumba

hiyo bila kuonekana inakulazimu kwanza kuuzima mfumo mzima wa SNSA kitu alichokifanya Ruby

“Agai utabaki garini kumlinda Ruby.Mimi na Gosu Gosu tunakwenda ndani.*Let’s go!*” alisema Mathew.Wakashuka garini na kukimbia kuelekea katika nyumba ya Maurine.Hakukuwa na muda wa kupoteza,Agai akainamisha mgongo,Mathew akapanda na kushika kingo za ukuta akarukia ndani na kutua bila kutoa kishindo kikubwa.Gosu Gosu naye akapanda na kurukia ndani.Agai akarejea garini alikokuwa Ruby.

Ndani ya nyumba ya Maurine kulikuwa na mwangaza hafifu kutoka katika taa za nyumba ya jirani.Wakiwa

na bastola zao mikononi,Mathew na Gosu Gosu wakatembea kwa tahadhari hadi katika mlango mkuu wa kuingilia sebuleni.Akajaribu kuufungua mlango, lakini ulikuwa umefungwa kwa funguo.

Mathew alikuwa amejiandaa, akachomoa vifaa vidogo kutoka mfukoni na kutumia sekunde chache tu kuufungua mlango uliofungwa.Wakaingia ndani,wakawasha tochi huku Gosu Gosu akianza kupekua sebuleni.Mathew akaenda katika chumba cha kulala cha Maurine.Alikuta kuna sanduku likiwa limewekwa kitandani huku lundo la nguo likiwa pembeni.

“Inaonekana huyu mwanamke aliweka tayari sanduku hili akijiandaa kutoroka!” Mathew aliwaza,akaanza

upekuzi.Alifungua droo zote za makabati, lakini hakupata kitu chochote cha maana.

"*There's must be something in here*." Aliwaza Mathew akiendelea kuangaza angaza

"Kuna kila dalili kuwa aliondoka ghafla na hakuwa amemaliza kupakia vitu vyake,hivyo lazima atarejea kuja kumalizia kupakia.Naamini kila kitu chake bado kimo humu humu ndani!"Aliwaza Mathew na kwenda katika kabati la nguo, akaanza kutoa nguo.Ghafla akagusa kitu chenye vitufe vyenye namba kama simu kando ya kabati.

"Kitu gani hiki?"Alijiuliza na kumuita Gosu Gosu.Wote hawakujua

namba zile ni za nini.Kwa kutumia simu ya Gosu Gosu,Mathew akapiga picha halafu akamtumia Ruby picha ya kile kifaa.

“Mathew, kuna chumba cha siri humo ndani.Hilo kabati ni mlango wa kuingilia chumba hicho.Akibonyeza namba anazozifahamu, kabati hujitenga na kuacha njia ya kuingia ndani ya chumba hicho.Ili kuingia humo, lazima umeme uwake!” alisema Ruby baada ya kuiona picha ya kile kifaa.

“Ahsante,Ruby,tutakujulisha baada ya muda!” alisema Mathew na kukata simu.

“Gosu Gosu, tafuta kitu kama shoka au chochote ambacho tunaweza kutumia kuvunja kabati hili,” alisema

Mathew.Gosu Gosu akaenda kutafuta kifaa alichotumwa,baada ya dakika tatu, akarejea akiwa na shoka na jembe.

“*Good!*” alisema Mathew na kulishika shoka.Akaanza kulibomoa kabati.Kama alivyosema Ruby, ni kweli kulikuwa na uwazi.Mathew akapata njia akapenya. Gosu Gosu naye akamfuata, wakaingia katika chumba kikubwa.Kulikuwa na meza iliyokuwa na makaratasi mengi.

Kulikuwa pia na kompyuta, akaikunjua ikawaka, lakini ilihitaji neno la siri ili iweze kufunguka.Akajaribu kuvuta moja ya droo za meza, lakini ilikuwa imefungwa kwa funguo.Gosu Gosu akaipiga teke droo ile

ikasambaratika.Ndani ya droo wakakuta kuna simu.Mathew akaishika.

“*Satelite phone*! Alisema Mathew huku akiiweka mezani.Gosu Gosu akavunja droo nyingine ambamo walikuta mkoba ukiwa umejaa fedha dola za Marekani.Chini yake wakakuta kuna hati ya kusafiria.Mathew akampigia simu Ruby.

“Ruby, tafadhali tunahitaji uje huku!” alisema Mathew.Akamtuma Gosu Gosu aende kufungua geti.Gosu Gosu akakipiga na shoka kifaa ambacho kinatumika kuliongoza geti kikasambaratika,akalifungua,Ruby akaingia ndani,Agai akabaki nje akiangalia usalama.

Ruby akaingia ndani ya kile chumba cha siri cha Maurine.Mathew akampatia ile simu.

“Nahisi hii ndiyo ile simu uliyokuwa unaizungumzia.Unaweza kujua ni akina nani waliopigiwa kwa kutumia simu hii?” Aliuliza Mathew.Ruby akaiwasha halafu akaanza kuipitia huku akiandika namba kadhaa katika karatasi kisha akaanza kubonyeza kompyuta yake.Baada ya dakika chache akasema

“Amempigia simu Mwasi Jumbe ambaye ni Nicole.Vile vile akampigia simu ..*oh my God*!”alisema Ruby kwa mshangao.

“Nini Ruby?”

“Amempigia simu mtu mwingine hizi namba si za Tanzania.Itabidi

tufanyie uchunguzi tujue ni namba za nani, lakini ili tuweze kujua alichokizungumza na Nicole ni hadi pale mfumo wa SNSA utakaporejea,'alisema Ruby.

"Bado muda gani mfumo huo urejee?"Aliuliza Mathew.Ruby akaitazama saa yake.

"Bado dakika nane!"

"Hatuna muda huo wa kusubiri.Unaweza kuurejesha sasa?" Aliuliza Mathew.

"Ndiyo!"

"Good.Urudishe!" alisema Mathew.Ruby akacheza na kompyuta yake na baada ya sekunde kadhaa, taa zikawaka na mfumo ukarejea.King'ora cha kuashiria kuna hatari kikaanza kulia.

“Tuondoke.King’ora hicho kilicholia kinaashiria kuna uvamizi katika nyumba hii.SNSA watafika hapa muda si mrefu!” alisema Ruby.Wakaichukua ile simu ya Maurine na kompyuta bila kusahau ile hati ya kusafiria ya Maurine wakaondoka navyo.Wakatoka haraka haraka hadi katika gari lao na kutoweka katika eneo lile.Ruby alijielekeza katika kompyuta yake akibonyeza haraka haraka.Baada ya muda mfupi,akamwomba Gosu Gosu kusimamisha gari.

“Tayari nimeyapata mazungumzo ya Maurine na Nicole” alisema Ruby halafu akacheza mazungumzo yale.

“Nicki, nimezima simu yangu ya kawaida ndiyo maana nimekupigia kwa

kutumia simu hii ya satelaiti!” ilisikika sauti ya Maurine.

“Unasemaje,Maurine?” Iliuliza sauti ya Nicole

*“Muda mfupi uliopita nmepokea taarifa kuwa Rais alikuwa katika kikao na akina Mathew.Inasemekana tayari wamejua kilichomo ndani ya lile sanduku kuwa ni kirusi.Tumekuwa tunalitafuta sanduku hilo kumbe liko kwa Ruby.Hivi sasa sanduku hilo linakwenda kuhamishwa kutoka nyumbani kwa Ruby kupelekwa sehemu salama alikoelekeza Rais!”*alisema Maurine

“Dah!Hizi ni taarifa njema sana!” alisema Nicole.

“Nicole tunakaribia kumaliza kazi.Kila kitu kinamalizika usiku wa leo

na kesho mapema tunaondoka hapa nchini!”alisema Maurine

“Tunafanyaje kulipata hilo sanduku?”Aliuliza Nicole.

“Tayari nimeshatuma timu ya vijana wangu wanawafuata watu waliolibeba.Hao jamaa hawajui kama wanafuatiliwa hivyo kazi haitakuwa ngumu.Nataka umfuate Joseph mwambie tunalipata sanduku usiku huu na ajiandae ili tuikamilishe kazi.Baada ya kulipata,nitawafuata na kumaliza kazi.Kesho asubuhi na mapema tutaondoka na helkopta ya SNSA hadi mpakani mwa Tanzania na Rwanda.Sasa ninaelekea mahala nilikoahidiana kukutana na vijana wangu ambao

watanikabidhi sanduku halafu nikitoka hapo nitawafuata!” alisema Maurine.

“Sawa!Na mimi ninaelekea kwa Joseph tutakutana huko,” alisema Nicole na kukata simu.

Mathew aliuma meno kwa hasira

“Mazungumzo haya yanaonesha wazi kuwa Maurine na wenzake hawakufahamu mahala lilipo sanduku lenye kirusi na taarifa hizo wamezipata usiku huu baada ya sisi kutoka Ikulu.Kuna mtu ambaye aidha alifuatilia mazungumzo yetu na Rais au kwa namna yoyote ile ameweza kufahamu kuhusu kirusi na akampigia simu Maurine kumtaarifu.Naye akatumia vijana wake kwenda kuvamia gari lililokuwa na sanduku.Wakaua watu na kulichukua.

Kwa sasa tunahitaji kufahamu mahala alipo Nicole.Kwa maana Maurine alimweleza kuwa baada tu ya kukipata kirusi atawafuata.Kitu kingine ni kwamba Joseph Nahimana yuko hapa Dar es Salaam.Hivyo tukifahamu mahala alipo Nicole, basi tutawapata wote pamoja na kirusi!" alisema Mathew.

"Hatuwezi kumpigia Nicole kwa simu hii ya Maurine? Aliuliza Agai.

"Hapana!Hatuwezi kumpigia kwa simu hii.Yawezekana kabisa akawa na Maurine ambaye anafahamu simu yake ameiacha nyumbani.Hilo linaweza kuamsha kengele ya hatari kwamba tayari wamejulikana.*We have to find another way!*" alisema Mathew.

“Kuna namna ambayo tunaweza kumpata Nicole.Ni kwa kumtumia dada yake Mwasi Jumbe.Huyu ndiye ambaye Nicole anatumia laini yake ya simu.Tukifanikiwa kumpata huyu anaweza akatusaidia kumpata Nicole!” alisema Gosu Gosu.

“Kama una hakika anaweza akawa na msaada tumfuate.Anaishi wapi?”Mathew aliuliza.

“Ngoja nimpigie simu!” alisema Gosu Gosu,akuchukua simu yake akampigia Mwasi Jumbe.Simu ikaita na kukatika.

“Hapokei simu.Yawezekana amelala!”alisema Gosu Gosu.

“Piga tena.Unafahamu anakoishi?” Aliuliza Mathew.

“Hapana sifahamu!” alijibu Gosu Gosu na kupiga simu.Ikaita tena bila kupokelewa.Akapiga mara ya tatu,simu ikapokelewa.

“Hallow!” ilisema sauti ya mwanamke akionekana alitoka katika usingizi mzito.

“Hallow, Mwasi, habari yako? Habari za usiku huu?”Aliuliza Gosu Gosu.

“Nzuri kabisa! Nazungumza na nani? Aliuliza Mwasi

“Gosu Gosu.Unanikumbuka? kutoka ikulu”

“Ndiyo nakukumbuka.Unasemaje usiku huu Gosu Gosu!”alisema Mwasi

“Mwasi, nina shida nawe usiku huu.Nahitaji kukuona.”

“Unataka kuniona usiku huu?”Aliuliza Mwasi huku sauti yake ikipanda.Alionesha kushangaa

“Ndiyo, Mwasi!Ninahitaji kukuona nina jambo la muhimu sana!”

“Jambo gani hilo? Hatuwezi kuzungumza simuni au kusubiri hadi kesho?”Mwasi aliuliza

“Hapana.Hatuwezi kuzungumza simuni.Nielekeze tafadhali unapoishi nitakufuata hapo mara moja!” alisema Gosu Gosu.Mwasi akasita.

“Mwasi!”aliita Gosu Gosu.

“Gosu Gosu, unanipa wasiwasi sana.Jambo gani hilo la usiku huu?”

“Usihofu, Mwasi.Naomba unielekeze mahala ulipo nikufuate mara moja,” alisema Gosu Gosu.Mwasi

akakata shauri, akaamua kumuelekeza mahala anapoishi.

“Ahsante, Mwasi!Ninakuja hapo sasa hivi,” alisema Gosu Gosu na kukata simu.

“*Let’s go!”*alisema Mathew.Gosu Gosu akawasha gari, wakaondoka kuelekea kwa Mwasi,

“Lazima tumpate mtu ambaye amewapa akina Maurine taarifa za kile kirusi.Ruby, endelea kufuatilia ile namba ambayo imewasiliana na Maurine tufahamu ni namba ya nani,” alisema Mathew wakiwa njiani kuelekea kwa Mwasi.

****

Kwa kufuata maelekezo waliyopewa,wakafika katika nyumba anayoishi Mwasi. Mtaa ulikuwa kimya sana, Gosu Gosu akampigia simu Mwasi kumjulisha kuwa tayari amefika.Mwasi akaufungua mlango wa sebuleni na kuchungulia nje.

“Yule pale!” alisema Gosu Gosu kisha akashuka garini na kuelekea katika mlango mdogo.Nyumba ilikuwa na uzio wa wavu na geti jeusi.

“Gosu Gosu, karibu sana!Kuna nini usiku huu?”Aliuliza Mwasi huku akilifungua geti.Ghafla akastuka baada ya akina Mathew kushuka garini.

“Wale ni akina nani?”Aliuliza kwa hofu.

“Usiogope!Ni wenzangu!” alisema Gosu Gosu.Mwasi akasalimiana na akina Mathew, akawakaribisha sebuleni,

“Mwasi, samahani sana kwa ujio huu wa usiku.Lakini tumekuja hapa kutaka msaada wako.Hawa hapa ni wenzangu tunafanya kazi pamoja hivyo usiwe na hofu hata kidogo!” alisema Gosu Gosu.

“Niwasaidie nini?”aliuliza Mwasi

“Tunataka kumpata Nicole.Ni wewe pekee unayeweza kutusaidia kumpata,” alisema Gosu Gosu.

“Nicole hajaonekana hapa nyumbani kama nilivyokueleza pindi uliponifuata kumuulizia.Hata simu hapigi.Wewe hukufanikiwa kuonana naye?” Mwasi alisema kwa sauti ya wasiwasi.

“Sikuonana naye.Ila nilifahamu watu anaoshirikiana nao si watu wazuri.Hivi tuzungumzavyo wanajiandaa kufanya kitu kibaya sana hapa Dar es Salaam,” alisema Gosu Gosu,sura ya Mwasi ikabadilika.

“Nicole anataka kufanya nini? Anashirikiana na akina nani?”Mfululizo wa maswali ulimtoka Mwasi.

“Nicole amejiunga na kundi la watu wabaya.Kuna jambo baya sana wanataka kulifanya hapa nchini hivyo basi tunataka utusaidie kumpata ili tuweze kuzuia hicho wanachotaka kukifanya kisifanikiwe,” alisema Gosu Gosu.

“Sijakuelewa, Gosu Gosu, unasema Nicole amejiunga na akina nani? Wanataka kufanya nini?”Aliuliza Mwasi

huku akishikwa vilivyo na mshangao.Mathew akainuka, akamfuata Mwasi alipo, akaketi pembeni yake.

“Sikiliza, Mwasi!Kuna kundi la watu ambao wanatumiwa na nchi za kigeni wanataka kusambaza kirusi hatari hapa nchini.Kirusi hicho kinasambaa kwa haraka sana na kuua watu wengi ndani ya muda mfupi.Nicole ni mmoja wa watu hao, hivyo tumekuja kwako utusaidie tuweze kujua mahala alipo ili tuweze kumfuata na kuzuia mpango huo.Maelfu ya watu wataangamia kama tutashindwa kukipata kirusi usiku wa leo.Kwa maana hiyo, chukua simu na umpigie mdogo wako mara moja tufahamu mahala alipo!”alisema Mathew kwa sauti ambayo ilimuogopesha

Mwasi,akajikuta tu anaachukua simu na kuuliza.

“Nimwambie nini?”

“Usimweleze chochote kuhusu haya niliyokueleza,bali mweleze kitu chochote kile kinachohusiana na familia.Hakikisha unamuweka katika laini ya simu kwa muda ili tuweze kujua mahali alipo,” alisema Mathew.

Huku mikono ikimtetemeka, Mwasi akampigia simu Nicole.Punde, ikapokelewa.Mwasi akaweka sauti kubwa ili kila mtu aweze kusikia.

“Hallow, Nicole!” alisema Mwasi.

“Mwasi, kuna nini usiku huu? Si kawaida yako kupiga simu usiku kama huu!”

“Nicole, uko wapi wewe? Nimepigiwa simu kuna tatizo limetokea usiku huu nikaona nikupigie nikujulishe!”

“Tatizo gani, Mwasi?” Nicole aliuliza akionekana kushtuka.Ghafla kupitia spika za simu, akamsikia Mwasi akilia.

“Mwasi, kuna nini?”Nicole aliuliza kwa kihoro, lakini bado Mwasi aliendelea kulia.

“Mwasi, tafadhali nieleze kuna nini?”

“Ni mjomba!” alisema Mwasi huku akiendelea kulia.

“Mjomba kafanya nini?”Aliuliza Nicole.Ruby akamfanyia ishara kuwa

bado sekunde kumi ili aweze kujua mahali alipo Nicole.

“Mwasi, mjomba kafanya nini?”

“Mjomba alikuwa anatoka Arusha kuja Dar es Salaam….” Mwasi akanyamaza na kuanza tena kulia.

“Mwasi, mjomba amefanya nini? *Is he okay*?”Aliuliza Nicole. Lakini Mwasi akaendelea kulia.

“Mwasi, ninakuuliza tena, mjomba kafanya nini?”Aliuliza Nicole.Mwasi akiwa ameyaelekeza macho yake kwa Ruby, akapewa ishara kuwa tayari kazi imemalizika.Mwasi akanyamaza.

“Nicole,mjomba alikuwa anatokea Arusha kuja Dar es Salaam,alipofika Korogwe, gari lake limegongana na gari la mizigo.Watu wanne wamefariki dunia

na yeye nimeambiwa hali yake ni mbaya,” alisema Mwasi.

“Dah! Pole sana Mwasi!Tumuombee mjomba aweze kupona.Mwasi, imekuwa vyema umenipigia nataka uanze kujiandaa kesho tunaondoka!”

“Tunaondoka?”Mwasi alishangaa

“Ndiyo!”

“Tunakwenda wapi?”

“Tutakuwa na safari ya nje ya nchi.”

“Nje ya nchi? Mbona mimi sina hati ya kusafiria?”aliuliza Mwasi

“Usihofu.Kila kitu kitafanyika.Nataka hadi kufika saa mbili asubuhi uwe umejiandaa nitakuja kukuchukua tuondoke.”

“Nicki ….”

“Mwasi,tutazungumza kesho nitakapokuja!” alisema Nicole na kukata simu.

“Mmefanikiwa kujua mahali alipo?”Aliuliza Mwasi.

“Ndiyo!” alijibu Ruby.

“Good job, Mwasi!Unaweza sana kuigiza!”alisema Mathew.

“Nataka mniambie nini kitamtokea mdogo wangu?”

“Kwanza tunataka kukipata kirusi kwa haraka sana kabla hawajakisambaza.Vilevile kuwakamata wahusika wote walioshiriki katika mpango huo na kuwafikisha sehemu husika,” alisema Mathew.

“Jamani naombeni mnisaidie msimfikishe Nicki katika vyombo vya

sheria.Nimewasaidia kujua mahali alipo na pale mtakapokipata kirusi mnachokitafuta muachieni aende,”alisema Mwasi kwa huruma.

“Ndugu yako ni muuaji.Ana roho mbaya zaidi ya shetani.Kirusi anachoshiriki kutaka kukisambaza kinaweza kuua maelfu ya watu ndiyo maana amekutaka ujiandae ili muweze kuondoka nchini hiyo kesho.Hastahili huruma hata kidogo.”alisema Mathew na kumfuata Ruby wakazungumza kidogo kisha Mathew akasema

“*Guys we need to go*!”

“*What about her*?”Aliuliza Ruby akimaanisha Mwasi.

“*She’s coming with us*!”alisema Mathew,Agai akamchukua

Mwasi,akampeleka garini.Wakaondoka naye.

****

Walikaribia kufika katika nyumba ambayo Nicole alikuwemo wakati akizungumza na dada yake Mwasi.Gari likasimamishwa.

“Kutokea hapa,tutakwenda kwa miguu.Ruby utabaki garini na Mwasi,” alisema Mathew huku akifungua droo ya gari na kutoa kisanduku kidogo,akakifungua na kuchukua kifaa kidogo akakiweka sikioni kwa ajili ya mawasiliano. Gosu Gosu na Agai nao kila mmoja akapewa kifaa kile.Ruby akaweka program ya mawasiliano katika

kompyuta yake, wakajaribu vifaa vyao vilikuwa vinafanya kazi vizuri kabisa.

“*Guys*, kwa namna yoyote ile lazima tukipate kirusi!”alisema Mathew kisha wakashuka garini na kuanza kutembea kwa miguu kuelekea katika nyumba aliyokuwemo Nicole na wenzake.Mtaa ulikuwa kimya kabisa.Walikaribia kufika katika nyumba ile ghafla geti likafunguliwa Mathew na wenzake wakarukia mtaroni.Gari moja likatoka kisha geti likafungwa tena.

Akina Mathew walitoka mtaroni,wakanyata na kulisogelea geti.Mathew akawapa ishara Gosu Gosu na Agai kila mmoja azunguke upande mwingine.Akang’oa matofali ambayo yalikuwa katika bustani ya majani,

akayapanga halafu akapanda na kushika kingo za ukuta.Akachungulia ndani, akayaona magari mawili na watu watatu wamekaa wanazungumza huku mmoja wao akichambua kitu kilichoonekana kama bangi.

“Watatu upande wa mbele!” Mathew aliwaeleza wenzake .

“Hakuna kitu upande wa nyuma!” alisema Gosu Gosu.

“Wawili upande wa kulia!”alisemaAgai.

“Gosu Gosu, tangulia ndani na uwaondoe hawa jamaa huku mbele ili nami niweze kupata nafasi ya kuingia,” alisema Mathew.

Gosu Gosu akarukia ndani kwa kupitia upande wa nyuma wa ile nyumba

ambako hakukuwa na mlinzi yeyote.Akaokota tofali, akalirusha.Wale jamaa wawili waliokuwa upande wa mashariki mwa ile nyumba, wakashtuka na kuelekea upande wa nyuma kuangalia kuna nini.

Gosu Gosu aliyekuwa amejibanza nyuma ya ukuta wa tanki la maji hakuwakawiza.Kwa kutumia bastola yake yenye kiwambo cha kuzuia sauti, akawatawanya ubongo kwa risasi halafu akawavuta akawaficha mahali alipokuwa amejificha.

"*It's clear*,Agai unaweza kuingia!" alisema Gosu Gosu.Agai akarukia ndani,akaungana na Gosu Gosu.Wale jamaa waliokuwa mbele ya nyumba hawakuwa na habari na kile kilichokuwa

kinaendelea nyuma ya ile nyumba. Ghafla wakajikuta wamevamiwa na akina Gosu Gosu.Hakukuwa na mahojiano wote wakatangulizwa mbele za haki.

Mathew akaingia ndani kuungana na wenzake.Tayari eneo lote la nje walikuwa wanalidhibiti.Kutokea nje,waliweza kusikia sauti za watu ndani wakizungumza na kucheka.

“Tutakachokifanya,tunawasha moto katika gari moja.Wote waliomo ndani watatoka nje kuja kutazama nini kimetokea!” alisema Mathew.Agai akavua fulana yake, akaifunga katika kijiti.Akafungua kifuniko cha mafuta katika moja ya magari yaliyokuwapo

ndani ya ile nyumba, akaichovya ile fulana katika mafuta.

Mathew akawapekua wale jamaa na kuchukua kiberiti, akampa Agai.Akaiwasha ile fulana yake na kuiweka chini ya moja ya gari kisha, wakajificha.Moto ulianza kuwaka kwa kasi. Ghafla mlango mkubwa ukafunguliwa, wakatoka watu wanne haraka haraka wanaume wawili na wanawake wawili kwa kujua kile kilichotokea.

“Ahsante,Mathew, kwa wazo hili.Kweli bwana wametoka wote.Ninawaona Nicki,Maurine Kyaso na Joseph Nahimana.Yule mwingine simfahamu ni nani,” alisema Gosu Gosu.

“Chesko!”aliita Maurine kwa nguvu, lakini hakujibiwa.

“Chesko!” akaita tena lakini hakuna mtu aliyejitokeza.Moto nao ulizidi kukolea.Maurine akatoa bastola na kuwapigia kelele akina Joseph.

“*Get inside it’s a trap*!”

Wenzake waliokuwa nje wakabaki wanamshangaa Maurine kwa tahadhari ile hawakumwelewa.

“*Get inside now*!”alifoka Maurine, lakini kabla hawajapiga hatua moja, tayari Mathew na wenzake walikwisha jitokeza.Joseph Nahimana akatoa bastola haraka haraka,lakini Mathew alikuwa mwepesi zaidi yake, akamuwahi kwa kumpiga risasi ya bega la kulia, akaanguka chini.Licha ya kupigwa

risasi,Joseph aligeuka haraka na kwa kutumia mkono wake wa kushoto,akaiokota bastola yake iliyoanguka karibu yake akaachia risasi kadhaa kumuelekea Mathew.

Mathew ambaye jicho lake liligeuka kama kinyonga, alishang'amua kile alichokuwa amekusudia kukifanya Joseph. Alijirusha na kubiringika hadi nyuma ya gari lililokuwa linawaka moto.Joseph akajitahidi kunyanyuka ili aweze kukimbia mara Mathew akajitokeza.

"Joseph, stop!"alisema Mathew kwa kufoka.Joseph akageuka kwa lengo la kukabiliana na Mathew, lakini kabla jicho lake halijamuona,risasi mfululizo kutoka katika bastola ya Mathew

zikampata, akaanguka chini.Yule jamaa mwingine ambaye alikuwa na akina Maurine, naye alikuwa amelala chini damu zikimvuja.Dhahiri hakuwa na uhai.Mathew akamfuata Joseph, akamgeuza.Alikuwa anakoroma.

“Joseph, unanisikia?”Aliuliza Mathew.Muda huo huo Joseph akakata roho.Mathew akamfuata yule jamaa mwingine, akamgeuza naye hakuwa na uhai.Mara akatokea Agai akiwa amemtanguliza Nicole ambaye alikuwa anatiririkwa damu usoni

“Muingize ndani!” alisema Mathew kisha akazunguka upande wa nyuma akamkuta Gosu Gosu tayari alikwisha mdhibiti Maurine Kyaso.Hakuwa

anatazamika kwa kipigo alichopewa na Gosu Gosu.

“*Good job, Gosu Gosu!*” alisema Mathew huku akimuinua Maurine.Wakampeleka sebuleni, akaungana na Nicole.

“Kirusi lazima kimo ndani ya nyumba hii.Tafuteni kila mahali” alielekeza Mathew.Gosu Gosu na Agai wakaanza upekuzi. Mathew akampigia simu Ruby,akamtaka aje pale ndani kwani tayari wamekwisha wapata akina Maurine.

Gosu Gosu na Agai wakaingia vyumbani na kuanza kutafuta sanduku lenye kirusi.Baada ya muda wakarejea.

“Hakuna dalili zozote za kuwepo kwa sanduku lenye kirusi mahali hapa,”

alisema Gosu Gosu.Kwa hasira,Mathew akatoa bastola na kumfuata Maurine.

“*Where is the virus*?”Aliuliza kwa ukali.Maurine akatema mate chini kisha akasema.

“Sifahamu unachokizungumza!”

“Maurine, nakuuliza kwa mara nyingine tena.Kirusi kiko wapi?”

“Sifahamu!”alijibu Maurine. Mathew akamfuata Nicole.

“Kirusi kiko wapi?”Aliuliza Mathew,badala yake, Nicole akamtemea mate.Mathew akainua mkono kutaka kumtandika kofi Nicole ,ghafla akasikia sauti ya mtu ikiita.

“Nicole!” ilikuwa sauti ya Mwasi.Nicole akapatwa na mshangao mkubwa.Hakuyaamini macho yake.

“Mwasi?” Nicole alisema kwa mshangao.

“Nicole, ni nini hiki unakifanya?” aliuliza Mwasi na kuanza kulia.

“Nicole, nakuuliza kwa mara nyingine tena kirusi kiko wapi?”Aliuliza Mathew.

“Shetani wewe.Dada yangu anafanya nini hapa?”Nicole alifoka kwa ukali.Akataka kuinuka, lakini Gosu Gosu akamnasa kofi zito, akaanguka chini.

“Jamani msimuumize mdogo wangu!”alisema Mwasi kwa kihoro.Mathew akamfuata, akamshika mkono na kumtoa nje.

“Mwasi, sikiliza.Tumewapata wahusika, lakini kirusi hakipo hapa.Tunataka kufahamu mahala

kilipo.Nataka ukazungumze na mdogo wako jaribu kumshawishi akubali kusema mahala kilipo," alisema Mathew.

"Siwezi jamani.Hapa nilipo mwili wote unanitetemeka!" alisema Mwasi.

"Usihofu utaweza.Tunatakiwa kufanya kila tuwezalo kukipata kirusi,kwani kunakaribia mapambazuko.Hawa watu wawili mle ndani wanafahamu mahala kilipo ndiyo maana ninakuomba ukazungumze na mdogo wako ili akueleze mahali kilipo," alisema Mathew kwa upole na kurejea ndani.Akawapa maelekezo akina Gosu Gosu, wakamchukua Nicole na kumpeleka katika chumba kimojawapo.Wakamfunga katika kiti

halafu akaingizwa Mwasi.Akamtazama mdogo wake na kufuta machozi.

“Kwa nini unafanya haya, Nicole? Nini kimekuingiza katika mambo haya?”Aliuliza Mwasi huku akifuta machozi. Nicole akainua kichwa, akamtazama dada yake na kuuliza.

“Wamekwambia nini hawa jamaa? Umekutana nao wapi?”

“Nicole, tayari ninafahamu kila kitu unachokifanya!”alisema Mwasi.Nicole akamtazama dadaye kwa hasira kisha akasema kwa sauti ya lawama.

“Kumbe ni wewe uliyewasaidia hadi wakajua mahala nilipo.Ile simu uliyonipigia haikuwa na ukweli wowote ulikuwa ni mtego.Kwa nini umefanya hivi, Mwasi? Wamekupa kiasi gani hadi

ukamsaliti ndugu yako wa damu? *I hate you* Mwasi!.Nikifanikiwa kutoka hapa, ninaapa nitakuua!”alisema Nicole kwa hasira.

“Nicole, tafadhali, waeleze hawa watu mahala kilipo kirusi ambacho mnataka kukisambaza.Utapata faida gani kama kirusi hicho kitasambaa?Watu wengi watapoteza maisha wakiwamo ndugu zako.Kwa nini unafanya haya Nicole?”aliuliza Mwasi

“Mwasi, nimesema toka nje!”Alifoka Nicole.

Wakati Mwasi akijaribu kumshawishi Nicole kueleza mahala kilipo kirusi,Mathew alikuwa akiendelea kumuhoji Maurine Kyaso, lakini hakuthubutu kufunguka mahala kilipo.

“Maurine, tayari tunafahamu kila kitu.Mmejiandaa kuondoka kesho baada ya kusambaza kirusi.Mipango yenu yote tunaijua na ninataka kukuhakikishia kwamba hamtaondoka tena na kama ni kufa,basi tutakufa wote.Ninakueleza kwa yakini pale watu watakapoanza kuumwa,mimi mwenyewe kwa mikono yangu nitakuingiza katika wodi ya wagonjwa hao ili upate maambukizi na ufe kwa mateso kama wengine.Maurine, maelfu ya watu wataambukizwa na hatimaye kufa.Akina mama,watoto wadogo,wazee na sisi sote tutakuwa katika hatari kubwa kwani hakuna kinga ya kirusi hicho.Bado tunao muda wa kuiepusha nchi yetu dhidi ya janga hilo kubwa.Nataka unioneshe wapi kilipo

kirusi?” Mathew aliendelea kumbembeleza Maurine. Sura ya Maurine haikuwa hata na punje ya kujali maneno ya Mathew.

“*You think I’m scared? I’m not.I’m ready to die*!”alisema Maurine.Mathew akamtazama kwa makini halafu akasema.

“No,Maurine!You are not ready to die!”

“Mathew Mulumbi, *you’ve lost*.Huwezi kuwa shujaa katika hili!”alisema Maurine bila woga.

“Nini kimekuingiaMaurine hadi ukawa na roho mbaya kiasi hiki?Kwa nini unataka kuwaua ndugu zako?”Mathew aliuliza kwa masikitiko, lakini Maurine hakujibu kitu.

Nje Moto ulizidi kuwa mkubwa.Magari mawili tayari yalikuwa yanaungua, hivyo ikawalazimu majirani kupiga simu kikosi cha zimamoto ili wafike haraka sana eneo lile.Ving'ora vya magari ya zimamoto vikasikika nje ya ile nyumba.Gosu Gosu akamfuata Mathew, akamjulisha kuwa magari ya zimamoto yamefika.

"Nenda kawazuie wasiingie ndani hadi pale tutakapomaliza kazi yetu.Magari yale yako mbali na nyumba na hayataweza kuleta madhara yoyote.Hatutaki kuingiliwa katika kazi!"alisema Mathew.Gosu Gosu akatoka kwenda kuzungumza na wale jamaa kutoka katika kikosi cha zimamoto wakamuelewa.

“Maurine, muda unakwenda sana.Nitakuuliza kwa mara ya mwisho. Ni wapi kilipo kirusi?”

“Unapoteza muda wako bure Mathew Mulumbi.Siogopi kufa.*All I want is Tanzania to pay*!”

“*Pay for what*?”Mathew aliuliza kwa ukali.

“Unataka Tanzania ilipie nini?”Mathew aliuliza tena, lakini Maurine akawa kimya.Mathew akasimama.

“Maurine, hujawahi kukutana na mimi nikiwa katika harakati za ulinzi wa taifa.Mimi ni mtu mbaya sana ukinikuta katika sehemu hiyo.Sina ubinadamu hata kidogo kwa watu weye roho za kishetani kama wewe,Maurine.*For the very last*

time where is the virus?”Mathew alisema huku akiuma meno.Maurine akamtazama kwa jicho la dharau halafu akasema.

“Siogopi sura ya shetani sembuse wewe Mathew Mulumbi! Hunitishi kwa chochote!” alisema Maurine.Mathew akamtazama kwa muda kisha akasema.

“*Fine*”

Mathew akaenda katika chumba ambacho Mwasi alikuwa anazungumza na Nicole, akaufungua mlango, akaingia ndani.Akamkuta Mwasi akilia.

“Amekueleza chochote huyu?”Aliuliza Mathew.

“Hapana!Hajasema chochote,” alijibu Mwasi.Mathew akamfuata Nicole alipo.

“Nicole, ninakuuliza kwa mara ya mwisho kirusi kiko wapi?”Kwa jeuri,Nicoleakamtazama Mathew kisha akamtemea mate usoni.Mathew akayafuta,akamuinua na kumtoa nje

“Mnampeleka wapi?”Mwasi aliuliza kwa kihoro,lakini Mathew hakumjibu kitu.Akamuelekeza Agai kumfungia Mwasi ndani ya kile chumba.Kama haitoshi, akamuelekeza Gosu Gosu amtoe nje Maurine.

“Ninawauliza kwa mara ya mwisho kabisa, wapi kilipo kirusi?”Mathew alisema akiwa kakunja ndita lakini hakuna aliyemjibu.Mathew akamkamata Nicole na kumvuta kuelekea katika magari yanayoungua.

“Nicole, hii ni mara ya mwisho ninakuuliza.Kirusi kiko wapi?”aliuliza Mathew.

*“Go ahead kill me!”*alisema Nicole.Mathew akafanya kitu ambacho hakuna aliyekitarajia.Alimuinua Nicole na kumrusha katika moto ule mkali.Pingu za plastiki alizokuwa amefungwa Nicole, zikaungua.Akakurupuka akikimbia huku akipiga kelele,mavazi yake yote yakiwaka moto.Gosu Gosu akamkimbilia,akamdaka na kumrushia katika bwawa la kuogelea.Moto ukazima,akamtoa nje. Tayari alikwisha ungua vibaya sana. Yowe la uchungu likamtawala Nicole.Mathew hakumjali akamfuata Maurine.

“*It’s your turn.Where is the virus?*”Mathew aliuliza. Maurine akabaki kimya.

“*Again, where is the virus?*Mathew aliendelea kuunguruma. Lakini haikusaidia.Maurine hakujibu kitu.Machozi yalianza kumtoka.

“*For the last time,where is the virus?”*Aliuliza Mathew huku akimvuta Maurine kuelekea katika ule moto.Akamuinua ili aweze kumrusha kama alivyofanya kwa Nicole. Maurine akapiga yowe.

“Nitakwambia! Nitakwambia!”

Mathew akamtupa chini.Akamtazama kwa hasira.

“Tafadhali usinitupe katika moto.Nitasema ukweli!”alisema kwa kihoro, Maurine.

“Where is the virus?”Mathew aliuliza

“Kirusi hakipo hapa!” alijibu Maurine huku akitetemeka.

“Kiko wapi?”

“Kituo cha treni ya umeme!”

“Kina kwenda wapi? Nani amekibeba?”

“Mtu mwenye sanduku lenye kirusi hajui kama sanduku alilobeba lina kirusi.Amedanganywa alipeleke sanduku hilo Morogoro ambako atamkabidhi mtu ambaye watakutana kituoni,”alijibu Maurine.

“Nani atakutana na huyo mtu Morogoro?”Mathew aliuliza

“Hakuna mtu yoyote wa kukutana naye.Tulimueleza hivyo ili asijue kama amebeba kirusi!”

“Nini sababu ya kumda nganya?”

“Lengo ni kukisambaza kirusi hicho katika stesheni ya treni ya umeme.Treni ya kwanza huondoka saa kumi na moja alfajiri kwenda Dodoma na wakati huo huwa kunakuwa na watu wengi sana kituoni hapo.Muda tuliouweka utakapofika,kompyuta yetu italifungua sanduku lenye kirusi na kitaanza kusambaa kwa njia ya hewa kuanzia hapo stesheni hadi Morogoro.”

“Huyo mtu aliyebeba sanduku anaitwa nani na amevaaje?”Mathew aliuliza

“Anaitwa Dastan.Kichwani ana rasta na amevaa suruali ya *jeans* ya bluu,fulana nyeupe na kofia nyeupe ya mduara.”alijibu Maurine

“Una namba yake ya simu?”Mathew aliuliza

“Hana simu.Tumeichukua ili asiweze kuwasiliana na mtu yeyote!”

Mathew akapandwa na hasira.Akamvurumishia Maurine makonde mfululizo kisha akamchukua na kumuingiza ndani.

“Nataka utuoneshe namna mnavyomfuatilia huyo mtu mliyempa sanduku lenye kirusi,” alisema

Mathew.Maurine akawaelekeza.Katika kompyuta ilionesha yule mtu mwenye kirusi tayari alikwishafika katika stesheni ya treni ya umeme.Gosu Gosu aliitambua diski iliyokuwa katika kompyuta ile ya Maurine kuwa ni ile aliyoitoa katika paja la Fabrice Kayembe

“Zimebaki dakika thelathini chombo hicho kifunguke ndani ya sanduku na kirusi kuanza kusambaa.Ruby, hakuna namna yoyote unaweza ukaizima program hii ili kuzuia sanduku kufunguka?Aliuliza Mathew.Ruby akaitazama program ile halafu akasema.

“I can give it a try!”

“Ruby utabaki hapa mimi,Agai na Gosu Gosu tunakwenda kumfuatilia huyo jamaa kuhakikisha tunakipata

kirusi hicho kabla hakijaanza kusambaa," Alisema Mathew.Wakamchukua Maurine, wakaondoka naye kuelekea katika stesheni kuu ya treni ya umeme.Gosu Gosu aliendesha gari kwa mwendo mkali mno.

"Maurine, kwa nini lakini ukafanya haya uliyoyafanya? Uliaminiwa na kupewa nafasi kubwa na nyeti,badala ya kuwatumikia Watanzania na kuhakikisha wanakuwa salama,badala yake umewasaliti na kutaka kuwaangamiza tena kwa maelfu.Nini sababu ya kufanya haya?"Aliuliza Mathew.Maurine akabaki kimya.

"Nchi zetu zinaendelea kuwa masikini,zinaendelea kunyonywa na mabeberu kwa sababu ya watu kama

ninyi.Ndugu zenu wote wako huku Afrika, lakini mnadanganywa na mabeberu na unakubali kuwaua ndugu zako ili uweze kupata maisha bora katika nchi zao.Unadhani kirusi hicho kisingeweza kufika katika nchi waliko? Mnajidanganya sana ninyi watu!”alisema Mathew huku akimtazama Maurine kwa hasira.

“Bado mimi nawe tutazugumza zaidi baada ya kukipata kirusi!” alisema Mathew akiuma meno kwa hasira.

****

Waliwasili katika kituo cha treni ya umeme.Zilibaki dakika kumi na sita itimu saa kumi na moja alfajiri, muda

ambao treni ya kwanza huondoka kuelekea Dodoma.Mathew akamweleza Agai abaki garini akimlinda Maurine,yeye na Gosu Gosu wakaingia ndani.Moja kwa moja wakaelekea katika kituo kidogo cha polisi stesheni hapo.Walifanikiwa kuonana na mkuu wa kituo.

“Afande, ninaitwa Mathew Mulumbi.Ni mkurugenzi wa Shirika la Ujasusi Tanzania,” alisema Mathew.Mkuu wa kituo akamtazama kwa makini kuanzia juu mpaka chini kisha akatoa kicheko kidogo.

“Mbona hufananii na hicho unachokisema?”Aliuliza mkuu wa kituo.Mathew akakunja ndita.

“Afande,kuna jambo kubwa la kiusalama limetuleta hapa.Naomba unisikilize tafadhali” alisema Mathew.

“Kitambulisho chako kiko wapi?”Aliuliza mkuu wa kituo.

“Afande, hatuna muda wa vitambulisho.Tumekuja hapa kwako kutaka msaada.Kuna mtu yuko hapa kituoni amebeba sanduku ambalo ndani yake kuna kirusi hatari.Ni kirusi kinachosambaa kwa njia ya hewa.Tunaomba msaada wako afande tunataka tulipate sanduku hilo lenye kirusi!” alisema Mathew.Mkuu wa kituo akatoa kicheko kingine, tena cha kebehi.

“Umesema kuna kirusi hapa stesheni? Ninyi ni watu wa ajabu sana.Unakuja hapa unadai ni mkuu wa

Shirika la UjasusiTanzania.Huna kitambulisho halafu unaleta mambo ya kirusi!”alisema mkuu wa kituo.Mathew akamtazama kwa hasira.

“Afande,naomba umpigie mkuu wako wa jeshi la polisi ananifahamu vyema!” alisema Mathew.

“Siwezi kupoteza muda na watu kama ninyi.Hebu naomba muondoke hapa haraka sana ama nitawaweka ndani!”alifoka mkuu wa kituo

“Gosu Gosu, nipatie simu yako” alisema Mathew.Akatafuta namba ya Ruby na kumwendea hewani.

“Ruby, kuna mafanikio yoyote hadi sasa?”

“Bado sijafanikiwa ila ninaendelea.Tayari mmefika kituoni?”

“Ruby, nataka ndani ya dakika mbili umpigie simu Rais na umweleze kuwa kirusi kiko hapa stesheni ya treni ya umeme na tuko katika ofisi ya mkuu wa kituo mwenye namba hizi,” Mathew alimtajia Ruby namba za mkuu wa kituo huku akisikia.

“Mweleze Rais kuwa huyu mkuu wa kituo amegoma kutoa ushirikiano ili tuweze kukipata kirusi hicho.Ndani ya dakika mbili kama hatakuwa ametoa ushirikiano nitakujulisha ili uwasiliane na Rais,” alisema Mathew.Mkuu wa kituo akashtuka.Akashikwa na mtanziko.

“Ndugu ni kweli hayo unayosema kuwa kuna kirusi hapa stesheni?”Aliuliza kwa sauti ya kihoro. Wingu la hofu limetanda kichwani mwake.

“Kwa nini unashindwa kuniamini,Afande? Subiri upokee maelekezo kutoka kwa Rais mwenyewe!” alisema Mathew.Kwa hofu, mkuu wa kituo akasimama.

“Ndugu zangu haya mambo hayapaswi kufika kwa Rais.Hebu nielezeni kuhusu hicho kirusi!”

“Afande hatuna muda wa kueleza.Kinachotakiwa ni kuchukua hatua za haraka sana za kuhakikisha tuna lipata sanduku haraka sana,” alisema Mathew huku akiitazama saa yake.

“Muda unakimbia afande.Utatusaidia kulipata sanduku au utasubiri maelekezo kutoka kwa Rais mwenyewe?Naomba ufahamu kuwa

endapo kirusi kitasambaa hakuna atakayepona hapa," alisema Mathew.

"Nini mnakihitaji niwasaidie?"Aliuliza mkuu wa kituo.

"Kwanza kabisa,tunataka kuzuia treni isiondoke.Pili,watu wote wanatakiwa kutoka nje mmoja mmoja kwa kupitia mlango mkuu wa kuingilia ili tuweze kumpata huyo jamaa aliyebeba kirusi," alisema Mathew kisha wakatoka wakikimbia mbio kuelekea katika ofisi ya mkuu wa stesheni.Watu walibaki wanajiuliza kumetokea nini.

Waliingia katika ofisi ya mkuu wa stesheni,bila kupoteza muda, mkuu wa kituo cha polisi akamtaka mkuu wa stesheni kuzuia treni kuondoka hadi hapo atakapopewa maelekezo mengine.Mkuu

wa stesheni akapiga simu haraka kuzuia treni isiondoke.Papo hapo ikapigwa kengele ya dharura, watu wote wakatangaziwa kuingia ndani ya nyumba ya abiria.Huko ikaamriwa watoke nje mmoja mmoja kupitia mlango mkuu wa kuingilia ndani.Askari waliuzunguka mlango huku akina Mathew wakiwa macho kuangalia kila anayetoka.Mara akatoka mtu ambaye alifanana na yule aliyemtaja Maurine.Alikuwa na rasta,suruali ya *jeans* rangi ya bluu,fulana nyeupe na kofia.

"*That's him*!"alisema Mathew.Askari wakamsogelea na kumtia nguvuni.Mathew akamfuata mkuu wa kituo, akamnong'oneza.

“Afande,hawa watu wote wakae mbali kabisa na mahali hapa. Ila tu,asiondoke hata mtu mmoja kwa ajili ya tahadhari endapo kirusi kitakuwa tayari kimesambaa ili wasiweze kwenda kuwaambukiza watu wengine.Njia zote za kuingia na kutoka hapa stesheni zifungwe.Asiruhusiwe mtu kuingia tena wala kutoka!”alielekeza Mathew.Mkuu wa kituo akatoa maelekezo kwa askari wake, wakaanza kuwakusanya watu mbali kidogo na stesheni huku wakihakikisha hakuna hata mmoja anayeondoka.

“Nimefanya nini?”Aliuliza yule jamaa.

“Sanduku lako liko wapi?”Mathew aliuliza.

“Liko ndani ya treni!”

“Twende haraka ukatuoneshe!” alisema Mathew kisha wakaanza kukimbia pamoja na mkuu wa kituo hadi ndani ya treni.Wakafika sehemu ambayo yule jamaa aliliweka sanduku.Akawaonesha.

“Oh thank you lord!”alisema Mathew na kushusha pumzi.

“Una hakika ni hili ?”Aliuliza mkuu wa kituo huku wajihi wake ukijawa na hadhari kubwa.

“Ndiyo.Ni hili!” akajibu yule jamaa.

“Nini kinafuata baada ya kulipata?”Mkuu wa kituo alihoji.

Mathew akalifungua sanduku,katikati ya nguo akakuta kuna kisanduku kidogo ambacho kilikuwa na

kifaa kama saa kwa chini ikiwaka kwa rangi nyekundu.Akawataka watu wote watoke nje, akabaki yeye na Gosu Gosu tu.

“*8 minutes left.Call Ruby*!”alisema Mathew.Upesi Gosu Gosu akampigia simu Ruby kisha akamkabidhi Mathew simu azungumze naye.

“Ruby,tumekipata kirusi, lakini kuna dakika nane tu zimebaki kuweza kusambaa.Umefikia wapi katika kuisimamisha hii program yake?”Mathew alisema akihema.

“Umetumika utaalamu wa hali ya juu sana katika kutengeneza program hii. Hata hivyo,ninajitahidi.Naomba unipe muda kidogo,” alisema Ruby.

“Ruby,*it’s only 8 minutes left*.Jitahidi ama sivyo tutaangamia sote!”alisema Mathew.

“Mathew, nawashauri mliache sanduku hilo na msogee mbali na hapo endapo nitashindwa kufanikiwa kuisimamisha programu hii.”

“Ruby,*I’m not going anywhere*.Kama kirusi hiki kitafunguka na kusambaa,napaswa kuwa wa kwanza kufa.Siwezi kuishi na kushuhudia watu wakiangamizwa na kirusi hiki.*So stop talking and save us!*”Alisema Mathew na kukata simu.

“Mathew,*are you sure you want to do this?*”Aliuliza Gosu Gosu baada ya kubaki dakika tatu.

“Gosu Gosu, tafadhali ondoka muda unakwenda zimebaki dakika chache kirusi kisambae,” alisema Mathew.

“Mathew,*I’m not going anywhere.I’m staying!”*alisema Gosu Gosu.

“Gosu Gosu!Please go now!”alisema kwa sauti kali Mathew.

“Hapana,Mathew!Siwezi kuondoka.*I trust Ruby she won’t let us die*.Lazima atafanya kila awezalo kuhakikisha anaisimamisha program hii!”Alisema Gosu Gosu ikiwa imebaki dakika moja na sekunde ishirini tu.

“*C’mon*,Ruby fanya maajabu yako!”alisema Mathew kwa sauti ndogo akiwa ameiweka mikono kifuani.

Sekunde zilibaki arobaini.

“*Don’t let us die*,Ruby!”alisema Mathew lakini bado sekunde ziliendelea kuhesabu haraka haraka zikabaki kumi, hatimaye nane, mwisho tano.

“Hatuna namna, Gosu Gosu nadhani muda wetu umefika!”Alisema Mathew zikiwa zimebaki sekunde tatu.Ghafla kukatokea mlio,saa ikasimama.Mathew akakishika kisanduku na kukitazama huku akihema na jasho likimtiririka.

“*She did it! She did it*!”alisema Mathew kwa furaha na kumkumbatia Gosu Gosu.

“Nilijua tu,Ruby ni mchawi wa teknolojia!”alisema Mathew.Punde simu ya Gosu Gosu ikaita. Kutazama, alikuwa ni Ruby.

“Ruby, ahsante kwa kuyaokoa maisha yetu! Tunakuja huko.Tutazungumza zaidi,”alisema Mathew na kukata simu.Wakatoka na kumfuata mkuu wa kituo aliyekuwa nje ya jengo la abiria.

“Tumefanikiwa kuisimamisha program ya kukisambaza kirusi.Kila kitu ni shwari sasa.Safari inaweza kuendelea,” alisema Mathew ambaye alikuwa ameloa jasho.

“Una hakika kirusi hakijasambaa?”Mkuu wa kituo aliuliza kwa hofu.

“Hapana!Hakijasambaa hata kidogo.Kila kitu kiendelee kama kawaida,” alisema Mathew.

“Yule jamaa aliyekuwa na sanduku hili yuko wapi?”Mathew akauliza.

‘Tumemuweka mahabusu!”

“Good.Ninataka kuzungumza naye!” alisema Mathew.Wakaelekea katika mahabusu alikowekwa,akatolewa na kuingizwa katika ofisi ya mkuu wa kituo.

“Ndugu zangu kuna nini?”Aliuliza jamaa aliyebeba sanduku lenye kirusi huku akiwa na wasiwasi mwingi.

“Unaitwa nani ?”Mathew aliuliza.

“Dastan Mbega!”

“Unafanya kazi wapi, Dastan?”

“Kwani kuna nini ndugu zangu?”

“Jibu swali haraka unafanya kazi gani?”Alidakia mkuu wa kituo.

“Mimi ni fundi wa kutengeneza masofa.”

“Unamfahamu Maurine Kyaso?”Mathew aliuliza

“Maurine?”Dastan aliuliza kwa mshangao.

“Ndiyo.Unamfahamu?”

“Namfahamu!” alijibu Dastan. Ghafla akaingia mmoja wa askari, akampa taarifa mkuu wa kituo.

“Vijana wameangalia katika mtandao wetu.Huyu jamaa ni mhalifu sugu.Amekuwa akitafutwa kwa muda mrefu na jeshi la polisi kwa makosa ya ujambazi wa kutumia silaha.Hatimaye leo amepatikana!”alisema mkuu wa kituo.

“Unafahamu kitu ulichokuwa umekibeba ndani ya sanduku hili?”Mathew akamuuliza Dastan.

“Hapana!” alijibu Dastan.

“Ulibeba kirusi hatari.Laiti kama tusingewahi, basi wewe na sisi wote hapa tungepata maambuziki na hatimaye kupoteza maisha.Kirusi hicho kinaua ndani ya muda mfupi. Kama haitoshi,kinasambaa kwa njia ya hewa!” alisema Mathew huku akimtazama Dastan kwa hasira..

Mathew alimuhoji Dastan,akakiri kuwa ni wao waliovamia magari mawili na kuua watu wote waliokuwamo ndani yake kisha wakaondoka na sanduku ambalo hawakujua kama lina kirusi.Walifanya hivyo kwa maelekezo

ya Maurine.Aliwapa ahadi ya kuwalipa fedha nyingi.Baada ya kuridhika na maelezo aliyoyatoa Dastan,Mathew akamkabidhi kwa jeshi la polisi.

“Nakushukuru sana ndugu Mathew na wenzako kwa kutuokoa.Bila ninyi sijui nini kingetokea!” alisema mkuu wa kituo.Mathew akampatia mkono,wakaagana wakaondoka

****

Akina Mathew walirejea mahala walikomuacha Ruby.Tayari moto ulishazimwa.Askari polisi walikuwepo eneo la tukio, kwa minajili ya uchunguzi wa mauaji yale yaliyotokea.Miili ya

Joseph na mtu mwingine ambaye hakufahamika ilichukuliwa na kupelekwa hospitali.

Mathew akajitambulisha kwa askari,akawaeleza kuwa bado walikuwa wakiendelea na operesheni eneo lile.Wakaaingia ndani na kuelekea sebuleni ambako Ruby alikuwa anaendelea na kazi.Alipomuona Mathew, akasimama na kumkumbatia.

“Hongereni sana kwa kazi kubwa mliyoifanya hadi mmefanikiwa kukipata kirusi!” alisema Ruby huku akitirikwa na machozi ya furaha.

“Ruby, wewe ndiye umefanya kazi kubwa.Hakuna namna tunayoweza kukupongeza kwa kazi nzuri uliyoifanya.Y*ou saved the country and*

the whole world!” alisema Mathew akisindikiza na tabasamu jepesi.

“Ahsante,Mathew.Nicole amepelekwa hospitali.Hali yake si nzuri.Tukiachana na hayo,kuna jambo lingine nimelipata.Tuligundua Maurine kwa kutumia ile simu ya satelaiti aliwasiliana na watu wawili usiku huu.Mmoja wao alikuwa Nicole, lakini mwingine tulishindwa kumtambua.Nimegundua namba ile ni ya Rais wa Burundi!”

“Rais wa Burundi?”Mathew alimaka.

“Ndiyo.Namba ile ni ya Didier Manirakiza ambaye ni Rais wa Burundi.Inaonesha kuwa Rais Manirakiza ndiye aliyempigia Maurine,”

alisema Ruby.Mathew akageuka kumtazama Maurine ambaye aliinamisha kichwa.

“Ruby,kazi nzuri sana.Kitu cha kufanya kwa sasa ni kuharibu kabisa program ya kuliongoza hili sanduku ili asitokee tena mtu mwingine yeyote wa kutaka kuhatarisha usalama wa nchi hii na dunia.Kirusi hiki kitakwenda kuwekwa mbali kabisa mahala pa siri ambako hakuna mtu atapafahamu.Kabla ya hapo, nahitaji kuzungumza na Rais!” alisema Mathew.Ruby akampigia simu Rais.

“Ruby, mnaendeleaje?”Aliuliza Rais baada ya kupokea simu.

“Mheshimiwa Rais, zungumza na Mathew.”

“Mheshimiwa Rais,Mathew hapa!”

“Mathew,sijafunga jicho nikisubiri kupata taarifa kutoka kwenu.Tayari kumepambazuka, kuna mafanikio yoyote?”aliuliza Rais Pius akionekana kuwa na wasiwasi mwingi

“Mheshimiwa Rais, tayari tumekipata kirusi tunacho hapa pamoja na ile diski!” alisema Mathew.

“Ahsante, Yehova!” alisema Rais Pius na kushusha pumzi.

“Mheshimiwa Rais, kuna jambo limetokea wakati tunapambana kukipata kirusi.Joseph Nahimaha ameuawa.” Alisema Mathew na ukimya mfupi ukapita.Mathew akaendelea

“Wameuawa watu wawili,tunamshikilia pia Maurine Kyaso

na mwingine ambaye aliyebeba kirusi kukisambaza.Nicole amejeruhiwa na moto kwa sasa amepelekwa hospitali.”

“Mathew, naomba unihakikishie kwa mara nyingine tena kuwa kirusi kiko salama na hakijaweza kusambaa,” alisema Rais Pius.

“Mheshimiwa Rais, ninakuhakikishia kuwa kirusi kiko salama na hakijasambaa!”alisema Mathew

“Kazi nzuri sana,Mathew.Wewe na timu yako.Ninawahitaji hapa Ikulu mara moja mje na hicho kirusi,” alisema Rais.

“Mheshimiwa Rais,tunakuja, lakini kwanza nahitaji kumuhoji Maurine Kyaso kufahamu sababu za yeye na wenzake kufanya haya waliyoyafanya na

kuliweka taifa letu katika hatari.Nikipata majibu, tutakuja Ikulu kukukabidhi kirusi hiki,”alisema Mathew.

“Sawa,Mathew!Hakikisheni ameeleza kila kitu pamoja na mtandao wake wote!

“Mheshimiwa Rais,kuna suala pia nataka kulifahamu.Uliwasiliana na Rais wa Burundi jana usiku?”

“Ndiyo.Kuna nini?”Aliuliza Rais Pius.

“Anafahamu kuhusu hili suala la kirusi?”

“Ndiyo.Nilimweleza kila kitu kuhusiana na mipango ya Joseph Nahimana kuweka nchi zetu katika hatari kubwa.”

“Mheshimiwa Rais, samahani kwa kuuliza maswali nataka kujua, je, uliwasiliana naye baada ya sisi kuondoka Ikulu?”

“Ndiyo,Mathew!Baada ya ninyi kuondoka ndipo nilipowasiliana naye.Kuna nini,Mathew?”

“Mheshimiwa Rais, nitakuja kuzungumza nawe tutakapokuja huko.Kwa sasa nataka nipate majibu kutoka kwa Maurine,” alisema Mathew na kukata simu.Akageuka na kumfuata Maurine.

“Maurine,*it’s time now for you and I to talk*!”alisema Mathew.

“Agai, kata pingu yake,” Mathew aliongeza huku akijiweka sawa.

“*It’s over*” alisema Mathew akiendelea kumkazia macho Maurine

“Hatimaye Mchezo umemalizika na tumeibuka washindi huku wewe na vibaraka wenzio wa mabeberu mkishindwa vibaya.Nchi yetu bado ina amani na usalama wa kutosha,” alisema Mathew akitawaliwa na tabasamu la ushindi.Akanyamaza akamtazama Maurine aliyekuwa ameinamisha kichwa chini kwa fadhaa na aibu.

“Ulinishuhudia nikimtupa mwenzako Nicole katika moto baada ya kujifanya kiburi kueleza mahala kilipo kirusi.Sitaki unilazimishe nawe nikufanyie kitu kibaya kama nilichomfanya mwenzako.Nataka unieleze ukweli kila kitu kuanzia watu

unaoshirikiana nao,na kwa nini mkataka kuwaangamiza Watanzania.Nieleze kila kitu tafadhali," alisema Mathew.Maurine aliendelea kuinamisha kichwa chini.

"Maurine, inua kichwa.Nitazame usoni na unieleze kwa nini ulitaka kuwaangamiza ndugu zako kwa kirusi?"Mathew aliuliza.Maurine akainua kichwa juu, akamtazama Mathew.

"Nitazungumza na Rais pekee!"alisema

"Kabla ya kuzungumza na Rais, utazungumza na mimi kwanza na utanieleza kila kitu!"

"Siwezi kuzungumza nawe.Kama unataka niseme kitu, basi nitazungumza na Rais pekee na si mtu mwingine," Maurine alisisitiza.Mathew akamtazama

halafu akachukua simu ya Ruby.Akampigia Rais kumjulisha juu ya jambo hilo.Rais akaelekeza Maurine apelekwe Ikulu.Wakaingia garini wakaondoka kuelekea Ikulu.

17

Tayari kijua kilianza kuchomoza akina Mathew walipowasili Ikulu.Rais aliwapokea kwa furaha kubwa,akawakaribisha katika chumba cha chakula kwa ajili ya kupata kifungua kinywa.Wakati akina Ruby wakiendelea kupata kifungua kinywa, Rais na Mathew wakaenda katika chumba alimowekwa Maurine.

“Maurine, nimeambiwa unataka kuzungumza na mimi.”alisema Rais Pius

“Ndiyo.Lakini ni wewe peke yako.Sitaki huyu jamaa awepo”alisisitiza Maurine

“Kama una kitu cha kuzungumza, basi utazungumza mbele ya Mathew Mulumbi.Ni mtu ninayemuamini!”

alisema Rais. Kauli iliyomkata maini Maurine.Akavuta pumzi ndefu.

“Unamkumbuka Aamira Oduho?”Maurine aliuliza.Rais Pius akashtuka.

“*Do you know her, Mr President*?”Mathew aliuliza baada ya kumuona Rais amestuka baada ya kuulizwa swali.

“Ndiyo ninamfahamu.Ni mwanamke niliyekutana naye nikiwa katika shughuli za kulinda amani nchini Sudan zaidi ya miaka thelathini iliyopita.Mimi na yeye tulikuwa katika mahusiano,nilipoondoka Sudan kurejea Tanzania,hatukuwa na mawasiliano tena!”Alisema Rais Pius.

“Mwongo mkubwa!Ulimuacha Aamira akiwa na mimba

yako.Ulimuahidi utaondoka naye kuja Tanzania.Ajabu ukaondoka kimyakimya hata alipojifungua alikupigia simu, lakini ukamkana na ukatishia kumuua kama angeendelea kukusumbua.Aliteseka mno.Mtoto wake alipofikisha miaka nane, Aamira aliamua kujiunga na kundi la waasi ili aweze kujikimu.Kwa bahati mbaya akauawa na vikosi vya Tanzania vilivyovamia kambi yao.Mtoto wake alichukuliwa na kupelekwa nchini Marekani kusomeshwa.Mtoto ambaye ulimkana na kupelekea aishi maisha ya shida kubwa ni mimi!”alisema Maurine.Rais Pius akabaki kinywa wazi akishangaa.

“Unashangaa? Ndiyo!Ni mimi hapa.Mama yangu alinieleza kila kitu

kuhusu wewe na alinipa hadi picha zako.Kifo cha mama yangu kiliniumiza mno.Niliweka ahadi ya kuhakikisha siku moja ninalipiza kisasi kwako na kwa Tanzania.Kama si wewe kumkana mtoto,basi mama asingeweza kujiunga na kikundi cha waasi.Vilevile kama si vikosi vya Tanzania,basi mpaka leo hii mama angekuwa hai.Nakuchukia wewe,naichukia pia nchi hii," alisema Maurine kwa hasira kisha akanyamaza.

"Endelea kutueleza kila kitu," alisema Mathew.

"Nikiwa nchini Marekani,nilijitahidi sana kusoma na kujifunza Kiswahili kwa bidii kupitia mtandao na program mbalimbali.Baada ya kuhitimu masomo yangu nilijiunga na mafunzo ya

ujasusi.Baada ya kuhitimu, niliomba niletwe nchini Tanzania kwa ajili ya kuifanyia ujasusi Marekani.Ulifanywa mpango nikaonekana kama mmarekani mwenye asili ya Tanzania.Ilionekana wazazi wangu ni watanzania waliokuwa na uraia wa Marekani.Niliingia hapa nchini nikaukana uraia wa Marekani na kupewa uraia wa Tanzania.Nataka nikueleze kuwa Marekani tayari walikwisha tengeneza mtandao wao mrefu hapa nchini wengine ni watu wanaokuzunguka ambao walinipendekeza kwako ukaniteua kuwa mkuu wa idara ya siri ya usalama wa ndani wa nchi, yaani SNSA.Nikiwa SNSA kazi yangu ilikuwa kutafuta siri mbali mbali za nchi na kuzipeleka kwa

walionituma.Nilikutanishwa na Joseph Nahimana,akanieleza kuhusu mpango wa kuziunganisha nchi za Rwanda na Burundi kuwa sehemu ya Tanzania.Nilipewa maelekezo ya kuhakikisha jambo hilo halifanikiwi.Ili kujua kile kilichokuwa kinaendelea tulimuua waziri wa mambo ya nje na tukafanikiwa kupata taarifa ya mahala mazungumzo ya muungano yalikofikia.Pamoja na maelekezo ya kuzuia muungano usifanikiwe,binafsi nilikuwa na malengo ya kulipiza kisasi kwako na kwa nchi hii.Ajali iliyochukua uhai wa mkeo, ulikuwa mpango wangu.Nilitaka uumie!" Maurine akanyamaza. Rais Pius akauma meno kwa hasira.

“Mheshimiwa Rais,huyu tutaendelea kumuhoji kwa kina na atatueleza kila kitu.Nilikuuliza kama uliwasiliana na Rais wa Burundi na ulikubali uliwasiliana naye mara tu baada ya sisi kuondoka Ikulu.Tumegundua Rais Didier Manirakiza ana mawasiliano na huyu Maurine.Alimpigia simu jana usiku.Nina kila sababu ya kuamini ndiye aliyempa maelezo yote kuhusu kirusi na Maurine akatuma watu wakavamia watu uliowatuma wakalichukue sanduku,” alisema Mathew.Rais alibaki na mshangao.

“Unasema kweli?”aliuliza

“Ndiyo,Mheshimiwa Rais.Maurine ana mawasiliano na Rais Manirakiza.”

“*I can’t believe this*!”alisema Rais Pius akimtazama Maurine kwa hasira.

“Ni kweli haya anayoyasema Mathew? Una mawasiliano na Rais Didier Manirakiza?”

Maurine akacheka kidogo kisha akasema.

“Mnapoteza muda wenu bure kuzungumza eti muungano. Didier Manirakiza si mwenzenu na ndiye aliyevujisha siri zenu kwa mataifa makubwa.Rais,umezungukwa na nyoka wenye vichwa vya binadamu.Kama nisingekuwa na hasira nawe, basi ningekusaidia kuwaondoa mmoja baada ya mwingine,lakini kufanya hivyo ni kinyume na dhamira yangu kuu.!” Alisema Maurine

“Maurine, nataka utueleze kuhusu mtandao wenu wote.Nani unashirikiana nao hapa nchini? Hakuna haja ya kuficha, hawatakusaidia kwa sasa,” alisema Mathew. Maurine akameza funda la mate. Akainua kichwa na kumtazama Mathew, akamgeukia Rais Pius.

“Kwa kuwa mambo yameharibika!” Alisema Maurine kisha akaweka tuo. Akaendelea.

“Siwezi kufa mwenyewe nitawataja wote pamoja na mambo wanayoyafanya ya hujuma na ufisadi mkubwa.Wako viongozi serikalini,wanasiasa,wafanya biashara,wanahabari na wengine wengi.Ni mtandao mrefu”alisema Maurine

Rais Pius alizama katika lindi la mawazo.

“Baada ya kugundua kuwa mimi ni mwanao, je, utanifunga gerezani?”Maurine aliuliza swali la mtego.Rais Pius akakuna kichwa na kusema.

“Yote uliyoyasema kuhusu Aamira ni ya kweli kabisa.Nilikuwa na mahusiano naye wakati niko Sudan katika ulinzi wa amani.Alipata ujauzito ambao niliukana kuwa si wangu.Niliondoka na kurejea Tanzania,akafanya juhudi za kutafuta mawasiliano yangu, akayapata.Akanijulisha kuwa amejifungua mtoto wa kike, lakini nilimkana kuwa si mwanangu.Nikamtaka

asiendelee kunifuatilia.Alifika hadi katika ubalozi wetu wa Sudan, akaonana na balozi wetu kwa lengo la kutaka nigharamie matunzo ya mtoto kwa kuwa yeye hakuwa na kazi yoyote ya kumpatia kipato.Lakini bado niliendelea kubaki na msimamo wangu wa kukana kuwa mtoto si wangu.Baada ya hapo, sikuwahi kumsikia tena hadi leo hii.Sikutegemea mtoto ambaye nilimkana, ndiye wewe Maurine.Nisamehe sana!" alisema Rais Pius kwa masikitiko.

"Nimekuuliza swali, baada ya kujua mimi ni mwanao, je, utanishitaki?"Maurine aliuliza swali la awali.

"Elewa kwamba si mimi ninayekushitaki, bali umevunja sheria za

nchi na lazima ushitakiwe kwa mujibu wa sheria hizo. Maurine, hakuna namna ya kukusaidia katika hilo.Lazima sheria ichukue mkondo wake.Ni vipi kama kirusi kile kingeweza kusambaa? Maelfu ya Watanzania wangekufa.Hukupaswa kufanya jambo kama hili.Kama ulikuwa na hasira nami, ulipaswa kuelekeza kisasi chako kwangu na si kuua watu wasio na hatia," alisema kwa uchungu Rais Pius akatoka akiwa amefura kwa hasira.Mathew akabaki ndani.Akaendelea kuzungumza na Maurine ambaye alimtajia mtandao wote wa watu wanaoshirikiana nao nchini Tanzania kisha akatoka na kumfuata Rais.Akampatia orodha ya majina ya

wahusika wote, akayasoma na kushika kichwa.

“Hiki kilichotokea ninaona kama ndoto.Ama kweli dunia imekuwa ndogo.Sikutarajia eti Maurine ndiye mtoto niliyemkataa tangu akiwa tumboni.Dah ! alisema Rais Pius akimtazama Mathew.

“Mathew,*am I a bad person*?”Aliuliza Rais Pius.

“Mheshimiwa Rais, umeniuliza swali gumu ambalo nashindwa nijibu vipi.Lakini kila mtu ana mazuri na mabaya yake. Kikawaida,Watu unaowatendea mazuri watakuona kwa mazuri yako.Watu unaowatendea mabaya, watakuona kwa ubaya wako.*That’s it. No need to think too*

much over what happened in your past life. You can't fix the past. Mimi binafsi niko upande wa mazuri.Na jibu lake tayari umeshalifahamu!"

"Unadhani ninafanya kitu sahihi kwa mwanangu? Maurine ni damu yangu kabisa!" alisema Rais Pius.

"Mheshimiwa Rais, umefanya kitu sahihi kabisa.Amevunja sheria za nchi na lazima aadhibiwe kwa makosa aliyoyatenda.Hakuna namna ya kumsaidia katika hili," alisema Mathew.Rais Pius akafikiri kisha akasema.

"Mathew, kuna jambo nataka kukuonya kijana wangu.Ninyi mnazunguka sana mnakutana na wanawake wengi.Hata siku moja

usithubutu kumkataa mwanamke kama una uhakika amepata mimba yako.Usithubutu kumkataa mtoto angali akiwa tumboni mwa mama yake.Mimi nilifanya kosa kubwa kumkataa Maurine.Na haya ndiyo matokeo yake,Laiti kama nisingemkataa Maurine, hivi sasa asingekuwa hivi alivyo. Angekuwa na maisha bora zaidi.Ile roho ya kisasi asingekuwa nayo.Ni mimi ambaye nimeyaharibu maisha yake.Ninajuta sana,lakini sina namna ya kufanya kumsaidia.Sheria lazima ichukue mkondo wake!" alisema Rais Pius

"Uko sahihi,Mheshimiwa Rais!" alisema Mathew.Rais akachukua simu

yake na kumpigia Rais Alpha Nahimana wa Rwanda

“Mheshimiwa Rais Pius, habari za asubuhi. Mmeamka salama huko Tanzania?” aliuliza Rais Alpha.

“Huku kwema, tunashukuru jana tumefanikiwa kuwapata watoto wetu waliotekwa na magaidi pamoja na ile ndege yetu mpya iliyopotea.Rais Alpha, kuna jambo kubwa limetokea usiku wa kuamkia leo mkuu wangu ujasusi atakueleza kwa undani,” alisema Rais Pius akampa simu Mathew Mulumbi azungumze na Rais Alpha.

“Mheshimiwa Rais, shikamoo.Ninaitwa Mathew Mulumbi.Ni mkuu wa Shirika la UjasusiTanzania!”

“Nashukuru kuzungumza nawe,Mathew Mulumbi!”alisema Rais Alpha.

Mathew akamueleza Rais Alpha Nahimana kuhusiana na mipango ya mabeberu kuhakikisha nchi za Rwanda na Burundi hazijiungi na kuwa sehemu ya Tanzania.Alimshtua alipomtaja mwanae Joseph Nahimana kuwa ndiye aliyetumiwa na mabeberu akishirikiana na Maurine Kyaso.Alimweleza kuhusiana na kirusi walichotaka kukisambaza halafu akampa simu Rais Pius.

“Mheshimiwa Rais Alpha, umemsikia mkuu wangu wa ujasusi alichokisema?”

“Ndiyo,Mheshimiwa Rais.Nimeshtuka sana.Sikutegemea kabisa.Haya mambo yetu ya siri wameyafahamu vipi?”Aliuliza Rais Alpha.

“Didier!” akajibu Rais Pius.

“Didier?" Una hakika?”Aliuliza Rais Alpha.

“Ndiyo.Tulikuwa tunashirikiana na nyoka wa vichwa viwili bila kujua kuwa Didier ni kibaraka wa mabeberu!”

“Umenishtua sana,Mheshimiwa Rais,” alisema Rais Alpha.

“Hata mimi nilishtuka sana nilipopata taarifa hizi.Mheshimiwa Rais Alpha, kuna mengi tutazungumza, lakini kuna jambo moja nataka kukujulisha

mimi mwenyewe” alisema Rais Pius na kuvuta pumzi ndefu.

“Joseph ameuawa!”alisema Rais Pius

“Ameuawa?” Rais Alpha akashtuka.

“Mheshimiwa Alpha,mwanao Joseph aliuawa wakati vijana wangu walipovamia katika nyumba aliyokuwa amejificha yeye na wenzake wakiendelea na mipango ya kusambaza kirusi”

“Jenerali Pius,kweli mwanangu ameuawa?”aliuliza Rais Pius

“Ndiyo, ameuawa!”

“Kwa nini hakukamatwa na badala yake akauawa? Ulitoa maelekezo auawe?” Aliuliza Rais Alpha huku sauti yake ikisikika kutetemeka katika spika za simu.

“Nilitoa maelekezo hayo kwa watu wangu kwamba yeyote anayehusika katika kutaka kusambaza kirusi aidha **akamatwe** au **auawe**!”alisema Jenerali Pius.

“Jenerali Pius, umenisikitisha sana.Sikutarajia kama ungeweza kunifanyia kitu kama hiki.”alilalamika Rais Alpha

“Mwanao ni mhalifu na alikuwa tayari kuua maelfu ya Watanzania.Alpha, unapaswa kushukuru badala ya kusikitika kwa sababu endapo kirusi hicho kingesambaa kingefika hadi Rwanda.Unadhani mngesalimika?”aliuliza Rais Pius

“Pius sihitaji maelezo mengine tena.Ninachohitaji kwa sasa ni mwili wa

mwanangu uweze kuwasili hapa Rwanda leo.Wakati mwili huo utakapotua,tambua kuwa mazungumzo yetu ya muungano yamefikia mwisho.Siwezi kukaa meza moja na wauaji!”Alisema Rais Alpha na kukata simu kwa hasira.

Mathew na Rais, kwa pamoja wakaenda katika chumba cha mapumziko ambako akina Gosu Gosu walikuwa wamejipumzisha.Waliwaeleza kila kitu alichokisema Maurine.

“Vijana wangu, ninawashukuru sana na kuwapongeza kwa uzalendo mkubwa kwa nchi yenu.Nawashukuru kwa kukipata kirusi.Nitakikabidhi kwa jeshi la wananchi, wao watakifukia ardhini mahali ambako hakuna atakayepafahamu.Kabla ya kufika jioni

ya leo, lazima wale wote ambao wametajwa na Maurine ambao ni mtandao unaoshirikiana na mabeberu wawe wamekamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria,”Rais Pius alisema.

Alizungumza mengi na akina Mathew kisha wakaagana. Kila mmoja akarejea nyumbani kwake kupumzika.

MWAKA MMOJA BAADAYE

Magari mawili yaliwasili katika gereza kuu la Uwangwa na kuelekea moja kwa moja maegesho.Kutoka katika moja ya gari,alishuka Perpetua Mawingu mtoto wa Rais Pius Mawingu.Aliongozana na walinzi wake,

wakaelekea ndani ya gereza.Walilakiwa na mkuu wa gereza,akawaongoza katika ukumbi ambao wafungwa hukutana na ndugu au watu waliowatembelea.Baada ya dakika tano, akatokea Maurine Kyaso akiwa ameongozana na askari magereza.Akapelekwa katika meza aliyokuwa amekaa Perpetua.Wakatazamana kwa sekunde kadhaa kisha Perpetua akasema .

“Shikamoo, dada!”

Maurine Kyaso alishindwa kujibu, akabaki anabubujikwa na machozi.

“Baba amenieleza kila kitu kuhusu wewe.Amenieleza ukweli wote kwamba wewe ndiye uliyemuua mama yangu mzazi.Nililia sana!” alisema Perpetua

“Perpetua,*I’m sorry.Very sorry,*” alisema Maurine.

“Maurine, hupaswi kuniomba msamaha mimi.Unapaswa kumuomba msamaha Mungu baba wa mbinguni kwani ni yeye ndiye uliyemkosea.Mimi ni mwanadamu kama wewe tu,” Perpetua alitulia kidogo. Akaendelea.

“Mimi nimekwisha kusamehe kwa yote uliyonitendea,” akanyamaza tena.

“Tunafundishwa kuwasamehe wale wote waliotukosea.Mimi sina sababu yoyote ya kutokukusamehe.Maisha yetu ni mafupi sana hapa duniani hivyo tunapaswa kuishi kwa kupendana.Nimekuja mimi leo hii kukutembelea hapa gerezani na kukueleza kuwa sina tatizo na wewe hata

kidogo.Sisi ni ndugu, na nitakuwa ninakuja hapa mara kwa mara kukutembelea.Naomba ufahamu pia, baba anakupenda vile vile.Ulitie akilini neno hili, kila siku anajutia nafsi yake kwa kile alichokifanya.” alisema Perpetua huku akidondokwa na machozi.

“Maurine, unatumikia kifungo cha maisha gerezani.Sijawahi kukaa gerezani, lakini najua ni sehemu pweke sana.Nimekuletea kitabu,” alisema Perpetua.Akatoa ishara akamuita askari magereza

“Ninaruhusiwa kumpa kitabu?”Aliuliza Perpetua.Kabla ya kujibu,askari magereza akakichukua kile kitabu, akakikagua kama kiko salama au la.Akachungua mpaka ndani, kurasa

baada ya kurasa kutazama kama hakuna chochote ndani. Hakukuta kitu.Akamrudishia Perpetua.

“Nimekuletea biblia.Isome na humu ndimo utakamopata faraja.Utapata nafasi ya kumfahamu Mungu hata maisha yako humu gerezani yatakuwa na furaha na amani,” alisema Perpetua.

Walizungumza mambo mengi hadi muda wa Perpetua kuondoka ulipofika.Maurine akamuita askari, akamuomba ruhusa amkumbatie Perpetua.Akaruhusiwa. Akafanya hivyo na hatimaye Perpetua akaondoka moyo ukiwa mkunjufu.

“Sasa nina amani ya moyo!” aliwaza wakati akifunguliwa mlango na kuingia

garini.Safari ya kutembelea gereza la Uwangwa iliishia hapo.

Kila aliyeshiriki kwa namna moja au nyingine katika kuihujumu nchi alikutana na mkono wa sheria. Watu zaidi ya sitini waliokuwa wakishirikiana na mabeberu katika hujuma mbali mbali likiwamo shambulio la kigaidi Arusha walikuwa wanatumikia adhabu mbali mbali katika gereza kuu la Uwangwa.

Mazungumzo ya kuziunganisha nchi za Rwanda na Burundi kuwa sehemu ya Tanzania yaliyeyuka kama moshi.Mipango yote ya mabeberu kuihujumu Tanzania ilishindwa na Tanzania ilizidi kupaa kiuchumi kuelekea kuwa taifa lenye uchumi mkubwa zaidi katika bara la Afrika.

TAMATI